JAMHURI YA KENYA

Mali ya
Serikali ya Kenya
**HAKIUZWI**

# Kiswahili 3

## Mazoezi ya Lugha

### Mwongozo wa Mwalimu



KIMEIDHINISHWA
KIMEAINISHWA KWA MTAALA ULIOJIKITA KWENYE UFARISI
KICD

**Tusome Early Literacy Programme**

# Kiswahili 3

Mazoezi ya Lugha

Mwongozo wa Mwalimu

## Yaliyomo


Utangulizi ........ ii
Dibaji ........ ii
Mwongozo wa Mwalimu ........ iv
Utangulizi ........ v
Mwongozo wa Mwalimu wa Kiswahili kwa Darasa la 3 ........ vi
Tathmini ........ vii
**Marejeleo 1** ........ 1
(Kipindi cha 1 hadi 5)
**Shambani 1** ........ 11
(Kipindi cha 6 hadi 10)
**Sokoni 1** ........ 20
(Kipindi cha 11 hadi 15)
**Uzalendo 1** ........ 27
(Kipindi cha 16 hadi 20)
**Miezi ya mwaka 1** ........ 32
(Kipindi cha 21 hadi 25)
**Kazi mbalimbali 1** ........ 37
(Kipindi cha 26 hadi 30)
**Usalama 1** ........ 42
(Kipindi cha 31 hadi 35)
**Usafi wa mazingira 1** ........ 48
(Kipindi cha 36 hadi 40)
**Dukani 1** ........ 55
(Kipindi cha 41 hadi 45)
**Ndege nimpendaye 1** ........ 60
(Kipindi cha 46 hadi 50)
**Marejeleo 2** ........ 67
(Kipindi cha 51 hadi 55)
**Sokoni 2** ........ 72
(Kipindi cha 56 hadi 60)
**Shambani 2** ........ 78
(Kipindi cha 61 hadi 65)
**Uzalendo 2** ........ 84
(Kipindi cha 66 hadi 70)
**Miezi ya mwaka 2** ........ 89
(Kipindi cha 71 hadi 75)
**Kazi mbalimbali 2** ........ 94
(Kipindi cha 76 hadi 80)
**Usalama 2** ........ 99
(Kipindi cha 81 hadi 85)
**Usafi wa mazingira 2** ........ 104
(Kipindi cha 86 hadi 90)
**Dukani 2** ........ 109
(Kipindi cha 91 hadi 95)
**Ndege nimpendaye 2** ........ 114
(Kipindi cha 96 hadi 100)
**Marejeleo 3** ........ 119
(Kipindi cha 101 hadi 105)
**Shambani 3** ........ 124
(Kipindi cha 106 hadi 110)
**Sokoni 3** ........ 129
(Kipindi cha 111 hadi 115)
**Uzalendo 3** ........ 134
(Kipindi cha 116 hadi 120)
**Kazi mbalimbali 3** ........ 139
(Kipindi cha 121 hadi 125)
**Usalama 3** ........ 144
(Kipindi cha 126 hadi 130)
**Usafi wa mazingira 3** ........ 149
(Kipindi cha 131 hadi 135)
**Kazi mbalimbali 4** ........ 154
(Kipindi cha 136 hadi 140)
**Dukani 3** ........ 159
(Kipindi cha 141 hadi 145)
**Ndege nimpendaye 3** ........ 164
(Kipindi cha 146 hadi 150)



© 2021 ya RTI International kwa nchi zote isipokuwa Jamhuri ya Kenya.

RTI International ni alama na jina la kibiashara la Research Triangle institute.

Haki ya Kunakili ya Jamhuri ya Kenya inashikiliwa na wizara ya elimu Kenya.



Chapisho hili limefanikishwa kupitia kwa ufadhili kutoka kwa shirika la kimataifa na maendeleo la America (USAID) kupitia mradi wa USAID -Tusome.



Kazi hii inapatikana chini ya leseni ya Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 International (CC BY-NC-ND 4.0). Ili kuona nakala ya leseni hii, tembelea https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/ ama tuma barua kwa Creative Commons, sanduku la posta 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

**Kunukuu na kutambua kazi asili** — Ukinakili na kusambaza kazi hii tafadhali nukuu kama ifuatavyo: *Imenakiliwa kutokana na kazi asili ya RTI International na kuruhusiwa chini ya leseni ya Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 International (CC BY-NC-ND 4.0).*

**Si ya Biashara** — Usitumie kazi hii kwa nia ya biashara.

**Si ya Kuigaiga na Kusambazwa** — Usisambaze kazi hii kama utaifanyia mabadiliko kazi asili pamoja na kuichanganya na kazi nyingine, kuitumia kama msingi wa kazi nyingine au kuibadilisha kwa njia yoyote ile.

**Kazi ya Mtu wa Tatu** — Sio lazima RTI International kumiliki kila kipengele cha maudhui yaliyomo katika kazi hii. Hivyo basi, RTI international haikuhakikishii ya matumizi ya kipengele chochote cha kazi ya mtu mwingine au baadhi ya kazi yake haitakiuka haki za watu hao. Utawajibika kutokana na hatari ya kudaiwa kutokana na kuingilia haki za wengine. Ukitaka kutumia tena kipengele cha kazi hii, ni jukumu lako kuamua kama imeruhusiwa kutumia tena na kupata ruhusa kutoka kwa mwenye hati ya kunakili. Baadhi ya mifano ya vipengele hivi ni majedwali, maumbo na picha.



Kimechapishwa nchini Kenya kwa ufadhili kutoka kwa USAID (U.S. Agency for International Development) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

ISBN: 978 9966 110 03 9

Toleo la Kwanza

Kimechapishwa 2018

# Utangulizi

Serikali ya Kenya imejitolea kutoa elimu bora kama haki ya kimsingi kwa wanafunzi wote. Azma hii inaambatana na majukumu ya kitaifa na kimataifa yanayohitaji kila nchi kukimu mahitaji ya kielimu na kijamii ya raia wake. Ingawa juhudi zimefanywa kuhakikisha elimu inapatikana kwa urahisi, lengo kuu la serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu bora. Serikali ya Kenya imewekeza zaidi katika kuboresha vifaa vya kielimu, miundomsingi pamoja na wafanyakazi ili kuinua kiwango cha elimu inayotolewa katika viwango vyote vya elimu nchini. Mfumo wa elimu unaolengwa umebuniwa kutokana na matokeo ya utafiti wa kina. Kadhalika umejumuisha mbinu zingine zinazokubalika na kutumiwa kimataifa. Msukumo uliopo katika mageuzi ya elimu unatokana na haja ya kuifanya elimu nchini Kenya kuwa kwenye kiwango ya kimataifa na kuwa ya manufaa kiuchumi katika jamii. Serikali inahakikisha kwamba kupitia kwa elimu, wananchi watakuwa wabunifu na kupata stadi za karne ya 21 ukiwemo utafiti, kutatua matatizo, kufikiria kwa kina na kufanya kazi katika hali zote.

Vitabu vya TUSOME ambavyo vimeshirikisha maadili ya mtaala mpya vimeandikwa ili kuimarisha uwezo wa kujua kusoma na kuandika, uwezo ambao ni stadi ya kimsingi katika elimu bora. Kitabu hiki kitatumika katika Gredi ya 3 kujifunza na kufundishia Kiswahili katika mtaala mpya. Mpangilio wa kitabu hiki unatilia maanani maantiki na mikakati inayotokana na utafiti ili kukuza stadi za kusoma na kuandika. Vilevile, mpangilio huu utahakikisha kuwa wanafunzi wanapata umilisi ambao ni muhimu kwa viwango vyao.

Ninawasihi washikadau wote kuendelea kuunga mkono mageuzi yanayoshughulikiwa katika sekta ya elimu nchini Kenya ili kufikia matokeo bora.

[redacted]

# Dibaji

Wizara ya Elimu imejitolea kuwapa wakenya elimu bora kama ilivyo katika Katiba ya Kenya, 2010. Mabadiliko yanayoendelea katika elimu yanalenga kushughulikia elimu bora. Mipango ya utafiti kama vile Tathmini ya Kitaifa ya Ufuatiliaji wa Mafanikio ya Masomo (NASMLA) na Muungano wa Kusini na Mashariki ya Afrika wa Kufuatilia Ubora wa Elimu (SACMEQ) imeangazia mianya ambayo inafaa kushughulikiwa ili kuboresha matokeo ya elimu.

Matukio ya hivi punde katika mfumo wa elimu yanasisitiza uwezo wa kusoma na kufanya hesabu kama nguzo ya kujifunza katika darasa tangulizi .Umakinifu katika elimu umechangia hatua ambazo zimeimarisha matokeo ya kusoma na kufanya hesabu. Mradi wa kitaifa wa Tusome umeimarisha uwezo wa mwanafunzi wa kusoma na kuandika katika Gredi ya 1 na ya 2. Matokeo haya bora yamechangia kuendelezwa kwa mradi huu hadi gredi ya 3. Kitabu hiki kimeandikwa ili kuelekeza mafunzo ya Kiswahili; kiwango cha Gredi ya 3 katika mtaala mpya. Mbinu za ubunifu katika kujifunza na kufundisha pamoja na Masuala Mtambuko yameangaziwa kulingana na mtaala mpya.

Wizara ya Elimu inatambua usaidizi wa kifedha kutoka kwa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID). Kadhalika, ningependa kutoa shukrani zangu kwa washirika na washikadau wengine kwa mchango wao katika uandishi na uchapishaji wa vitabu hivi.

[redacted]

Katibu Mkuu, Elimu ya Msingi

Wizara ya Elimu.

# Mwongozo kwa Mwalimu

Mwongozo huu wa mwalimu umejikita kwenye mfumo wa kufundisha wa moja kwa moja. Mbinu hii humsaidia mwalimu kufundisha wanafunzi akitumia ujuzi wa kimsingi ambao unahitajika katika kuboresha ufasaha wa kusoma, kufahamu na kuandika. Mbinu hii huzingatia hatua tatu rahisi: kuonyesha kwa mfano, maongozi kwenye mazoezi na mazoezi huru au tathmini. Kwa kutumia mbinu hii, Mwalimu huweka mikakati iliyosawazishwa ya kufundishia na kuonyesha mkusanyiko wa shughuli ndani ya darasa. Japo mbinu hii huruhusu ubunifu wa mwalimu, matayarisho ya mwalimu ni sharti kwa kufanikisha somo kwenye mwongozo huu. Walimu wanahimizwa kubuni, kutayarisha na kutumia nyenzo za kufundishia zinazolingana na muktadha utakaoboresha umilisi wa maudhui yanayofundishwa. Nyenzo hizi zinaweza kujumuisha vifaa halisi na vya kidijitali, picha, ramani, kamusi, na kadhalika.

Matumizi ya ubao ni muhimu na yanatiliwa mkazo katika mwongozo huu. Hata hivyo, inampasa kila mwanafunzi kuwa na kitabu chake mwenyewe ili kuongeza uzoefu wake wa kusoma. Zaidi ya hayo, kuna mazoezi kwenye kitabu cha mwanafunzi ambayo yanawahitaji wanafunzi kuyafanya pekee yao darasani. Kazi ya ziada pia imejumuishwa ili wanafunzi wafanye mazoezi wakiwa nyumbani. Lengo kuu haswa ni kuhakikisha kuwa mlezi au mzazi anashirikishwa katika jitihada za kumwezesha mwanafunzi kunawiri kimasomo. Walimu wanahimizwa kuangalia kazi ya wanafunzi ili kuhakikisha kuwa mazoezi yote yanafanywa na kutoa tathmini yenye maana kwa wakati ufaao. Ni vyema kukumbuka pia kwamba walimu hawapaswi kuhisi kuwa wamezuiwa kuwapa wanafunzi kazi zingine zifaazo za ziada tu. Ikiwa wanahisi kuwa wanafunzi wanahitaji mazoezi zaidi, wanapaswa kutumia uamuzi wao kutoa mazoezi yanayofaa kama kazi ya ziada.

Walimu pia wanahimizwa kuchagua shughuli zitakazofanikisha uelewa wa wanafunzi wa dhana zinazofundishwa. Shughuli hizi zinajumuisha maonyesho, maigizo au maelezo kwa kutumia maneno mafupi, rahisi na yanayoeleweka.

Mwongozo huu wa mwalimu umeundwa kwa njia inayoondoa vizuizi kwa ujifunzaji bora. Hivyo basi, mwongozo huu unakidhi mahitaji ya wanafunzi wote (hata wenye ulemavu) kwa kuzingatia viwango vyao vya kuelewa na changamoto zao. Wanafunzi kama hawa wanaweza kusaidiwa na walimu kwa njia kadha wa kadha. Zifuatazo ni baadhi ya njia anazoweza kutumia mwalimu kuwasaidia wanafunzi wenye changamoto tofauti za kujifunza.

**Namna ya kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.**

1. Mwalimu anapaswa kutafuta mbinu ya kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji maluum. Baadhi ya mahitaji haya ni kama vile:
   a) matatizo ya kusikia.
   b) matatizo ya kuona.
   c) udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo haraka.
   d) udhaifu wa kuwasiliana. Kwa mfano, mtoto aliyekigugumizi na kadhalika.
   e) udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili.
   f) walio hodari katika kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani.
2. Ni muhimu kwa mwalimu kutambua uwezo na udhaifu wa kila mwanafunzi kabla ya, wakati wa na baada ya somo. Kufanya hivi kutamwezesha kushughulikia mahitaji hayo kwa njia inayofaa ili yasiadhiri mafanikio ya somo. Mifano ya mahitaji maalumu na namna ya kuyashughulikia imetolewa katika Jedwali la 1.



Hakiuzwi

**Jedwali la 1: Mahitaji Maalum ya Wanafunzi na Mapendekezo na Namna ya Kuyashughulikia**

| Mahitaji | Mapendekezo na Namna ya Kuyashughulikia |
|---|---|
| a) Matatizo ya kutosikia | - Tumia lugha ya ishara inapowezekana.<br>- Mwanafunzi aketi karibu na mwalimu au pale anapoweza kusikia vizuri.<br>- Himiza matumizi ya vipaza sauti inapowezekana.<br>- Matumizi ya vifaa halisi kunahimizwa. |
| b) Matatizo ya kutoona vyema | - Mwanafunzi aketi karibu au mbali na ubao kulingana na mahitaji yake.<br>- Himiza matumizi ya breli (braille) inapofaa.<br>- Jadili na wazazi au walezi matumizi ya miwani au vioo vya kukuza kimo cha maandishi.<br>- Epuka ama ondoa vifaa vinavyoathiri uwezo wa kuona.<br>- Mwanafunzi aketi karibu au mbali na mwangaza kulingana na mahitaji yake.<br>- Matumizi ya vifaa halisi kunahimizwa. |
| c) Udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo kwa haraka | - Wape wanafunzi hawa muda mwingi wa ziada kuliko wanafunzi wengine.<br>- Watengewe muda maalumu wa kurejelea waliyosoma baada ya somo.<br>- Gawa somo kwa hatua fupi fupi kuanzia nyepesi hadi hatua tatanishi.<br>- Wape mazoezi ya ziada.<br>- Mwalimu awakinge wanafunzi walio na udhaifu dhidi ya kudunishwa kwa njia yoyote ile. |
| d) Udhaifu wa kuwasiliana/ kigugumizi | - Wape wanafunzi muda wa kuwasilisha mawazo yao.<br>- Mwalimu aepukane na vitendo vinavyoweza kuathiri hisia au maono ya wanafunzi.<br>- Mwalimu atumie mbinu tofauti za mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. |
| e) Udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili | - Mwanafunzi apewe muda wa ziada ili kukidhia upungufu (ulemavu) wake.<br>- Wapewe vifaa vya teknolojia ikiwezekana au vya kubuniwa kulingana na hali ya ulemavu ili kuongeza uwezo wa utenda kazi wao.<br>- Mwalimu anaweza kushauriana na wahudumu wa walemavu kwa usaidizi zaidi. |
| f) Walio hodari katika kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani | - Wanafunzi wapewe kazi ya ziada ili watumie muda wao vyema.<br>- Wanafunzi wapewe nafasi za kukuza vipawa vyao.<br>- Wanafunzi wapewe kazi zenye changamoto zaidi ili kufanyisha kazi akili zao na kuwapa fursa ya kutumia uhodari wao. |

# Utangulizi

Mwongozo huu umendaliwa kwa maelekezo ya wataalamu wa kimataifa na wa hapa nchini wa kusoma na wa lugha kwa kufuata mchakato uliopangwa kwa utaratibu. Kwenye warsha ya kwanza ya maafisa wa Wizara ya Elimu na ya Taasisi ya Mitaala ya Kenya, upeo na mpangilio ulibuniwa ambao umekuwa ramani kwa kuendeleza mpangilio wa somo. Kwenye warsha hiyo, maamuzi yaliafikiwa kuhusu ujuzi wa kukuzwa miongoni mwa wanafunzi kwa kila muhula na shughuli maalum ambazo zingetumiwa kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kuna jaribio la wazi la kuwa na mwendelezo wa herufi na sauti kutoka kwa darasa la 2 na msisitizo wa kusoma maneno magumu zaidi yenye uwiano tata kati ya herufi na sauti na kuwasilisha kwa mwanafunzi mikakati mingine ya kusoma maneno.

Matini kwenye masomo yanawiana kimandhari na silibasi ya Taasisi ya Mitaala ya Kenya na yameundwa kwa uangalifu ili kumfidua mwanafunzi kwa aina tofauti ya maandishi huku pia yakitilia maanani misamiati ya kimandhari. Kila matini inajumuisha mifumo ya maneno na miundo husika ya lugha. Ili kuboresha ufahamu wa wanafunzi wa matini, baadhi ya mbinu za ufahamu zinazolingana na kiwango chake zimetumiwa ili kumpa mwanafunzi mbinu tofauti za kuelewa matini.

Katika darasa la 3, mwanafunzi anafunzwa kutumia hatua tano katika mchakato wa kuandika. Hatua hizi ni kabla ya kuandika/kupanga, kuandika nakala ya kwanza, kuhakiki, kurejelea na kuchapisha. Kila hatua hufunzwa kwa wiki moja. Mbinu hii hutoa nafasi kwa mwanafunzi kufanya mazoezi ya kila hatua kwenye mchakato huku wakikuza uwezo wa kuandika insha bila msaada.

Kila mpango wa somo unajumuisha shughuli tofauti zilizopangwa ili kukuza ujuzi na ufahamu wa mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Shughuli za somo ni simulizi na za kuandika zikizingatia stadi nne za lugha (kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika). Katika masomo manne ya kwanza, wanafunzi hujifunza na kufanya mazoezi ya matumizi ya maneno, kusoma hadithi, ufahamu na sarufi. Somo la tano linazingatia marejeleo na shughuli za kutathmini zitakazosaidia mwalimu kufuatiliza maendeleo ya mwanafunzi. Mambo haya yametolewa, japo kwa muhtarasi katika Jedwali la 3.



Hakiuzwi

## Jedwali la 2: Mwongozo wa Mwalimu wa Kiswahili kwa Darasa la 3

| Shughuli | Utangulizi | Kipindi cha mazoezi 1 | Utangulizi 2 | Kipindi cha mazoezi 2 | Kipindi cha marejeleo (Tathmini) |
|---|---|---|---|---|---|
| Masamiati | 8 | | 8 | | 8 |
| Kujifunza Maneno | | 6 | | 6 | |
| Mwanafunzi kusoma matini | 10 | 7 | 10 | 7 | 4 |
| Ufahamu | 7 | | 7 | | |
| Uhakiki wa matini | | | | | |
| Sarufi | 5 | 4 | 5 | 4 | 17 |
| Mchakato wa kuandika | | 13 | | 13 | 5 |
| Mwalimu Kusoma matini | | | | | |
| Uhakiki wa matini | | | | | |

## Jedwali la 3: Mwongozo wa Mwalimu wa Kiswahili kwa Darasa la 3

| Utangulizi 1 | Kipindi cha mazoezi 1 | Utangulizi 2 | Kipindi cha mazoezi 2 | Kipindi cha marejeleo (Tathmini) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 26 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | 32 | 33 | 34 | 35 |
| 36 | 37 | 38 | 39 | 40 |
| 41 | 42 | 43 | 44 | 45 |
| 46 | 47 | 48 | 49 | 50 |
| 51 | 52 | 53 | 54 | 55 |
| 56 | 57 | 58 | 59 | 60 |
| 61 | 62 | 63 | 64 | 65 |
| 66 | 67 | 68 | 69 | 70 |
| 71 | 72 | 73 | 74 | 75 |
| 76 | 77 | 78 | 79 | 80 |
| 81 | 82 | 83 | 84 | 85 |
| 86 | 87 | 88 | 89 | 90 |
| 91 | 92 | 93 | 94 | 95 |
| 96 | 97 | 98 | 99 | 100 |
| 101 | 102 | 103 | 104 | 105 |
| 106 | 107 | 108 | 109 | 110 |
| 111 | 112 | 113 | 114 | 115 |
| 116 | 117 | 118 | 119 | 120 |
| 121 | 122 | 123 | 124 | 125 |
| 126 | 127 | 128 | 129 | 130 |
| 131 | 132 | 133 | 134 | 135 |
| 136 | 137 | 138 | 139 | 140 |
| 141 | 142 | 143 | 144 | 145 |
| 146 | 147 | 148 | 149 | 150 |

# Tathmini

Mfumo mpya wa elimu unadhamiria kuhakikisha kuwa matokeo ya mafunzo ni ujenzi wa umilisi utakaomwezesha mwanafunzi kutumia ujuzi wake kujiendeleza. Kutokana na hayo, mwongozo huu umezingatia tathmini katika kila kipindi na mwishoni mwa kila wiki.

| Mada | Mada Ndogo | Mapendekezo ya tathmini |
|---|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | Kusikiliza kwa makini | - Tathmini matumizi ya mwanafunzi ya ishara.<br>- Uliza maswali |
| | matamshi | - Tathmini anavyotamka maneno.<br>- Tathmini matumizi ya maneno katika mazungumzo. |
| | Msamiati | - Tathmini anavyotamka msamiati lengwa na anavyotumia msamiati huo kujieleza au kutunga setensi na katika maandishi. |
| | Muundo wa lugha na matumizi yake. | - Tathmini anavyotunga sentensi katika miktadha tofautitofauti na ikiwa anazingatia muundo mwafaka wa lugha katika mazungumzo na katika maaandishi.<br>- Unaweza kutumia maswali kupima uelewa wao wa muundo lengwa wa lugha. |
| Kusoma | Ufahamu wa jina na sauti ya herufi. | - Tathmini ufahamu wao wa jina na sauti ya herufi lengwa na anavyotumia ujuzi huo kusoma maneno mapya. |
| | Kusoma maneno | - Tathmini ufasaha wao wa kusoma maneno, kucheza michezo ya maneno na mbinu wanazotumia kusoma maneno mapya. |
| | Kusoma matini kwa ufasaha. | - Tathmini ufasaha wao wanaposomeana wakiwa wawiliwawili, katika darasa zima au akiwa peke yake.<br>- Tathmini iwapo anazingatia shadda na kiimbo wakati wa usomaji. |
| | Ufahamu | - Waulize watabiri kitakachotendeka katika hadithi kabla na wakati wa kusoma.<br>- Tathmini pia wanavyosimulia hadithi waliyoisoma, jibu maswali ya ufahamu au kujadili wahusika na muktadha wa matini lengwa. |
| Kuandika | Hati | - Tathmini nakala zao za maneno na sentensi au michoro hasa wakati wa imla na kuandika (kwa mfano picha hadithi na insha za wasifu). Zingatia maumbo na mpangilio mwafaka wa maneno. Tumia kazi zao kujadili kuhusu hati nadhifu. |
| | Tahajia | - Tathmini ikiwa wamezingatia tahajia katika maandishi yao. Unaweza kutumia kadi herufi na kamusi katika tathmini hiyo. |
| | Uakifishaji | - Tathmini usahihi wa uakifishaji wao (herufi kubwa/ndogo, koma, kituo na kiulizi) katika maandishi na ikiwa wanaweza kutambua alama lengwa za uafikishaji. |
| | Mwongozo wa uandishi. | - Tathmini mazoezi yao yanayozingatia kujaza nafasi katika sentensi, kuandika sentensi kutokana na jedwali au picha hadithi. Zingatia usahihi wa sentensi zao katika maandishi. |



Hakiuzwi

Kipindi cha | 1 na 2 | **Marejeleo 1**

Matini

**Wanyama Wapenda Kazi**

Katika mji wa Songo paliishi simba, sungura, fisi, mbweha, kifaru na twiga. Simba aliwaita mkutanoni. Akasema, "Tutasafisha mazingira yetu. Kila mnyama atakuwa na sehemu yake ya kusafisha." Sungura kwa ujanja wake akasema, "Naumwa na jino. Siwezi kufanya kazi." Simba alinguruma kama radi na kusema, "Kila mnyama atafanya kazi!"



Mbweha alimwambia sungura, "Sungura, njoo twende ndani tupanguse matone ya mchuzi na chai iliyomwagika mezani. Tutasaidiana." Sungura alikubali shingo upande, akapangusa meza vibaya. Simba alipokuja mezani, akauliza kwa ukali, "Ni nani aliyepangusa meza hii vibaya?" Sungura alitetemeka aliposikia mngurumo wa simba. Aliipangusa meza iliyokuwa chafu ikawa safi. Mbweha naye akapanga viti alivyopangua sungura. Twiga alitumia mdomo wake kukata matawi. Simba aliziba ua huku akisema, "Lazima tuzibe nyua. Zinatulinda kutokana na maadui." Fisi naye aliokota takataka na kuzitupa kwenye shimo maalum. Wanyama hawa walifurahishwa na usafi wa mazingira yao.

1 Hakiuzwi

Kipindi cha | 1 na 2 | **Marejeleo 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

safi mazingira chafu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

tutasafisha alipangusa tutasaidiana alitetemeka

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Taja wanyama walioishi katika mji wa Songo.
2. Kwa nini ni muhimu kusafisha mazingira yetu?
3. Ni nani aliyepangusa meza v baya?
4. Hadithi hii inatufunza nini?

Sarufi - Kinyume cha vitenzi

**Jaza mapengo ukitumia kinyume cha vitenzi. Chagua kinyume sahihi kwenye jedwali.**

| walihuzunishwa | alibomoa | aliketi | alichafua |
|---|---|---|---|

**Mfano:** Fundi alipanga matofali. – Fundi alipangua matofali.

| Kauli yakini | Kinyume |
|---|---|
| 1. Mbweha alisafisha sebule. | Mbweha ___________ sebule. |
| 2. Simba alijenga ua. | Simba _________ ua. |
| 3. Wanyama walifurahishwa. | Wanyama ___________. |
| 4. Twiga alisimama. | Twiga ___________. |

Mali ya Serikali ya Kenya 2

## Msamiati

**Tunafanya:** Ningependa tuanze kwa kutazama picha katika **ukurasa wa 1**. Mnaona nini kwenye picha?
Je, mnajua nini kuhusu wanyama?
Sasa tutazame maneno haya mapya. Neno la kwanza ni **safi.**
Je, ni nani anayejua maana ya neno hili? (*Waelekeze wanafunzi ipasavyo eleza maana ya neno hili. Ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana).*
**Ninafanya:** *Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno hilo.*
**Unafanya:** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi ya kueleza maana ya neno hili.*
Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **safi.**
Mweleze mwenzako sentensi uliyoitunga. *(Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.)*
**Tunafanya:** Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo: **mazingira, chafu**.
**Unafanya:** Sasa fungueni **ukurasa wa 2** vitabu vyenu. Tafuta msamiati tuliojifunza. Nataka tusome msamiati huo pamoja.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**Tunafanya:** *Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi.*
Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu **wanyama wapenda kazi**?
**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo utajifunza kwenye hadithi au ni nini kitakachotendeka kwenye hadithi? (*Waulize wanafunzi 2-4 kutoa majibu yao*).
**Tunafanya:** *Mwalimu na mwanafunzi wanasoma pamoja.*
**Unafanya:** *Wanafunzi wasome peke yao.*
Mwambie mwenzako iwapo utabiri wako ulitimia na kama haukutimia, ni nini kilichotendeka. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.

## Ufahamu: Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kusoma jibu kutoka kwenye hadithi.* Swali la: 1: Taja wanyama walioishi katika mji wa Songo.
Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu.
Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu hilo sahihi.
Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo.
Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. (*Jibu swali la kwanza ukiwaonyesha wanafunzi mahali jibu hilo linapatikana).*
**unafanya:** Swali la 2: Ni kwa nini ni muhimu kusafisha mazingira yetu?
Je, kuna jibu katika hadithi? Soma sentensi iliyo na jibu au fikiria jibu sahihi iwapo halipo kwenye hadithi. Soma jibu lako kikamilifu.
**Unafanya:** *Mwanafunzi anajibu swali la tatu peke yake. Mwalimu anapeana mwelekeo unaofaa kwa wanafunzi wanapojibu maswali.*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 1 na 2 | **Marejeleo 1**

Matini

**Wanyama Wapenda Kazi**

Katika mji wa Songo paliishi simba, sungura, fisi, mbweha, kifaru na twiga. Simba aliwaita mkutanoni. Akasema, "Tutasafisha mazingira yetu. Kila mnyama atakuwa na sehemu yake ya kusafisha." Sungura kwa ujanja wake akasema, "Naumwa na jino. Siwezi kufanya kazi." Simba alinguruma kama radi na kusema, "Kila mnyama atafanya kazi!"



Mbweha alimwambia sungura, "Sungura, njoo twende ndani tupanguse matone ya mchuzi na chai iliyomwagika mezani. Tutasaidiana." Sungura alikubali shingo upande, akapangusa meza vibaya. Simba alipokuja mezani, akauliza kwa ukali, "Ni nani aliyepangusa meza hii vibaya?" Sungura alitetemeka aliposikia mngurumo wa simba. Aliipangusa meza iliyokuwa chafu ikawa safi. Mbweha naye akapanga viti alivyopangua sungura. Twiga alitumia mdomo wake kukata matawi. Simba aliziba ua huku akisema, "Lazima tuzibe nyua. Zinatulinda kutokana na maadui." Fisi naye aliokota takataka na kuzitupa kwenye shimo maalum. Wanyama hawa walifurahishwa na usafi wa mazingira yao.

1 Hakiuzwi

Kipindi cha 1 na 2 | **Marejeleo 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

safi mazingira chafu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

tutasafisha alipangusa tutasaidiana alitetemeka

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Taja wanyama walioishi katika mji wa Songo.
2. Kwa nini ni muhimu kusafisha mazingira yetu?
3. Ni nani aliyepangusa meza vibaya?
4. Hadithi hii inatufunza nini?

Sarufi – Kinyume cha vitenzi

**Jaza mapengo ukitumia kinyume cha vitenzi. Chagua kinyume sahihi kwenye jedwali.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| walihuzunishwa | alibomoa | al keti | alichafua |

**Mfano:** Fundi alipanga matofali. – Fundi alipangua matofali.

| Kauli yakini | Kinyume |
|---|---|
| 1. Mbweha alisafisha sebule. | Mbweha ____________ sebule. |
| 2. Simba alijenga ua. | Simba _________ ua. |
| 3. Wanyama walifurahishwa. | Wanyama ___________. |
| 4. Twiga alisimama. | Twiga ___________. |

Mali ya Serikali ya Kenya 2

**Unafanya:** Jibu maswali yaliyosalia.

3. Ni nani alipangusa meza vibaya?
4. Hadithi hii inatufunza nini kuhusu mazingira yetu?

**Majibu**

1. Wanyama walioishi mji wa Songo ni simba, sungura, mbweha, fisi na twiga.
2. Kubali jibu sahihi k.m. Ni muhimu kusafisha mazingira ili tusipate magonjwa.
3. Sungura alipangusa meza vibaya.
4. Kubali jibu sahihi k.m. Inatufunza kufanya kazi pamoja.

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

*Andika maneno haya ubaoni* **Kinyume cha vitenzi**

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu kinyume cha vitenzi.

Kinyume cha vitenzi ni neno au maneno yanayopinga mambo yalivyokuwa au yatakavyokuwa.

Mifano ya maneno haya ni: **safi-chafu**.

*Waulize wanafunzi kusoma mifano ya sentensi katika hadithi.*

**Tunafanya:** Alipangusa meza tena ikawa safi. Kinyume cha neno safi ni chafu.

**Tunafanya:** Hebu tusome sentesi kutoka katika hadithi. Alipangusa meza iliyokuwa chafu. Ikawa safi.

Sasa tutafute sentensi ya pili kutoka katika hadithi. Sentensi ni: Mbweha naye akapanga viti alivyopagwa sungura.

Hebu tuandika sentensi pamoja. Alipangusa meza iliyokuwa chafu ikawa safi. (*Waongoze wanafunzi katika kuandika sentensi.*).

**Unafanya:** Mwandikie rafiki yako sentensi iliyo na neno safi. *Waulize wanafunzi wachache waseme sentensi zao. Wape wanafunzi mwongozo ipasavyo.*

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Hadithi tuliyoisoma leo inatufunza nini?

**Jibu**

Hadithi hii inatufunza:

- Kufanya kazi pamoja
- Kuhifadhi mazingira

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Kipindi cha 1 na 2 **Marejeleo 1**

Matini

**Wanyama Wapenda Kazi**

Katika mji wa Songo paliishi simba, sungura, fisi, mbweha, kifaru na twiga. Simba aliwaita mkutanoni. Akasema, "Tutasafisha mazingira yetu. Kila mnyama atakuwa na sehemu yake ya kusafisha." Sungura kwa ujanja wake akasema, "Naumwa na jino. Siwezi kufanya kazi." Simba alinguruma kama radi na kusema, "Kila mnyama atafanya kazi!"



Mbweha alimwambia sungura, "Sungura, njoo twende ndani tupanguse matone ya mchuzi na chai iliyomwagika mezani. Tutasaidiana." Sungura alikubali shingo upande, akapangusa meza vibaya. Simba alipokuja mezani, akauliza kwa ukali, "Ni nani aliyepangusa meza hii vibaya?" Sungura alitetemeka aliposikia mngurumo wa simba. Aliipangusa meza iliyokuwa chafu ikawa safi. Mbweha naye akapanga viti alivyopangua sungura. Twiga alitumia mdomo wake kukata matawi. Simba aliziba ua huku akisema, "Lazima tuzibe nyua. Zinatulinda kutokana na maadui." Fisi naye aliokota takataka na kuzitupa kwenye shimo maalum. Wanyama hawa walifurahishwa na usafi wa mazingira yao.

1 Hakiuzwi

Kipindi cha 1 na 2 **Marejeleo 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

safi mazingira chafu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

tutasafisha alipangusa tutasaidiana alitetemeka

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Taja wanyama walioishi katika mji wa Songo.
2. Kwa nini ni muhimu kusafisha mazingira yetu?
3. Ni nani aliyepangusa meza v baya?
4. Hadithi hii inatufunza nini?

Sarufi – Kinyume cha vitenzi

**Jaza mapengo ukitumia kinyume cha vitenzi. Chagua kinyume sahihi kwenye jedwali.**

walihuzunishwa alibomoa aliketi alichafua

**Mfano:** Fundi alipanga matofali. – Fundi alipangua matofali.

| Kauli yakini | Kinyume |
|---|---|
| **1.** Mbweha alisafisha sebule. | Mbweha ____________ sebule. |
| **2.** Simba alijenga ua. | Simba _________ ua. |
| **3.** Wanyama walifurahishwa. | Wanyama ___________. |
| **4.** Twiga alisimama. | Twiga ____________. |

Mali ya Serikali ya Kenya 2

## Kusoma Maneno

**Ninafanya:** *(Andika maneno haya ubaoni).* **tutasafisha, alipangusa, tulitetemeka, iliyomwagika, zinatulinda**Hebu tujifunze kusoma maneno yetu. Ni nini unaweza kutambua kuhusu maneno haya? Je, maneno haya yanafanana kwa njia yoyote? (*Tarajia majibu kutoka kwa wanafunzi*).
Haya ni maneno marefu. Nisikilizeni huku nikisoma neno la kwanza. Neno la kwanza ni: **tutasafisha**. (*Pitisha kidole chini ya neno huku ukilisoma).*
**Tunafanya:** Hebu sasa tusome pamoja. (*Pitisha kidole chini ya neno huku ukilisoma na wanafunzi. Wape wanafunzi mwelekeo panapobidi).*
**Unafanya:** Sasa soma neno hili peke yako.
**tutasafisha.**
**Ninafanya:** (*Waonyeshe neno la pili kwa kidole).* Neno hili ni **alipangusa**. Hili ni neno refu pia. *(Soma neno huku ukionyesha kwa kidole sauti/silabi/husika).*
**Tunafanya:** Sasa tusome neno hili pamoja. (P*itisha kidole chini ya neno kuonyesha sauti/silabi husika huku ukisoma. Wape wanafunzi mwelekeo na uwakosoe panapobidi).*
**Unafanya:** Sasa, soma neno peke yako. (*Pitisha kidole chini ya neno huku wakisoma. Walekeze wanafunzi panapohitajika).*
**alipangusa.**
*Rudia huku wanafunzi wakiyasoma maneno yaliyobakia wao wenyewe kwa sauti. Wanafunzi wasome maneno ipasavyo katika makundi ya 2 au 3.*
**Unafanya:** Fungua vitabu vyenu **ukurasa wa 2** kisha msome maneno hayo.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**Tunafanya:** Nani atatukumbusha tulichosoma wakati uliopita? **Unafanya:** Sasa tusome hadithi tena. Mgeukie mwenzako msome naye. Nyote mtasoma kwa zamu mmoja baada ya mwingine. Wakati mwenzako anaposoma, wewe utifuatilia hadithi na kumsaidia kusoma au kutamka maneno yanayomtatiza.

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

**Tunafanya:** Jana tulizungumza kuhusu **Kinyume cha vitenzi**. Ni nani anakumbuka **Kinyume cha vitenzi** ni nini? (*Kubali majibu sahihi).*
**Unafanya:** Tutazame jedwali la kinyume cha vitenzi kutoka katika vitabu vyenu. Tutatumia kinyume cha vitenzi kujaza mapengo katika jedwali letu. Sehemu ya kwanza ya kauli yakini ina sentensi zenye vitenzi tutakazo kanusha.
**Ninafanya:** Sentensi ya kwanza ni. Mbweha alisafisha sebule. Tunaweza kujaza pengo kwa kutumia neno **alichafua**. Neno chafu ni kinyume cha kitenzi safi. Tusome sentensi yetu ya pili. Hebu tujaze pengo katika sentensi ya pili. Vizuri. Jibu linafaa kuwa **alibomoa**.
**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jazeni mapengo kwenye sentensi zilizosalia kwenye jedwali.

**Majibu**

1. alichafua
2. alibomoa
3. walikasirishwa/walihuzunishwa
4. aliketi

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 1 na 2 **Marejeleo 1**

Matini

**Wanyama Wapenda Kazi**

Katika mji wa Songo paliishi simba, sungura, fisi, mbweha, kifaru na twiga. Simba aliwaita mkutanoni. Akasema, "Tutasafisha mazingira yetu. Kila mnyama atakuwa na sehemu yake ya kusafisha." Sungura kwa ujanja wake akasema, "Naumwa na jino. Siwezi kufanya kazi." Simba alinguruma kama radi na kusema, "Kila mnyama atafanya kazi!"



Mbweha alimwambia sungura, "Sungura, njoo twende ndani tupanguse matone ya mchuzi na chai iliyomwagika mezani. Tutasaidiana." Sungura alikubali shingo upande, akapangusa meza vibaya. Simba alipokuja mezani, akauliza kwa ukali, "Ni nani aliyepangusa meza hii vibaya?" Sungura alitetemeka aliposikia mngurumo wa simba. Aliipangusa meza iliyokuwa chafu ikawa safi. Mbweha naye akapanga viti alivyopangua sungura. Twiga alitumia mdomo wake kukata matawi. Simba aliziba ua huku akisema, "Lazima tuzibe nyua. Zinatulinda kutokana na maadui." Fisi naye aliokota takataka na kuzitupa kwenye shimo maalum. Wanyama hawa walifurahishwa na usafi wa mazingira yao.

1 Hakiluzwi

Kipindi cha 1 na 2 **Marejeleo 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

safi mazingira chafu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

tutasafisha alipangusa tutasaidiana alitetemeka

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Taja wanyama walioishi katika mji wa Songo.
2. Kwa nini ni muhimu kusafisha mazingira yetu?
3. Ni nani aliyepangusa meza vibaya?
4. Hadithi hii inatufunza nini?

Sarufi – Kinyume cha vitenzi

**Jaza mapengo ukitumia kinyume cha vitenzi. Chagua kinyume sahihi kwenye jedwali.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| walihuzunishwa | alibomoa | al keti | alichafua |

**Mfano:** Fundi alipanga matofali. – Fundi alipangua matofali.

| Kauli yakini | Kinyume |
|---|---|
| 1. Mbweha alisafisha sebule. | Mbweha ____________ sebule. |
| 2. Simba alijenga ua. | Simba _________ ua. |
| 3. Wanyama walifurahishwa. | Wanyama ___________. |
| 4. Twiga alisimama. | Twiga ___________. |

Mali ya Serikali ya Kenya 2

## Kuandika

**Masimulizi - Kupanga**

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuandika hadithi. Tuko na hatua 5 za kuandika hadithi. Tutajifunza na kuandika kwa kutumia hatua ya kwanza wiki hii. Hatua ya kwanza ni kupanga jinsi ya kuandika hadithi.

Kupanga yale ambayo unataka kuandika ni muhimu katika uandishi. Kwanza unafikiria kuhusu hadithi ambayo unataka kuandika. Fikiria kuhusu mambo muhimu ya hadithi. Tazama huku nikiwaongoza jinsi ya kupanga kuandika hadithi. (*Andika hatua hizi ubaoni na uwaeleze wanafunzi hatua hizi kwa kutumia sentensi.)*

Mambo muhimu katika hadithi huwa ni:

**Muktadha** – Lini na wapi hadithi inafanyika: Mahali na wakati.

**Wahusika** – Watu au wanyama kwenye hadithi.

**Utangulizi** – Jinsi hadithi inaanza – Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi?

**Changamoto** – Jambo ambalo linawasumbua wahusika. Tatizo au shida kwenye hadithi.

**Suluhisho** – Jinsi na namna tatizo linavyosuluhishwa.

**Ninafanya:** Nataka kupanga jinsi ya kuandika hadithi. Kwanza nitafikiria kuhusu muktadha. Je, nataka hadithi yangu ifanyike wapi? Je, wahusika wakuu kwa hadithi yangu watakuwa akina nani? Je, kila mhusika atakuwa anafanya nini? Wahusika watakuwa na tabia gani? Ni nini kitakachofanyika mwanzoni, katikati na mwishoni mwa hadithi? Je, changamoto ya hadithi itakuwa nini na wahusika watasuluhisha hili tatizo vipi kwenye hadithi? Wakati ujao utajaribu kufikiria na kuandika wewe mwenyewe. Sasa fikiria kuhusu hadithi ambayo ungependa kuandika.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Nakili maneno haya mara mbili kisha uyasome:
**tutasafisha, alipangusa, tutasaidiana, tutatetemeka**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 3 na 4 **Marejeleo 1**

**Matini**

**Siku ya Mazingira**



Mnamo sikukuu ya mazingira, shule zilialikwa zisherehekee siku hiyo. Sherehe ilifanyika shuleni mwetu. Siku moja kabla ya sherehe, tulifanya matayarisho. Tulitundika hema na kuokota takataka na kuweka kwenye pipa maalum lililotengewa taka. Nyasi zilifyekwa kwa kifyekeo na kutupwa shimoni. Viti vilipangwa siku hiyo jioni. Siku ya sherehe ilipofika, watu wengi walihudhuria. Wachuuzi barabarani waliuza ndizi, maembe, barafu na miwa. Waliohudhuria walivinunua vitu hivi kabla ya sherehe, wakavila na kutupa takataka na maganda kiwanjani. Shule ikawa chafu.

Mwalimu Mkuu aliwapeleka wageni kwenye hema ili waketi. Sherehe ilianza kwa Wimbo wa Taifa. Wakati wa hotuba Bi. Makame Waziri wa Mazingira alisema, "Ni lazima tuyatunze mazingira yetu. Wanafunzi, hebu tazama kiwanja hiki. Niliwaona mkinunua vitu na kutupa takataka ovyoovyo. Sasa uchafu umeenea kote. Mnapotafuna miwa au kula ndizi, tupa ganda au maganda kwenye pipa au jaa. Tusipoyatunza mazingira tutaangamia. Ninatumaini kuwa nikirudi, jambo hili halitatokea tena." Bi. Makame alipomaliza hotuba, wanafunzi pamoja na baadhi ya wazazi walikusanya takataka na kuzitupa kwenye pipa.

3 Hakiuzwi

Kipindi cha 3 na 4 **Marejeleo 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

takataka shimoni maganda

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

zisherehekee aliwapeleka walivinunua walihudhuria

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya baada ya kusoma hadithi.**

1. Shule zilialikwa zifanye nini kwenye siku ya mazingira?
2. Tunaweza kuyatunza mazingira ya shule yetu vipi?
3. Waliohudhuria walifanya nini kabla ya sherehe?
4. Unafikiria ni kwa nini takataka zinafaa kutupwa kwenye pipa?

**Sarufi: Umoja – Wingi**

**Andika wingi wa sentensi hizi.**

**Mfano:** Ganda hili ni la ndizi. - Maganda haya ni ya ndizi.

1. Pipa hili lina takataka. ____________________.
2. Mgeni aliwasili mapema. ____________________.
3. Mwanafunzi aliokota takataka. ____________________.
4. Mlezi alimpa zawadi. ____________________.

Mali ya Serikali ya Kenya 4

## Msamiati

**Tunafanya:** Ningependa tuanze kwa kutazama picha katika **ukurasa wa 3**. Mnaona nini kwenye picha?
Je, mnajua nini kuhusu mazingira?
Sasa tutazame maneno haya mapya. Neno la kwanza ni **takataka.**
Je, ni nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana.*
**Ninafanya:** *Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno hilo.*
**Unafanya:** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.*
Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **takataka.** Mweleze mwenzako sentensi uliyoitunga. *(Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.)*
**Tunafanya:** *Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo*: **shimoni, maganda.**
**Unafanya:** Sasa fungueni **ukurasa wa 4** vitabu vyenu. Tafuta msamiati tuliojifunza. Nataka tusome msamiati huo pamoja.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**Tunafanya:** *Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi.* Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu siku ya mazingira?
**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo utajifunza kwenye hadithi au ni nini kitakachotendeka kwenye hadithi. (*Waulize wanafunzi 2-4 kutoa majibu yao*).
**Tunafanya:** *Mwalimu na mwanafunzi wanasoma pamoja.*
**Unafanya:** *Wanafunzi wanasoma peke yao.*
Mwambie mwenzako iwapo utabiri wake ulitimia na kama haukutimia, ni nini kilichotendeka. Inua mkono iwapo utabiri wako ulitimia. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuielewe hadithi hii zaidi.

## ? Ufahamu: Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka kwenye hadithi*. Swali la: 1. Shule zilialikwa zifanye nini siku ya mazingira?
Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu.
Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo.
Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. (*Jibu swali la kwanza huku ukiwaonyesha wanafunzi mahali jibu hilo linapatikana.*)
**Tunafanya:** Swali la 2. Tunawezaje kuyatunza mazingira ya shule yetu? Je, kuna jibu kwenye hadithi?
Soma sentensi iliyo na jibu au fikiria jibu la sentensi iwapo halipo kwenye hadithi.
Soma jibu lako kikamilifu.
**Unafanya:** *Mwanafunzi anajibu swali. Mwalimu anapeana mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswalis.*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 3 na 4 **Marejeleo 1**

**Matini**

**Siku ya Mazingira**



Mnamo sikukuu ya mazingira, shule zilialikwa zisherehekee siku hiyo. Sherehe ilifanyika shuleni mwetu. Siku moja kabla ya sherehe, tulifanya matayarisho. Tulitundika hema na kuokota takataka na kuweka kwenye pipa maalum lililotengewa taka. Nyasi zil fyekwa kwa kifyekeo na kutupwa shimoni. Viti vilipangwa siku hiyo jioni. Siku ya sherehe ilipofika, watu wengi walihudhuria. Wachuuzi barabarani waliuza ndizi, maembe, barafu na miwa. Waliohudhuria walivinunua vitu hivi kabla ya sherehe, wakavila na kutupa takataka na maganda kiwanjani. Shule ikawa chafu.

Mwalimu Mkuu aliwapeleka wageni kwenye hema ili waketi. Sherehe ilianza kwa Wimbo wa Taifa. Wakati wa hotuba Bi. Makame Waziri wa Mazingira alisema, "Ni lazima tuyatunze mazingira yetu. Wanafunzi, hebu tazama kiwanja hiki. Niliwaona mkinunua vitu na kutupa takataka ovyoovyo. Sasa uchafu umeenea kote. Mnapotafuna miwa au kula ndizi, tupa ganda au maganda kwenye pipa au jaa. Tusipoyatunza mazingira tutaangamia. Ninatumaini kuwa nikirudi, jambo hili halitatokea tena." Bi. Makame alipomaliza hotuba, wanafunzi pamoja na baadhi ya wazazi walikusanya takataka na kuzitupa kwenye pipa.

 Hakiluzwi

Kipindi cha 3 na 4 **Marejeleo 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

takataka shimoni maganda

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

zisherehekee aliwapeleka walivinunua walihudhuria

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya baada ya kusoma hadithi.**

1. Shule zilialikwa zifanye nini kwenye siku ya mazingira?
2. Tunaweza kuyatunza mazingira ya shule yetu vipi?
3. Waliohudhuria walifanya nini kabla ya sherehe?
4. Unafikiria ni kwa nini takataka zinafaa kutupwa kwenye pipa?

**Sarufi: Umoja – Wingi**

**Andika wingi wa sentensi hizi.**

**Mfano:** Ganda hili ni la ndizi. - Maganda haya ni ya ndizi.

1. Pipa hili lina takataka. ______________________.
2. Mgeni aliwasili mapema. ______________________.
3. Mwanafunzi aliokota takataka. ______________________.
4. Mlezi alimpa zawadi. ______________________.

Mali ya Serikali ya Kenya 

**Unafanya:** Rudia maswali yaliyosalia.

3. Waliohudhuria walifanya nini kabla ya sherehe?
4. Unafikiri ni kwa nini takataka inafaa kutupwa kwenye pipa?

**Majibu**

1. Zisherehekee
2. Kubali jibu lolote sahihi kwa mfano; kuzoa takataka na kuzichoma.
3. Walivinunua vitu kutoka kwa wachuuzi.
4. Kubali jibu sahihi kwa mfano ili ichomwe kwa pamoja.

### Sarufi: Umoja-Wingi

**Tunafanya:** Ni nani anakumbuka mpangilio wa sarufi yetu wiki hii? Tazama sentensi zilizo kwenye ukurasa wa 4. Kwa mfano: Ganda hili ni la ndizi. Wingi wa sentensi hii ni: Maganda haya ni ya ndizi.
Hebu tusome sentensi hizi pamoja zikiwa katika hali ya umoja na wingi. (*Waulize wanafunzi waseme sentensi hizi katika hali ya wingi).*
**Unafanya:** Ni zamu yenu. Sasa kamilisheni sentensi zilizosalia kwenye madaftari yenu. Andika wingi wa sentensi hizi.

**Majibu**

1. Mapipa haya yana takataka.
2. Wageni waliwasili mapema.
3. Wanafunzi waliokota takataka.
4. Walezi waliwapa zawadi.

### Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika kinyume cha maneno haya.

1. safi (chafu)
2. furahi (kasirika/huzunika nuna)
3. refu (fupi)
4. jenga (bomoa)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 3 na 4 **Marejeleo 1**

Matini

**Siku ya Mazingira**



Mnamo sikukuu ya mazingira, shule zilialikwa zisherehekee siku hiyo. Sherehe ilifanyika shuleni mwetu. Siku moja kabla ya sherehe, tulifanya matayarisho. Tulitundika hema na kuokota takataka na kuweka kwenye pipa maalum lililotengewa taka. Nyasi zilifyekwa kwa kifyekeo na kutupwa shimoni. Viti vilipangwa siku hiyo jioni. Siku ya sherehe ilipofika, watu wengi walihudhuria. Wachuuzi barabarani waliuza ndizi, maembe, barafu na miwa. Waliohudhuria walivinunua vitu hivi kabla ya sherehe, wakavila na kutupa takataka na maganda kiwanjani. Shule ikawa chafu.

Mwalimu Mkuu aliwapeleka wageni kwenye hema ili waketi. Sherehe ilianza kwa Wimbo wa Taifa. Wakati wa hotuba Bi. Makame Waziri wa Mazingira alisema, "Ni lazima tuyatunze mazingira yetu. Wanafunzi, hebu tazama kiwanja hiki. Niliwaona mkinunua vitu na kutupa takataka ovyoovyo. Sasa uchafu umeenea kote. Mnapotafuna miwa au kula ndizi, tupa ganda au maganda kwenye pipa au jaa. Tusipoyatunza mazingira tutaangamia. Ninatumaini kuwa nikirudi, jambo hili halitatokea tena." Bi. Makame alipomaliza hotuba, wanafunzi pamoja na baadhi ya wazazi walikusanya takataka na kuzitupa kwenye pipa.

3 Hakiuzwi

Kipindi cha 3 na 4 **Marejeleo 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

takataka shimoni maganda

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

zisherehekee aliwapeleka walivinunua walihudhuria

Ufahamu

**Jibu maswali haya baada ya kusoma hadithi.**

1. Shule zilialikwa zifanye nini kwenye siku ya mazingira?
2. Tunaweza kuyatunza mazingira ya shule yetu vipi?
3. Waliohudhuria walifanya nini kabla ya sherehe?
4. Unafikiria ni kwa nini takataka zinafaa kutupwa kwenye pipa?

Sarufi: Umoja – Wingi

**Andika wingi wa sentensi hizi.**

**Mfano:** Ganda hili ni la ndizi. - Maganda haya ni ya ndizi.

1. Pipa hili lina takataka. ________________.
2. Mgeni aliwasili mapema. ________________.
3. Mwanafunzi aliokota takataka. ________________.
4. Mlezi alimpa zawadi. ________________.

Mali ya Serikali ya Kenya 4

## Kusoma Maneno

**Ninafanya:** *Andika maneno haya ubaoni*. **walivinunua, zitengeneze, zisherehekee, aliwapeleka, walihudhuria, tusipoyatunzaTunafanya:** Hebu tujifunze kusoma maneno yetu mapya.Je, maneno haya yanafanana kwa njia yoyote? *(Tarajia majibu kutoka kwa wanafunzi).*

**Ninafanya:** Haya ni maneno marefu. Nisikilizeni huku nikisoma neno la kwanza. Neno la kwanza ni: **walivinunua.** (*Pitisha kidole chini ya neno huku ukilisoma).*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome pamoja. (*Pitisha kidole*

**Unafanya:** Sasa soma neno hili peke yako.

**walivinunua.**

*Waonyeshe neno la pili kwa kidole*. Neno hili ni **zitengeneze.** Hili ni neno refu pia. *(Soma neno huku ukionyesha kwa kidole sauti/silabi husika).*

**Tunafanya:** Sasa tusome neno hili pamoja. (P*itisha kidole chini ya neno kuonyesha sauti/silabi husika huku ukisoma. Wape wanafunzi mwelekeo na uwakosoe ipasavyo).*

**Unafanya:** Sasa, soma neno peke yako. (*Pitisha kidole chini ya neno huku wakisoma. Wape wanafunzi mwelekeo unaofaa panapohitajika).*

**zitengeneze.**

**Ninafanya:** *(Rudia huku wanafunzi wakisoma maneno yaliyobakia. Wanafunzi wasome maneno ipasavyo kwa vikundi vya 2-3).*

**Unafanya:** Fungua **ukurasa wa 4** vitabu vyenu kisha msome maneno hayo.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**Tunafanya:** Nani atatukumbusha tulichosoma wakati uliopita?

**Unafanya:** Sasa tusome hadithi tena. Chagua mwenzako mtakayesoma naye. Nyote mtasoma kwa zamu mmoja baada ya mwingine. Wakati mwenzako anaposoma, wewe utafuatilia hadithi na kumsaidia kusoma au kutamka maneno yanayomtatiza.

## Kuandika

### Masimulizi - Kupanga

**Tunafanya:** Juzi tulijifunza jinsi ya kuandika hadithi. Je, hatua ya kwanza ilihusu nini?

**Unafanya:** Kupanga jinsi ya kuandika.

**Ninafanya:** Vizuri. Kupanga yale utakayoandika ni muhimu. Sasa tujikumbushe hatua za kuandika. Je, ni nani anakumbuka hatua hizi? *Andika hatua zifuatazo ubaoni na uwaelezee wanafunzi.*

**Muktadha** – Lini na wapi hadithi inafanyika

**Wahusika** – Watu au wanyama kwenye hadithi.

**Utangulizi** – Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi?

**Changamoto** – Tatizo au shida kwenye hadithi.

**Suluhisho** – Jinsi na namna tatizo linavyosuluhishwa.


**Unafanya:** Sasa fungueni madaftari yenu. Ninataka

Tarehe: ____________ Muda: __________ Idadi: __________

Kipindi cha 3 na 4 **Marejeleo 1**

Matini

**Siku ya Mazingira**



Mnamo sikukuu ya mazingira, shule zilialikwa zisherehekee siku hiyo. Sherehe ilifanyika shuleni mwetu. Siku moja kabla ya sherehe, tulifanya matayarisho. Tulitundika hema na kuokota takataka na kuweka kwenye pipa maalum lililotengewa taka. Nyasi zilifyekwa kwa kifyekeo na kutupwa shimoni. Viti vilipangwa siku hiyo jioni. Siku ya sherehe ilipofika, watu wengi walihudhuria. Wachuuzi barabarani waliuza ndizi, maembe, barafu na miwa. Waliohudhuria walivinunua vitu hivi kabla ya sherehe, wakavila na kutupa takataka na maganda kiwanjani. Shule ikawa chafu.

Mwalimu Mkuu aliwapeleka wageni kwenye hema ili waketi. Sherehe ilianza kwa Wimbo wa Taifa. Wakati wa hotuba Bi. Makame Waziri wa Mazingira alisema, "Ni lazima tuyatunze mazingira yetu. Wanafunzi, hebu tazama kiwanja hiki. Niliwaona mkinunua vitu na kutupa takataka ovyoovyo. Sasa uchafu umeenea kote. Mnapotafuna miwa au kula ndizi, tupa ganda au maganda kwenye pipa au jaa. Tusipoyatunza mazingira tutaangamia. Ninatumaini kuwa nikirudi, jambo hili halitatokea tena." Bi. Makame alipomaliza hotuba, wanafunzi pamoja na baadhi ya wazazi walikusanya takataka na kuzitupa kwenye pipa.

3 Hakizwi

Kipindi cha 3 na 4 **Marejeleo 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

takataka shimoni maganda

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

zisherehekee aliwapeleka walivinunua walihudhuria

Ufahamu

**Jibu maswali haya baada ya kusoma hadithi.**

1. Shule zilialikwa zifanye nini kwenye siku ya mazingira?
2. Tunaweza kuyatunza mazingira ya shule yetu vipi?
3. Waliohudhuria walifanya nini kabla ya sherehe?
4. Unafikiria ni kwa nini takataka zinafaa kutupwa kwenye pipa?

Sarufi: Umoja – Wingi

**Andika wingi wa sentensi hizi.**

**Mfano:** Ganda hili ni la ndizi. - Maganda haya ni ya ndizi.

1. Pipa hili lina takataka. ______________________.
2. Mgeni aliwasili mapema. ______________________.
3. Mwanafunzi aliokota takataka. ______________________.
4. Mlezi alimpa zawadi. ______________________.

Mali ya Serikali ya Kenya 4

usaidiane na mwenzako kufikiria juu ya hadithi ambayo ungependa kusimulia. Pangeni hadithi kwa kutumia hatua tulizozisoma. Je, ungependa hadithi yako isimuliwe wapi? Ni nani atakuwa mhusika mkuu? Wahusika wako ni wa aina gani? Je, wahusika wako wanafananaje?
Ni kitu gani kitafanyika mwanzoni mwa hadithi?
Changamoto kwenye hadithi itakuwa ni nini?
Wahusika hawa watatatua changamoto kwa njia gani?

### Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia maneno haya:

1. mazingira
2. chafu
3. takataka
4. maganda

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 5 **Marejeleo 1**

**Msamiati**

Tumia maneno yaliyo kwenye jedwali kujaza mapengo.

| | | | |
|---|---|---|---|
| takataka | uchafu | yote | maganda |

1. Shimoni ni mahali pa kutupa ___________.
2. Takataka ni ___________.
3. ___________ ya matunda hutupwa kwenye pipa.
4. Mazingira ni yale ___________ yanayotuzunguka.

**Sarufi: Umoja – Wingi**

Jaza mapengo kwa neno linalofaa katika umoja au wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Ganda lilitupwa. | ___________ yalitupwa. |
| 2. ________ alinunua kalamu. | Wanafunzi walinunua kalamu. |
| 3. Mgeni aliketi. | ___________ waliketi. |
| 4. Mwanafunzi aliokota pesa. | Wanafunzi ___________ pesa. |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.

Soko la Sokomoko



5 Hakiuzwi

**Soko la Sokomoko**

Soko la Sokomoko lilikuwa kijijini Mbea. Lilijulikana kwa shughuli nyingi za kibiashara na usafi. Taka iliyomwagika ilifagiliwa na kutupwa shimoni.
Siku baada ya siku watu waliongezeka sokoni. Wanabiashara walianza kuyatupa maganda ya ndizi nje ya pipa badala ya ndani. Takataka ilitapakaa barabarani. Idadi ndogo ya wasafishaji ilizidiwa na idadi kubwa ya wanabiashara. Mmoja wa wasafishaji akasikika akisema, "Wanabiashara wa hapa wamenisinya. Wamekataa kufuata sheria za soko za kudumisha usafi."

Mazingira ya soko hili yaliharibika kabisa. Soko lilianza kutoa harufu mbaya ya uvundo. Idadi ya wanabiashara ikaanza kupunguka. Wanakijiji wakajawa na wasiwasi. Soko walilolitegemea lilikuwa karibu kufungwa. Mzee Safi, aliyekuwa na sifa za kuwashawishi watu, aliamua kuita mkutano wa wanakijiji. Wanakijiji wengi walihudhuria mkutano huo. Mzee Safi alianza kwa kusema, "Shughuli za soko hili zinatulinda sisi wanakijiji. Soko likifungwa tutakosa mahali pa kuuzia mazao yetu. Maisha yetu yataharibika. Naomba sote tulisafishe soko hili." Watu wote walikubaliana naye.

Shughuli zote za biashara zilisimamishwa kwa siku mbili. Watu wote wakubwa kwa wadogo wakajitolea kusafisha soko. Kila familia iliwakilishwa katika shughuli hii. Askari wa soko aliwashika mbwakoko akawapeleka kwa Shirika la Watunza Wanyama wa Nyumbani. Soko likawa safi. Biashara ikanawiri tena. Wanabiashara wakajawa na furaha kuona kuwa soko limeng'aa tena. Siku ya usafi sokoni ikatengwa ili famillia zisherehekee siku hii kwa kulisafisha.

## Msamiati

**Unafanya:** Fungua **ukurasa wa 5** wa vitabu vyenu.

Tumia maneno yaliyo kwenye jedwali kujaza mapengo:
**Majibu**

1. takataka
2. uchafu
3. maganda
4. yote

## Kusoma Maneno

**Unafanya:** Leo tunaenda kupitia maneno yale tuliyojifunza wiki hii. Kwanza nitatamka neno kisha mtaliandika katika madaftari yenu. Mko tayari? Nitalisoma neno mara mbili huku mkiliandika. *(Sema au tamka neno mara mbili huku wanafunzi wakiliandika.)*
Neno la kwanza ni **tutasaidiana.**
*Rudia hatua hii ukitumia maneno yafuatayo.*
**tutatetemeka, zitengeneze, walihudhuria, tusipoyatunza, walivinunua, aliwapeleka**

## Hadithi ya Mwalimu

### Kabla ya Kusoma

Leo mtasikiliza kwa makini nikiwasomea hadithi kisha baadaye tuzungumze kuhusu hadithi hiyo tukiandika. Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi huku tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma hadithi kuna baadhi ya maneno mapya ambayo tutazungumzia kwanza. Neno la kwanza ni **ilizidiwa.** Neno hili humaanisha kupita kiwango fulani.
(*Rudia hatua hii na maneno;* **mazingira, kuwashawishi**)

### Kusoma Hadithi

Sasa sikiliza kwa makini ninaposoma. Sikiliza na utambue maneno mapya. Inua mkono wako wa kushoto utakaposikia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia ukisikia neno la pili.
*(Soma hadithi kwa ufasaha huku ukibadilisha sauti. Sitisha unapofikia tukio la kufurahisha. Uliza mwanafunzi ni kitu gani ambacho kinaweza kutokea.)*

### Baada ya kusoma

Uliza maswali yafuatayo:

1. Ni nani wahusika katika hadithi. (wanabiashara, wasafishaji, wanakijiji, Mzee Safi na askari wa soko.)
2. Je, afikiri ni kwa nini wakazi wa soko la Sokomoko walipuuza usafi wa mazingira? (Kubali jibu lolote sahihi.)

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 5 **Marejeleo 1**

**Msamiati**

**Tumia maneno yaliyo kwenye jedwali kujaza mapengo.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| takataka | uchafu | yote | maganda |

1. Shimoni ni mahali pa kutupa __________.
2. Takataka ni __________.
3. __________ ya matunda hutupwa kwenye pipa.
4. Mazingira ni yale __________ yanayotuzunguka.

**Sarufi: Umoja – Wingi**

**Jaza mapengo kwa neno linalofaa katika umoja au wingi.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Ganda lilitupwa. | __________ yalitupwa. |
| 2. ________ alinunua kalamu. | Wanafunzi walinunua kalamu. |
| 3. Mgeni aliketi. | __________ waliketi. |
| 4. Mwanafunzi aliokota pesa. | Wanafunzi __________ pesa. |

**Hadithi ya mwalimu**

**Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.**

Soko la Sokomoko



5 Hakiuzwi

3. Ni kwa nini wanabiashara walijawa na furaha tena? Hebu tuandike baadhi ya mambo tuliyosoma. (kwa sababu soko lilisafishwa likawa safi.)

## Sarufi

**Tunafanya:** Hebu sasa turejelee sarufi tuliyojifunza wiki hii. Je, unakumbuka sarufi tuliyojifunza?

Fungua vitabu vyenu **ukurasa wa 5**. Jaza mapengo kwenye jedwali ukitumia hali ya umoja na wingi.

**Majibu**

1. maganda
2. mwanafunzi
3. wageni
4. waliokota

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa: Umoja - Wingi

Unafikiri ni kwa nini takataka inafaa kutupwa kwenye pipa?

## Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji.

Unafanya ashiriki katika shughuli za usafi wa mazingira nyumbani.

## Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji

Kushiriki katika vikundi vya ushirika shuleni vinavyohusu usafi wa mazingira.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 6 na 7 — **Shambani 1**

**Matini**

**Kiangazi Kijijini Kinga**



Kijijini Kinga kulikuwa na kiangazi. Jua liliwaka na joto likawa jingi. Mvua haikunyesha. Mimea yote ilikauka hata kando ya mito. Kijiji kizima kikapatwa na njaa. Wanyama wengi kama mbwa wakafa. Mabwawa ya maji yakakauka. Hata hivyo, wanakijiji hawakufa moyo. Waliendelea kulima na kutayarisha mashamba yao ili wapande mbegu.

Jioni moja mawingu meusi yalionekana angani. Mzee Ukweli, mjuzi wa hali ya anga alitangaza, "Wanakijiji, leo mvua itanyesha." Wanakijiji walimuamini Mzee Ukweli kwani hakuwahi kudanganya. Yeye aliaminiwa na wanakijiji wote. Walitayarisha vyombo vya kukinga na kuh fadhi maji. Punde si punde, matone makubwa ya mvua yakaanza kuanguka. Mvua kubwa ilinyesha. Watoto walionekana wakikinga na kuhifadhi maji mbele ya nyumba zao. Mito ilijaa maji.

Mama alichukua jembe na upanga akaenda shambani. Alitumia mbolea kupanda mahindi na maharagwe. Udongo ukawa na rutuba. Mbegu zilimea na kukua haraka. Wanakijiji walivuna na kuweka vyakula ndani ya maghala. Chakula kikawa kingi. Njaa iliisha kijijini Kinga. Wanakijiji walisikikika wakisema wangeendelea kulima kwa bidii ili watoto wao wasipatwe na njaa tena.

Mali ya Serikali ya Kenya

6

Kipindi cha 6 na 7 — **Shambani 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

jembe mbolea rutuba

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

mbwa mabwawa kubwa ukweli

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni nani wanaozungumziwa kwenye hadithi hii?
3. Hadithi hii inafanyika wapi?
4. Ni nini kilichofanyika mwanzoni mwa hadithi?

**Sarufi: Nafsi ya tatu - Umoja na wingi**

**Jaza mapengo kwa maneno sahihi.**

1. __________ atafanya mtihani kesho. (Wewe, Yeye)
2. Mwanafunzi __________ ataenda shuleni kesho. (huyu, wale)
3. __________ watacheza mpira Jumatatu. (Yeye, Wao)
4. Wanakijiji __________ watapanda mbegu. (hao, hawa)

7

Hakiuzwi

## Msamiati

**Tunafanya:** Ningependa tuanze kwa kutazama picha katika **ukurasa wa 6**. Mnaona nini kwenye picha?Je, umewahi kuwa mahali kama hapa?

Sasa tutazame maneno haya mapya. Neno la kwanza ni **jembe.** Je, ni nani anayejua maana ya neno hili. (*Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana.)*

*Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno hili.*

**Unafanya:** (*Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.)*

Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno jembe. Mweleze mwenzako sentensi uliyoitunga. *(Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.)*

*Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* **mbolea, rutuba**

Sasa fungua vitabu vyenu **ukurasa wa 7.** Tafuta msamiati tuliojifunza. Ningepanda tusome msamiati huo pamoja.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**Unafanya:** *Soma kichwa cha hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Tunafanya:** Kumbuka yale tuliyoyazungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu kiangazi?


**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo utajifunza kutoka kwenye hadithi au ni nini kitakachotendeka kwenye hadithi (*Waulize wanafunzi 2-4 kutoa majibu yao).*

**Tunafanya:** (*Mwalimu na mwanafunzi wanasoma hadithi pamoja.*

**Unafanya:** *Wanafunzi wanasoma hadithi peke yao).* Mwambie mwenzako iwapo utabiri wako ulitimia na kama haukutimia, ni nini kilichotendeka. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia.

## Ufahamu: Kusimulia Hadithi

**N:** *Chora umbo la nyumba ubaoni kisha useme:* Tutatumia umbo hili la nyumba kujibu maswali yafuatayo huku tukisimulia hadithi tena.




**T:** Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 6 na 7 **Shambani 1**

**Matini**

**Kiangazi Kijijini Kinga**



Kijijini Kinga kulikuwa na kiangazi. Jua liliwaka na joto likawa jingi. Mvua haikunyesha. Mimea yote ilikauka hata kando ya mito. Kijiji kizima kikapatwa na njaa. Wanyama wengi kama mbwa wakafa. Mabwawa ya maji yakakauka. Hata hivyo, wanakijiji hawakufa moyo. Waliendelea kulima na kutayarisha mashamba yao ili wapande mbegu.

Jioni moja mawingu meusi yalionekana angani. Mzee Ukweli, mjuzi wa hali ya anga alitangaza, "Wanakijiji, leo mvua itanyesha." Wanakijiji walimuamini Mzee Ukweli kwani hakuwahi kudanganya. Yeye aliaminiwa na wanakijiji wote. Walitayarisha vyombo vya kukinga na kuh fadhi maji. Punde si punde, matone makubwa ya mvua yakaanza kuanguka. Mvua kubwa ilinyesha. Watoto walionekana wakikinga na kuhifadhi maji mbele ya nyumba zao. Mito ilijaa maji.

Mama alichukua jembe na upanga akaenda shambani. Alitumia mbolea kupanda mahindi na maharagwe. Udongo ukawa na rutuba. Mbegu zilimea na kukua haraka. Wanakijiji walivuna na kuweka vyakula ndani ya maghala. Chakula kikawa kingi. Njaa iliisha kijijini Kinga. Wanakijiji walisikikika wakisema wangeendelea kulima kwa bidii ili watoto wao wasipatwe na njaa tena.

Mali ya Serikali ya Kenya 6

Kipindi cha 6 na 7 **Shambani 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

jembe mbolea rutuba

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

mbwa mabwawa kubwa ukweli

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni nani wanaozungumziwa kwenye hadithi hii?
3. Hadithi hii inafanyika wapi?
4. Ni nini kilichofanyika mwanzoni mwa hadithi?

**Sarufi: Nafsi ya tatu - Umoja na wingi**

**Jaza mapengo kwa maneno sahihi.**

1. __________ atafanya mtihani kesho. (Wewe, Yeye)
2. Mwanafunzi __________ ataenda shuleni kesho. (huyu, wale)
3. __________ watacheza mpira Jumatatu. (Yeye, Wao)
4. Wanakijiji __________ watapanda mbegu. (hao, hawa)

7 Hakiuzwi

**N:** *Simulia darasa lote hadithi.*
**U:** Msimulie mwenzako hadithi.

### Maswali

1. Taja kichwa cha hadithi. (Kiangazi Kijijini Kinga)
2. Ni nani wanaozungumziwa kwenye hadithi hii? (Mzee ukweli)
3. Hadithi hii inafanyika wapi?
4. Ni nini kilichofanyika mwanzoni mwa hadithi?

### Sarufi: Nafsi ya Tatu

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu nafsi ya tatu katika hali ya umoja na wingi pamoja na kurejelea maneno. Tutajikumbusha nafsi ya kwanza ni **mimi.** Nafsi ya pili ni **wewe** na ya tatu ni **yeye.** Nafsi hizi kwa wingi huwa **sisi, nyinyi, wao.**

**Andika ubaoni**

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| Nafsi ya kwanza | mimi | sisi |
| Nafsi ya pili | wewe | nyinyi |
| Nafsi ya tatu | yeye | wao |

**Tunafanya:** *Waulize wanafunzi kusoma mifano ya sentensi katika hadithi.*

**Ninafanya:** Nafsi ya tatu **yeye** imetumika katika sentensi ifuatayo: *Yeye aliaminiwa na wanakijiji wote.* Hebu tusome sentensi ya pili. Hebu tuiandike sentensi hii kwa pamoja. *Yeye aliaminiwa na wanakijiji wote. (Waongoze wanafunzi katika kuandika sentensi.)*

**Unafanya:** Mwandikie rafiki yako sentensi iliyo na nafsi ya tatu katika wingi **wao.** *(Waulize wanafunzi wachache waseme sentensi zao. Wape wanafunzi mwongozo ipasavyo).*

Rudia hatua hizi ukitumia **yeye, huyo, yule, hawa, hao, wale.**

### Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tambua nafsi na nyakati katika sentensi zifuatazo. **Mfano: Wao** watalima shamba.

1. Sisi tutapalilia mahindi. (**Sisi** tutapalilia mahindi.)
2. Nyinyi mtapanda miti. (**Nyinyi** mtapanda miti)
3. Yeye ataenda shambani. (**Yeye ataenda shambani**)
4. Mwanafunzi yule atafaulu mtihani. (Mwanafunzi **yule** atafaulu mtihani)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

Kipindi cha 6 na 7 — Shambani 1

Matini

**Kiangazi Kijijini Kinga**



Kijijini Kinga kulikuwa na kiangazi. Jua liliwaka na joto likawa jingi. Mvua haikunyesha. Mimea yote ilikauka hata kando ya mito. Kijiji kizima kikapatwa na njaa. Wanyama wengi kama mbwa wakafa. Mabwawa ya maji yakakauka. Hata hivyo, wanakijiji hawakufa moyo. Waliendelea kulima na kutayarisha mashamba yao ili wapande mbegu.

Jioni moja mawingu meusi yalionekana angani. Mzee Ukweli, mjuzi wa hali ya anga alitangaza, "Wanakijiji, leo mvua itanyesha." Wanakijiji walimuamini Mzee Ukweli kwani hakuwahi kudanganya. Yeye aliaminiwa na wanakijiji wote. Walitayarisha vyombo vya kukinga na kuh fadhi maji. Punde si punde, matone makubwa ya mvua yakaanza kuanguka. Mvua kubwa ilinyesha. Watoto walionekana wakikinga na kuhifadhi maji mbele ya nyumba zao. Mito ilijaa maji.

Mama alichukua jembe na upanga akaenda shambani. Alitumia mbolea kupanda mahindi na maharagwe. Udongo ukawa na rutuba. Mbegu zilimea na kukua haraka. Wanakijiji walivuna na kuweka vyakula ndani ya maghala. Chakula kikawa kingi. Njaa iliisha kijijini Kinga. Wanakijiji walisikikika wakisema wangeendelea kulima kwa bidii ili watoto wao wasipatwe na njaa tena.

Mali ya Serikali ya Kenya 6

Kipindi cha 6 na 7 — Shambani 1

Msamiati

**Soma maneno haya.**

jembe mbolea rutuba

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

mbwa mabwawa kubwa ukweli

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni nani wanaozungumziwa kwenye hadithi hii?
3. Hadithi hii inafanyika wapi?
4. Ni nini kilichofanyika mwanzoni mwa hadithi?

Sarufi: Nafsi ya tatu - Umoja na wingi

**Jaza mapengo kwa maneno sahihi.**

1. __________ atafanya mtihani kesho. (Wewe, Yeye)
2. Mwanafunzi __________ ataenda shuleni kesho. (huyu, wale)
3. __________ watacheza mpira Jumatatu. (Yeye, Wao)
4. Wanakijiji __________ watapanda mbegu. (hao, hawa)

7 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**Ninafanya:** *Andika maneno haya ubaoni*: **mbwa, mabwawa, kubwa, ukweli, ubwabwa, kwaniTunafanya:** Hebu tujifunze kusoma maneno haya. Ni nini unaweza kutambua kuhusu maneno haya? Je, maneno haya yanafanana kwa njia yoyote? *(Tarajia majibu kutoka kwa wanafunzi.)*

**Ninafanya:** Maneno haya yana sauti **/bw/** na **/kw/.** Herufi **bw** na **kw** zinapatikana katika maneno yote. Nisikilizeni huku nikisoma neno la kwanza. Neno la kwanza ni **mbwa.** (*Pitisha kidole chini ya neno huku ukilisoma.)*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome pamoja. (*Pitisha kidole kwa sehemu za neno huku ukilisoma na wanafunzi. Wape wanafunzi mwelekeo ufao.*

**Unafanya:** Sasa soma neno hili peke yako.

**mbwa**

**Ninafanya:** *Waonyeshe neno la pili kwa kidole*. Neno hili ni **ukweli**. Neno hili lina sauti **/kw/**. (*Soma neno huku ukionyesha kwa kidole sauti/silabi husika).*

**Tunafanya:** Sasa tusome neno hili pamoja. (*Pitisha kidole chini ya neno kuonyesha sauti/silabi husika huku ukisoma. Wape wanafunzi mwelekeo ufaao.*

**Unafanya:** Sasa, soma neno peke yako. (*Pitisha kidole chini ya neno huku wakisoma. Wape wanafunzi mwelekeo unaofaa panapohitajika.)*

**ukweli**

*(Rudia huku wanafunzi wakiyasoma maneno yaliyobakia wao wenyewe kwa sauti. Wanafunzi wasome maneno ipasavyo kwa vikundi vya 2-3).*

**Unafanya:** Fungueni **ukurasa wa 7** wa vitabu vyenu kisha msome maneno hayo.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**Tunafanya:** Nani atatukumbusha tulichosoma katika somo lililopita?**Unafanya:** Kaa karibu na mwenzako mtakayesoma naye. Nyote mtasoma kwa zamu mmoja baada ya mwingine. Wakati mwenzako anasoma, wewe utafuatilia hadithi na kumsaidia kusoma au kutamka maneno yanayomtatiza.

## Sarufi: Nasfi ya Tatu

**Ninafanya:** Jana tulizungumza kuhusu **nafsi ya tatu-umoja na wingi.** Ni nani atatupatia mfano wa nafsi ya tatu. Tazama zoezi kutoka katika wa vitabu vyenu **ukurasa wa 7.** Tutatumia nafsi ya tatu na maneno ya kurejelea sahihi kujaza mapengo katika sentensi.

Sentensi ya kwanza ni. ______ atafanya mtihani kesho. Tunaweza kujaza pengo kwa kutumia yeye. *Yeye atafanya mtihani kesho.*

**Tunafanya:** Tusome sentensi yetu ya pili. Hebu tujaze pengo katika sentensi ya pili. Vizuri, jibu sahihi ni **yule**.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jazeni mapengo kwa kutumia jibu sahihi kutoka mabano.

**Majibu**

1. yeye 2. yule 3. wao 4. hao

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 6 na 7 | Shambani 1

**Matini**

**Kiangazi Kijijini Kinga**



Kijijini Kinga kulikuwa na kiangazi. Jua liliwaka na joto likawa jingi. Mvua haikunyesha. Mimea yote ilikauka hata kando ya mito. Kijiji kizima kikapatwa na njaa. Wanyama wengi kama mbwa wakafa. Mabwawa ya maji yakakauka. Hata hivyo, wanakijiji hawakufa moyo. Waliendelea kulima na kutayarisha mashamba yao ili wapande mbegu.

Jioni moja mawingu meusi yalionekana angani. Mzee Ukweli, mjuzi wa hali ya anga alitangaza, "Wanakijiji, leo mvua itanyesha." Wanakijiji walimuamini Mzee Ukweli kwani hakuwahi kudanganya. Yeye aliaminiwa na wanakijiji wote. Walitayarisha vyombo vya kukinga na kuh fadhi maji. Punde si punde, matone makubwa ya mvua yakaanza kuanguka. Mvua kubwa ilinyesha. Watoto walionekana wakikinga na kuhifadhi maji mbele ya nyumba zao. Mito ilijaa maji.

Mama alichukua jembe na upanga akaenda shambani. Alitumia mbolea kupanda mahindi na maharagwe. Udongo ukawa na rutuba. Mbegu zilimea na kukua haraka. Wanakijiji walivuna na kuweka vyakula ndani ya maghala. Chakula kikawa kingi. Njaa iliisha kijijini Kinga. Wanakijiji walisikikika wakisema wangeendelea kulima kwa bidii ili watoto wao wasipatwe na njaa tena.

Mali ya Serikali ya Kenya 6

Kipindi cha 6 na 7 | Shambani 1

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

jembe mbolea rutuba

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

mbwa mabwawa kubwa ukweli

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni nani wanaozungumziwa kwenye hadithi hii?
3. Hadithi hii inafanyika wapi?
4. Ni nini kilichofanyika mwanzoni mwa hadithi?

**Sarufi: Nafsi ya tatu - Umoja na wingi**

**Jaza mapengo kwa maneno sahihi.**

1. __________ atafanya mtihani kesho. (Wewe, Yeye)
2. Mwanafunzi __________ ataenda shuleni kesho. (huyu, wale)
3. __________ watacheza mpira Jumatatu. (Yeye, Wao)
4. Wanakijiji __________ watapanda mbegu. (hao, hawa)

7 Hakiuzwi

## Kuandika

### Masimulizi - Nakala ya Kwanza

*Sehemu hii itafanywa pamoja na wanafunzi. Mwalimu atawaongoza wanafunzi kutunga sentensi ili kuwa na hadithi. Waulize wanafunzi maswali yafuatayo ili kuwawezesha kutunga sentensi sahihi kwa kurejelea mipango ya uandishi waliyofanya wiki iliyopita.*

**Tunafanya:** Wiki iliyopita tulipanga jinsi ya kuandika. Nani atatukumbusha maana ya kupanga kuandika. Ni nini tulifanya tulipokuwa tukipanga kuandika? *(Kubali majibu sahihi.)*

Wiki hii tutaandika sehemu yetu ya kwanza. Sehemu hii ni muhimu kwa sababu ndiyo chanzo cha kuandika. Ni sehemu ya kwanza ya kuandika wala si nakala ya mwisho ya kuandika. Haitakuwa nakala sahihi, kwa hivyo itahitajika kurudiwa na kuandikwa upya ili kuwa nakala safi na sahihi mwishoni. Hebu tufanye mazoezi ya kuandika nakala ya kwanza pamoja.

**Ninafanya:** Kwanza tutarejelea yale tuliyokuwa tumepanga wiki iliyopita. Hebu tuangalie yale tuliyopanga.

Kila sehemu ya uandishi huanza na utangulizi. Katika hadithi huwa tunazungumza kuhusu wahusika na mahali hadithi inatendeka katika aya au sentensi ya kwanza. *(Wanafunzi watahitaji mwongozo kwenye hatua hii ya kwanza. Itakuwa bora kuwapa hoja kama wameshindwa kutoa hoja zao.)*

**Tunafanya:** Sasa tulisema ni nini kitafanyika kwanza? Nani atanisaidia kufikiria kuhusu sentensi ya kwanza itakayoelezea tukio la kwanza?

Tulisema kuwa changamoto itakuwa nini? Ni sentensi gani tunaweza kuandika kuonyesha kuwa wahusika wana changamoto hii?

Tulisema tutasuluhisha changamoto hii kwa njia gani? Tunaweza kueleza vipi jinsi ya kusuluhisha jambo hili katika sentensi?

Hebu tusome hadithi yetu kuhakikisha kuwa tumefuata yale tuliyokuwa tumeandika katika mipango yetu. Msomee rafiki yako na umwambie kama kuna kitu kinachokosekana kwenye hadithi kwa kurejelea yale tuliyopanga hapo awali.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Ambatanisha sentensi na msamiati sahihi.**

| | |
|---|---|
| 1. Shamba letu lilimea vitu vingi.<br>2. Shamba letu lina mchanga mzuri.<br>3. Tulivuna mazao mengi katika shamba letu.<br>4. Majani yaliyooza au chumvichumvi itumiwayo kurutubisha udongo. | mimea<br>rutuba<br>mavuno<br>mbolea |

Tarehe: __________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 8: Shambani 1

Kipindi cha 8 na 9 **Shambani 1**

**Matini**

## Ukulima Bora



Mzee Johari alikuwa na shamba kubwa na wafanyakazi wengi. Alifuga ng'ombe na mbuzi ambao walikuwa na afya nzuri. Katikati ya mwaka jana, Mzee Johari hakupata mazao mengi hata baada ya kulima shamba lake na kupanda. Alimtembelea mshauri wa kilimo aliyeishi karibu naye ili apate ushauri wa ukulima bora.

Mshauri alimwambia, "Ili kupata mazao mengi, ni bora kuzingatia mambo yafuatayo: Kwanza fyeka kwekwe zote shambani. Tumia mbolea ya kununua pamoja na mbolea ya mifugo. Hii itaongeza rutuba kwenye udongo na mimea itanawiri.Vilevile, palilia mimea wakati ufaao."

Mzee Johari akasema, "Asante mshauri wetu. Nitafuata maagizo kama ulivyosema".

Alipofika nyumbani, Mzee Johari aliwaita wafanyakazi wake na kuwaeleza namna ambavyo wangeboresha kilimo chao. Siku iliyofuata waliweka mbolea na kupanda mbegu. Walipalilia na kuyatupa magugu nyuma ya zizi. Mazao yalitolewa shambani wakati wa jua kali. Walipata mavuno mengi, wakauza sokoni. Mzee Johari akapata fedha nyingi na kuwalipia watoto wake karo shuleni.

Mali ya Serikali ya Kenya

8

Kipindi cha 8 na 9 **Shambani 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kwekwe mbegu mavuno

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

fyeka fyata afya kifyekeo

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni nani aliyekuwa na shamba kubwa?
2. Mzee Johari alifanya nini alipogundua kuwa hakupata mazao mengi?
3. Mbolea ina umuhimu gani kwa mimea?
4. Kando na kuwalipia watoto wake karo, unafikiri pesa alizozipata Mzee Johari baada ya kuuza mavuno zingefanya kazi gani nyingine?

**Sarufi: Umoja – Wingi**

**Andika sentensi hizi kwa wingi.**

**Mfano:** Yeye atalima. - Wao watalima.

1. Mkulima yule atapanda mahindi. ________________.
2. Yeye atamwita mshauri. ________________.
3. Mti ule utakatwa. ________________.
4. Zao lile litavunwa kesho. ________________.

9 Hakiuzwi

### Msamiati

**Tunafanya:** Ningependa tuanze kwa kutazama picha katika **ukurasa wa 8**. Mnaona nini kwenye picha?Je, mnajua nini kuhusu ukulima?
Sasa tutazame maneno haya mapya. Neno la kwanza ni **kwekwe.**
**Ninafanya:** Je, ni nani anayejua maana ya neno kwekwe? *(Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana.) unga sentensi inayoonyesha maana ya neno kwekwe.*
**Unafanya:** Jadiliana na mwenzako huku mkitumia maneno yenu wenyewe kueleza maana ya neno hili. (*Wanafunzi 2-4 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili).*
Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **kwekwe.** Msomee mwenzako sentensi uliyoitunga. *(Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.)*
**Tunafanya:** Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo: **mbegu, mavuno**
**Unafanya:** Sasa fungueni **ukurasa wa 9** wa vitabu vyenu. Tafuta msamiati tuliojifunza. Nataka tusome msamiati huo pamoja.

### Kusoma Matini: Masimulizi

**Tunafanya:** *Soma kichwa cha hadithi pamoja na wanafunzi*. Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu ukulima bora?
**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo utajifunza kwenye hadithi au ni nini kitakachotendeka kwenye hadithi? (*Waulize wanafunzi 2-4 kutoa majibu yao.)***Tunafanya:** *(Mwalimu na mwanafunzi wanasome kuwa pamoja.)*

**Unafanya:** *Wanafunzi wanasoma peke yao.*

Mwambie mwenzako iwapo utabiri wako ulitimia na kama haukutimia, ni nini kilichotendeka. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia.

### Ufahamu: Kusimulia Hadithi

**N:** *Chora umbo la nyumba ubaoni kisha useme:* Tutatumia umbo hili la nyumba kujibu maswali yafuatayo huku tukisimulia hadithi tena.




**T:** Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 8 na 9 **Shambani 1**

**Matini**

**Ukulima Bora**



Mzee Johari alikuwa na shamba kubwa na wafanyakazi wengi. Alifuga ng'ombe na mbuzi ambao walikuwa na afya nzuri. Katikati ya mwaka jana, Mzee Johari hakupata mazao mengi hata baada ya kulima shamba lake na kupanda. Alimtembelea mshauri wa kilimo aliyeishi karibu naye ili apate ushauri wa ukulima bora.

Mshauri alimwambia, "Ili kupata mazao mengi, ni bora kuzingatia mambo yafuatayo: Kwanza fyeka kwekwe zote shambani. Tumia mbolea ya kununua pamoja na mbolea ya mifugo. Hii itaongeza rutuba kwenye udongo na mimea itanawiri.Vilevile, palilia mimea wakati ufaao."

Mzee Johari akasema, "Asante mshauri wetu. Nitafuata maagizo kama ulivyosema".

Alipofika nyumbani, Mzee Johari aliwaita wafanyakazi wake na kuwaeleza namna ambavyo wangeboresha kilimo chao. Siku iliyofuata waliweka mbolea na kupanda mbegu. Walipalilia na kuyatupa magugu nyuma ya zizi. Mazao yalitolewa shambani wakati wa jua kali. Walipata mavuno mengi, wakauza sokoni. Mzee Johari akapata fedha nyingi na kuwalipia watoto wake karo shuleni.

Mali ya Serikali ya Kenya 8

Kipindi cha 8 na 9 **Shambani 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kwekwe mbegu mavuno

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

fyeka fyata afya kifyekeo

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni nani aliyekuwa na shamba kubwa?
2. Mzee Johari alifanya nini alipogundua kuwa hakupata mazao mengi?
3. Mbolea ina umuhimu gani kwa mimea?
4. Kando na kuwalipia watoto wake karo, unafikiri pesa alizozipata Mzee Johari baada ya kuuza mavuno zingefanya kazi gani nyingine?

**Sarufi: Umoja – Wingi**

**Andika sentensi hizi kwa wingi.**

**Mfano:** Yeye atalima. - Wao watalima.

1. Mkulima yule atapanda mahindi. ________________.
2. Yeye atamwita mshauri. ________________.
3. Mti ule utakatwa. ________________.
4. Zao lile litavunwa kesho. ________________.

9 Hakiuzwi

**N:** *Simulia darasa lote hadithi.*
**U:** Msimulie mwenzako hadithi.

### Maswali

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Ni nani aliyekuwa na shamba kubwa? (Mzee Johari.)
2. Mzee Johari alifanya nini alipogundua kuwa hakupata mazao mengi? (Alimtembelea mshauri wa kilimo.)
3. Mbolea ina umuhimu gani kwa mimea? (Kuongeza rutuba kwenye udongo ili mimea inawiri. Kuboresha mazao.)
4. Kando na kuwalipia watoto wake karo, unafikiri pesa alizozipata Mzee Johari baada ya kuuza mavuno zingefanya kazi gani nyingine? (Kubali jibu lolote sahihi.)

### Sarufi: Nafsi ya Tatu

**Tunafanya:** Ni nani anayekumbuka tuliyoyasoma kwenye sarufi? Ndio. Nafsi ya tatu-umoja na wingi. Pamoja na maneno ya kurejelea.
Hebu tutazame **ukurasa wa 9**. Sasa tutaandika wingi wa sentensi. (*Waonyeshe wanafunzi jinsi ya kuandika wingi wa sentensi kwa usahihi.*)
**Unafanya:** Ni zamu yenu. Sasa kamilisheni sentensi zilizosalia kwenye madaftari yenu.

**Majibu ya sarufi**

1. Wakulima wale watapanda mahindi.
2. Wao watawaita washauri.
3. Miti ile itakatwa.
4. Mazao yale yatavunwa kesho.

### Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Chora vifaa hivi vya shambani.**

1. upanga
2. trekta
3. kifyekeo
4. jembe

Tarehe: ____________ Muda: __________ Idadi: __________

Kipindi cha 8 na 9 **Shambani 1**

Matini

### Ukulima Bora



Mzee Johari alikuwa na shamba kubwa na wafanyakazi wengi. Alifuga ng'ombe na mbuzi ambao walikuwa na afya nzuri. Katikati ya mwaka jana, Mzee Johari hakupata mazao mengi hata baada ya kulima shamba lake na kupanda. Alimtembelea mshauri wa kilimo aliyeishi karibu naye ili apate ushauri wa ukulima bora.

Mshauri alimwambia, "Ili kupata mazao mengi, ni bora kuzingatia mambo yafuatayo: Kwanza fyeka kwekwe zote shambani. Tumia mbolea ya kununua pamoja na mbolea ya mifugo. Hii itaongeza rutuba kwenye udongo na mimea itanawiri.Vilevile, palilia mimea wakati ufaao."

Mzee Johari akasema, "Asante mshauri wetu. Nitafuata maagizo kama ulivyosema".

Alipofika nyumbani, Mzee Johari aliwaita wafanyakazi wake na kuwaeleza namna ambavyo wangeboresha kilimo chao. Siku iliyofuata waliweka mbolea na kupanda mbegu. Walipalilia na kuyatupa magugu nyuma ya zizi. Mazao yalitolewa shambani wakati wa jua kali. Walipata mavuno mengi, wakauza sokoni. Mzee Johari akapata fedha nyingi na kuwalipia watoto wake karo shuleni.

Ma I ya Serikali ya Kenya 8

Kipindi cha 8 na 9 **Shambani 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kwekwe mbegu mavuno

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

fyeka fyata afya kifyekeo

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni nani aliyekuwa na shamba kubwa?
2. Mzee Johari alifanya nini alipogundua kuwa hakupata mazao mengi?
3. Mbolea ina umuhimu gani kwa mimea?
4. Kando na kuwalipia watoto wake karo, unafikiri pesa alizozipata Mzee Johari baada ya kuuza mavuno zingefanya kazi gani nyingine?

**Sarufi: Umoja – Wingi**

**Andika sentensi hizi kwa wingi.**

**Mfano:** Yeye atalima. - Wao watalima.

1. Mkulima yule atapanda mahindi. ____________________.
2. Yeye atamwita mshauri. ____________________.
3. Mti ule utakatwa. ____________________.
4. Zao lile litavunwa kesho. ____________________.

9 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**Mwalimu:** Andika maneno haya ubaoni: **fyeka**, **fyata**, **afya**, **fyonza**, **fyatika**, **kifyekeo**

**Mwalimu:** Hebu tujifunze kusoma maneno yetu mapya. Ni nini unaweza kutambua kuhusu maneno haya? Je, maneno haya yanafanana kwa njia yoyote? *(Tarajia majibu kutoka kwa wanafunzi).*

**Mwalimu:** Maneno haya yana sauti **fy.** Herufi **f,y** zinapatikana katika maneno yote. Nisikilizeni huku nikisoma neno la kwanza. Neno la kwanza ni **fyeka.** (*Pitisha kidole chini ya neno huku ukilisoma*).

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome pamoja. (*Pitisha kidole kwa sehemu za neno huku ukilisoma na wanafunzi. Wape wanafunzi mwelekeo ipasavyo panapo budi*).

**Unafanya:** Sasa soma neno hili peke yako.

**fyeka**.

**Mwalimu:** Waonyeshe neno la pili kwa kidole. Neno hili **fyata.** Neno hili lina sauti **/fy/**. (*Soma neno huku ukionyesha kwa kidole sauti/silabi husika*).

**Tunafanya:** Sasa tusome neno hili pamoja. (*Pitisha kidole chini ya neno kuonyesha sauti/silabi husika huku ukisoma. Wape wanafunzi mwelekeo na wakosoe ifaavyo.)*

**Unafanya:** Sasa, soma neno peke yako. (*Pitisha kidole chini ya neno huku wakisoma. Wape wanafunzi mwelekeo unaofaa panapohitajika)*

Kumpongeza

(*Rudia huku wanafunzi wakisoma maneno yaliyobakia wao wenyewe kwa sauti. Wanafunzi wasome maneno ipasavyo kwa vikundi vya 2-3).*

**Unafanya:** Fungua vitabu vyenu **ukurasa wa** 9 kisha msome maneno hayo.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**Tunafanya:** Nani atatukumbusha tulichosoma wakati uliopita?

**Unafanya:** Sasa tusome hadithi tena. Mtafute mwenzako mtakayesoma naye. Nyote mtasoma kwa zamu, mmoja baada ya mwingine. Wakati mwenzako anaposoma, wewe utafuatilia hadithi na kumsaidia kusoma au kutamka maneno yanayomtatiza.

## Kuandika

### Masimulizi - Nakala ya Kwanza

**Tunafanya:** Nani atatukumbusha hoja muhimu kuhusu nakala ya kwanza. Vizuri, ni muhimu kwa sababu ni hatua ya kwanza ya kuandika na itarejelewa na kusahihishwa huku makosa yakitolewa ili kuwa nakala sahihi baadaye.

**Unafanya:** Sasa wewe na mwenzako rejeleeni mahali mlipopanga hatua za kuandika hadithi wiki iliyopita. Mtaandika sentensi nne au zaidi ili kuwa na nakala ya kwanza ya hadithi. Nakala yako izingatie hoja hizi nne muhimu: *(Andika sentensi hizi ubaoni).*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 9: Shambani 1

Kipindi cha 8 na 9 **Shambani 1**

Matini

### Ukulima Bora



Mzee Johari alikuwa na shamba kubwa na wafanyakazi wengi. Alifuga ng'ombe na mbuzi ambao walikuwa na afya nzuri. Katikati ya mwaka jana, Mzee Johari hakupata mazao mengi hata baada ya kulima shamba lake na kupanda. Alimtembelea mshauri wa kilimo aliyeishi karibu naye ili apate ushauri wa ukulima bora.

Mshauri alimwambia, "Ili kupata mazao mengi, ni bora kuzingatia mambo yafuatayo: Kwanza fyeka kwekwe zote shambani. Tumia mbolea ya kununua pamoja na mbolea ya mifugo. Hii itaongeza rutuba kwenye udongo na mimea itanawiri.Vilevile, palilia mimea wakati ufaao."

Mzee Johari akasema, "Asante mshauri wetu. Nitafuata maagizo kama ulivyosema".

Alipofika nyumbani, Mzee Johari aliwaita wafanyakazi wake na kuwaeleza namna ambavyo wangeboresha kilimo chao. Siku iliyofuata waliweka mbolea na kupanda mbegu. Walipalilia na kuyatupa magugu nyuma ya zizi. Mazao yalitolewa shambani wakati wa jua kali. Walipata mavuno mengi, wakauza sokoni. Mzee Johari akapata fedha nyingi na kuwalipia watoto wake karo shuleni.



Kipindi cha 8 na 9 **Shambani 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kwekwe mbegu mavuno

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

fyeka fyata afya kifyekeo

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni nani aliyekuwa na shamba kubwa?
2. Mzee Johari alifanya nini alipogundua kuwa hakupata mazao mengi?
3. Mbolea ina umuhimu gani kwa mimea?
4. Kando na kuwalipia watoto wake karo, unafikiri pesa alizozipata Mzee Johari baada ya kuuza mavuno zingefanya kazi gani nyingine?

Sarufi: Umoja – Wingi

**Andika sentensi hizi kwa wingi.**

**Mfano:** Yeye atalima. - Wao watalima.

1. Mkulima yule atapanda mahindi. ________________.
2. Yeye atamwita mshauri. ________________.
3. Mti ule utakatwa. ________________.
4. Zao lile litavunwa kesho. ________________.



1: Utangulizi wa wahusika na mahali hadithi inatendeka.

2: Tukio la kwanza, ni nini kinafanyika wakati hadithi inapoanza?

3: Matukio au mazungumzo yanayoleta changamoto katika hadithi.

4: Tukio la mwisho ambalo ni suluhu kwa changamoto kwenye hadithi.

**Unafanya:** Sasa mtajaribu huku nikiwaongoza kufanya hivyo.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Tunga sentensi nne ukitumia nafsi mbali mbali.**

**Mfano:** Wao ni wanafunzi wazuri.

Tarehe: ____________ Muda: __________ Idadi: __________

Kipindi cha 10 **Shambani 1**

Sarufi: Tathmini ya sarufi

**Andika sentensi hizi katika wakati ujao.**

1. Bi. Nakitare alilima shamba lake. ____________
2. Mimea iliwekwa mbolea. ____________
3. Mvua nyingi imenyesha. ____________
4. Watoto wanapalilia mimea. ____________

**Unda maneno manne kutokana na jedwali hili.**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| kwe | ru | u | a | li |
| fye | pla | pa | tu | ng'a |
| mbo | ba | za | le | ka |

Mali ya Serikali ya Kenya 10

## Msamiati

**Unafanya:** Fungueni **ukurasa wa 10** wa vitabu vyenu. Unda maneno ukitumia silabi zilizo kwenye jedwali:

**Majibu**

1. kwekwe
2. plau
3. upanga
4. mbolea
5. rutuba
6. fyeka

## Kusoma Maneno

Leo tutajikumbisha maneno tuliyojifunza wiki hii. Kwanza nitatamka neno kisha mtaliandika katika madaftari yenu. Je, mko tayari? Nitalisoma neno mara mbili huku mkiliandika. *(Sema au tamka neno mara mbili huku wanafunzi wakiliandika).*

**Unafanya:** Neno la kwanza ni **mbwa.** *(Rudia hatua hii ukitumia maneno yafuatayo).* **mabwawa, kubwa, ukweli, fyeka, afya, kwekwe, plau,mbolea, rutuba**

## Kuchambua Matini: Hoja kuu

**Tunafanya:** Wiki hii tulisoma hadithi mbili, ni nani anakumbuka kuhusu hadithi hizi? *(Wape wanafunzi 2-3 nafasi ya kuhadithia yale wanayokumbuka kuhusu hadithi walizozisoma).*

**Tunafanya:** Leo nataka turejelee hadithi tulizozisoma na tuangalie miktadha ya hadithi hizi. Kisha tutaandika kuhusu miktadha hiyo. Hebu tuanze na hadithi ya kwanza kwenye **ukurasa wa 6** pamoja. Hoja kuu ya hadithi mara nyingi huwa mwanzoni mwa hadithi. Hebu tusome aya ya kwanza pamoja. Je, hadithi hii inafanyika wapi? Je, tunaelezwa ni lini? Je, inakueleza chochote kuhusu hoja kuu?

Tuandike sentensi moja au mbili kuelezea hoja kuu ya hadithi hii. *Andika yafuatayo kuhusu hoja kuu ya hadithi.* Hadithi inahusu Kiangazi Kijijini Kinga. Wanyama wengi walikufa. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Mimea ilikua na chakula kikawa kingi.

**Unafanya:** Ni zamu yako sasa, tazama hadithi ya pili pamoja na mwenzako kwenye **ukurasa wa 8.** Soma aya ya kwanza, tambua hoja kuu ya hadithi na uiandike kwenye daftari lako.

## Sarufi: Nafsi ya Tatu

Hebu sasa turejelee sarufi tuliyojifunza wiki hii. Je, unakumbuka sarufi tuliyojifunza? Fungueni **ukurasa wa 10** wa vitabu vyenu. Andika sentensi hizo kwa wakati ujao.

**Majibu**

1. Bi. Nakitare atalima shamba lake.
2. Mimea ile itawekwa mbolea.
3. Mvu nyingi itanyesha kesho.
4. Watoto wale watapalilia mimea.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Taja mambo manne ambayo hufanyika shambani.
**Mfano:** Kufyeka nyasi.

## Kazi ya Nyongeza

Mwalimu aandae zoezi la kuburuta na kutia kapuni akizingatia nafsi na nyakati mbalimbali katika hali ya umoja na wingi. *(Zoezi katika mwongozo wa mwalimu)*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 11 na 12 **Sokoni 1**

**Matini**

**Duka la Bi. Mambo**

Bi. Mambo alifanya biashara Sokotele. Aliuza nguo, mikeka, miswaki na mikate katika duka lake. Alikuwa anapata faida. Jumamosi moja, Bi. Mambo alirauka na kuelekea Sokotele. Alipofika, alikuta paa la duka lake limevunjwa. Ratili na nguo zote zilikuwa zimeibwa. Bi. Mambo alipiga ripoti katika kituo cha polisi. "Nguo zimeibwa dukani mwangu. Naomba kusaidiwa." Bi. Mambo aliwaeleza askari waliosimama nje ya kituo cha polisi. Mara maafisa wa polisi walianza kuwatafuta wezi.



Katika soko jirani, vijana wawili walisikika wakinadi nguo. Wauzaji hao wa nguo walisema, "Bei rahisi! Ukitoa hamsini, utapewa baki yako." Waendeshaji wa bodaboda waliokuwa pale hawakuwaamini vijana hao. "Ni kwa nini wanauza nguo za bei ya juu mno kwa bei rahisi?" Mmoja wao alichukua simu ya rununu na kuwapigia maafisa wa polisi. Muda si muda, maafisa wa polisi na Bi. Mambo walifika. Bi. Mambo alizitambua nguo zile. Vijana wezi walikamatwa. Waliambiwa watoe nguo walizoweka ndani ya mkoba. Bi. Mambo aliwashukuru watu ambao waliwaita polisi, "Asanteni kwa msaada wenu. Mnafanya kazi nzuri kusaidia katika kulinda usalama wetu."

11 Hakiuzwi

Kipindi cha 11 na 12 **Sokoni 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

wauzaji wakinadi faida

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

bega mbegu mbuni buni

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Bi. Mambo alikuwa akifanya biashara wapi?
2. Je ungekuwa Bi. Mambo ungewapa vijana wezi ushauri gani?
3. Ni kwa nini mojawapo wa vijana wa bodaboda alipiga simu kwa polisi?
4. Hadithi hii inatufunza nini?

**Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'**

**Unganisha maneno na kihusishi sahihi kutunga sentensi.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mahindi yako | nje ya | ofisi ya Mwalimu Mkuu. |
| 2. Mlingoti uko | | ghala la nyanya. |
| 3. Kuku alitaga yai | ndani ya | kikapu. |
| 4. Dereva ameketi | | gari. |

Mali ya Serikali ya Kenya 12

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha katika makundi ya wanafunzi watatu watatu au zaidi.

**N:** Andika neno **wauzaji** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno **wauzaji** kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuwaelezea wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno **wauzaji.**

Rudia ukitumia maneno haya: **wakinadi, faida**

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 12.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**N/T:**Soma kichwa cha hadithi pamoja na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:**Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri wa wanafunzi.

## Ufahamu: Kusimulia Hadithi

**N:** *Chora umbo la nyumba ubaoni kisha useme:* Tutatumia umbo hili la nyumba kujibu maswali yafuatayo huku tukisimulia hadithi tena.

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T:** Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?
**N:** *Simulia darasa lote hadithi.*
**U:** Msimulie mwenzako hadithi.

### Maswali

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Bi. Mambo alikuwa akifanya biashara wapi? (Sokotele)
2. Je ungekuwa Bi. Mambo ungewapa vijana wezi ushauri gani? (Kubali jibu lolote sahihi)
3. Ni kwa nini mojawapo wa vijana wa bodaboda alipiga simu kwa polisi? (aliwashuku vijana waliouza nguo ghali kwa bei rahisi)
4. Hadithi hii inatufunza nini? (Umuhimu wa kulinda usalama)

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 11: Sokoni 1

Kipindi cha 11 na 12 **Sokoni 1**

**Matini**

**Duka la Bi. Mambo**

Bi. Mambo alifanya biashara Sokotele. Aliuza nguo, mikeka, miswaki na mikate katika duka lake. Alikuwa anapata faida. Jumamosi moja, Bi. Mambo alirauka na kuelekea Sokotele. Alipofika, alikuta paa la duka lake limevunjwa. Ratili na nguo zote zilikuwa zimeibwa. Bi. Mambo alipiga ripoti katika kituo cha polisi. "Nguo zimeibwa dukani mwangu. Naomba kusaidiwa." Bi. Mambo aliwaeleza askari waliosimama nje ya kituo cha polisi. Mara maafisa wa polisi walianza kuwatafuta wezi.



Katika soko jirani, vijana wawili walisikika wakinadi nguo. Wauzaji hao wa nguo walisema, "Bei rahisi! Ukitoa hamsini, utapewa baki yako." Waendeshaji wa bodaboda waliokuwa pale hawakuwaamini vijana hao. "Ni kwa nini wanauza nguo za bei ya juu mno kwa bei rahisi?" Mmoja wao alichukua simu ya rununu na kuwapigia maafisa wa polisi. Muda si muda, maafisa wa polisi na Bi. Mambo walifika. Bi. Mambo alizitambua nguo zile. Vijana wezi walikamatwa. Waliambiwa watoe nguo walizoweka ndani ya mkoba. Bi. Mambo aliwashukuru watu ambao waliwaita polisi, "Asanteni kwa msaada wenu. Mnafanya kazi nzuri kusaidia katika kulinda usalama wetu."

11 Hakiuzwi

Kipindi cha 11 na 12 **Sokoni 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

wauzaji wakinadi faida

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

bega mbegu mbuni buni

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Bi. Mambo alikuwa akifanya biashara wapi?
2. Je ungekuwa Bi. Mambo ungewapa vijana wezi ushauri gani?
3. Ni kwa nini mojawapo wa vijana wa bodaboda alipiga simu kwa polisi?
4. Hadithi hii inatufunza nini?

**Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'**

**Unganisha maneno na kihusishi sahihi kutunga sentensi.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mahindi yako | nje ya | ofisi ya Mwalimu Mkuu. |
| 2. Mlingoti uko | | ghala la nyanya. |
| 3. Kuku alitaga yai | ndani ya | kikapu. |
| 4. Dereva ameketi | | gari. |

Mali ya Serikali ya Kenya 12

## Sarufi: Vihusishi

**N/T:** Leo, tutajifunza kuhusu **vihusishi**. Vihusishi ni maneno yanayotuarifu zaidi kuhusu uhusiano wa nomino na mazingira yake. Kwa mfano, **nje ya**, **ndani ya**.

**U:** *Wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye vihusishi kutoka kwenye hadithi. Andika sentensi hizo pamoja na wanafunzi.*

**T/U:** *Waelekeze wanafunzi watunge sentensi wakitumia vihusishi.*

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Ni nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi ya; Duka la Bi. Mambo?

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 11 na 12 **Sokoni 1**

**Matini**

**Duka la Bi. Mambo**

Bi. Mambo alifanya biashara Sokotele. Aliuza nguo, mikeka, miswaki na mikate katika duka lake. Alikuwa anapata faida. Jumamosi moja, Bi. Mambo alirauka na kuelekea Sokotele. Alipofika, alikuta paa la duka lake limevunjwa. Ratili na nguo zote zilikuwa zimeibwa. Bi. Mambo alipiga ripoti katika kituo cha polisi. "Nguo zimeibwa dukani mwangu. Naomba kusaidiwa." Bi. Mambo aliwaeleza askari waliosimama nje ya kituo cha polisi. Mara maafisa wa polisi walianza kuwatafuta wezi.



Katika soko jirani, vijana wawili walisikika wakinadi nguo. Wauzaji hao wa nguo walisema, "Bei rahisi! Ukitoa hamsini, utapewa baki yako." Waendeshaji wa bodaboda waliokuwa pale hawakuwaamini vijana hao. "Ni kwa nini wanauza nguo za bei ya juu mno kwa bei rahisi?" Mmoja wao alichukua simu ya rununu na kuwapigia maafisa wa polisi. Muda si muda, maafisa wa polisi na Bi. Mambo walifika. Bi. Mambo alizitambua nguo zile. Vijana wezi walikamatwa. Waliambiwa watoe nguo walizoweka ndani ya mkoba. Bi. Mambo aliwashukuru watu ambao waliwaita polisi, "Asanteni kwa msaada wenu. Mnafanya kazi nzuri kusaidia katika kulinda usalama wetu."

11 Hakluzwi

Kipindi cha 11 na 12 **Sokoni 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

wauzaji wakinadi faida

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

bega mbegu mbuni buni

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Bi. Mambo alikuwa akifanya biashara wapi?
2. Je ungekuwa Bi. Mambo ungewapa vijana wezi ushauri gani?
3. Ni kwa nini mojawapo wa vijana wa bodaboda alipiga simu kwa polisi?
4. Hadithi hii inatufunza nini?

**Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'**

**Unganisha maneno na kihusishi sahihi kutunga sentensi.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mahindi yako<br>2. Mlingoti uko<br>3. Kuku alitaga yai<br>4. Dereva ameketi | nje ya<br><br>ndani ya | ofisi ya Mwalimu Mkuu.<br>ghala la nyanya.<br>kikapu.<br>gari. |

Mali ya Serikali ya Kenya 12

## Kusoma Maneno

**N:** *Andika maneno haya ubaoni:* **bega, mbegu, bodaboda, ambao.**

**T:** *Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.*

**N:** Maneno haya yana sauti **b** na **mb.** *Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno*: **bega** na **mbegu.** *Yasome maneno huku ukifuatiliza kidole chini kuonesha sauti na silabi husika.*

**N/T/U: bega, mbegu**

**T/U: bodaboda, ambao**

**U:** *Wanafunzi wanasoma maneno* **ukurasa wa 12.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**N/T:** Nani anakumbuka tulichojifunza kuhusu Duka la Bi. Mambo.

**U:** *Wanafunzi wasomee wenzao.*

## Sarufi: Vihusishi

**T:** Nani anakumbuka sarufi tuliyojifunza? *Kubali jibu sahihi.* Sarufi tuliyojifunza ni vihusishi. Leo tutaambatanisha maneno kwenye jedwali ili kuunda sentensi sahihi. Pia sentensi inafaa ianze kwa herufi kubwa. *(Mwalimu aandike sentensi sahihi na kuisoma)*. Mahindi yako ndani ya ghala la nyanya.

**T:** Sasa tujaribu sentensi nyingine pamoja. Je, ni nani anaweza kuunda sentensi akitumia nje ya au ndani ya.

**Majibu**

1. Mahindi yako ndani ya ghala la nyanya.
2. Mlingoti uko nje ya ofisi ya mwalimu.
3. Kuku alitaga yai ndani ya kikapu.
4. Dereva ameketi ndani ya gari.

## Kuandika

### Masimulizi - Kuhakiki

**T:** Tumeweza kupanga, kuandika nakala ya kwanza na kuirejelea. Wiki hii tutaishughulikia nakala ya kwanza. Tutaiboresha na kuifanya sahihi ili tuichapishe wiki ijayo. Ili kusahihisha kazi yetu, lazima turejelee kazi tuliyofanya kwa kurejelea nakala ya kwanza. Itazame kazi yako na uangalie maneno ambayo hayajaendelezwa vizuri au yenye makosa ya tahajia. Kama hujui kuendeleza neno fulani, muulize mwenzako kwanza ili akusaidie na kama hawezi, inua mkono wako ili nikupe mwongozo. Ukimaliza kuisahihisha na kuirekebisha kazi yako, iandike kwenye **ukurasa** mpya bila makosa. Ukishamaliza, mpe mwenzako aisome mara ya pili tena na atoe uamuzi kama ni sahihi na tayari kupigwa chapa au kusomwa na wengine.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Nakili maneno haya kisha uyasome:**

1. mbuni 2. buni 3. mboga 4. boga

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 13: Sokoni 1

Kipindi cha 13 na 14 **Sokoni 1**

**Matini**

**Mkoba wa Mama Bidii**

Shughuli zilikuwa nyingi jijini Sokomoko. Mama Bidii alikuja sokoni kununua nyama na kusaga mahindi kwenye mtambo. Alipofika kwenye buchari, aliuweka mkoba wake chini. Alijiunga na wanunuzi wengine, ili apimiwe nyama kwa ratili. Foleni iliposonga, aliinama kuusongesha mkoba wake. Lo! Haukuwepo. Aliangalia huku na kule na kumwona kijana akitimua mbio na mkoba huo. Alipaza sauti na kusema, “Mwizi! Kamata huyo! Mkoba wangu!”



Mteja mmoja barobaro alimfuata kijana huyo mwizi mbio. Akampata nje ya kichinjio alipokuwa amejificha na kumbeba juu kwa juu. Alitaka kumpa mwizi huyo kichapo cha mbwa. Mama Bidii alipofika akamwomba, “Tafadhali, usimchape. Acha kuchukua sheria mikononi mwako. Tumewaita polisi. Wanakuja kumkamata.” Mama Bidii akapewa mkoba wake. Aliufungua ili kuhakikisha vitu vilivyokuwa ndani ya mkoba havikutolewa.

Maafisa wa polisi walipofika, walimshika yule kijana. Siku iliyofuata, polisi walimpeleka mahakamani. Kijana yule aliomba msamaha na kusema kuwa hatawahi kuiba tena. Hakimu alimhukumu kufanya kazi ya huduma kwa jamii kwa muda wa miezi miwili.

13 Hakiuzwi

Kipindi cha 13 na 14 **Sokoni 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kichinjio buchari ratili

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

barobaro mboga mbona barua

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Mama Bidii alikuja sokoni kufanya nini?
2. Ni nini kilifanyika foleni ilipsonga?
3. Ni kwa nini Mama Bidii alisema mwizi asichapwe?
4. Ni kwa nini si vizuri kumpiga mwizi anapokamatwa?

**Sarufi: Vihusishi 'nje ya' na 'ndani ya'**

**Kamilisha sentensi hizi ukitumia “nje ya” au “ndani ya”.**

1. Pesa za mama Bidii zilikuwa ____________ mfuko.
2. Kijana alikuwa ____________ buchari.
3. Vitabu vya Maria vimo ____________ mkoba.
4. Miti hupandwa ____________ darasa.

**Kuandika**

**Andika kisa kifupi kuhusu soko la kwenu.**

Mali ya Serikali ya Kenya 14

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha.

**N:** Andika neno **kichinjio** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuelezea wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno.

*(Rudia zoezi na maneno haya:* **buchari, ratili.***)*

**U:** Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **buchari**.

**U:** *Wanafunzi wanasoma maneno* mapya kwenye **ukurasa wa 13.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**N/T:** Soma kichwa cha hadithi pamoja na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu: Kusimulia Hadithi

N: Chora umbo la nyumba.




**T:** Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?

**N:** *Simulia darasa lote hadithi.*

**U:** Msimulie mwenzako hadithi.

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Mama Bidii alikuja sokoni kufanya nini? (kununua nyama na kusaga mahindi)
2. Ni nini kilifanyika foleni iliposonga? (Alipata mkoba wake umeibiwa)
3. Ni kwa nini Mama Bidii alisema mwizi asichapwe?(hakutaka wachukue sheria mikononi mwao)
4. Ni kwa nini si vizuri kumpiga mwizi anapokamatwa? (Kubali jibu lolote sahihi_

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 13 na 14 **Sokoni 1**

**Matini**

**Mkoba wa Mama Bidii**

Shughuli zilikuwa nyingi jijini Sokomoko. Mama Bidii alikuja sokoni kununua nyama na kusaga mahindi kwenye mtambo. Alipofika kwenye buchari, aliuweka mkoba wake chini. Alijiunga na wanunuzi wengine, ili apimiwe nyama kwa ratili. Foleni iliposonga, aliinama kuusongesha mkoba wake. Lo! Haukuwepo. Aliangalia huku na kule na kumwona kijana akitimua mbio na mkoba huo. Alipaza sauti na kusema, "Mwizi! Kamata huyo! Mkoba wangu!"



Mteja mmoja barobaro alimfuata kijana huyo mwizi mbio. Akampata nje ya kichinjio alipokuwa amejificha na kumbeba juu kwa juu. Alitaka kumpa mwizi huyo kichapo cha mbwa. Mama Bidii alipofika akamwomba, "Tafadhali, usimchape. Acha kuchukua sheria mikononi mwako. Tumewaita polisi. Wanakuja kumkamata." Mama Bidii akapewa mkoba wake. Aliufungua ili kuhakikisha vitu vilivyokuwa ndani ya mkoba havikutolewa.

Maafisa wa polisi walipofika, walimshika yule kijana. Siku iliyofuata, polisi walimpeleka mahakamani. Kijana yule aliomba msamaha na kusema kuwa hatawahi kuiba tena. Hakimu alimhukumu kufanya kazi ya huduma kwa jamii kwa muda wa miezi miwili.

13 Hakluzwi

Kipindi cha 13 na 14 **Sokoni 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kichinjio buchari ratili

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

barobaro mboga mbona barua

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Mama Bidii alikuja sokoni kufanya nini?
2. Ni nini kilifanyika foleni iliposonga?
3. Ni kwa nini Mama Bidii alisema mwizi asichapwe?
4. Ni kwa nini si vizuri kumpiga mwizi anapokamatwa?

**Sarufi: Vihusishi 'nje ya' na 'ndani ya'**

**Kamilisha sentensi hizi ukitumia "nje ya" au "ndani ya".**

1. Pesa za mama Bidii zilikuwa ____________ mfuko.
2. Kijana alikuwa ____________ buchari.
3. Vitabu vya Maria vimo ____________ mkoba.
4. Miti hupandwa ____________ darasa.

**Kuandika**

**Andika kisa kifupi kuhusu soko la kwenu.**

Mali ya Serikali ya Kenya 14

## Sarufi: Vihusishi

**N/T:** Nani anaweza kukumbuka yale tuliyojifunza jana katika sehemu ya sarufi? Sarufi tuliyojifunza jana ni **vihusishi**. Hebu tutazame sentensi hii pamoja. Soma sentensi ya kwanza katika **ukurasa wa 14.** Pesa za Mama Bidii zilikuwa _____ mfuko.

Tunafaa kujaza pengo kwa kutumia "ndani ya" kwa sababu tunaweka pesa ndani ya mkoba.

Sentensi sasa itasoma – Pesa za Mama Bidii zilikuwa ndani ya mkoba.

**U:** Sasa fungua **ukurasa wa 14** wa kitabu chako. Kamilisha sentensi hizo na uziandike kwenye daftari lako.

**Majibu**

1. ndani ya
2. ndani ya
3. ndani ya
4. nje ya

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Jaza mapengo ukitumia maneno "ndani ya" au "nje ya"**

1. Viatu vilivyokuwa _________ mfuko vimepotea. (ndani ya)
2. Miti iliyo _________ ofisi imekua. (nje ya)
3. Maji yamo _________ mkebe. (ndani ya)
4. Mpira ulichezewa _________ darasa. (nje ya )

## Kazi ya Nyongeza

Mkaririe mlezi wako shairi hili ufikapo nyumbani.

**Duka la Bi. Mambo**

Dukani kwa mama Mambo, jambo limekwenda kombo,
Na tena sio kitambo, wezi wamefanya mambo,
Kilo na nguo za mambo, wezi wamepiga kumbo,
Wamekamatwa kwa chambo, watacharazwa kwa fimbo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 14: Sokoni 1

Kipindi cha | 13 na 14 | **Sokoni 1**

**Matini**

**Mkoba wa Mama Bidii**

Shughuli zilikuwa nyingi jijini Sokomoko. Mama Bidii alikuja sokoni kununua nyama na kusaga mahindi kwenye mtambo. Alipofika kwenye buchari, aliuweka mkoba wake chini. Alijiunga na wanunuzi wengine, ili apimiwe nyama kwa ratili. Foleni ilposonga, aliinama kuusongesha mkoba wake. Lo! Haukuwepo. Aliangalia huku na kule na kumwona kijana akitimua mbio na mkoba huo. Alipaza sauti na kusema, "Mwizi! Kamata huyo! Mkoba wangu!"



Mteja mmoja barobaro alimfuata kijana huyo mwizi mbio. Akampata nje ya kichinjio alipokuwa amejificha na kumbeba juu kwa juu. Alitaka kumpa mwizi huyo kichapo cha mbwa. Mama Bidii alipofika akamwomba, "Tafadhali, usimchape. Acha kuchukua sheria mikononi mwako. Tumewaita polisi. Wanakuja kumkamata." Mama Bidii akapewa mkoba wake. Aliufungua ili kuhakikisha vitu vilivyokuwa ndani ya mkoba havikutolewa.

Maafisa wa polisi walipofika, walimshika yule kijana. Siku iliyofuata, polisi walimpeleka mahakamani. Kijana yule aliomba msamaha na kusema kuwa hatawahi kuiba tena. Hakimu alimhukumu kufanya kazi ya huduma kwa jamii kwa muda wa miezi miwili.

13 Hakiuzwi

Kipindi cha | 13 na 14 | **Sokoni 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kichinjio buchari ratili

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

barobaro mboga mbona barua

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Mama Bidii alikuja sokoni kufanya nini?
2. Ni nini kilifanyika foleni ilposonga?
3. Ni kwa nini Mama Bidii alisema mwizi asichapwe?
4. Ni kwa nini si vizuri kumpiga mwizi anapokamatwa?

**Sarufi: Vihusishi 'nje ya' na 'ndani ya'**

**Kamilisha sentensi hizi ukitumia "nje ya" au "ndani ya".**

1. Pesa za mama Bidii zilikuwa ____________ mfuko.
2. Kijana alikuwa ____________ buchari.
3. Vitabu vya Maria vimo ____________ mkoba.
4. Miti hupandwa ____________ darasa.

**Kuandika**

**Andika kisa kifupi kuhusu soko la kwenu.**

Mali ya Serikali ya Kenya 14

## Kusoma Maneno

**T:** *Andika maneno haya ubaoni:* **mbio, mbolea, barobaro, mboga,**
*Waulize wanafunzi kile wanachoweza kutambua kuhusu maneno haya.*
**N:** Maneno haya yana sauti **/b/** na **/mb/**. *(Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: boga na mboga. Yasome maneno huku ukifuatiliza kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.)*
**N/T/U: mbio, mbotela**
**T/U: barobaro, mboga**
**U:** *Wanafunzi wanasoma maneno katika* **ukurasa wa 14.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**N/T:** Nani anakumbuka tulichojifunza wakati uliopita. Tulijifunza kuhusu Mkoba wa Mama Bidii.
**U:** *Wanafunzi wasomee wenzao.*

## Kuandika

### Masimulizi - Kuhakiki

**U:** Leo tutaendelea kuboresha nakala zetu ili kuhakikisha ya kwamba ziko sahihi. Ukimalizia, uinue mkono ili nisahihisha kazi yako.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Jaza mapengo kwa neno sahihi kulingana na maelezo. Tumia maneno haya: wauzaji, buchari, ratili, kunadi**

1. Kifaa cha kupimia nyama. __________ (ratili)
2. Wachuuzi. __________ (wauzaji)
3. Mahali pa kuuzia nyama. __________ (buchari)
4. Kutangaza bidhaa kwa sauti ya juu. _______(kunadi)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 15: Sokoni 1

**Kipindi cha 15** | **Sokoni 1**

**Tathmini ya Msamiati**

**Unda maneno manne kutokana na silabi zilizo kwenye jedwali.**

**Mfano:** buchari

| | | |
|---|---|---|
| ba | bu | cha |
| ri | ki | fa |
| i | ni | na |
| nda | da | di |

**Tathmini ya Sarufi**

***Jaza mapengo kwa kutumia 'ndani ya' au 'nje ya'.***

1. Maziwa yako ___________ chupa.
2. Wanafunzi wanacheza ___________ darasa.
3. Mlingoti wa bendera uko ___________ ofisi ya Mwalimu Mkuu.
4. Mama anatoka ___________ nyumba.

15

Hakiuzwi

## Msamiati

**U:** Fungua vitabu vyenu **ukurasa wa 15**. Unda maneno manne kutokana na silabi zilizo kwenye jedwali. Mfano bukini, nani.

## Kusoma Maneno

**N:** Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **mbegu, mbuni, buni, mboga, boga, barobaro, mbona, barua, mbio, mbolea**

## Kuchambua Matini

**N:** Je muktadha wa hadithi ni nini? Muktadha ni mahali ambapo hadithi inafanyika.

Muktadha wa hadithi mara nyingi huwa mwanzoni mwa hadithi. Hebu tusome aya ya kwanza pamoja. Je, hadithi hii inafanyika wapi? Je, tunaelezwa ni lini? Je, inakueleza chochote kuhusu muktadha?

**T:** *Waulize wanafunzi waelezee kuhusu waliyosoma. Toa maelezo kuhusu hoja kuu katika aya ya kwanza.*

**N/T:** *Andika sentensi 1 au 2 kuhusu muktadha.* Hadithi inahusu wizi uliofanyika katika duka la Bi. Mambo. Hadithi hii ilifanyika sokoni.

**U:** Ni zamu yako, tazama hadithi ya pili ya pamoja na mwenzako **ukurasa wa 13**. Soma aya ya kwanza, tambua hoja kuu ya hadithi na uiandike kwenye daftari lako.

## Sarufi: Vihusishi

**T:** Nani anakumbuka sarufi tuliyojifunza wiki hii.
Sarufi tuliyojifunza ilikuwa vihusishi.
**U:** Fungua kitabu chako sehemu ya sarufi.
Kamilisha sentensi hizo na uziandike kwenye daftari lako.

**Majibu**

1. ndani ya
2. nje ya
3. nje ya
4. nje ya, ndani ya

**Unda maneno kutokana na jedwali la silabi lililo katika ukurasa wa 15.**

**Majibu**

1. faida
2. bucha
3. nadi
4. Kibanda

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Chagua jibu sahihi kutoka kwenye jedwali.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ratili | kichinjio | faida | nadi |

1. Mapato baada ya kuuza kitu na kuondoa gharama. (faida)
2. Mahali panapochinjiwa wanyama. (kichinjio)
3. Kifaa cha kupimia uzito. (ratili)
4. Kutangaza bei au jambo kwa sauti kubwa. (nadi)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 16 na 17 **Uzalendo 1**

**Wimbo wa Taifa**

**Wimbo wa Taifa**



Ee Mungu nguvu yetu,
Ilete baraka kwetu,
Haki iwe ngao na mlinzi,
Natukae na undugu,
Amani na uhuru,
Raha tupate na ustawi.

Amkeni ndugu zetu,
Tufanye sote bidii,
Nasi tujitoe kwa nguvu,
Nchi yetu ya Kenya,
Tunayoipenda,
Tuwe tayari kuilinda.

Natujenge taifa letu,
Ee, ndio wajibu wetu,
Kenya istahili heshima,
Tuungane mikono,
Pamoja kazini,
Kila siku tuwe na shukrani.

Mali ya Serikali ya Kenya 16

Kipindi cha 16 na 17 **Uzalendo 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

taifa nchi amani

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

undugu kulinda ndio tunayoipenda

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha wimbo huu.
2. Wimbo huu ni wimbo wa taifa wa nchi gani?
3. Kulingana na wimbo huu ni nini wajibu wa wanafunzi?
4. Wimbo huu wa taifa huimbwa wakati gani?
5. Ni mambo gani yanazungumziwa mwishoni mwa wimbo huu?

**Sarufi: Vimilikishi –ake, –ao, na –etu**

**Unganisha maneno na kimilikishi sahihi kutunga sentensi.**

| A | B | C |
|---|---|---|
| Vitabu | yetu | ni vizuri. |
| Mtoto | vyetu | alikimbia sana. |
| Matunda | wake | yaliiva vizuri. |
| Nchi | yao | inapendeza sana. |

17 Hakiuzwi

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika neno **taifa** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno taifa kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi wawaelezee wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno.
5. Rudia ukitumia maneno yafuatayo: **nchi, amani**

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 17.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** Soma kichwa cha wimbo na wanafunzi. Jadili picha. waulize wanafunzi watoe utabiri.
**T/U:** Imba wimbo.
**U:** Hakiki utabiri.

## ? Ufahamu

### Maswali

1. **N:** Taja kichwa cha wimbo huu. (Wimbo wa taifa.)
2. **T:** Wimbo huu ni wimbo wa taifa wa nchi gani? (Kenya)
3. **U:** Kulingana na wimbo huu, ni nini wajibu wa wanafunzi? (Kujenga taifa.)
4. **U:** Wimbo huu wa taifa huimbwa wakati gani? (Wakati wa kupandisha bendera.)
5. **U:** Ni mambo gani yanazungumziwa mwishoni mwa wimbo huu? (Kujenga taifa, kuheshimu Kenya, kuungana pamoja.)

## Sarufi: Vimilikishi –ake, –ao, na -etu

**N/T:** [Vimilikishi ni maneno yanayotueleza kitu ni cha nani. Kwa mfano, kitabu **changu au chake/chao.**]**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye vimilikishi kutoka kwenye hadithi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.
**U:** Waelekeze wanafunzi watunge sentensi wakitumia vimilikishi **–ake, –ao, na -etu**.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Taja rangi nne za bendera yetu.

**Majibu**

1. Nyeusi
2. Nyeupe
3. Nyekundu
4. Kijani kibichi

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 16 na 17 **Uzalendo 1**

Wimbo wa Taifa

**Wimbo wa Taifa**



Ee Mungu nguvu yetu,
Ilete baraka kwetu,
Haki iwe ngao na mlinzi,
Natukae na undugu,
Amani na uhuru,
Raha tupate na ustawi.

Amkeni ndugu zetu,
Tufanye sote bidii,
Nasi tujitoe kwa nguvu,
Nchi yetu ya Kenya,
Tunayoipenda,
Tuwe tayari kuilinda.

Natujenge taifa letu,
Ee, ndio wajibu wetu,
Kenya istahili heshima,
Tuungane mikono,
Pamoja kazini,
Kila siku tuwe na shukrani.

Mali ya Serikali ya Kenya 16

Kipindi cha 16 na 17 **Uzalendo 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

taifa nchi amani

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

undugu kulinda ndio tunayoipenda

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha wimbo huu.
2. Wimbo huu ni wimbo wa taifa wa nchi gani?
3. Kulingana na wimbo huu ni nini wajibu wa wanafunzi?
4. Wimbo huu wa taifa huimbwa wakati gani?
5. Ni mambo gani yanazungumziwa mwishoni mwa wimbo huu?

Sarufi: Vimilikishi -ake, -ao, na -etu

**Unganisha maneno na kimilikishi sahihi kutunga sentensi.**

| A | B | C |
|---|---|---|
| Vitabu | yetu | ni vizuri. |
| Mtoto | vyetu | alikimbia sana. |
| Matunda | wake | yaliiva vizuri. |
| Nchi | yao | inapendeza sana. |

17 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **undugu, kulinda, tuungane, nguvu**

Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya

**N:** Maneno haya yana sauti **nd** au **ng**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **undugu** na **nguvu.** (Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.)

**N/T/U: undugu, kulinda**

**U: tuungane, nguvu**

**U:** Wanafunzi wasome katika **ukurasa wa 17.**

## Kusoma Matini: Shairi

**N/T:** [Nani anakumbuka nini tulichojifunza wakati uliopita. Tulijifunza kuhusu **Wimbo wa Taifa.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vimilikishi –ake –ao , na -etu

**N:** [Vimilikishi ni maneno yanayotueleza kitu ni cha nani. Hebu tutazame jedwali letu katika **ukurasa wa 17.** Tutatunga sentensi kwa kuchagua na kutumia maneno kutoka kila sehemu ya jedwali yani A, B na C ili kuunda sentensi mpya. Nitawaelekeza kutunga sentensi ya kwanza. Nitachukua kifungu kwenye sehemu ya kwanza ya jedwali A kisha nichukue **kimilikishi** kwenye sehemu ya B na mwisho sehemu ya C ili kuunda sentensi moja sahihi. (*Tunga sentensi: **Vitabu vyetu ni vizuri).***]

**T:** Mwalimu na wanafunzi waunganishe maneno na kihusishi sahihi kutunga sentensi. (Rudia na maneno mengine. Kubali majibu sahihi.)

**Majibu**

1. Vitabu vyetu ni vizuri.
2. Mtoto wake alikimbia sana.
3. Matunda yao yaliiva vizuri.
4. Nchi yetu inapendeza sana.

## Kuandika

**Masimulizi - Kuhariri**

**T:** [Tumeweza kupanga, kuandika nakala ya kwanza na kuirejelea. Wiki hii tutaishughulikia nakala hii ya kwanza, tuiboreshe na kuifanya sahihi ili wiki ijayo tuichapishe. Ili kusahihisha kazi yetu, lazima turejelee na kukosoa nakala ya kwanza. Tutatazama nakala zetu na tuangalie ikiwa zina maneno ambayo hayajaendelezwa vizuri au yana makosa ya tahajia. *(Waongoze wanafunzi kurekebisha kila neno au sehemu ambayo inahitaji marekebisho.)* Sasa tutamaliza kurekebisha nakala zetu kwa mara ya mwisho ili tuamue kama ziko tayari kuchapishwa. *(Soma nakala na wanafunzi.)*]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa


Tunga sentensi 4 sahihi kwa kutumia kimilikishi -ao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 18 na 19 **Uzalendo 1**

**Matini**

**Rangi za Bendera**



Bendera yetu ya Kenya x2
Inayo rangi nyeusi...
Hiyo ndiyo rangi
Yetu wananchi...
Tunasimama imara, chini ya bendera yetu.

Bendera yetu ya Kenya x2
Inayo rangi nyeupe...
Hiyo ndiyo rangi
Ya maziwa yetu...
Tunasimama imara, chini ya bendera yetu.

Bendera yetu ya Kenya x2
Inayo rangi nyekundu...
Hiyo ndio rangi
Ya damu yetu...
Tunasimama imara, chini ya bendera yetu.

Bendera yetu ya Kenya x2
Inayo rangi ya kijani...
Hiyo ndiyo rangi
Ya mimea yetu...
Tunasimama imara, chini ya bendera yetu.

Mali ya Serikali ya Kenya 18

Kipindi cha 18 na 19 **Uzalendo 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

bendera    rangi za bendera    imara

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

mwananchi    bendera    nyekundu    ndio

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na wimbo.**

1. Taja kichwa cha wimbo huu.
2. Ni rangi gani inayozungumziwa mwanzoni mwa wimbo?
3. Ni rangi gani inayozungumziwa katika ubeti wa pili na wa tatu wa wimbo huu?
4. Ni rangi gani inayozungumziwa mwishoni mwa wimbo?

**Sarufi: Vimilikishi –ake, –ao na –etu**

**Andika sentensi hizi katika wingi.**

1. Kitabu hiki ni chake.
2. Kalamu hii ni yake.
3. Meza yake imevunjika.
4. Nchi hii ni yetu.

19 Hakiuzwi

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika neno **bendera** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno bendera kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuelezea wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno. Rudia na haya: **rangi za bendera, imara**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **imara.**]

**U:** Wanafunzi wanasoma maneno mapya kwenye **ukurasa wa 19.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** Soma kichwa cha shairi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma shairi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

### Maswali

1. **N:** Taja kichwa cha wimbo huu. (Rangi za Bendera)
2. **T:** Ni rangi gani inayozungumziwa mwanzoni mwa wimbo? (Rangi nyeusi)
3. **U:** Ni rangi gani inayozungumziwa katika ubeti wa pili na wa tatu wa wimbo huu? (Rangi nyeupe na nyekundu)
4. **U:** Ni rangi gani inayozungumziwa mwishoni mwa wimbo? (Rangi ya kijani)

## Sarufi: Vimilikishi –ake –ao, na -etu

**N/T:** [Vimilikishi ni maneno yanayotuonyesha kitu ni cha nani. Hebu tuandike sentensi ya kwanza katika wingi: **Vitabu hivi ni vyao.**]

**U:** [Sasa kamilisha sentensi hizi nyingine peke yako kwa kuziandika katika daftari lako.]

### Majibu

1. Vitabu hivi ni vyao.
2. Kalamu hizi ni zao.
3. Meza zao zimevunjika.
4. Nchi hizi ni zetu.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa


Tunga sentensi 4 sahihi kwa kutumia kimilikishi –ake. Kubali majibu sahihi.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 18 na 19 **Uzalendo 1**

**Matini**

**Rangi za Bendera**



Bendera yetu ya Kenya x2
Inayo rangi nyeusi...
Hiyo ndiyo rangi
Yetu wananchi...
Tunasimama imara, chini ya bendera yetu.

Bendera yetu ya Kenya x2
Inayo rangi nyeupe...
Hiyo ndiyo rangi
Ya maziwa yetu...
Tunasimama imara, chini ya bendera yetu.

Bendera yetu ya Kenya x2
Inayo rangi nyekundu...
Hiyo ndio rangi
Ya damu yetu...
Tunasimama imara, chini ya bendera yetu.

Bendera yetu ya Kenya x2
Inayo rangi ya kijani...
Hiyo ndiyo rangi
Ya mimea yetu...
Tunasimama imara, chini ya bendera yetu.

Mali ya Serikali ya Kenya 18

Kipindi cha 18 na 19 **Uzalendo 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

bendera rangi za bendera imara

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

mwananchi bendera nyekundu ndio

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na wimbo.**

1. Taja kichwa cha wimbo huu.
2. Ni rangi gani inayozungumziwa mwanzoni mwa wimbo?
3. Ni rangi gani inayozungumziwa katika ubeti wa pili na wa tatu wa wimbo huu?
4. Ni rangi gani inayozungumziwa mwishoni mwa wimbo?

**Sarufi: Vimilikishi -ake, -ao na -etu**

**Andika sentensi hizi katika wingi.**

1. Kitabu hiki ni chake.
2. Kalamu hii ni yake.
3. Meza yake imevunjika.
4. Nchi hii ni yetu.

19 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **mwananchi, bendera, ndio, undugu, kulinda, tunayoipenda.**
Waulize wanafunzi wanachoweza kutambua kuhusu maneno haya.
**U:** Maneno haya yana sauti **mw** au **nd**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **Mwanachi** na **benedera.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.
**N/T/U: mwananchi, bendera**
**U: undugu, kulinda, tunayoipenda**
**U:** Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 19.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** [Nani anakumbuka nini tulichosoma wakati uliopita? Tulisoma kuhusu **Rangi za Bendera.**]
**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

### Masimulizi - Kuhariri

**U:** [Leo tutaendelea kuzingatia nakala zetu ili kuhakikisha kuwa ziko sahihi. Ili kusahihisha kazi yetu, lazima turejelee na kukosoa nakala ya kwanza. Itazame nakala yako na uangalie ikiwa ina maneno ambayo hayajaendelezwa vizuri au yana makosa ya tahajia. Kama hujui kuendeleza neno fulani muulize mwenzako kwanza akusaidie na iwapo hajui inua mkono wako ili nije nikuelekeze. Ukishamaliza kusahihisha na kurekebisha kazi yako, iandike kwenye ukurasa mpya bila makosa. Kisha umpe mwenzako aisome tena na aamue kama ni sawa na tayari kuchapishwa au kusomwa na wengine.]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora mchoro wa bendera ya Kenya na uupake rangi.
Mwimbie mlezi wako ubeti wa kwanza wa wimbo wa taifa.

## Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji

Kushiriki katika uskauti na kupandisha bendera shuleni.

## Mapendekezo ya Shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji

Shiriki katika kuimba nyimbo zinazokuza uzalendo katika sherehe mbalimbali.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 20: Uzalendo 1

Kipindi cha 20 **Uzalendo 1**

**Tathmini ya msamiati**

**Ambatanisha maelezo ya sentensi na neno sahihi.**

| | |
|---|---|
| 1. Eneo la ardhi lenye mipaka. Kwa mfano, Kenya. | Amani |
| 2. Hali ya ukakamavu. | Nchi |
| 3. Hali ya kutokuwepo na vita. | Bendera |
| 4. Kitambaa chenye rangi kinachotambulisha nchi. | Imara |

**Tathmini ya Sarufi – Vimilikishi**

**Unganisha maneno na kimilikishi sahihi kutunga sentensi.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mwalimu | wake | kwa nchi ya Kenya unajulikana. |
| 2. Vitabu | vyake | inapendeza sana. |
| 3. Nchi | | viko chini ya meza. |
| 4. Upendo | yetu | hufunza somo la hesabu. |

**Hadithi ya mwalimu**

**Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.**

Bi. Wivu na Mwanawe



Mali ya Serikali ya Kenya 20

**Bi. Wivu na Mwanawe**

Mzee Jana alikuwa na wake wawili na watoto wawili. Alikuwepo Bi. Tumaini na mwanawe Bahati na Bi. Wivu na mwanawe Tamaa. Shamba la familia lilikuwa kando ya mto karibu na msitu. Walilima na kupanda mbegu za mimea mbalimbali. Walitia mbolea na kuufanya udongo uwe na rotuba. Walipata mavuno mengi.

Siku moja Bahati alitengeneza zumari ya kipekee. Alipoicheza, watu walishangilia na kumzawadia. Bi. Wivu alimwamuru Tamaa, "Tengeneza zumari uicheze kama mwenzako Bahati." Tamaa alitengeneza zumari, lakini haikupendeza alipoicheza.

Siku ya Jumamosi Bahati aliisahau zumari shambani. Aliomba ruhusa akaichukue. Mtoni alikutana na Bi. Kizee aliyesema, "Mjukuu wangu, njoo unitekee maji." Bahati alimchotea maji. Baada ya kunywa akasema, "Joto limepungua. Wewe ni mkarimu na mwenye heshima. Shika zumari nzuri zaidi, kacheze ujionee." Bahati alimshukuru. Nyumbani, alicheza zumari mbele ya familia. Zumari ilitoa mavazi yaliyometameta kama nyota na chakula kitamu. Walifurahia sana.

"Jidai umeisahau zumari shambani ili uende ukailete bora zaidi.'' Bi. Wivu aliamwamrisha Tamaa. Tamaa alitii na kuondoka. Alipokuwa katikati ya mto, Bi. Kizee akatokea na kusema, "Mjukuu wangu ninahisi njaa, nitundie tunda." Tamaa alikataa na kupita. Aliporudi Bi. Kizee alisema, "Umerudi? Shika zumari, kacheze ujionee." Tamaa hakushukuru. Mamake aliita kijiji chote kichezewe zumari. Tamaa alipoicheza zumari ilimchapa makofi. Akakasirika na kuitupa nyuma ya jaa.

## Kusoma Maneno

**U:** Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.
Maneno: **ndio, undugu, kulinda, tunayoipenda, imara, nchi, taifa**

## Hadithi ya Mwalimu

**Kabla ya kusoma**

**T:** [Leo mtasikiliza kwa makini nikiwasomea hadithi kisha baadaye tuizungumzie hadithi hiyo huku tukiandika. Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi kisha tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma hadithi, kuna baadhi ya maneno mapya ambayo tutazungumzia kwanza. Neno la kwanza ni **tumaini**. Neno hili humaanisha kuwa na imani kupata au kufanikiwa au kufanya vizuri katika jambo (*Rudia hatua hii na maneno* ***tamaa, wivu, zumari****)*.]

**Wakati wa kusoma**

**T:** [Sasa sikiliza kwa makini ninaposoma. Sikiliza na utambue maneno mapya. Inua mkono wako wa kushoto utakaposikia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia ukisikia neno la pili (*Soma hadithi kwa ufasaha. Sitisha unapofikia tukio la kufurahisha. Uliza wanafunzi ni kitu gani ambacho kinaweza kutokea.)*]

**Baada ya kusoma**

**T:** [Sasa tuzungumze kuhusu hadithi (*uliza maswali yafuatayo):*

1. Je, hadithi hii ilifanyika wapi na wakati gani?
2. Wahusika ni akina nani?
3. *(Waelekeze wanafunzi kusimulia hadithi tena)*. Nini kilitendeka mwanzoni mwa hadithi. Nini kilitendeka baadaye? Nini kilitendeka mwishoni?
4. Je, unakubaliana na ushauri wa Bi. Wivu kwa mwanawe Tamaa?]

**T:** [Hebu tuandike baadhi ya mambo tuliyosoma kwenye hadithi. Ikiwa hii hadithi ingeendelea unafikiria ni nini kingefanyika?]

## Sarufi: Vimilikishi –ake, –ao, na -etu

**N:** Vimilikishi ni maneno yanayotueleza kitu ni cha nani.
**U:** Wanafunzi waunganishe maneno na kimilikishi kutunga sentensi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Mwambie mwenzako ubeti wa kwanza wa wimbo wa taifa.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ______________


Kipindi cha 21 na 22 Miezi ya Mwaka 1

Shairi

Miezi ya Mwaka

Januari Februari Machi Aprili Mei Juni
Julai Agosti Septemba Oktoba Novemba Desemba


Mnamo mosi Januari, twasherehekea mwaka mpya,
Mwezi wa pili Februari, twasonga mambo mapya,
Machi mwezi wa tatu, mashamba kutayarishwa,
Hakika mwaka mmoja, miezi kumi na miwili.

Aprili mwezi wa nne, likizo njema pumzika,
Mei mwezi wa tano, tarehe ya Leba Dei,
Juni mwezi wa sita, siku mosi Madaraka,
Hakika mwaka mmoja, miezi kumi na miwili.

Julai mwezi wa saba, baridi kali nchini,
Agosti mwezi wa nane, ngano huvunwa shambani,
Septemba mwezi wa tisa, tamati twakaribia,
Hakika mwaka mmoja, miezi kumi na miwili.

Oktoba mwezi wa kumi, sherehe ya Mashujaa,
Novemba kumi na moja, mt hani hufanyika,
Desemba kumi na mbili, sherehe ya Jamhuri,
Hakika mwaka mmoja, miezi kumi na miwili.

21 Hakiuzwi


Kipindi cha 21 na 22 Miezi ya Mwaka 1

Msamiati
Soma maneno haya.
likizo mashujaa sherehe

Kusoma maneno
Soma maneno haya.
shangwe ngano njema upweke

Ufahamu
Jibu maswali yafuatayo.
1. Taja kichwa mwafaka cha shairi.
2. Tunaelezwa nini mwanzoni mwa shairi?
3. Je, ni jambo lipi linalofanyika mwezi wa Aprili?
4. Shairi hili linatufunza nini?

Sarufi: Matumizi ya kikomo (.)
Akifisha sentensi hizi ifaavyo kwa kutumia alama ya kikomo.
1. Alinipa kitabu chake
2. Ngamia anaishi jangwani
3. Mnunuzi alinunua njugu na ngano
4. Kunguru ni ndege mwoga
5. Mwezi wa Julai una baridi kali

Mali ya Serikali ya Kenya 22

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha.
Andika neno **likizo** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuoyesha maana.
3. Waulize wanafunzi waelezee wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno.

Rudia zoezi na maneno haya: **mashujaa, sherehe**
**N:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 22.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** Soma kichwa cha shairi na wanafunzi. Jadili picha. waulize wanafunzi watoe utabiri.
**T/U:** Soma shairi.
**N:** Hakiki utabiri.

## ? Ufahamu

### Maswali

1. **N:** Taja kichwa mwafaka cha shairi. (Miezi ya mwaka)
2. **T:** Tunaelezwa nini mwanzoni mwa shairi? (Mwanzoni twasherehekea mwaka mpya na kutayarisha mashamba)
3. **U:** Je, ni jambo lipi linalofanyika mwezi wa Aprili? (Aprili ni wakati wa likizo)
4. **U:** Shairi hili linatufunza nini? (Matukio mbalimbali katika miezi ya mwaka)

## Sarufi: Kikomo

**N:** Kikomo ni alama ya kuakifisha inayoonyesha mwisho wa sentensi.
**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye vikomo kutoka kwenye shairi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.
**U:** Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi zenye vikomo.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Jaza mapengo yafuatayo kwa jibu sahihi.

1. Sherehe ya Leba Dei hufanyika mwezi wa __________ (Juni, Mei).
2. Siku ya Mashujaa husherehekewa mwezi wa_________ (Januari, Oktoba).
3. Kulingana na shairi, mvua hunyesha mwezi wa__________(Februari, Machi).
4. Baridi kali huwa mwezi wa___________(Julai, Januari).

### Majibu

1. Mei
2. Oktoba
3. Machi
4. Julai

Tarehe: ____________________________ Muda: ____________________ Idadi: __________________

# Kipindi cha 22: Miezi ya Mwaka 1


Kipindi cha 21 na 22 **Miezi ya Mwaka 1**

Shairi

**Miezi ya Mwaka**




Mnamo mosi Januari, twasherehekea mwaka mpya,
Mwezi wa pili Februari, twasonga mambo mapya,
Machi mwezi wa tatu, mashamba kutayarishwa,
Hakika mwaka mmoja, miezi kumi na miwili.

Aprili mwezi wa nne, likizo njema pumzika,
Mei mwezi wa tano, tarehe ya Leba Dei,
Juni mwezi wa sita, siku mosi Madaraka,
Hakika mwaka mmoja, miezi kumi na miwili.

Julai mwezi wa saba, baridi kali nchini,
Agosti mwezi wa nane, ngano huvunwa shambani,
Septemba mwezi wa tisa, tamati twakaribia,
Hakika mwaka mmoja, miezi kumi na miwili.

Oktoba mwezi wa kumi, sherehe ya Mashujaa,
Novemba kumi na moja, mt hani hufanyika,
Desemba kumi na mbili, sherehe ya Jamhuri,
Hakika mwaka mmoja, miezi kumi na miwili.

21 Hakiuzwi


Kipindi cha 21 na 22 **Miezi ya Mwaka 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

likizo mashujaa sherehe

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

shangwe ngano njema upweke

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa mwafaka cha shairi.
2. Tunaelezwa nini mwanzoni mwa shairi?
3. Je, ni jambo lipi linalofanyika mwezi wa Aprili?
4. Shairi hili linatufunza nini?

Sarufi: Matumizi ya kikomo (.)

**Akifisha sentensi hizi ifaavyo kwa kutumia alama ya kikomo.**

1. Alinipa kitabu chake
2. Ngamia anaishi jangwani
3. Mnunuzi alinunua njugu na ngano
4. Kunguru ni ndege mwoga
5. Mwezi wa Julai una baridi kali

Mali ya Serikali ya Kenya 22

## Kusoma Maneno

T: Andika maneno haya ubaoni: **shangwe, ngano, ugonjwa, pwaguzi**Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.
N: Maneno haya yana sauti **sh, nj, pw,** na **ng.** Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **shangwe, njema, ngano na upweke.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini konyesha sauti na silabi husika.
**N/T/U: shangwe, njema**
**U: ugonjwa, pwaguzi**
**U:** Wanafunzi wasome maneno kwenye **ukurasa wa 22.**

## Kusoma Matini: Shairi

**N:** [Nani anakumbuka nini tulijifunza wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **Miezi ya Mwaka.**]
**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi - Kikomo

**N:** [Kikomo ni alama ya kuakifisha inayoonyesha mwisho wa sentensi.Leo tutarejelea sentensi zenye makosa ya kisarufi.
Hebu tusome sentensi ya kwanza (*Mwalimu na wanafunzi wasome sentensi.)*
Naona sentensi hii ina makosa. Mwishoni mwake hakuna kikomo. Sasa sentensi itakuwa (*Mwalimu aandike sentensi sahihi na kuisoma*). **Alinipa kitabu chake.**]
**T:** [Sasa tujaribu sentensi nyingine pamoja. Soma sentensi ya pili. Je, makosa yako wapi? Je, tutaikosoa vipi sentensi hii. (R*udia na sentensi zingine. Kubali majibu sahihi.)*]

**Majibu**
Waelekeze kuakifisha sentensi hizi ifaavyo.

1. Alinipa kitabu chake.
2. Ngamia anaishi jangwani.
3. Mnunuzi alinunua njugu na ngano.
4. Kunguru ni ndege mwoga.
5. Mwezi wa Julai wa baradi kali.

## Kuandika

**Masimulizi - Kuchapisha**
**T:** [Wiki hii tutachapisha kazi ambayo tumekuwa tukiandika. Kazi ya uandishi ikichapishwa huwekwa kwenye vitabu, magazeti au kwenye majarida tofauti ili kusomwa na watu. Lakini sisi tutachapisha kazi yetu kwa kuisoma huku rafiki zetu wakitusikiliza hapa darasani. Iwapo hutakuwa ukisoma, utasikiliza wakati wenzako wanasoma na kutambua jambo moja ambalo litakufurahisha kwenye hadithi. Aidha ni kuhusu mhusika au jinsi ambavyo neno limetumiwa. Tutashiriki somo hili sisi sote. (*Wanafunzi 2-3 wasimame na kuwasomea wenzao walichoandika, mmoja baada ya mwingine. Waulize wanafunzi 2-3 washiriki somo kwa kusema jambo moja au mhusika waliyemchangamkia kwenye hadithi.)*]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi kuhusu miezi wa mwaka.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 23: Miezi ya Mwaka 1

Kipindi cha 23 na 24 **Miezi ya Mwaka 1**

Matini

**Mwaka Mmoja Hakika**



Hodi hodi tunabisha, jamani ni mwanzo mpya,
Mwezi wa pili wa mwaka, Februari kiangazi,
Machi mwezi wa tatu, mawingu hutanda kote,
Kumi na mbili miezi, mwaka mmoja hakika.

Likizo hufurahisha, Aprili ziarani,
Pwani huvutia sana, kumwona pweza na nguru,
Mei ni mwezi wa tano, mvua huendelea,
Kumi na mbili miezi,mwaka mmoja hakika.

Juni mwezi wa sita, ni katikati ya mwaka,
Moja mbili hadi saba, Julai mwezi wa saba,
Mwalimu husisitiza, Agosti mwezi wa nane,
Kumi na mbili miezi, mwaka mmoja hakika.

Septemba ni mwezi wa tisa, bidii kwa wanafunzi,
Oktoba na Novemba, ni mitihani jamani,
Desemba mwezi wa mwisho, likizo njema kwa watu,
Kumi na mbili miezi, mwaka mmoja hakika.

23 Hakiuzwi

Kipindi cha 23 na 24 **Miezi ya Mwaka 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kiangazi hutanda ziarani

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kiangazi mawingu pweza kipupwe

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha shairi hili.
2. Taja miezi mitano ya mwisho ya mwaka.
3. Wanafunzi huenda likizo miezi ipi?
4. Je, wewe husherehekea siku ya kuzaliwa kwako mwezi upi?

Sarufi: Matumizi ya kikomo

**Tumia kikomo kuakifisha sentensi hizi baada ya kuziandika kwenye daftari lako.**

1. Mwanamuziki alipiga ngoma vizuri
2. Pweza ni samaki anayepatikana baharini
3. Mwalimu wetu alitutakia njozi njema
4. Mama atanunua unga wa ngano
5. Mwanafunzi alihisi njaa adhuhuri

Kuandika

**Andika sentensi nne kuhusu miezi ya mwaka.**

Mali ya Serikali ya Kenya 24

## Msamiati

Jadili picha. Andika neno **kiangazi** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kiangazi kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi waelezee wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno. Rudia zoezi na maneno haya: **hutanda, ziarani**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **kiangazi.**]

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 24.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** Soma kichwa cha shairi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma shairi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

### Maswali

1. **N:** Taja kichwa cha shairi hili. (Mwaka mmoja hakika)
2. **T:** Taja miezi mitano ya mwisho ya mwaka. (Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba na Desemba)
3. **U:** Wanafunzi huenda likizo miezi ipi? (Aprili, Agosti na Desemba)
4. **U:** Je, wewe husherehekea siku ya kuzaliwa kwako mwezi upi? (Kubali jibu sahihi)

## Sarufi: Kikomo

**N:** Kikomo ni alama ya kuakifisha inayoonyesha mwisho wa sentensi.

**T:** Waonyeshe wanafunzi kutumia kikomo kuafikisha sentensi ya kuanza.

**U:** Waelekeze wanafunzi watunge sentensi wakitumia vikomo.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika kwa maneno

1. Ngiri 100 (Ngiri mia moja)
2. Miti 91 (Miti tisini na moja)
3. Machungwa 69 (Machungwa sitini na tisa)
4. Ngoma 58 (Ngoma hamsini na nane)
5. Ngamia 74 (Ngamia sabini na wanne)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 23 na 24 **Miezi ya Mwaka 1**

Matini

**Mwaka Mmoja Hakika**




Hodi hodi tunabisha, jamani ni mwanzo mpya,
Mwezi wa pili wa mwaka, Februari kiangazi,
Machi mwezi wa tatu, mawingu hutanda kote,
Kumi na mbili miezi, mwaka mmoja hakika.

Likizo hufurahisha, Aprili ziarani,
Pwani huvutia sana, kumwona pweza na nguru,
Mei ni mwezi wa tano, mvua huendelea,
Kumi na mbili miezi,mwaka mmoja hakika.

Juni mwezi wa sita, ni katikati ya mwaka,
Moja mbili hadi saba, Julai mwezi wa saba,
Mwalimu husisitiza, Agosti mwezi wa nane,
Kumi na mbili miezi, mwaka mmoja hakika.

Septemba ni mwezi wa tisa, bidii kwa wanafunzi,
Oktoba na Novemba, ni mitihani jamani,
Desemba mwezi wa mwisho, likizo njema kwa watu,
Kumi na mbili miezi, mwaka mmoja hakika.

23 Hakiuzwi

Kipindi cha 23 na 24 **Miezi ya Mwaka 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kiangazi hutanda ziarani

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kiangazi mawingu pweza kipupwe

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha shairi hili.
2. Taja miezi mitano ya mwisho ya mwaka.
3. Wanafunzi huenda likizo miezi ipi?
4. Je, wewe husherehekea siku ya kuzaliwa kwako mwezi upi?

Sarufi: Matumizi ya kikomo

**Tumia kikomo kuakifisha sentensi hizi baada ya kuziandika kwenye daftari lako.**

1. Mwanamuziki alipiga ngoma vizuri
2. Pweza ni samaki anayepatikana baharini
3. Mwalimu wetu alitutakia njozi njema
4. Mama atanunua unga wa ngano
5. Mwanafunzi alihisi njaa adhuhuri

Kuandika

**Andika sentensi nne kuhusu miezi ya mwaka.**

Mali ya Serikali ya Kenya 24

## Kusoma Maneno

**N:** Andika maneno haya ubaoni: **kiangazi, mawingu, nguru, njema, pwani**

**T:** Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.

**T:** Maneno haya yana sauti **ng, nj,** na, **pw**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **kiangazi/njema/pwani.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: kiangazi, njema, pwani**

**U: nguru, mawingu**

**U:** Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 24.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** [Nani anakumbuka tulichojifunza wakati uliopita. Tulijifunza kuhusu **Mwaka Mmoja Hakika.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

### Masimulizi - Kuchapisha

**T:** [Hii wiki tutachapisha kazi ambayo tumekuwa tukiandika. Kazi ya uandishi ikichapishwa huwekwa kwenye vitabu, magazetini au kwenye majarida tofauti ilikusomwa na watu. Lakini sisi tutachapisha kazi yetu kwa kuisoma huku rafiki zetu wakitusikiliza hapa darasani. Iwapo hutakuwa ukisoma, utasikiliza wakati wenzako wanasoma na kutambua jambo moja ambalo litakufurahisha kwenye hadithi. Aidha ni kuhusu mhusika au jinsi ambavyo neno limetumiwa. Tutashiriki somo hili sisi sote. (*Wanafunzi 2-3 wasimame na kuwasomea wenzao walichoandika mmoja baada ya mwingine. Waulize wanafunzi 2-3 washiriki somo kwa kusema jambo moja au mhusika waliyemchangamkia sana kwenye hadithi.*)]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tumia kikomo kuakifisha sentensi hizi.

1. Agosti ni mwezi wa nane wa mwaka
2. wanafunzi wote walifika shuleni haraka
3. Baba anapenda kusoma gazeti
4. Darasa letu lina wanafunzi hamsini na sita

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

| Kipindi cha | 25 | Miezi ya Mwaka 1 |
|---|---|---|

**Tathmini ya msamiati**

**Ambatanisha maelezo na neno.**

| Maelezo | Neno |
|---|---|
| 1. Wakati wa mapumziko. | sherehe |
| 2. Shughuli za kufurahia jambo. | likizo |
| 3. Safari rasmi ya kwenda mahali. | kiangazi |
| 4. Wakati wa jua kali bila mvua. | ziara |

**Tathmini ya sarufi**

**Tumia kikomo kuakifisha sentensi hizi.**

1. Agosti ni mwezi wa nane wa mwaka
2. Wanafunzi wote walifika shuleni mapema
3. Baba anapenda kusoma gazeti
4. Darasa letu lina wanafunzi hamsini na sita

25 Hakizwi

## Msamiati

Tazama **ukurasa wa 25**.
Ambatanisha maelezo na neno.
**Majibu**

1. likizo
2. sherehe
3. ziara
4. kiangazi

## Kusoma Maneno

**T:** Soma maneno haya mara mbili polepole huku wanafunzi wakiyaandika.
Maneno: **kiangazi, mawingu, nguru, njema, pweza, kipupwe, shangwe, ngano, upweke, pwani**

## Kuchambua Matini: Muktadha

**N:** [Je, muktadha ni nini? Muktadha ni mahali ambapo hadithi au shairi linafanyika.]
**T:** Waulize wanafunzi kusema walichosoma wiki iliyopita. Eleza mahali ambapo shairi linafanyika.
**T:** Andika sentensi 1 au 2 kuhusu muktadha.
**U:** [Ni zamu yako, tazama shairi la pili pamoja na mwenzako **ukurasa wa 23.** Tambua muktadha katika shairi na uiandike sentensi moja au mbili kuhusu muktadha.]

## Sarufi: Kikomo

**U:** [Nani anakumbuka sarufi tuliyojifunza wiki hii? Sarufi tuliyojifunza ilikuwa kikomo. Kikomo ni alama ya kuafikisha inayoonyesha mwisho wa sentensi.
Fungua kitabu chako **ukurasa wa 25** sehemu ya sarufi. Akifisha sentensi hizo na uziandike kwenye daftari lako.]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Ambatanisha mwezi na nambari:

| | |
|---|---|
| Desemba | 3 |
| Julai | 9 |
| Machi | 12 |
| Septemba | 7 |

**Majibu**

| | |
|---|---|
| Desemba | 3 |
| Julai | 9 |
| Machi | 12 |
| Septemba | 7 |

Desemba – 12, Julai – 7, Machi – 3, Septemba – 9

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 26 na 27 **Kazi mbalimbali 1**

**Matini**

**Shule yangu**



Shule yangu inaitwa Bondeni. Ina madarasa manane na wanafunzi mia tano hamsini. Walimu wetu ni tisa. Walimu hawa hufanya kazi ya ualimu yaani, kufundisha wanafunzi. Mwalimu Mkuu ni Bwana Juma Mokaya.Yeye ndiye msimamizi mkuu wa shule. Bi. Chebet ni Naibu wa Mwalimu Mkuu. Yeye humsaidia Mwalimu Mkuu kusimamia shule hasa katika upande wa nidhamu. Bi. Chebet pia ni mwalimu wa darasa letu. Yeye hapendi wanafunzi wanaorandaranda ovyo darasani.

Kiranja wa darasa letu anaitwa Zafani Mwongera. Yeye ni mwanafunzi mwenye bidii za mchwa na hufanya vyema darasani. Siku moja, wakati wa mvua hakuweza kubeba vitabu kumpelekea mwalimu. Ilimbidi mwalimu ampe mwavuli wake ili avipeleke vitabu hivyo kwenye majilisi. Zaidi ya hayo, Zafani humsaidia mwalimu kudumisha nidhamu darasani. Yeye pia humsaidia mkutubu kupanga vitabu maktabani. Kwenye maktaba kuna vitabu vipya vya hadithi tamutamu. Mimi na wenzangu tunapenda kuviazima vitabu hivyo na kuvisoma.

Langoni mwa shule yetu kuna bawabu. Jina la bawabu wetu ni Bwana Adamu. Kabla ya kufanya kazi ya ubawabu, Bwana Adamu alifanya kazi ya uaskari wa polisi.

Mali ya Serikali ya Kenya 26

Kipindi cha 26 na 27 **Kazi mbalimbali 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

ualimu Mwalimu Mkuu kiranja

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vipya vyema vyake vyote

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Jina la shule ya msimulizi wa hadithi hii ni ____________.
2. Jina la Naibu wa Mwalimu Mkuu ni ____________.
3. Kiranja humsaidia mwalimu kufanya nini?
4. Unafurahia kusoma vitabu vipi?

**Sarufi – Ukanusho wa nyakati**

**Tambua makosa ya kisarufi kisha ukanushe sentensi hizi.**

1. Kiranja alikusanya madaftari kesho.
2. Bawabu atawalinda wanafunzi jana.
3. Bawabu alilinda lango kesho.
4. Kiranja atapanga vitabu jana.

27 Hakiuzwi

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika neno **ualimu** ubaoni.

1. Uliza maana ya neno.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi waeleze wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno.

Rudia na maneno haya: **mwalimu mkuu, kiranja.**

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 27.**


## Kusoma Matini: Masimulizi

**T/U:** Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.
**T/U:** Soma hadithi.
**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Masimulizi**

Chora umbo la nyumba.




**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]
**N:** Simulia darasa lote hadithi.
**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Jina la shule ya msimulizi wa hadithi hii ni (Bandeni)
2. Jina la Naibu wa Mwalimu Mkuu ni (Bi Chebet)
3. Kiranja humsaidia mwalimu kufanya nini? (Kudumisha nidhamu darasani; kupelekea vitabu majilisini shule ya Bondeni.)
4. Unafurahia kusoma vitabu vipi? (Kubali jibu sahihi)

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

**N:** [Nyakati hurejelea wakati ambapo tukio fulani lilifanyika. Kwa mfano: wakati uliopo, wakati uliopita au wakati ujao. Wakati mwingine nyakati hizi hukanushwa.]
**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye nyakati kutoka kwenye hadithi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.
**U:** Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi zenye nyakati kwa kukanusha.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi sahihi ukitumia maneno haya.
1. bawabu 2. kiranja 3. Mwalimu Mkuu

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 26 na 27 **Kazi mbalimbali 1**

Matini

**Shule yangu**



Shule yangu inaitwa Bondeni. Ina madarasa manane na wanafunzi mia tano hamsini. Walimu wetu ni tisa. Walimu hawa hufanya kazi ya ualimu yaani, kufundisha wanafunzi. Mwalimu Mkuu ni Bwana Juma Mokaya.Yeye ndiye msimamizi mkuu wa shule. Bi. Chebet ni Naibu wa Mwalimu Mkuu. Yeye humsaidia Mwalimu Mkuu kusimamia shule hasa katika upande wa nidhamu. Bi. Chebet pia ni mwalimu wa darasa letu. Yeye hapendi wanafunzi wanaorandaranda ovyo darasani.

Kiranja wa darasa letu anaitwa Zafani Mwongera. Yeye ni mwanafunzi mwenye bidii za mchwa na hufanya vyema darasani. Siku moja, wakati wa mvua hakuweza kubeba vitabu kumpelekea mwalimu. Ilimbidi mwalimu ampe mwavuli wake ili avipeleke vitabu hivyo kwenye majilisi. Zaidi ya hayo, Zafani humsaidia mwalimu kudumisha nidhamu darasani. Yeye pia humsaidia mkutubu kupanga vitabu maktabani. Kwenye maktaba kuna vitabu vipya vya hadithi tamutamu. Mimi na wenzangu tunapenda kuviazima vitabu hivyo na kuvisoma.

Langoni mwa shule yetu kuna bawabu. Jina la bawabu wetu ni Bwana Adamu. Kabla ya kufanya kazi ya ubawabu, Bwana Adamu alifanya kazi ya uaskari wa polisi.

Mali ya Serikali ya Kenya 26

Kipindi cha 26 na 27 **Kazi mbalimbali 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

ualimu Mwalimu Mkuu kiranja

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

vipya vyema vyake vyote

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Jina la shule ya msimulizi wa hadithi hii ni ____________.
2. Jina la Naibu wa Mwalimu Mkuu ni ___________.
3. Kiranja humsaidia mwalimu kufanya nini?
4. Unafurahia kusoma vitabu vipi?

Sarufi – Ukanusho wa nyakati

**Tambua makosa ya kisarufi kisha ukanushe sentensi hizi.**

1. Kiranja alikusanya madaftari kesho.
2. Bawabu atawalinda wanafunzi jana.
3. Bawabu alilinda lango kesho.
4. Kiranja atapanga vitabu jana.

27 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **vipya, vyema, chovya, vyetu.** Waulize wanafunzi kile wanachoweza kutambua kuhusu maneno hayo

**N:** [Maneno haya yana sauti **vy**. *Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno:* ***vipya*** *na* ***vyema.*** *Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.*]

**N/T/U: vipya, vyema**

**U: chovya, vyetu**

**U:** Wanafunzi wasome maneno kwenye **ukurasa wa 27.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** [Nani anaweza kutukumbusha hadithi tuliyoyaisoma kuhusu **Shule yangu?**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

**T:** [Ukanusho wa nyakati hukana au huonyesha kuwa kitendo hakikufanyika wakati unaozungumziwa. Hebu tusome sentensi ya kwanza **ukurasa wa 27.** Naona sentensi hii ina makosa. **Kiranja alikusanya madaftari kesho** inafaa iwe **Kiranja atakusanya madaftari kesho.** Atakusanya madaftari kesho kwa sababu tunatumia **ta** kuonyesha wakati ujao.]

**T:** [Tutakanusha sentensi hii: Kiranja atakusanya madaftari kesho.Ukanusho wake ni: Kiranja hatakusanya madaftari kesho.]

**U:** [Sasa kanusha sentensi nyingine. *(Wasahihishe wakanushe sentenzi zilizosalia).*]

## Kuandika

**Shairi - Kupanga**

**T:** [Leo tutajifunza namna ya kuandika shairi. Je, kuna yeyote ambaye amewahi kutunga shairi? Mnaweza kukumbuka tofauti ya shairi na hadithi? Ili kuandika chochote ni lazima tupange kwanza.
Tutajifunza kuhusu shairi ambalo unaweza kutumia neno moja kuunda maneno ambayo utatungia shairi. Kwa mfano, kutumia neno **paka** unaweza kuunda maneno yafuatayo.

PAKA- Penzi Anapenda Kaka Analilia
Hebu sasa tupange shairi letu. Lazima tufikirie kuhusu neno ambalo tutalitumia kuunda maneno mengi tutakayotumia kutungia shairi letu.
Neno letu ni **FAMILIA.** Tutatumia kila herufi kuunda maneno yanayozungumzia familia. Tuanze na herufi **F.**
Neno gani linaanza na herufi F? (Fagia, fanya, familia)
A. Maneno gani tunaweza kuunda tukimia **A? (**Anapenda, Analilia, Anika)

Rudia hatua hizi hadi utumie herufi zote. *(Waongoze wanafunzi kuunda maneno kwa kutumia kila herufi.)*
Weka kazi yako ili tuitumie wiki ijayo.]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi na ukanushe.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 28 na 29 **Kazi mbalimbali 1**

**Matini**

**Siku ya Michezo**

Sote tulifika shuleni alfajiri na mapema siku hiyo. Ilikuwa ni siku ya riadha. Tulivalia sare zetu mpya za spoti. Mara tu kengele ikalia na tukaenda kwenye gwaride. Mwalimu Mkuu alituhutubia, kisha tukaenda uwanjani kuanza michezo. Baadhi ya wanafunzi walipiga ngoma na kupuliza vuvuzela kuwashangilia wenzao.



Mbio za mita mia moja ndizo zilizotangulia. Kiranja wetu alisema, "Wewe utaliwakilisha darasa letu." Kipenga kilipopulizwa, mimi nilichomoka kama risasi. Nikashinda mbio hizo. Wanafunzi wa darasa letu waliimba, "Nani kama sisi? Sisi tuko juu."

Shindano la pili lilikuwa la kurusha mkuki wa chuma. Ingawa nilikuwa nimechoka, wanafunzi waliniita na kunitia moyo. Mashindano yakaanza mara moja. Nilijaribu kwa bidii zangu zote. Kwa bahati mbaya sikushinda.

Siku hii haikukosa mikosi kwani mmoja wa washindani aliteleza na kuanguka chini. Mkono wake ukachubuka. Alipelekwa hospitalini kutibiwa. Baada ya kutibiwa na daktari alipelekwa katika wodi. Hapo nesi alimshughulikia vyema kwa kumpa dawa na kusafisha kidonda.

Michezo ilipokwisha, Naibu wa Mwalimu Mkuu alinituma ofisini mwake kuleta zawadi. Washindi walizawadiwa jinsi walivyofuatana na wakafurahi.

Mali ya Serikali ya Kenya 28

Kipindi cha 28 na 29 **Kazi mbalimbali 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

Naibu wa Mwalimu Mkuu nesi daktari

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vyakula mpya walivyofuatana vyema

**Kusimulia hadithi**

1. Mwanafunzi mmoja asimulie hadithi darasani.
2. Katika vikundi vya wanafunzi wawili, wanafunzi wawasimulie wenzao hadithi.

**Sarufi: Ukanusho wa nyakati**

**Tambua makosa ya kisarufi kisha ukanushe sentensi hizi.**

1. Jana nitaenda shambani asubuhi.
2. Kesho nilifua nguo zangu.
3. Jana nitacheza na rafiki yangu.
4. Leo nilifanya kazi ya ziada.

29 Hakiuzwi

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika **Naibu wa Mwalimu Mkuu** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia Naibu wa Mwalimu Mkuu kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuelezea wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno.

   Rudia na haya: **nesi, daktari.**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **Naibu wa Mwalimu Mkuu.**]

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 29.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Masimulizi**

Chora umbo la nyumba.




**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]

**N:** Simulia darasa lote hadithi.

**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

**T:** [Ukanusho wa nyakati hukana au huonyesha kuwa kitendo hakikufanyika wakati unaozungumziwa. Hebu turejelee sentensi **ukurasa wa 29** pamoja. **Jana nitaenda shambani asubuhi.** Je, unaona makosa yoyote kwenye sentensi hii? Ndio, inafaa iwe. **Jana nilienda shambani asubuhi.**]

**U:** [Tambua makosa ya kisarufi kwenye sentensi salia na usahihishe makosa hayo kisha uzikanushe.]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi kuhusu siku ya michezo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 28 na 29 **Kazi mbalimbali 1**

**Matini**

**Siku ya Michezo**

Sote tulifika shuleni alfajiri na mapema siku hiyo. Ilikuwa ni siku ya riadha. Tulivalia sare zetu mpya za spoti. Mara tu kengele ikalia na tukaenda kwenye gwaride. Mwalimu Mkuu alituhutubia, kisha tukaenda uwanjani kuanza michezo. Baadhi ya wanafunzi walipiga ngoma na kupuliza vuvuzela kuwashangilia wenzao.



Mbio za mita mia moja ndizo zilizotangulia. Kiranja wetu alisema, "Wewe utaliwakilisha darasa letu." Kipenga kilipopulizwa, mimi nilichomoka kama risasi. Nikashinda mbio hizo. Wanafunzi wa darasa letu waliimba, "Nani kama sisi? Sisi tuko juu."

Shindano la pili lilikuwa la kurusha mkuki wa chuma. Ingawa nilikuwa nimechoka, wanafunzi waliniita na kunitia moyo. Mashindano yakaanza mara moja. Nilijaribu kwa bidii zangu zote. Kwa bahati mbaya sikushinda.

Siku hii haikukosa mikosi kwani mmoja wa washindani aliteleza na kuanguka chini. Mkono wake ukachubuka. Alipelekwa hospitalini kutibiwa. Baada ya kutibiwa na daktari alipelekwa katika wodi. Hapo nesi alimshughulikia vyema kwa kumpa dawa na kusafisha kidonda.

Michezo ilipokwisha, Naibu wa Mwalimu Mkuu alinituma ofisini mwake kuleta zawadi. Washindi walizawadiwa jinsi walivyofuatana na wakafurahi.



Kipindi cha 28 na 29 **Kazi mbalimbali 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

Naibu wa Mwalimu Mkuu    nesi    daktari

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vyakula    mpya    walivyofuatana    vyema

**Kusimulia hadithi**

1. Mwanafunzi mmoja asimulie hadithi darasani.
2. Katika vikundi vya wanafunzi wawili, wanafunzi wawasimulie wenzao hadithi.

**Sarufi: Ukanusho wa nyakati**

**Tambua makosa ya kisarufi kisha ukanushe sentensi hizi.**

1. Jana nitaenda shambani asubuhi.
2. Kesho nilifua nguo zangu.
3. Jana nitacheza na rafiki yangu.
4. Leo nilifanya kazi ya ziada.



## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **mpya, vyakula, vipya, vyema, kipya.** Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya:

**N:** Maneno haya yana sauti **py** na **vy**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **mpya** na **vyakula.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: mpya, vyakula**

**U: vipya, vyema, kipya**

**U:** Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 29.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** [Nani anakumbuka tulichojifunza wakati uliopita. Tulisoma hadithi kuhusu **Siku ya Michezo.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Shairi - Kupanga**

**U:** [Leo ni zamu yako. Utapanga jinsi ya kuandika shairi. Ni nani anakumbuka shairi tulilopanga juzi? Shairi letu lilihusu kutumia herufi moja au neno kuunda maneno mengine. Tumia jina la mnyama umpendaye kupanga shairi lako. Andika maneno tofauti kwa kila herufi yatakayotoa maelezo au sifa za mnyama huyo. Juma lijalo tutaamua ni maneno gani tutakayoyatumia kunakili shairi letu.]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika kwa wakati ujao.**

1. Mwalimu alifundisha vizuri.(Mwalimu atafundisha vizuri.)
2. Alicheza akashinda zawadi. (Atacheza na atashinda zawadi.)
3. Wanafunzi wanacheza uwanjani. (Wanafunzi watacheza uwanjani.)
4. Bawabu analinda lango la shule. (Bawabu atalinda lango la shule.)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 30 | Kazi mbalimbali 1

Tathmini ya msamiati

**Chora vifaa kama vile mpira, firimbi, mkuki na neti ambavyo hutumika siku ya michezo.**

Tathmini ya sarufi

| | Nafsi ya Kwanza | Nafsi ya Pili | Nafsi ya Tatu |
|---|---|---|---|
| **Hali halisi** | Mimi nitapalilia bustani ya shule. | Wewe ___palilia bustani ya shule. | Yeye atapalilia bustani ya shule. |
| **Ukanusho** | Mimi _____palilia bustani ya shule. | Wewe hautapalilia bustani ya shule. | Yeye___palilia bustani ya shule. |

Mali ya Serikali ya Kenya

30

## Msamiati

Chora vifaa ambavyo hutumika wakati wa michezo.

## Kusoma Maneno

**U:** Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **vyakula, vipya, vyema, vyake, mpya, vyote, walivyofuatana, kipya, chovya, kompyuta.**

## Kuchambua Matini: Mhusika

**T:** [Je, mhusika katika hadithi ni nani?
Ndio, mhusika katika hadithi ni mtu au mnyama anayezungumziwa kwenye hadithi. Wiki hii tulisoma hadithi mbili. Je, hadithi hizi mbili zilihusu nini? *(Wanafunzi 2-3 kushiriki somo huku ukiwapa mwongozo.)* Leo tutarejelea hadithi tulizozisoma ili tupate wahusika katika hadithi. Hebu turejelee hadithi ya kwanza kwenye **ukurasa wa 26**. Wahusika ni akina nani?

**T:** [Ni mhusika gani aliyekupendeza na ni kwa nini amekupendeza? Hebu tuandike sentensi moja au mbili kuhusu wahusika tunaowapenda. *Andika yafuatayo huku ukizungumza kuhusu wahusika*. Wahusika katika hadithi hii ni msimulizi wa hadithi, mwalimu mkuu, kiranja na bawabu. Nampenda Mwalimu mkuu kwa sababu yeye husimamia shule.]

**U:** [Sasa ni zamu yako. Hebu tuitazame hadithi ya pili kwenye **ukurasa wa 28**. Je, wahusika ni akina nani? Sasa fanya uamuzi kwa kumchagua mhusika unaye mpenda na uandike sentensi moja au mbili kumhusu na sababu zako za kumpenda mhusika huyu.]

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

**U:** Ukanusho wa nyakati hukana au huonyesha kuwa kitendo hakikufanyika wakati unaozungumziwa. Fungua vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa** 30 na kujaza mapengo ifaavyo.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora vifaa ambavyo hutumika siku ya michezo.

### Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji.

Kusaidia wazazi katika kazi za nyumbani na katika jamii. Kuthamini kazi zinazofanywa na wazazi, ndugu na watu wengine katika jamii.

### Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji

Kushiriki katika kuigiza, kuimba nyimbo na kukariri mashairi katika tamasha mbalimbali.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Hakiuzwi

Kipindi cha 31 na 32 **Usalama 1**

**Matini**

**Nyumbani kwa Bi. Amina**



Bi. Amina aliishi katika kijiji cha Kisimani. Yeye na mume wake walikuwa na watoto watatu. Waliwafunza watoto wao maadili. Waliwafunza kufanya kazi na kutii wakubwa kwa wadogo. Bi. Amina aliwafunza kuwaamkua watu kwa heshima na kuwaaga wageni wanapoondoka kwao. Pia, aliwafunza kusali kila asubuhi walipoamka na jioni kabla ya kulala. Vilevile, aliwafunza watoto wake kufungua na kufunga madirisha na milango asubuhi wanapoamka. Hii ni kwa sababu ya kuruhusu hewa safi kuingia ndani ya nyumba.

Siku moja, Bi. Amina aliwaaga watoto wake na kuwatakia siku njema. Alienda kijijini kuhudhuria arusi. Alimwacha yaya nyumbani kuwalea watoto wake.

Yaya alimtamkia safari njema. Jioni moja, mtoto aliteleza na kuumia mguu kutokana na maji yaliyomwagika sakafuni. Mtoto alilia kwa uchungu. Yaya alimpa huduma ya kwanza kwa kutumia dawa kutoka kwenye kisanduku cha huduma ya kwanza. Kisanduku hiki huwa na vitu kama vile pamba, bandeji, dawa, makasi na spiriti. Yaya aliwakanya watoto wasimwage maji ovyoovyo. Aliwafunza jinsi ya kupangusa maji kila yanapomwagika chini. Yaya alihakikisha kuwa kuna usalama nyumbani. Hakuwaruhusu watoto wacheze jikoni. Hii ni kwa sababu wangeweza kupata ajali kwa kuchomeka.

Jioni, yaya aliyafunga madirisha na milango ili kuzuia wanyama na wezi kuingia nyumbani. Kabla ya kulala watoto walitakiana usiku mwema. Yaya hakuruhusiwa kumkaribisha mtu yeyote asiyemjua. Amri hii iliwalinda kutokana na walaghai. Bi. Amina aliporudi alifurahi kuipata familia yake ikiwa salama. Alimshukuru yaya kwa kazi nzuri aliyoifanya.

31 Hakiuzwi

Kipindi cha 31 na 32 **Usalama 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

usalama huduma ya kwanza walaghai

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

maadili madirisha anapenda kisanduku

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Bi. Amina aliwafunza watoto wake nini?
2. Ni vitu gani vinavyopatikana katika kisanduku cha huduma ya kwanza?
3. Bi. Amina alipokuwa akisafiri, yaya alimtakia nini?
4. Je, unaweza kumpa mwenzako huduma ya kwanza akitokwa na damu puani?

**Sarufi: Kinyume cha vitenzi**

**Andika kinyume cha maneno haya.**

| Kitendo | Kinyume |
|---|---|
| Mfano: enda | rudi |
| 1. lala | ____________ |
| 2. ____________ | cheka |
| 3. panga | __________ |
| 4. ______________ | simama |

Mali ya Serikali ya Kenya 32

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika neno: **usalama**

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno usalama kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuwaelezea wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno.

Rudia maneno haya: **huduma ya kwanza, walaghai**

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 32.**

## Kusoma Matini: Maimulizi

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Kusimulia Hadithi**

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]

**N:** Simulia darasa lote hadithi.

**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Bi. Amina aliwafunza watoto wake nini? (Kufanya kazi pamoja, kutii wakubwa kwa wadogo, kuomba kila asubuhi na jioni.)
2. Ni vitu gani vinavyopatikana katika kisanduku cha huduma ya kwanza? (Kubali jibu lolote sahihi.)
3. Bi. Amina alipokuwa akisafiri, yaya alimtakia nini? (Yaya alimtakia safari njema.)
4. Je, unaweza kumpa mwenzako huduma ya kwanza akitokwa na damu puani? (Kubali jibu lolote sahihi.)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 31 na 32 **Usalama 1**

**Matini**

### Nyumbani kwa Bi. Amina



Bi. Amina aliishi katika kijiji cha Kisimani. Yeye na mume wake walikuwa na watoto watatu. Waliwafunza watoto wao maadili. Waliwafunza kufanya kazi na kutii wakubwa kwa wadogo. Bi. Amina aliwafunza kuwaamkua watu kwa heshima na kuwaaga wageni wanapoondoka kwao. Pia, aliwafunza kusali kila asubuhi walipoamka na jioni kabla ya kulala. Vilevile, aliwafunza watoto wake kufungua na kufunga madirisha na milango asubuhi wanapoamka. Hii ni kwa sababu ya kuruhusu hewa safi kuingia ndani ya nyumba.

Siku moja, Bi. Amina aliwaaga watoto wake na kuwatakia siku njema. Alienda kijjini kuhudhuria arusi. Alimwacha yaya nyumbani kuwalea watoto wake.

Yaya alimtamkia safari njema. Jioni moja, mtoto aliteleza na kuumia mguu kutokana na maji yaliyomwagika sakafuni. Mtoto alilia kwa uchungu. Yaya alimpa huduma ya kwanza kwa kutumia dawa kutoka kwenye kisanduku cha huduma ya kwanza. Kisanduku hiki huwa na vitu kama vile pamba, bandeji, dawa, makasi na spiriti. Yaya aliwakanya watoto wasimwage maji ovyoovyo. Aliwafunza jinsi ya kupangusa maji kila yanapomwagika chini. Yaya alihakikisha kuwa kuna usalama nyumbani. Hakuwaruhusu watoto wacheze jikoni. Hii ni kwa sababu wangeweza kupata ajali kwa kuchomeka.

Jioni, yaya aliyafunga madirisha na milango ili kuzuia wanyama na wezi kuingia nyumbani. Kabla ya kulala watoto walitakiana usiku mwema. Yaya hakuruhusiwa kumkaribisha mtu yeyote asiyemjua. Amri hii iliwalinda kutokana na walaghai. Bi. Amina aliporudi alifurahi kuipata familia yake ikiwa salama. Alimshukuru yaya kwa kazi nzuri aliyoifanya.

31 Hakiuzwi

Kipindi cha 31 na 32 **Usalama 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

usalama huduma ya kwanza walaghai

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

maadili madirisha anapenda kisanduku

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Bi. Amina aliwafunza watoto wake nini?
2. Ni vitu gani vinavyopatikana katika kisanduku cha huduma ya kwanza?
3. Bi. Amina alipokuwa akisafiri, yaya alimtakia nini?
4. Je, unaweza kumpa mwenzako huduma ya kwanza akitokwa na damu puani?

**Sarufi: Kinyume cha vitenzi**

**Andika kinyume cha maneno haya.**

| Kitendo | Kinyume |
|---|---|
| **Mfano:** enda | rudi |
| 1. lala | ____________ |
| 2. ____________ | cheka |
| 3. panga | ____________ |
| 4. ____________ | simama |

Mali ya Serikali ya Kenya 32

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

**N:** Kinyume cha vitenzi ni neno au maneno yanayopinga mambo yalivyokuwa au yatakavyokuwa. Mifano ya maneno haya ni: funga; fungua; enda; rudi; lia; cheka.

**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi kwenye hadithi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.

**U:** Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi zenye kinyume cha vitenzi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Taja njia nne unazoweza kutumia kuzingatia usalama.

Andika kinyume cha maneno haya:

1. Fungua
2. Cheka
3. Keti
4. Lala
5. Rudi

Tarehe: ____________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

Kipindi cha 31 na 32 — **Usalama 1**

### Matini

**Nyumbani kwa Bi. Amina**



Bi. Amina aliishi katika kijiji cha Kisimani. Yeye na mume wake walikuwa na watoto watatu. Waliwafunza watoto wao maadili. Waliwafunza kufanya kazi na kutii wakubwa kwa wadogo. Bi. Amina aliwafunza kuwaamkua watu kwa heshima na kuwaaga wageni wanapoondoka kwao. Pia, aliwafunza kusali kila asubuhi walipoamka na jioni kabla ya kulala. Vilevile, aliwafunza watoto wake kufungua na kufunga madirisha na milango asubuhi wanapoamka. Hii ni kwa sababu ya kuruhusu hewa safi kuingia ndani ya nyumba.

Siku moja, Bi. Amina aliwaaga watoto wake na kuwatakia siku njema. Alienda kijijini kuhudhuria arusi. Alimwacha yaya nyumbani kuwalea watoto wake.

Yaya alimtamkia safari njema. Jioni moja, mtoto aliteleza na kuumia mguu kutokana na maji yaliyomwagika sakafuni. Mtoto alilia kwa uchungu. Yaya alimpa huduma ya kwanza kwa kutumia dawa kutoka kwenye kisanduku cha huduma ya kwanza. Kisanduku hiki huwa na vitu kama vile pamba, bandeji, dawa, makasi na spiriti. Yaya aliwakanya watoto wasimwage maji ovyoovyo. Aliwafunza jinsi ya kupangusa maji kila yanapomwagika chini. Yaya alihakikisha kuwa kuna usalama nyumbani. Hakuwaruhusu watoto wacheze jikoni. Hii ni kwa sababu wangeweza kupata ajali kwa kuchomeka.

Jioni, yaya aliyafunga madirisha na milango ili kuzuia wanyama na wezi kuingia nyumbani. Kabla ya kulala watoto walitakiana usiku mwema. Yaya hakuruhusiwa kumkaribisha mtu yeyote asiyemjua. Amri hii iliwalinda kutokana na walaghai. Bi. Amina aliporudi alifurahi kuipata familia yake ikiwa salama. Alimshukuru yaya kwa kazi nzuri aliyoifanya.

31 Hakiluzwi

Kipindi cha 31 na 32 — **Usalama 1**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

usalama huduma ya kwanza walaghai

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

maadili madirisha anapenda kisanduku

### Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Bi. Amina aliwafunza watoto wake nini?
2. Ni vitu gani vinavyopatikana katika kisanduku cha huduma ya kwanza?
3. Bi. Amina alipokuwa akisafiri, yaya alimtakia nini?
4. Je, unaweza kumpa mwenzako huduma ya kwanza akitokwa na damu puani?

### Sarufi: Kinyume cha vitenzi

**Andika kinyume cha maneno haya.**

| Kitendo | Kinyume |
|---|---|
| **Mfano:** enda | rudi |
| 1. lala | ____________ |
| 2. ____________ | cheka |
| 3. panga | ____________ |
| 4. ____________ | simama |

Mali ya Serikali ya Kenya 32

## Kusoma Maneno

T: Andika maneno haya ubaoni: **maadili, kisanduku, ndani, madirisha, bandeji.** Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.

N: Maneno haya yana sauti **nd** na **d**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **maadili** na **kisanduku.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: maadili, kisanduku**

**U: ndani, bendeji, madirisha**

U: Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 32.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

T: [Nani anaweza kutukumbusha habari tuliyoisoma ilihusu nini?]

U: Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

T: [Kinyume cha vitenzi ni neno au maneno yanayopinga. Leo tutaandika kinyume cha vitenzi. Tazama **ukurasa wa 32.** *(Toa mifano ya zoezi hili.)*]

U: [Sasa andika kinyume cha vitenzi vilivyosalia.]

**Majibu**

1. amka
2. lia
3. pangua
4. keti

## Kuandika

**Shairi - Nakala ya Kwanza**

N: Waonyeshe wanafunzi kazi mliyopanga wakati uliopita kisha uwaulize walikuwa wamepanga kuhusu nini.

T:Waelekeze wanafunzi jinsi ya kuandika utangulizi. Waongoze watunge sentensi ya kwanza itakayotoa maelezo kuhusu tukio la kwanza.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Nakili maneno haya mara tatu kisha uyasome.

1. usalama
2. huduma ya kwanza
3. walaghai
4. madirisha

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 33 na 34 **Usalama 1**

**Matini**

**Tuzingatie Usalama**



Familia ya Cherop iliishi jijini Nairobi. Akina Cherop walishirikiana na majirani zao kila wakati. Cherop alimsaidia mama yake kufanya kazi za nyumbani. Yeye alikuwa mtoto mtiifu aliyependa kufanya kazi.

Siku moja alipomaliza kazi, Cherop alitoka kwenda kwa rafiki yake Rehema. Mama yake alikuwa amemhimiza kufungua na kufunga lango kila wakati alipotoka. Aligeuka ili alifunge lango lile. Mara tu alishtukia ameshikwa mkono na mtu asiyemjua. Moyo wake ulidunda kwa kasi. Alijaribu kutoroka lakini hakuweza.

Alipoulizwa jina lake, Cherop alisita kujibu. Mtu huyo alimwamrisha arudi nyumbani kwao amfungulie mlango. Cherop alipiga mayowe. Kwa bahati nzuri, baba yake Rehema aliyekuwa ameenda kazini alirudi nyumbani mapema. Alimshika mtu huyo na kumhoji kabla ya kumpeleka katika kituo cha polisi. Baadaye, alimpeleka Cherop nyumbani kwao. Alimpongeza kwa ujasiri alioonyesha aliposhikwa na mtu yule mbaya. Alimhimiza aendelee kujihadhari na watu asiowajua. Alisisitiziwa umuhimu wa kuwajulisha watu wazima iwapo anataka kutoka nyumbani. Cherop aliahidi kuwa mtiifu na kufuata maagizo.

33 Hakiuzwi

Kipindi cha 33 na 34 **Usalama 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

amemhimiza mayowe kujihadhari

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

ulidunda aende punde baadaye

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Cherop alifanya nini akiwa nyumbani?
2. Cherop alishikwa mkono na nani?
3. Taja mambo mengine ambayo huhakikisha usalama nyumbani.
4. Hadithi hii inakufunza nini?

**Sarufi: Kinyume cha vitenzi**

**Ambatanisha kitenzi na kinyume chake.**

| Kitenzi | Kinyume |
|---|---|
| 1. funga | lia |
| 2. washa | rudi |
| 3. cheka | fungua |
| 4. enda | zima |

Mali ya Serikali ya Kenya 34

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika neno **amemhimiza** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno amemhimiza kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuwaelezea wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno. Rudia na haya: **mayowe, kujihadhari**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **amemhimiza.**]

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 34.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Kusimulia Hadithi**

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]

**N:** Simulia darasa lote hadithi.

**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Cherop alifanya nini akiwa nyumbani? ( Alimsaidia mama yake kufanya kazi.)
2. Cherop alishikwa mkono na nani? (Mtu asiyemjua.)
3. Taja mambo mengine yanayohakikisha usalama nyumbani. (Kubali jibu lolote sahihi.
4. Hadithi hii imekufunza nini? ( Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

**T/U:** Kinyume cha vitenzi ni neno au maneno yanayopinga. Hebu tuangalie vitendo zaidi na vinyume vyake. Ambatanisha kitenzi na kinyume chake.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi mbili kuhusu hadithi uliyoisoma.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 33 na 34 **Usalama 1**

Matini

**Tuzingatie Usalama**



Familia ya Cherop iliishi jijini Nairobi. Akina Cherop walishirikiana na majirani zao kila wakati. Cherop alimsaidia mama yake kufanya kazi za nyumbani. Yeye alikuwa mtoto mtiifu aliyependa kufanya kazi.

Siku moja alipomaliza kazi, Cherop alitoka kwenda kwa rafiki yake Rehema. Mama yake alikuwa amemhimiza kufungua na kufunga lango kila wakati alipotoka. Aligeuka ili alifunge lango lile. Mara tu alishtukia ameshikwa mkono na mtu asiyemjua. Moyo wake ulidunda kwa kasi. Alijaribu kutoroka lakini hakuweza.

Alipoulizwa jina lake, Cherop alisita kujibu. Mtu huyo alimwamrisha arudi nyumbani kwao amfungulie mlango. Cherop alipiga mayowe. Kwa bahati nzuri, baba yake Rehema aliyekuwa ameenda kazini alirudi nyumbani mapema. Alimshika mtu huyo na kumhoji kabla ya kumpeleka katika kituo cha polisi. Baadaye, alimpeleka Cherop nyumbani kwao. Alimpongeza kwa ujasiri alioonyesha aliposhikwa na mtu yule mbaya. Alimhimiza aendelee kujihadhari na watu asiowajua. Alisisitiziwa umuhimu wa kuwajulisha watu wazima iwapo anataka kutoka nyumbani. Cherop aliahidi kuwa mtiifu na kufuata maagizo.

33 Hakiuzwi

Kipindi cha 33 na 34 **Usalama 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

amemhimiza mayowe kujihadhari

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

ulidunda aende punde baadaye

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Cherop alifanya nini akiwa nyumbani?
2. Cherop alishikwa mkono na nani?
3. Taja mambo mengine ambayo huhakikisha usalama nyumbani.
4. Hadithi hii inakufunza nini?

Sarufi: Kinyume cha vitenzi

**Ambatanisha kitenzi na kinyume chake.**

| Kitenzi | Kinyume |
|---|---|
| 1. funga | lia |
| 2. washa | rudi |
| 3. cheka | fungua |
| 4. enda | zima |

Mali ya Serikali ya Kenya 34

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **ulidunda, waliahidi, aende, kwenda.**

Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.

**N:** Maneno haya yana sauti **nd** na **d**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **ulidunda** na **waliahidi.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: ulidunda, waliahidi**

**U: aende, kwenda**

**U:** Wanafunzi wasome maneno kwenye **ukurasa wa 34.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** [Ni nani anakumbuka nini tulichojifunza wakati uliopita? Tulisoma hadithi kuhusu **Tuzingatie Usalama.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

### Shairi - Nakala ya Kwanza

**T:** Waulize wanafunzi warejelee waliyopanga wakati uliopita.

**U:** Waulize wanafunzi waandike nakala pamoja na wenzao. Nakala iwe na angalau sentensi nne.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

**kisanduku, aende, punde, baadaye**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 35 **Usalama 1**

Imla

**Sikiliza maneno atakayosoma mwalimu, kisha uyaandike kwa usahihi.**

Tathmini ya Sarufi

**Jaza mapengo kwa kuandika kinyume cha kitendo kilicho kwenye mabano.**

1. Msichana ali __________ juu ya kiti. (simama)
2. Baba anapenda ku ______ panya. (tegua)
3. Yaya hu __________ mlango jioni. (fungua)
4. Maria hu ________ kitanda chake vizuri. (tandua)

Hadithi ya mwalimu

**Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.**

Zawadi ya Abrahamu



35 Hakiuzwi

**Zawadi ya Abrahamu**

Mama alimwita Abrahamu akisema, “Mwanangu, umefanya vyema shuleni muhula huu.” Akaendelea, “Nitakutuza zawadi.” “Asante, mama. Zawadi gani?” Abrahamu aliuliza kwa hamu na ghamu. “Usijali. Utaiona. Kesho rauka ufanye kazi zako, halafu tutaelekea sokoni,” Mama alimweleza. Abrahamu alipolala, alitamani usiku uishe haraka.

Keshoye, Abrahamu na mama walijiandaa na kuelekea kwenye kituo cha basi. Waliabiri na kusubiri kabla basi kung’oa nanga. Njiani usingizi ulimwiba Abrahamu, akalala. “Abrahamu, amka!” Mama alimwamsha walipofika sokoni.

Sokoni kulikuwa na wachuuzi waliouza bidhaa mbalimbali. Abrahamu alisongea kutazama miwani iliyokuwa karibu. Akaivaa. Mchuuzi alimsongezea kioo ili ajitazame. Aliibadilisha miwani hii na ile hadi akapata iliyomfaa ya rangi nyekundu.

“Mama! Ninunulie miwani hii!” Aliita. Lahaula! Hakumuona mama. Hofu ilimjaa. Alibabaika na kumtafuta huku na kule. Alilia kwi! Kwi! Msamaria mwema alimuuliza, “Mbona unalia?” Abrahamu alimwambia kuwa hamwoni mamake. Msamaria mwema alimpeleka Abrahamu sehemu salama ambayo watoto waliwekwa walipopotea sokoni.

“Mama atanipata vipi?” Abrahamu aliuliza kwa hofu. “Usijali. Tutatangaza.” Mara kipaza sauti kilisikika, “Tangazo! Tangazo! Kuna mtoto wa miaka tisa hivi ambaye amempoteza mamake. Popote ulipo mama, fika kwenye kibanda nambari 999.”

Ghafla bin vuu, Abrahamu alisikia sauti ya mama, “Nimekuja kumchukua mwanangu.” “Mwanao anaitwaje,” Mlinzi alimuuliza. “Abrahamu,” Mama alijibu haraka. “Naam, unamjua mama huyu?” Mlinzi alimuuliza Abrahamu. “Ndiyo,” aliitikia. Abrahamu alimkumbatia mama. Machozi ya furaha yalimtiririka. Mama alimtuliza. Alimwonyesha zawadi aliyomnunulia.

## Kusoma Maneno

**U:** Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **ulidunda, aende, punde, baadaye, madirisha, kisanduku, maadili, anapenda, mdundo, mdundiko**

## Hadithi ya Mwalimu

**Kabla ya kusoma**

**T:** [Leo mtasikiliza kwa makini nikiwasomea hadithi kisha baadaye tulizungumzie hadithi hiyo tukiandika. Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi kisha tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma hadithi, kuna baadhi ya maneno mapya ambayo tutazungumzia kwanza. Neno la kwanza ni **nitakutuza**. Neno hili humaanisha kumpa mtu zawadi baada ya kufanya vizuri *(Rudia hatua hii na maneno: **mchuuzi, msamaria mwema, waliabiri**.)*]

**Wakati wa kusoma**

**T:** [Sasa sikiliza kwa makini ninaposoma. Sikiliza na utambue maneno mapya. Inua mkono wako wa kushoto utakaposikia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia ukisikia neno la pili. *(Soma hadithi kwa ufasaha. Uliza wanafunzi ni kitu gani ambacho kinaweza kutokea)*]

**Baada ya hadithi**

**T:** [Sasa tuzungumzie hadithi. *(Uliza maswali yafuatayo.)*

1. Je, hadithi hii ilifanyika wapi na wakati gani?
2. Ungependa Abrahamu apewe zawadi ya aina gani?
3. Abrahamu alisaidiwaje alipomkosa mama yake?]

[Hebu tuandike baadhi ya mambo tuliyoyasoma kwenye hadithi.]

**Amua:** Je, unafikiri mama alifanya vizuri kunizawadia Abrahamu? Andika sentensi 1-2 kueleza uamuzi wako.

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

**U:** Sarufi tuliyojifunza ni kinyume cha vitenzi. Tazama **ukurasa wa 35**. Jaza mapengo kwa kuandika kinyume cha kitendo kilicho kwenye mabano.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi moja ukitumia neno mchuuzi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 36: Usafi wa Mazingira 1

Kipindi cha 36 na 37 **Usafi wa Mazingira 1**

Matini

**Mazingira ya Binadamu**



Mazingira ya binadamu ni muhimu kwa maisha yake. Mazingira haya yanajumuisha ndege, miti, misitu, wanyama, maji, nyumba na hata binadamu wengine. Ni muhimu kuyatunza na kuyathamini mazingira ili kulinda afya.

Kwanza, mtu anafaa kuanza kwa usafi wa mwili wake. Ili kuimarisha usafi wa mwili, mtu anapaswa kuoga, kuvaa nguo safi, kukata kucha na kuchana nywele.

Usafi wa nyumba pia ni muhimu. Nyasi karibu na nyumba lazima zikatwe ili mbu wasipate makao. Taka zote ziwekwe katika pipa la taka lililotengewa maalum. Choo pia kiwe safi. Ufagio wa chooni ni vyema ubaki chooni na usitumiwe kufagia nyumba.

Ni muhimu chemichemi za maji zihifadhiwe na maji yasichafuliwe. Isitoshe, mifereji ya maji taka haifai kuelekezwa mitoni. Kila pahali, taka zinafaa ziokotwe na kuzolewa kila siku haraka iwezekanavyo.

Usafi wa mazingira ukidumishwa, magonjwa yatapungua na taifa litakuwa na watu wenye afya. Watu wenye afya hufanya kazi kwa bidii. Usafi wa mazingira ni kinga dhidi ya maradhi na umaskini. Mazingira machafu hueneza maradhi ambayo tiba huwa polepole na ya gharama ya juu. Je, ni nani asiyejua thamani ya mazingira safi?

Mali ya Serikali ya Kenya 36

Kipindi cha 36 na 37 **Usafi wa Mazingira 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kuzolewa z hifadhiwe gharama

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

zihifadhiwe maradhi thamani kuyathamini

Kusimulia hadithi

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni mambo gani yanazungumziwa katika aya ya kwanza?
3. Eleza jinsi usafi wa nyumba unafaa kufanywa kulingana na aya ya tatu?
4. Mwishoni mwa hadithi tunashauriwa kufanya nini ili kuimarisha afya yetu?

Sarufi: Vielezi

**Kamilisha sentensi ukitumia "haraka" au "polepole"**

1. Mwendo wa kobe ni wa ____________.
2. Ukichelewa kuamka unafaa kwenda shuleni kwa mwendo wa ____________.
3. Mwanafunzi mzuri huandika ____________.
4. Gari kuukuu huendeshwa ____________.

**Katika vikundi vya wanafunzi wawili, igiza kwa kurejelea maneno yaliyo kwenye mabano.**

1. Andika (polepole)
2. Fungua mlango (haraka)
3. Tembea (polepole)
4. Keti (haraka)

**Tunga sentensi mbili ukitumia neno 'polepole' na mbili ukitumia neno 'haraka'.**

37 Hakiuzwi

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika neno **kuzolewa** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuzolewa. Hakikisha sentensi inaonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi wawaeleze wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno.

Rudia zoezi maneno na haya: **zihifadhiwe, gharama.**

**U:** Wanafunzi wanasoma maneno mapya kwenye **ukurasa wa 37.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. waulize wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Kusimulia Hadithi**

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]

**N:** Simulia darasa lote hadithi.

**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Taja kichwa cha hadithi. (Mazingira ya Binadamu)
2. Ni mambo gani yanayozungumziwa katika aya ya kwanza? (Vitu vinavyopatikana katika mazingira.)
3. Eleza jinsi usafi wa nyumba unafaa kufanywa kulingana na aya ya tatu? (Kukata nyasi, kuzoa takataka na kuosha choo.)
4. Mwishoni mwa hadithi tunashauriwa kufanya nini ili kuimarisha afya yetu? (Tunashauriwa kudumisha usafi wa mazingira.)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 36: Usafi wa Mazingira 1

Kipindi cha 36 na 37 **Usafi wa Mazingira 1**

### Matini

**Mazingira ya Binadamu**



Mazingira ya binadamu ni muhimu kwa maisha yake. Mazingira haya yanajumuisha ndege, miti, misitu, wanyama, maji, nyumba na hata binadamu wengine. Ni muhimu kuyatunza na kuyathamini mazingira ili kulinda afya.

Kwanza, mtu anafaa kuanza kwa usafi wa mwili wake. Ili kuimarisha usafi wa mwili, mtu anapaswa kuoga, kuvaa nguo safi, kukata kucha na kuchana nywele.

Usafi wa nyumba pia ni muhimu. Nyasi karibu na nyumba lazima zikatwe ili mbu wasipate makao. Taka zote ziwekwe katika pipa la taka lililotengewa maalum. Choo pia kiwe safi. Ufagio wa chooni ni vyema ubaki chooni na usitumiwe kufagia nyumba.

Ni muhimu chemichemi za maji zihifadhiwe na maji yasichafuliwe. Isitoshe, mifereji ya maji taka haifai kuelekezwa mitoni. Kila pahali, taka zinafaa ziokotwe na kuzolewa kila siku haraka iwezekanavyo.

Usafi wa mazingira ukidumishwa, magonjwa yatapungua na taifa litakuwa na watu wenye afya. Watu wenye afya hufanya kazi kwa bidii. Usafi wa mazingira ni kinga dhidi ya maradhi na umaskini. Mazingira machafu hueneza maradhi ambayo tiba huwa polepole na ya gharama ya juu. Je, ni nani asiyejua thamani ya mazingira safi?

Mali ya Serikali ya Kenya

36

Kipindi cha 36 na 37 **Usafi wa Mazingira 1**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

kuzolewa z hifadhiwe gharama

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

zihifadhiwe maradhi thamani kuyathamini

### Kusimulia hadithi

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni mambo gani yanazungumziwa katika aya ya kwanza?
3. Eleza jinsi usafi wa nyumba unafaa kufanywa kulingana na aya ya tatu?
4. Mwishoni mwa hadithi tunashauriwa kufanya nini ili kuimarisha afya yetu?

### Sarufi: Vielezi

**Kamilisha sentensi ukitumia "haraka" au "polepole"**

1. Mwendo wa kobe ni wa ____________.
2. Ukichelewa kuamka unafaa kwenda shuleni kwa mwendo wa ____________.
3. Mwanafunzi mzuri huandika ____________.
4. Gari kuukuu huendeshwa ____________.

**Katika vikundi vya wanafunzi wawili, igiza kwa kurejelea maneno yaliyo kwenye mabano.**

1. Andika (polepole)
2. Fungua mlango (haraka)
3. Tembea (polepole)
4. Keti (haraka)

**Tunga sentensi mbili ukitumia neno 'polepole' na mbili ukitumia neno 'haraka'.**

37 Hakiuzwi

## Sarufi: Vielezi

**N:** Vielezi ni maneno yanayotumiwa kueleza zaidi kuhusu kitenzi au kitendo fulani.

**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye vielezi kutoka kwenye hadithi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.

**U:** Waelekeze wanafunzi kukamilisha sentensi zilizosalia.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Ni mambo gani yanasisitizwa mwishoni mwa hadithi ya **Mazingira ya Binadamu.**

### Majibu

Mambo yanayosisitizwa katika mwisho wa hadithi ni kudumisha usafi wa mazingira ili kupunguza magonjwa na kuimarisha afya katika taifa.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha | 36 na 37 | **Usafi wa Mazingira 1**

Matini

**Mazingira ya Binadamu**



Mazingira ya binadamu ni muhimu kwa maisha yake. Mazingira haya yanajumuisha ndege, miti, misitu, wanyama, maji, nyumba na hata binadamu wengine. Ni muhimu kuyatunza na kuyathamini mazingira ili kulinda afya.

Kwanza, mtu anafaa kuanza kwa usafi wa mwili wake. Ili kuimarisha usafi wa mwili, mtu anapaswa kuoga, kuvaa nguo safi, kukata kucha na kuchana nywele.

Usafi wa nyumba pia ni muhimu. Nyasi karibu na nyumba lazima zikatwe ili mbu wasipate makao. Taka zote ziwekwe katika pipa la taka lililotengewa maalum. Choo pia kiwe safi. Ufagio wa chooni ni vyema ubaki chooni na usitumiwe kufagia nyumba.

Ni muhimu chemichemi za maji zihifadhiwe na maji yasichafuliwe. Isitoshe, mifereji ya maji taka haifai kuelekezwa mitoni. Kila pahali, taka zinafaa ziokotwe na kuzolewa kila siku haraka iwezekanavyo.

Usafi wa mazingira ukidumishwa, magonjwa yatapungua na taifa litakuwa na watu wenye afya. Watu wenye afya hufanya kazi kwa bidii. Usafi wa mazingira ni kinga dhidi ya maradhi na umaskini. Mazingira machafu hueneza maradhi ambayo tiba huwa polepole na ya gharama ya juu. Je, ni nani asiyejua thamani ya mazingira safi?

Mali ya Serikali ya Kenya 36

Kipindi cha | 36 na 37 | **Usafi wa Mazingira 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kuzolewa z hifadhiwe gharama

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

zihifadhiwe maradhi thamani kuyathamini

Kusimulia hadithi

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni mambo gani yanazungumziwa katika aya ya kwanza?
3. Eleza jinsi usafi wa nyumba unafaa kufanywa kulingana na aya ya tatu?
4. Mwishoni mwa hadithi tunashauriwa kufanya nini ili kuimarisha afya yetu?

Sarufi: Vielezi

**Kamilisha sentensi ukitumia "haraka" au "polepole"**

1. Mwendo wa kobe ni wa ___________.
2. Ukichelewa kuamka unafaa kwenda shuleni kwa mwendo wa ___________.
3. Mwanafunzi mzuri huandika ___________.
4. Gari kuukuu huendeshwa ___________.

**Katika vikundi vya wanafunzi wawili, igiza kwa kurejelea maneno yaliyo kwenye mabano.**

1. Andika (polepole)
2. Fungua mlango (haraka)
3. Tembea (polepole)
4. Keti (haraka)

**Tunga sentensi mbili ukitumia neno 'polepole' na mbili ukitumia neno 'haraka'.**

37 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **zihifadhiwe, theluji, dhidi, maradhi, huhifadhi, theruji.**

Waulize wanafunzi ni nini wanachoweza tambua kuhusu maneno haya.

**N:** Maneno haya yana sauti **dh** na **th**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno **zihifadhiwe** na **theluji.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: zihifadhiwe, theluji**

**U: dhidhi, maradhi, kuhifadhi, themanini**

**U:** Wanafunzi wasome maneno kwenye **ukurasa wa 37**.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** [Nani anakumbuka tulichojifunza wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **Mazingira ya Binadamu.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vielezi

**N:** [Vielezi ni maneno yanayotumiwa kueleza zaidi kuhusu kitenzi au kitendo fulani. Leo tutaandika sentensi zenye aina hii ya sarufi]

**T:** Kamilisha sentensi ukitumia haraka au pole pole kwenye **ukurasa wa 37.**

**U:** Waelekeze wanafunzi kukamilisha sentensi zilizosalia.

## Kuandika

**Shairi - Kuhakiki**

**N:** Wasomee wanafunzi nakala uliyokuwa umeandika. Waeleze kuwa utairejelea baadaye.

**T:** Rejelea nakala pamoja na wanafunzi kwa kuuliza maswali haya:

1. **Herufi kubwa** – Je, sentensi zote zinaanza kwa herufi kubwa?
2. **Maelezo** – Je, kila kitu kwenye hadithi ni shwari na wazi. Hadithi inasomeka na ni ya kuburudisha?
3. **Uakifishaji** – Je, sentensi zina alama sahihi ya uakifishaji mwishoni?
4. **Tahajia** – Je, maneno yote yameendelezwa ipasavyo?

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Nakili maneno haya mara tatu kisha uyasome:

1. dhidi
2. thamani
3. zihifadhiwe
4. maradhi

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 38: Usafi wa Mazingira 1

Kipindi cha 38 na 39 **Usafi wa Mazingira 1**

### Matini

**Mazingira Yetu**



Ni jambo la muhimu sana kuyatunza mazingira yetu ili yawe safi kila wakati. Ili kuyatunza mazingira yetu, ni lazima kukusanya takataka zote zilizo karibu nasi na kuzitupa pahali ambapo panafaa. Mimi hutumia reki kukusanya takataka polepole karibu na nyumba yetu.

Taka ambazo haziwezi kuoza, kama vile vipande vya chupa au chuma, zinafaa kuwekwa kando kwa ajili ya kusagwa na kutumiwa upya. Taka zisizoweza kusagwa zinafaa kutumbukizwa shimoni na kufukiwa.

Taka zilizofukiwa shimoni zitazuia maji kusalia karibu na makazi yetu, hivyo kuepuka makazi ya mbu. Hivyo, tutajikinga dhidi ya magonjwa yanayoenezwa na mbu kama vile malaria. Kusaga na kutumia taka upya ni muhimu kwani zinatumiwa kama rasilmali.

Kusafisha sakafu ni njia moja ya kuhakikisha kuwa wadudu kama vile funza hawaingii miguuni mwetu. Ni vizuri pia kufyeka nyasi ndefu zilizo karibu na mahali tunapoishi au kuchezea. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa wanyama hatari kama vile nyoka wanakaa mbali na sisi. Vilevile, nyasi ndefu zinaweza kututatiza tunapotembea haraka.

Ni jambo zuri sana kupanda miti. Miti ni thamani kwa kuwa hutupatia kivuli na mahali pa kupumzika tunapohisi joto. Miti pia husaidia kutukinga dhidi ya upepo mkali ambao unaweza kung'oa paa za nyumba. Zaidi ya hayo, sehemu mbalimbali za miti fulani hutumiwa kama dawa. Kwa ufupi, miti ina matumizi mengi na huhifadhi mazingira.

Mali ya Serikali ya Kenya

38

Kipindi cha 38 na 39 **Usafi wa Mazingira 1**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

reki kufukiwa kufyeka

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

huhifadhi kadhalika dhidi ya thamani

### Kusimulia hadithi

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni mambo gani yanazungumziwa katika aya ya kwanza?
3. Eleza jinsi ya kushughulikia aina tofauti za taka kulingana na aya ya pili.
4. Mwishoni mwa hadithi tunashauriwa kufanya nini ili kung'arisha mazingira yetu?

### Sarufi: Vielezi - Matumizi ya polepole na haraka

**Jaza mapengo kwa kutumia haraka au polepole.**

1. Tulipotumia garimoshi la kasi, tulifika Nairobi ___________.
2. Konokono anajulikana kwa kutembea __________.
3. Fanya ____________ tuondoke, tusichelewe.
4. ____________ ndio mwendo.

39 Hakiuzwi

## Msamiati

**T:** Jadili picha. Andika neno **reki**.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno reki kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuwaelezea wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno.

Rudia zoezi na maneno haya: **kufukiwa, kufyeka**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **kufyeka.**]

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 39**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliwaze wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Kusimulia Hadithi**

Kichwa

Wanaozungumziwa

Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?

Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?

Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]

**N:** Simulia darasa lote hadithi.

**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Taja kichwa cha hadithi. (Mazingira yetu)
2. Ni mambo gani yanazungumziwa katika aya ya kwanza? (Namna ya kuweka mazingira yakiwa safi.)
3. Eleza jinsi ya kushughulikia aina tofauti za taka kulingana na aya ya pili. (Kutupa na kufukia kwenye shimo.)
4. Mwishoni mwa hadithi tunashauriwa kufanya nini ili kung'arisha mazingira yetu? (Kupanda miti kwa wingi.)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 38: Usafi wa Mazingira 1

Kipindi cha 38 na 39 **Usafi wa Mazingira 1**

**Matini**

### Mazingira Yetu



Ni jambo la muhimu sana kuyatunza mazingira yetu ili yawe safi kila wakati. Ili kuyatunza mazingira yetu, ni lazima kukusanya takataka zote zilizo karibu nasi na kuzitupa pahali ambapo panafaa. Mimi hutumia reki kukusanya takataka polepole karibu na nyumba yetu.

Taka ambazo haziwezi kuoza, kama vile vipande vya chupa au chuma, zinafaa kuwekwa kando kwa ajili ya kusagwa na kutumiwa upya. Taka zisizoweza kusagwa zinafaa kutumbukizwa shimoni na kufukiwa.

Taka zilizofukiwa shimoni zitazuia maji kusalia karibu na makazi yetu, hivyo kuepuka makazi ya mbu. Hivyo, tutajikinga dhidi ya magonjwa yanayoenezwa na mbu kama vile malaria. Kusaga na kutumia taka upya ni muhimu kwani zinatumiwa kama rasilmali.

Kusafisha sakafu ni njia moja ya kuhakikisha kuwa wadudu kama vile funza hawaingii miguuni mwetu. Ni vizuri pia kufyeka nyasi ndefu zilizo karibu na mahali tunapoishi au kuchezea. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa wanyama hatari kama vile nyoka wanakaa mbali na sisi. Vilevile, nyasi ndefu zinaweza kututatiza tunapotembea haraka.

Ni jambo zuri sana kupanda miti. Miti ni thamani kwa kuwa hutupatia kivuli na mahali pa kupumzika tunapohisi joto. Miti pia husaidia kutukinga dhidi ya upepo mkali ambao unaweza kung'oa paa za nyumba. Zaidi ya hayo, sehemu mbalimbali za miti fulani hutumiwa kama dawa. Kwa ufupi, miti ina matumizi mengi na huhifadhi mazingira.

Mali ya Serikali ya Kenya 38

Kipindi cha 38 na 39 **Usafi wa Mazingira 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

reki kufukiwa kufyeka

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

huhifadhi kadhalika dhidi ya thamani

**Kusimulia hadithi**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni mambo gani yanazungumziwa katika aya ya kwanza?
3. Eleza jinsi ya kushughulikia aina tofauti za taka kulingana na aya ya pili.
4. Mwishoni mwa hadithi tunashauriwa kufanya nini ili kung'arisha mazingira yetu?

**Sarufi: Vielezi – Matumizi ya polepole na haraka**

**Jaza mapengo kwa kutumia haraka au polepole.**

1. Tulipotumia garimoshi la kasi, tulifika Nairobi ___________.
2. Konokono anajulikana kwa kutembea __________.
3. Fanya ____________ tuondoke, tusichelewe.
4. ____________ ndio mwendo.

39 Hakiuzwi

## Sarufi: Vielezi

**T:** Vielezi ni maneno yanayotumiwa kueleza zaidi kuhusu kitenzi au kitendo fulani.

**T/U:** Waelekeze wanafunzi kujaza pengo kwa sentensi zilizosalia.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Igiza kwa kurejelea maneno kwenye mabano.

1. Andika (polepole)
2. Funga mlango (haraka)
3. Tembea (haraka)
4. Kesi (polepole)

Tunga sentensi nne ukitumia neno 'polepole' na 'haraka'.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 38 na 39 **Usafi wa Mazingira 1**

**Matini**

### Mazingira Yetu



Ni jambo la muhimu sana kuyatunza mazingira yetu ili yawe safi kila wakati. Ili kuyatunza mazingira yetu, ni lazima kukusanya takataka zote zilizo karibu nasi na kuzitupa pahali ambapo panafaa. Mimi hutumia reki kukusanya takataka polepole karibu na nyumba yetu.

Taka ambazo haziwezi kuoza, kama vile vipande vya chupa au chuma, zinafaa kuwekwa kando kwa ajili ya kusagwa na kutumiwa upya. Taka zisizoweza kusagwa zinafaa kutumbukizwa shimoni na kufukiwa.

Taka zilizofukiwa shimoni zitazuia maji kusalia karibu na makazi yetu, hivyo kuepuka makazi ya mbu. Hivyo, tutajikinga dhidi ya magonjwa yanayoenezwa na mbu kama vile malaria. Kusaga na kutumia taka upya ni muhimu kwani zinatumiwa kama rasilmali.

Kusafisha sakafu ni njia moja ya kuhakikisha kuwa wadudu kama vile funza hawaingii miguuni mwetu. Ni vizuri pia kufyeka nyasi ndefu zilizo karibu na mahali tunapoishi au kuchezea. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa wanyama hatari kama vile nyoka wanakaa mbali na sisi. Vilevile, nyasi ndefu zinaweza kututatiza tunapotembea haraka.

Ni jambo zuri sana kupanda miti. Miti ni thamani kwa kuwa hutupatia kivuli na mahali pa kupumzika tunapohisi joto. Miti pia husaidia kutukinga dhidi ya upepo mkali ambao unaweza kung'oa paa za nyumba. Zaidi ya hayo, sehemu mbalimbali za miti fulani hutumiwa kama dawa. Kwa ufupi, miti ina matumizi mengi na huhifadhi mazingira.

Mali ya Serikali ya Kenya 38

Kipindi cha 38 na 39 **Usafi wa Mazingira 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

reki kufukiwa kufyeka

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

huhifadhi kadhalika dhidi ya thamani

**Kusimulia hadithi**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kichwa cha hadithi.
2. Ni mambo gani yanazungumziwa katika aya ya kwanza?
3. Eleza jinsi ya kushughulikia aina tofauti za taka kulingana na aya ya pili.
4. Mwishoni mwa hadithi tunashauriwa kufanya nini ili kung'arisha mazingira yetu?

**Sarufi: Vielezi – Matumizi ya polepole na haraka**

**Jaza mapengo kwa kutumia haraka au polepole.**

1. Tulipotumia garimoshi la kasi, tulifika Nairobi ___________.
2. Konokono anajulikana kwa kutembea __________.
3. Fanya ____________ tuondoke, tusichelewe.
4. ____________ ndio mwendo.

39 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **huhifadhi, athumani, kadhalika, dhambi.**
Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.
**N:** Maneno haya ya na sauti **th** na **dh**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **huhifadhi, athumani.** (Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.)
**N/T/U: huhifadhi, athumani.**
**U: kadhalika, dhambi.**
**U:** Wanafunzi wasome maneno kwenye **ukurasa wa 39.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** [Nani anakumbuka nilichojifunza wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **mazingira yetu.**]
**U:** Wanafunzi wawawasomee wenzao.

## Kuandika:

**Shairi Kuhakiki**

**T:** Leo mtashirikiana na mwenzako kurejelea kazi uliyoandika. Nani atatukumbusha hoja muhimu tunazingatia wakati wa kurejelea kazi tuliyoandika?

1. **Herufi kubwa** – Je, sentensi zote zinaanza kwa herufi kubwa?
2. **Maelezo** –Je, kila kitu kwenye hadithi ni shwari na wazi? Hadithi inasomeka na ni ya kuburudisha?
3. **Uakifishaji** – Je, sentensi zina alama sahihi ya uakifishaji mwishoni?
4. **Tahajia** – Je, maneno yote yameendelezwa ipasavyo?


**U:** Sasa ni zamu yako. Mpe mwenzako nakala yako aisome huku akizingatia hoja hizi nne.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo: **pipa la taka, kifyekeo, reki, malaria**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 40: Usafi wa Mazingira 1



Kipindi cha 40 Usafi wa Mazingira 1

Tathmini ya msamiati

Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo.

1. zihifadhiwe
2. kuzolewa
3. reki
4. kufyeka

Tathmini ya Sarufi

Tunga sentensi mbili ukitumia kielezi 'haraka' na mbili ukitumia kielezi 'polepole'.

Mali ya Serikali ya Kenya 40

## Msamiati

**U:** Fungua vitabu vyenu **ukurasa wa 40**.
Tazama sehemu ya msamiati.
Tunga sentensi ukitumia maneno uliopewa.

## Kusoma Maneno

**U:** Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika
Maneno: **huhifadhi, kadhalika, dhidi, thamani, mdhamini, zinifadhiwe, maradhi, kuyathamini, thabiti**

## Kuchambua Matini

### Mhusika

**T:** [Je, mhusika katika hadithi ni nani?
Mhusika katika hadithi ni mtu au mnyama anayezungumziwa kwenye hadithi. Wiki hii tulisoma hadithi mbili. Je, hadithi hizi mbili zilihusu nini? *(Wanafunzi 2-3 kushiriki somo huku ukiwapa mwongozo.)*
Leo tutarejelea hadithi tulizosoma ili tupate wahusika katika hadithi. Hebu turejelee hadithi ya kwanza kwenye **ukurasa wa 36**. Wahusika ni akina nani? (*binadamu*).]
**T:** [Ni mhusika gani amekupendeza na ni kwa nini amekupendeza? Hebu tuandike sentensi moja au mbili kuhusu wahusika tunaowapenda. *Andika yafuatayo huku ukizungumia kuhusu wahusika:* Binadamu amenipendeza zaidi kwa sababu alinionyesha jinsi ya kutunza mazingira yangu.]
**U:** [Sasa ni zamu yako. Hebu tuitazame hadithi ya pili kwenye **ukurasa wa 38**. Je, wahusika ni akina nani? Andika sentensi mbili kumhusu mhusika huyo. Toa sababu zako za kumpenda mhusika huyo.]

## Sarufi: Vielezi

**U:** Vielezi ni maneno yanayotumiwa kueleza zaidi kuhusu kitenzi au kitendo fulani. Andika sentensi daftarini mwako ukionyesha matumizi ya vielezi 'haraka' na 'polepole'.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora wanyama hawa wawili wanaojulikana kwa mwendo wa polepole.

**Majibu**

1. Konokono
2. Kobe

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 41 na 42 **Dukani 1**

Shairi

**Duka la Bi. Musa**



Shughuli za mapema, wateja pale dukani,
Bidhaa zionekane, bei imeandikwa,
Usafi anadumisha, wanunuzi asiwakose,
Dukani kwa Bi. Musa, sikosi nitakacho.

Kupanga bidhaa rafuni, duka lake lipendeze,
Utiifu na bidii kazini, hasara atapataje?
Kuuza ndiyo shughuli, faida isimponyoke,
Dukani kwa Bi. Musa, sikosi nitakacho.

Boflo, maziwa, majani, sukari, unga na pipi,
Vyote huviuza dukani, na vingine vingi sijataja,
Kilo kamili huipima, kutumia ratili yake,
Dukani kwa Bi. Musa, sikosi nitakacho.

Jioni pesa huzihesabu, sarafu na pia noti,
Bidhaa huwa zimeuzwa, kidogo huwa imebaki,
Kukopesha hakopeshi, wengi huuliza kwa nini?
Dukani kwa Bi. Musa, sikosi nitakacho.

41 Hakiuzwi

Kipindi cha 41 na 42 **Dukani 1**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

bei kilo sarafu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

bidhaa pima boflo pipi

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Duka la Bi. Musa hufunguliwa lini?
2. Kwa nini ni muhimu kwa Bi. Musa kudumisha usafi?
3. Sukari hupimwa kwa kutumia nini?
4. Shairi hili linatufundisha nini?

Sarufi: Alama ya kuuliza (?)

**Tumia alama sahihi kuakifisha sentensi zifuatazo.**

1. Hasara atapataje
2. Sheila ana vitabu vingapi
3. Mwalimu wa hisabati ni nani
4. Shule zitafungwa lini

Mali ya Serikali ya Kenya 42

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika neno **bei** ubaoni.

1. Uliza maana - ya neno bei
2. Tunga sentensi ukitumia neno bei kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuwaelezea wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno. Rudia zoezi ukitumia maneno haya: kilo, sarafu.

**U:** Wanafunzi wanasoma maneno mapya kwenye **ukurasa wa 42.**

## Kusoma Matini:Shairi

**T:** Soma kichwa cha shairi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.
**T/U:** Soma shairi.
**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Kusimulia Hadithi**

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]
**N:** Simulia darasa lote hadithi.
**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

## Sarufi: Kiulizi

**N:** [Kiulizi ni alama inayoonyesha swali limeulizwa.]
**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye viulizi kutoka katika shairi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.
**U:** Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi zenye viulizi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tumia alama ya kiulizi kuandika maswali mawili.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 42: Dukani 1

Kipindi cha 41 na 42 **Dukani 1**

**Shairi**

**Duka la Bi. Musa**



Shughuli za mapema, wateja pale dukani,
Bidhaa zionekane, bei imeandikwa,
Usafi anadumisha, wanunuzi asiwakose,
Dukani kwa Bi. Musa, sikosi nitakacho.

Kupanga bidhaa rafuni, duka lake lipendeze,
Utiifu na bidii kazini, hasara atapataje?
Kuuza ndiyo shughuli, faida isimponyoke,
Dukani kwa Bi. Musa, sikosi nitakacho.

Boflo, maziwa, majani, sukari, unga na pipi,
Vyote huviuza dukani, na vingine vingi sijataja,
Kilo kamili huipima, kutumia ratili yake,
Dukani kwa Bi. Musa, sikosi nitakacho.

Jioni pesa huzihesabu, sarafu na pia noti,
Bidhaa huwa zimeuzwa, kidogo huwa imebaki,
Kukopesha hakopeshi, wengi huuliza kwa nini?
Dukani kwa Bi. Musa, sikosi nitakacho.

41

Hakiuzwi

Kipindi cha 41 na 42 **Dukani 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

bei kilo sarafu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

bidhaa pima boflo pipi

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Duka la Bi. Musa hufunguliwa lini?
2. Kwa nini ni muhimu kwa Bi. Musa kudumisha usafi?
3. Sukari hupimwa kwa kutumia nini?
4. Shairi hili linatufundisha nini?

**Sarufi: Alama ya kuuliza (?)**

**Tumia alama sahihi kuakifisha sentensi zifuatazo.**

1. Hasara atapataje
2. Sheila ana vitabu vingapi
3. Mwalimu wa hisabati ni nani
4. Shule zitafungwa lini

Mali ya Serikali ya Kenya

42

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **bidhaa, pima, bei, bidii, pika**

Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.

**N:** Maneno haya yana sauti **b** na **p**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **bidhaa** na **pima.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: bidhaa, pima**

**U: bei, bidii, pika**

**U:** Wanafunzi wawasomee maneno **ukurasa wa 42**.

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** [Nani anakumbuka tulichojifunza wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **Duka la Bi Musa.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Kiulizi

**U:** Kiulizi ni alama ya kuonyesha swali limeulizwa. Hebu tutazame sentensi katika **ukurasa wa 42**. Akifisha sentensi ya kwanza ukitumia alama ya kiulizi.

**T:**Wanafunzi waziakifishe sentensi kwa kutumia alama ya kiulizi.

## Kuandika

**Shairi - Kuhariri**

**N:** Sasa tutarejelea nakala tulioiandika wakati uliopita.

**T:** Hakiki na uone kama kuna makosa yeyote pamoja na wanfunzi. Andika upya nakala yako huku ukisahihisha makosa pamoja na wanafunzi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Nakili maneno haya mara tatu kisha uyasome:

**pesa, basi, pima, bima, pipi.**

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 43 na 44 **Dukani 1**

**Shairi**

**Unapotumwa Dukani**



Unapotumwa dukani, hakikisha una pesa,
Usipokuwa na pesa, cha kununua utakosa,
Muuzaji atakuuliza, ni nini wataka?
Endapo hela hunazo, dukani usikimbilie.

Muuzaji nakwambia, faida ndiyo anataka,
Hasara haitaki, bei anapoiweka,
Noti ukimpatia, hata sarafu ataishika,
Endapo hela hunazo, dukani usikimbilie.

Ratili nayo dukani, kazi yake nitaeleza,
Hutumika kupima bidhaa, basi hata utapata,
Kilo ngapi unataka? atakuuliza muuzaji,
Endapo hela hunazo, dukani usikimbilie.

43 Hakiuzwi

Kipindi cha 43 na 44 **Dukani 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

hela noti pesa

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

bei anapoiweka endapo basi

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kutokana na shairi unatakiwa kuwa na nini unapoenda dukani?
2. Muuzaji anataka kupata nini katika biashara yake?
3. Mnunuzi anaweza kutumia pesa za aina gani dukani?
4. Taja bidhaa zingine ambazo zinaweza kupimwa kwenye ratili.

**Sarufi: Alama ya kuuliza (?)**

**Msomee mwenzako sentensi zifuatazo kwa usahihi.**

1. Unataka kuandika nini?
2. Shule yako inaitwaje?
3. Unataka kununua nini?
4. Unaenda wapi?

**Kuandika**

**Katika vikundi vya wanafunzi wawili, andikeni kisa kifupi kuhusu umuhimu wa kufanya biashara.**

Mali ya Serikali ya Kenya 44

## Msamiati

Jadili picha. Andika neno **hela** ubaoni.
1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi waeleze wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno.

Rudia zoezi kwa kutumia maneno haya: **noti, pesa**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno hela.]

**U:** Wanafunzi wanasoma maneno mapya kwenye **ukurasa wa 44.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** Soma kichwa cha shairi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma shairi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**kusimulia Hadithi**

Chora umbo la nyumba.




**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]

**N:** Simulia darasa lote hadithi.

**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Kutokana na shairi unatakiwa kuwa na nini unapoenda dukani? (Pesa)
2. Muuzaji anataka kupata nini katika biashara yake? (Faida)
3. Mnunuzi anaweza kutumia pesa za aina gani dukani? (Noti)
4. Taja bidhaa zingine ambazo zinaweza kupimwa kwenye ratili. (Kubali jibu lolote sahihi.)

## Sarufi: Kiulizi

**T:** [Kiulizi ni alama ya kuonyesha swali limeulizwa. *Afikisha sentensi ya kwanza ukitumia alama ya kiulizi.*]

**U:** Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi zilizo na alama ya kiulizi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia maneno haya:- hela, noti, pesa.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 44: Dukani 1

Kipindi cha 43 na 44 **Dukani 1**

**Shairi**

**Unapotumwa Dukani**



Unapotumwa dukani, hakikisha una pesa,
Usipokuwa na pesa, cha kununua utakosa,
Muuzaji atakuuliza, ni nini wataka?
Endapo hela hunazo, dukani usikimbilie.

Muuzaji nakwambia, faida ndiyo anataka,
Hasara haitaki, bei anapoiweka,
Noti ukimpatia, hata sarafu ataishika,
Endapo hela hunazo, dukani usikimbilie.

Ratili nayo dukani, kazi yake nitaeleza,
Hutumika kupima bidhaa, basi hata utapata,
Kilo ngapi unataka? atakuuliza muuzaji,
Endapo hela hunazo, dukani usikimbilie.

43 Hakiuzwi

Kipindi cha 43 na 44 **Dukani 1**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

hela noti pesa

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

bei anapoiweka endapo basi

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kutokana na shairi unatakiwa kuwa na nini unapoenda dukani?
2. Muuzaji anataka kupata nini katika biashara yake?
3. Mnunuzi anaweza kutumia pesa za aina gani dukani?
4. Taja bidhaa zingine ambazo zinaweza kupimwa kwenye ratili.

**Sarufi: Alama ya kuuliza (?)**

**Msomee mwenzako sentensi zifuatazo kwa usahihi.**

1. Unataka kuandika nini?
2. Shule yako inaitwaje?
3. Unataka kununua nini?
4. Unaenda wapi?

**Kuandika**

**Katika vikundi vya wanafunzi wawili, andikeni kisa kifupi kuhusu umuhimu wa kufanya biashara.**

Mali ya Serikali ya Kenya 44

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **bei, anapoiweka, pasi, bidhaa.**
Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.
**N:** Maneno haya yana sauti **b** na **p**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **bei** na **anapoiweka.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.
**N/T/U: bei, anapoiweka**
**U: pasi, bidhaa**
**U:** Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 44**.

## Kusoma Matini: Shairi

**N:** [Nani anakumbuka tulijifunza nini wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **unapotumwa Dukani.**]
**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika


**Shairi - Kuhariri**

**N:** Sasa tutarejelea nakala tuliyoiandika wakati uliopita.
**U:** Hakiki na uone kama kuna makosa yoyote. Andika upya nakala yako huku ukisahihisha makosa kisha umwonyeshe mwenzako.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi zinazoonyesha matumizi ya kiulizi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Kipindi cha 45 **Dukani 1**

Tathmini ya msamiati

**Jaza mapengo kwa kutumia neno sahihi kutoka kwenye mabano.**

1. Nilitumia ________ kununulia bidhaa dukani. (pesa, bofulo)
2. Pesa za ________ hutengenezwa kwa karatasi. (bei, noti)
3. ________ ni jina lingine la pesa. (Dukani, Hela)
4. Pesa za ________ hutengenezwa kwa madini. (hela, sarafu)

Tathmini ya Sarufi

**Akifisha sentensi hizi kwa kutumia alama ya kiulizi (?) au kikomo (.).**

1. Sarafu ni pesa gani
2. Nilimwona mchuuzi dukani
3. Nitaenda kumtembelea baba
4. Unataka nini hapa dukani

45 Hakiuzwi

## Msamiati

**T:** Fungua **ukurasa wa 45** wa vitabu vyenu.
**U:** Tazama sehemu ya msamiati.
**U:** Jaza mapengo kwa kutumia neno sahihi kutoka kwenye mabano.

## Kusoma Maneno

**U:** Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.
Maneno: **bei, basi, anapoiweka, pima, baki, pasi, endapo, bidhaa, boflo, pipi**

## Kuchambua Matini: Mhusika

**T:** [Je, mhusika katika hadithi au shairi ni nani? Ndio, mhusika katika hadithi au shairi ni mtu au mnyama anayezungumziwa kwenye hadithi au shairi. Wiki hii tulisoma mashairi mawili. Je, mashairi haya yalihusu nini? *(Wakubali wanafunzi 2-3 kushiriki somo huku ukiwapa mwongozo.)*]
**T:** [Leo tutarejelea mashairi tuliyoyasoma ili tupate wahusika katika mashairi. Hebu turejelee shairi la kwanza **ukurasa wa 41**. Wahusika ni akina nani? *Bi. Musa na wateja wake.* Hebu tusome ubeti wa kwanza pamoja. *Soma ubeti wa kwanza pamoja na wanafunzi.*]
**T:** [Ni mhusika gani amekupendeza na kwa nini amekupendeza? Hebu tuandike sentensi moja au mbili kuhusu wahusika tunaowapenda. *Andika yafuatayo huku ukizungumza kuhusu wahusika:* Nampenda mhusika anayesimulia shairi kwa jinsi alivyo mtiifu kazini.]
**U:** [Sasa ni zamu yako. Hebu tulitazame shairi la pili kwenye **ukurasa wa 43**. Je, wahusika ni akina nani? Sasa fanya uamuzi kwa kumchagua mhusika unayempenda na uandike sentensi moja au mbili kumhusu na sababu zako za kumpenda mhusika huyu.]

## Sarufi: Kiulizi

**T:** Kiulizi ni alama ya kuonyesha swali. Akifisha sentensi ya kwanza **ukurasa wa 45.**
**U:** Wanafunzi waakifishe sentensi kwa alama ya kuulizi au kikomo.

**Majibu**

1. Sarafu ni pesa gani?
2. Nilimwona mchuuzi dukani.
3. Nitaenda kumtembelea baba.
4. Unataka nini hapa dukani?

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi tatu kuhusu umuhimu wa pesa.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 46: Ndege Nimpendaye 1

Kipindi cha 46 na 47 **Ndege Nimpendaye**

**Shairi**

**Ndege wa nyumbani**



Naomba mnisikilize, ya ndege nielezee,
Chini ya mti niongeze, uzuri niwatajie,
Machoni wawapendeze, mazuri muwatendee,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Bata ana rangi zake, mwingine wa kuvutia,
Mayai bila makeke, kwenye nyasi hututagia,
Batamzinga na yake, nyama twaitumia,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Ndege hawa nilotaja, ndege wa maana sana,
Mwito kwa yeyote mja, utunzi watakikana,
Tena sote kwa pamoja, tuwajali kwa mapana,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Mali ya Serikali ya Kenya

46

Kipindi cha 46 na 47 **Ndege Nimpendaye**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

makeke batamzinga ndege

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

nyasi nyumbani kweli kwenye

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni ndege yupi anayependwa sana?
2. Batamzinga anatusaidia vipi?
3. Tunaombwa kuwafanyia ndege nini?
4. Taja ndege wengine wanaofugwa.

**Sarufi: Vihusishi – 'juu ya', 'chini ya'**

**Soma sentensi hizi.**

1. Kasuku amepaa juu ya mti.
2. Maria ameweka mayai chini ya kabati.
3. Kuku aliruka juu ya mtungi.
4. Bata amelala chini ya ghala.

**Tumia "juu ya" au "chini ya" kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo.**

1. Chungu kiko ________ meko.
2. Meli iko _______ maji.
3. Ameketi ______ kivuli.
4. Viatu vichafu viko ______ kitanda.

47

Hakiluzwi

## Msamiati

Jadili picha. Andika neno **makeke** ubaoni.

1. Uliza maana ya neno.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi kuwaelezea wenzao maana ya neno kwa maneno yao wenyewe.
4. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno.

Rudia zoezi ukitumia maneno haya: **batamzinga, ndege**

**U:** Wanafunzi wasoma maneno mapya kwenye **ukurasa wa 47.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** Soma kichwa cha shairi pamoja na wanafunzi. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma shairi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Kusimulia Hadithi**

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati ya hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**N:** Chora umbo la nyumba ubaoni. Waulize wanafunzi maswali yafuatayo huku ukiwaelekeza ipasavyo.

**T/U:** [Kichwa cha shairi ni nini? Shairi hili linafanyika wapi? Shairi hili linazungumzia nini sana? Nini kinafanyika katika ubeti wa kwanza? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika katika ubeti wa mwisho?]

**N:** Kariria darasa lote shairi.

**U:** [Kariria mwenzako shairi.]

### Maswali

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Ni ndege yupi anayependwa sana? (Kuku)
2. Batamzinga anatusaidia vipi? (Anatupa nyama)
3. Tunaombwa kuwafanyia ndege nini? (Kuwatunza ndege.)
4. Taja ndege wengine wanaofugwa. (Kubali majibu sahihi)

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 46 na 47 **Ndege Nimpendaye**

**Shairi**

**Ndege wa nyumbani**



Naomba mnisikilize, ya ndege nielezee,
Chini ya mti niongeze, uzuri niwatajie,
Machoni wawapendeze, mazuri muwatendee,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Bata ana rangi zake, mwingine wa kuvutia,
Mayai bila makeke, kwenye nyasi hututagia,
Batamzinga na yake, nyama twaitumia,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Ndege hawa nilotaja, ndege wa maana sana,
Mwito kwa yeyote mja, utunzi watakikana,
Tena sote kwa pamoja, tuwajali kwa mapana,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Mali ya Serikali ya Kenya

46

Kipindi cha 46 na 47 **Ndege Nimpendaye**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

makeke batamzinga ndege

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

nyasi nyumbani kweli kwenye

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni ndege yupi anayependwa sana?
2. Batamzinga anatusaidia vipi?
3. Tunaombwa kuwafanyia ndege nini?
4. Taja ndege wengine wanaofugwa.

**Sarufi: Vihusishi – 'juu ya', 'chini ya'**

**Soma sentensi hizi.**

1. Kasuku amepaa juu ya mti.
2. Maria ameweka mayai chini ya kabati.
3. Kuku aliruka juu ya mtungi.
4. Bata amelala chini ya ghala.

**Tumia "juu ya" au "chini ya" kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo.**

1. Chungu kiko ________ meko.
2. Meli iko _______ maji.
3. Ameketi ______ kivuli.
4. Viatu vichafu viko ______ kitanda.

47

Hakiuzwi

## Sarufi: Vihusishi: 'juu' ya na 'chini ya'

**N:** [Vihusishi ni maneno yanayotuarifu zaidi kuhusu uhusiano wa nomino na mazingira yake. Kwa mfano: **juu ya, chini ya.**]

**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye vihusishi kutoka kwenye shairi la **ukurasa wa 47**. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.

**U:** Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi zenye vihusishi zilizoko **ukurasa wa 47**.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora ndege wafuatao.

1. Batamzinga
2. Kuku

Andika sentensi moja kuhusu ndege uliowachora.

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 47: Ndege Nimpendaye 1

Kipindi cha 46 na 47 **Ndege Nimpendaye**

**Shairi**

**Ndege wa nyumbani**



Naomba mnisikilize, ya ndege nielezee,
Chini ya mti niongeze, uzuri niwatajie,
Machoni wawapendeze, mazuri muwatendee,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Bata ana rangi zake, mwingine wa kuvutia,
Mayai bila makeke, kwenye nyasi hutuatagia,
Batamzinga na yake, nyama twaitumia,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Ndege hawa nilotaja, ndege wa maana sana,
Mwito kwa yeyote mja, utunzi watakikana,
Tena sote kwa pamoja, tuwajali kwa mapana,
Kuku ndege wangu kweli, wa nyumbani nampenda.

Mali ya Serikali ya Kenya 46

Kipindi cha 46 na 47 **Ndege Nimpendaye**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

makeke batamzinga ndege

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

nyasi nyumbani kweli kwenye

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni ndege yupi anayependwa sana?
2. Batamzinga anatusaidia vipi?
3. Tunaombwa kuwafanyia ndege nini?
4. Taja ndege wengine wanaofugwa.

**Sarufi: Vihusishi - 'juu ya', 'chini ya'**

**Soma sentensi hizi.**

1. Kasuku amepaa juu ya mti.
2. Maria ameweka mayai chini ya kabati.
3. Kuku aliruka juu ya mtungi.
4. Bata amelala chini ya ghala.

**Tumia "juu ya" au "chini ya" kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo.**

1. Chungu kiko ________ meko.
2. Meli iko _______ maji.
3. Ameketi ______ kivuli.
4. Viatu vichafu viko ______ kitanda.

47 Hakluzwi

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **nyasi, kweli, kwekwe, nyuni, kwetu.**
Waulize wanafunzi wanaweza kutambua nini kuhusu maneno haya.
**N:** Maneno haya yana sauti **ny** na **kw**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **nyasi** na **kweli.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.
**N/T/U: nyasi, kweli**
**U: Nyuni, kwekwe, kwetu.**
**U:** Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 47.**

## Kusoma Matini: Shairi

**N:** [Nani anakumbuka tulijifunza nini wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **Ndege wa nyumbani.**]
**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao

## Sarufi: Vihusishi 'juu ya', 'chini ya'

**T:** [Vihusishi ni maneno yanayoonyesha uhusiano uliopo baina ya neno moja na jingine. Hebu tutazame zoezi katika **ukurasa wa 47.** Tutatumia **juu ya** au **chini ya** kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo.
Nitawaelekeza kujaza pengo katika sentensi ya kwanza *(Jaza pengo: Chungu kiko juu ya meko.)*]
**U:** Wanafunzi wajaze mapengo katika sentensi zilizosalia.

**Majibu**

1. juu ya
2. juu ya
3. chini ya
4. chini ya

## Kuandika

**Shairi - Kuchapisha**

Waulize wanafunzi 2 - 3 wasimame na kusoma nakala zao kwa zamu.
Waulize wanafunzi 2 - 3 waseme walichofurahia kuhusu nakala zilizosomwa.


## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Ni ushauri gani mwandishi anatupatia katika ubeti wa mwisho katika shairi la ndege wa nyumbani?

**Jibu**

Anatuihimiza kuwatunze ndege na pia kuwajali.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Kipindi cha 48 na 49 Ndege Nimpendaye

Shairi

**Ndege Ninayempenda**

Salamu natanguliza, ya moyoni niwajuze,
Mandhari ya kutuliza, chini ya mti mujikalize,
Mwenyezi Mungu kaumba, nafsiyo kaitulize,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Kanga na mbayuwayu, darajale sifikie,
Haya njiwa afugwaye, karibu asimfikie,
Maneno mengi aigayo, hasira nyingi takuondolea,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Wenye uzuri na umbo, wavutiao machoni,
Heroe tausi wana mambo, maringo wao mwendoni,
Siwapi langu jambo, rohoni niwawekeni,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Atakayefuga kasuku, lishe tamwandalia,
Tundu lake madhubuti, juu ya mti katulia,
Uhuru wake ni dhati, kukupasha aloyakalia,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Mali ya Serikali ya Kenya 48


Kipindi cha 48 na 49 Ndege Nimpendaye

Msamiati

**Soma maneno haya.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| kasuku | mbayuwayu | njiwa | atakayefuga |

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| dhati | madhara | ndege | ninayempenda |

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Eleza ni kwa nini mwandishi anampenda kasuku kulingana na ubeti wa kwanza.
2. Taja ndege wanaolinganishwa na kasuku.
3. Ni ndege gani wenye maringo?
4. Anayetaka kufuga kasuku anashauriwa afanye nini?

Sarufi: Vihusishi

**Tunga sentensi kulingana na picha ukitumia vihusishi "chini ya" au "juu ya".**

1. 2. 3. 4.

49 Hakiuzwi

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha. Andika neno **kasuku** ubaoni.

1. Uliza maana ya neno.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi wawaelezee wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno hilo.

Rudia zoezi ukitumia maneno haya: **mbayuwayu, njiwa ata kayefuga.**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **mbayuwayu, njiwa**]

**U:** Wanafunzi wanasoma maneno mapya kwenye **ukurasa wa 49.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** Soma kichwa cha shairi na wanafunzi. Jadili picha. waulize wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma shairi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

### Kusimulia Hadithi




**N:** Chora umbo la nyumba ubaoni. Waulize wanafunzi maswali yafuatayo huku ukiwaelekeza ipasavyo.

**T/U:** [Kichwa cha shairi ni nini? Shairi hili linafanyika wapi? Shairi hili linazungumzia nini sana? Nini kinafanyika katika ubeti wa kwanza? Ni nini kinafuata? Ni ushauri gani tunapata katika ubeti wa mwisho?]

**N:** Kariria darasa lote shairi.

**U:** [Kariria mwenzako shairi.]

### Maswali

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Eleza ni kwa nini mwandishi anampenda kasuku kulingana na ubeti wa kwanza. (Kwa sababu ni ndege wa ajabu.)

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

# Kipindi cha 48: Ndege Nimpendaye 1

Kipindi cha 48 na 49 **Ndege Nimpendaye**

**Shairi**

**Ndege Ninayempenda**





Salamu natanguliza, ya moyoni niwajuze,
Mandhari ya kutuliza, chini ya mti mujikalize,
Mwenyezi Mungu kaumba, nafsiyo kaitulize,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Kanga na mbayuwayu, darajale sifikie,
Haya njiwa afugwaye, karibu asimfikie,
Maneno mengi aigayo, hasira nyingi takuondolea,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Wenye uzuri na umbo, wavutiao machoni,
Heroe tausi wana mambo, maringo wao mwendoni,
Siwapi langu jambo, rohoni niwaweken,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Atakayefuga kasuku, lishe tamwandalia,
Tundu lake madhubuti, juu ya mti katulia,
Uhuru wake ni dhati, kukupasha aloyakalia,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.



Kipindi cha 48 na 49 **Ndege Nimpendaye**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kasuku mbayuwayu njiwa atakayefuga

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

dhati madhara ndege ninayempenda


**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Eleza ni kwa nini mwandishi anampenda kasuku kulingana na ubeti wa kwanza.
2. Taja ndege wanaolinganishwa na kasuku.
3. Ni ndege gani wenye maringo?
4. Anayetaka kufuga kasuku anashauriwa afanye nini?

**Sarufi: Vihusishi**

**Tunga sentensi kulingana na picha ukitumia vihusishi "chini ya" au "juu ya".**






Hakiuzwi

2. Taja ndege wanaolinganishwa na kasuku. (Njiwa)
3. Ni ndege gani wenye maringo? (Heroe na tausi)
4. Anayetaka kufuga kasuku anashauriwa afanye nini? (Amwandalie lishe)

### Sarufi: Vihusishi 'juu ya', 'chini ya'

**N:** [Vihusishi ni maneno tuarifu zaidi kuhusu nomino na mazingira yake.]

**T:** [Tunga sentensi kulingana na picha ukitumia vihusishi.]

**U:** [(Waelekeze wanafunzi watunge sentensi katika **ukurasa wa 49** kutoka kwenye picha zilizochorewa.)]

**Majibu**

1. Kisu kiko chini ya meza
2. Kikombe kiko juu ya meza
3. Kitabu kiko juu ya meza.
4. Ndege yuko chini ya mti.

### Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentesi nne ukitumia vihusishi '**chini ya**' na '**juu ya**'

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 49: Ndege Nimpendaye 1

Kipindi cha 48 na 49 **Ndege Nimpendaye**

**Shairi**

**Ndege Ninayempenda**





Salamu natanguliza, ya moyoni niwajuze,
Mandhari ya kutuliza, chini ya mti mujikalize,
Mwenyezi Mungu kaumba, nafsiyo kaitulize,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Kanga na mbayuwayu, darajale sifikie,
Haya njiwa afugwaye, karibu asimfikie,
Maneno mengi aigayo, hasira nyingi takuondolea,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Wenye uzuri na umbo, wavutiao machoni,
Heroe tausi wana mambo, maringo wao mwendoni,
Siwapi langu jambo, rohoni niwawekeni,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Atakayefuga kasuku, lishe tamwandalia,
Tundu lake madhubuti, juu ya mti katulia,
Uhuru wake ni dhati, kukupasha aloyakalia,
Kasuku ndege ajabu, ndege ninayempenda.

Mali ya Serikali ya Kenya 48

Kipindi cha 48 na 49 **Ndege Nimpendaye**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kasuku mbayuwayu njiwa atakayefuga

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

dhati madhara ndege ninayempenda


**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Eleza ni kwa nini mwandishi anampenda kasuku kulingana na ubeti wa kwanza.
2. Taja ndege wanaolinganishwa na kasuku.
3. Ni ndege gani wenye maringo?
4. Anayetaka kufuga kasuku anashauriwa afanye nini?

**Sarufi: Vihusishi**

**Tunga sentensi kulingana na picha ukitumia vihusishi "chini ya" au "juu ya".**




49 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **dhati, sanduku, madhara, mwendo**. Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya

**N:** Maneno haya yana sauti **dh** na **nd**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **dhati, sanduku** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: dhati, sanduku**

**U: madhara, mwendo**

**U:** Wanafunzi wanasoma maneno katika **ukurasa wa 49.**

## Kusoma Matini: Shairi

**T:** Nani anakumbuka tulijifunza nini wakati uliopita. Tulijifunza kuhusu **Ndege Ninayempenda.**

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

### Shairi - Kuchapisha

Waulize wanafunzi 2-3 wasimame na kusoma nakala zao.


Waulize wanafunzi 2-3 waseme walichofurahia kuhusu nakala zilizosomwa.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora ndege umpendaye na umpake rangi.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 50: Ndege Nimpendaye 1



Kipindi cha 50 **Ndege Nimpendaye**

**Tathmini ya Msamiati**

**Tunga sentensi ukitumia majina ya ndege wafuatao.**

1. batamzinga
2. vijiwa
3. kasuku
4. kuku

**Tathmini ya Sarufi**

**Tunga sentensi mbili ukitumia kihusishi "chini ya" na mbili ukitumia kihusishi "juu ya".**

1. ______________________________.
2. ______________________________.
3. ______________________________.
4. ______________________________.

**Tazama maneno yaliyomo kwenye gurudumu la maneno. Soma maneno hayo haraka iwezekanavyo huku mwenzako akihesabu kutoka moja hadi kumi.**



Mali ya Serikali ya Kenya 50

## Msamiati

Fungua vitabu vyenu **ukurasa wa 50.**

Tunga sentensi ukutumia majina ya ndege uliopewa.

## Kusoma Maneno

**U:** Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **dhati, ndege, madhara, ninayempenda, sanduku, mbayuwayu, nyasi, nyumbani, kwenye, mwendo.**

## Kuchambua Matini: Mhusika

**T:** [Je, mhusika katika shairi ni nani?

Ndiyo, mhusika katika shairi ni mtu au mnyama anayezungumziwa kwenye hadithi. Wiki hii tulisoma mashairi mawili. Je mashairi haya mawili yalihusu nini? *(Waruhusu wanafunzi 2-3 kushiriki kusoma huku ukiwaelekeza.)*

Leo tutarejelea mashairi tuliyoyasoma ili tutambue wahusika waliomo. Hebu turejelee shairi la kwanza **ukurasa wa 46.** Wahusika ni akina nani? *Bata, batamzinga na kuku.*Hebu tusome ubeti wa kwanza pamoja. *(Soma ubeti wa kwanza pamoja na wanafunzi.)*

Ni mhusika gani amekupendeza? Kwa nini amekupendeza? Hebu tuandike sentensi moja au mbili kuhusu wahusika tunaowapenda. *Andika yafuatayo huku ukizungumzia kuhusu wahusika.* Mhusika aliyenipendeza zaidi ni kuku, kwa sababu hutupa mayai.]

**U:** Sasa ni zamu yako. Hebu tulitazame shairi la pili kwenye **ukurasa wa 48.** Je, wahusika ni akina nani? Sasa chagua mhusika unayempenda. Andika sentensi moja au mbili kumhusu. Toa sababu zako za kumpenda mhusika huyu.

## Sarufi: Vihusishi

**U:** [Vihusishi ni maneno yanayotuarifu zaidi kuhusu uhusiano wa nomino na mazingira yake. Unda sentensi sahihi ukitumia vihusishi 'chini ya' na 'juu ya' kisha uandike sentensi hizo kwenye daftari lako.]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi tatu kuhusu mhusika mkuu kwenye hadithi ya **Ndege Nimpendaye.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 51: Marejeleo 2

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 2**

Matini

**Umewahi Kumwona Pomboo?**



Jina langu ni Sasha. Wakati wa likizo, nilimtembelea shangazi Helena anayeishi Mombasa. Alinipa kitabu chake kipya ambacho kilikuwa na picha za wanyama wa majini. Nilipotazama picha, niliingiwa na hamu ya kwenda kuwaona wanyama hao baharini. Nilimwomba shangazi anipeleke kisha jioni, tukaenda na yeye ufuoni. Tulipofika ufuoni, tuliwaona watu wengi. Meli kubwa kutoka taifa jirani ilipita ikielekea kutia nanga bandarini mwetu. "Meli hii kubwa itatia nanga bandarini mwetu," Wavuvi walisema.

Baadaye, nilisikia kelele kutoka upande wa kulia. Hatua kama thelathini hivi mbele yangu, niliona kioja. Samaki mkubwa alikuwa akiruka juu ya maji. Mvuvi mmoja alisema, "Lo! Pomboo. Mnyama mwenye kasi ajabu."

Nilipigwa na butwaa. Kumbe pomboo anaogelea kwa kasi majini! Ngozi yake ilimetameta kama dhahabu. Macho yake yalikuwa meupe kama theluji. Nilimwangalia pomboo huyo akiruka baharini, nikampenda. Nilitamani kuwa mwanaharakati wa kulinda viumbe wa baharini na kuacha ndoto yangu ya kuwa daktari.

Jioni tuliporudi nyumbani, nilimsimulia mjomba yote kumhusu pomboo. Mjomba alicheka na kusema, "Sasha, baharini kuna viumbe wengi." Baadaye shangazi aliandaa vyakula vya aina nyingi tukala na kulala.



Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

taifa pomboo daktari

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kipya kiumbe ndoto vyakula

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Sasha alimtembelea nani Mombasa?
2. Taja sifa mbili za pomboo.
3. Ni viumbe gani wengine wanaopatikana baharini?
4. Unafikiria meli ilikuwa imebeba nini?

Sarufi: Vimilikishi -angu, -ako, -ake

**Chagua kimilikishi sahihi kujaza mapengo: changu, lako, chake, yangu.**

1. Alinipa kitabu ____________.
2. Kichwa ____________ si kikubwa.
3. Shangazi ____________ alicheka kwa furaha.
4. Jembe ____________ limepotea.



## Msamiati

Jadili picha. Andika neno **taifa** ubaoni.

1. Waulize wanafunzi maana ya neno.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi wawaeleze wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno **taifa.**

Rudia zoezi na maneno haya: **pomboo, daktari.**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno taifa.]

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya katika **ukurasa wa 52.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Maswali**

1. N: Sasha alimtembelea nani Mombasa? (Shangazi yake)
2. T: Taja sifa tatu za pomboo. (Kubali sifa zozote tatu.)
3. U: Ni viumbe gani wengine wanaopatikana baharini? (Kubali jibu lolote sahihi.)
4. U: Unafikiria meli ilikuwa imebeba nini? (Kubali jibu lolote sahihi.)

## Sarufi: Vimilikishi: -angu, -ako na -ake

**N:** [Kimilikishi ni neno linaloonyesha kitu ni cha nani. Mifano ya vimilikishi ni: changu, chako, chake, chetu.]

**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye vimilikishi kutoka kwenye hadithi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.

**U:** Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi zenye vimilikishi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tumia maneno haya kujaza mapengo: langu, yake, wako.

1. Mama ________ alimpeleka hospitalini. (yake)
2. Mkoba ________ utaanguka. (wake)
3. Jino ________ limevunjika. (langu)
4. Kisugudi ________ kimeumia. (chake)
5. Kalamu ________ imepotea. (yake)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 2**

Matini

**Umewahi Kumwona Pomboo?**



Jina langu ni Sasha. Wakati wa likizo, nilimtembelea shangazi Helena anayeishi Mombasa. Alinipa kitabu chake kipya ambacho kilikuwa na picha za wanyama wa majini. Nilipotazama picha, niliingiwa na hamu ya kwenda kuwaona wanyama hao baharini. Nilimwomba shangazi anipeleke kisha jioni, tukaenda na yeye ufuoni. Tulipofika ufuoni, tuliwaona watu wengi. Meli kubwa kutoka taifa jirani ilipita ikielekea kutia nanga bandarini mwetu. "Meli hii kubwa itatia nanga bandarini mwetu," Wavuvi walisema.

Baadaye, nilisikia kelele kutoka upande wa kulia. Hatua kama thelathini hivi mbele yangu, niliona kioja. Samaki mkubwa alikuwa akiruka juu ya maji. Mvuvi mmoja alisema, "Lo! Pomboo. Mnyama mwenye kasi ajabu."

Nilipigwa na butwaa. Kumbe pomboo anaogelea kwa kasi majini! Ngozi yake ilimetameta kama dhahabu. Macho yake yalikuwa meupe kama theluji. Nilimwangalia pomboo huyo akiruka baharini, nikampenda. Nilitamani kuwa mwanaharakati wa kulinda viumbe wa baharini na kuacha ndoto yangu ya kuwa daktari.

Jioni tuliporudi nyumbani, nilimsimulia mjomba yote kumhusu pomboo. Mjomba alicheka na kusema, "Sasha, baharini kuna viumbe wengi." Baadaye shangazi aliandaa vyakula vya aina nyingi tukala na kulala.


Hakiuzwi

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

taifa pomboo daktari

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kipya kiumbe ndoto vyakula

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Sasha alimtembelea nani Mombasa?
2. Taja sifa mbili za pomboo.
3. Ni viumbe gani wengine wanaopatikana baharini?
4. Unafikiria meli ilikuwa imebeba nini?

Sarufi: Vimilikishi -angu, -ako, -ake

**Chagua kimilikishi sahihi kujaza mapengo: changu, lako, chake, yangu.**

1. Alinipa kitabu ____________.
2. Kichwa ______________ si kikubwa.
3. Shangazi ________________ alicheka kwa furaha.
4. Jembe ________________ limepotea.

Mali ya Serikali ya Kenya


## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **kipya, kiumbe, ndovu, vya.**

Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua nini kuhusu maneno haya.

**N:** Maneno haya yana sauti **nd, mb, vy** na **py**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **kipya** na **viumbe**. Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: kipya, viumbe**

**U: nduru, vya**

**U:** Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 52**.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** [Nani anakumbuka tulijifunza nini wakati uliopita. Tulijifunza kuhusu **Umewahi Kumwona Pomboo**?]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vimilikishi 'angu'; -'ako'-'ake'

**T:** [Kimilikishi ni neno linaloonyesha kitu ni cha nani. Ni nani anajua neno sahihi la kujaza pengo? Vizuri, hebu tujaribu sentensi ya pili pamoja.

**U:** [Sasa tutazame sentensi zilizoko kwenye **ukurasa wa 52**. Jaza mapengo kwa kutumia vimilikishi sahihi vilivyotolewa.]

**Majibu**

1. changu/chake
2. changu/chake
3. yangu
4. lako

## Kuandika

**Maelezo - Kupanga**

**T:** Panga na wanafunzi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Nakili maneno haya mara tatu kisha uyasome.

**mpya, vyema, kamba, waliandamana**

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Mali ya Serikali ya Kenya

# Kipindi cha 53: Marejeleo 2

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 2**

**Matini**

**Nyanja na Matoi**



Nyanja na Matoi walikuwa marafiki wa dhati. Siku moja, walitumwa dukani kununua kamba mpya ya kumfunga ng'ombe. "Tufunge bembea," alisema Matoi mara tu walipoinunua kamba yao. Matoi alipanda mtini na Nyanja akamtupia kamba afunge kwenye tawi. Kwa bahati mbaya, tawi lilivunjika. Matoi alianguka chini, pu! "Nisaidie!" Matoi alilia.

Nyanja alimkimbilia ili kumpa huduma ya kwanza. Baadaye, alienda kumwita mama yake. Al kutana na Mama Matoi njiani akienda mtoni. "Matoi ameanguka. Ameumia," alisema Nyanja huku akilia. Nyanja na Mama Matoi waliandamana hadi alipokuwa Matoi. Matoi alipomwona mama yake, alimlilia kwa uchungu. "Mama! Mkono wangu! Nimegongwa kisugudi."

Mama alimfunga Matoi kitambaa safi ili asivuje damu. Wote watatu waliandamana hadi kwenye zahanati. Tarishi alimwita nesi. Nesi akamkagua Matoi. Aliona jeraha lake ni dogo. Aliliosha jeraha kwa dawa na akalifunga bendeji. Baada ya sekunde chache, daktari alifika na kumwangalia Matoi vyema. Akasema, "Mnaweza kumpeleka nyumbani." Wakitoka pale langoni walimpata bawabu aliyewatakia afueni ya haraka.

Wakiwa njiani kuelekea nyumbani, Matoi alimwomba mama yake msamaha. Mama alimsamehea na kumkanya kutoshiriki katika michezo kama hiyo.

53 Hakiuzwi

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| tarishi | nesi | daktari | bawabu |

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| mpya | vyema | kamba | waliandamana |

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni nani aliyepanda mtini?
2. Kamba ilikuwa ya kufanyia nini?
3. Mtu akiumia, husaidiwa vipi?
4. Hadithi hii inakufunza nini?

**Sarufi: Vimilikishi -angu, -ako, -ake**

**Tumia vimilikishi sahihi kujaza nafasi: langu, yake, wako, chake.**

1. Mama ________ alimpeleka hospitalini.
2. Mkoba ______ utaanguka.
3. Jino ________ limevunjika.
4. Kisugudi _______ kimeumia.
5. Kalamu ________ imepotea.

Mali ya Serikali ya Kenya 54

## Msamiati

Jadili picha. Andika neno **tarishi** ubaoni.

1. Uliza maana.
2. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
3. Waulize wanafunzi wawaeleze wenzao maana.
4. Waulize wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno.

Rudia zoezi na maneno haya: **nesi, daktari, bawabu**.

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **tarishi**.]

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya kwenye **ukurasa wa 54.**

## Kusoma Matini: Masimulizi

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

### Maswali

1. N: Ni nani aliyepanda mtini? (Matoi )
2. T: Kamba ilikuwa ni ya nini? (Kumfunga ng'ombe)
3. U: Mtu akiumia, husaidiwa vipi? (Hupewa huduma ya kwanza)
4. U: Hadithi hii inatufunza nini? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Vimilikishi 'angu ' '-ako' '-ake'

**N:** [Kimilikishi ni neno linaloonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano chao, chenu, chake.]

**T:** Tumia vimilikishi sahihi kujaza nafsi.

**U:** Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi zenye vimilikishi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tumia maneno haya kujaza nafasi: langu, yake, wako, chake.

1. Babu __________ amepata nafuu. (yake)
2. Mpira __________ umepotea. (wako)
3. Jiji __________ ni kubwa sana. (langu)
4. Kiti __________ kimepotea (chake)

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 2**

**Matini**

**Nyanja na Matoi**



Nyanja na Matoi walikuwa marafiki wa dhati. Siku moja, walitumwa dukani kununua kamba mpya ya kumfunga ng'ombe. "Tufunge bembea," alisema Matoi mara tu walipoinunua kamba yao. Matoi alipanda mtini na Nyanja akamtupia kamba afunge kwenye tawi. Kwa bahati mbaya, tawi lilivunjika. Matoi alianguka chini, pu! "Nisaidie!" Matoi alilia.

Nyanja alimkimbilia ili kumpa huduma ya kwanza. Baadaye, alienda kumwita mama yake. Al kutana na Mama Matoi njiani akienda mtoni. "Matoi ameanguka. Ameumia," alisema Nyanja huku akilia. Nyanja na Mama Matoi waliandamana hadi alipokuwa Matoi. Matoi alipomwona mama yake, alimlilia kwa uchungu. "Mama! Mkono wangu! Nimegongwa kisugudi."

Mama alimfunga Matoi kitambaa safi ili asivuje damu. Wote watatu waliandamana hadi kwenye zahanati. Tarishi alimwita nesi. Nesi akamkagua Matoi. Aliona jeraha lake ni dogo. Aliliosha jeraha kwa dawa na akalifunga bendeji. Baada ya sekunde chache, daktari alifika na kumwangalia Matoi vyema. Akasema, "Mnaweza kumpeleka nyumbani." Wakitoka pale langoni walimpata bawabu aliyewatakia afueni ya haraka.

Wakiwa njiani kuelekea nyumbani, Matoi alimwomba mama yake msamaha. Mama alimsamehea na kumkanya kutoshiriki katika michezo kama hiyo.

53 Hakiuzwi

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

tarishi nesi daktari bawabu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

mpya vyema kamba waliandamana

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni nani aliyepanda mtini?
2. Kamba ilikuwa ya kufanyia nini?
3. Mtu akiumia, husaidiwa vipi?
4. Hadithi hii inakufunza nini?

**Sarufi: Vimilikishi -angu, -ako, -ake**

**Tumia vimilikishi sahihi kujaza nafasi: langu, yake, wako, chake.**

1. Mama ________ alimpeleka hospitalini.
2. Mkoba ______ utaanguka.
3. Jino ________ limevunjika.
4. Kisugudi _______ kimeumia.
5. Kalamu ________ imepotea.

Mali ya Serikali ya Kenya 54

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **mpya, vyema, mbaya, ndani**

Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.

**N:** Maneno haya yana sauti **py, vy, nd** na **mb.** Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: mpya, vyema**

**T/U: mbaya, ndani**

**U:** Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 54**.

## Kusoma Matini: Masimulizi

**N:** [Nani anakumbuka tulijifunza nini wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **Nyanja na Matoi.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Maelezo - Kupanga**

U: Wanafunzi wapange watakavyoandika.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo:

1. nesi
2. tarishi
3. daktari
4. bawabu

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 55: Marejeleo 2

Kipindi cha 55 **Marejeleo 2**

**Tathmini ya msamiati**

**Andika sentensi sahihi ukitumia maneno yafuatayo.**

1. pomboo 2. kasi 3. tarishi
4. sekunde 5. kisugudi

**Tathmini ya sarufi**

**Tumia maneno haya kujaza mapengo: yetu, wenu, yao, yenu, vyetu.**

1. Mikoba _______ ilianguka.
2. Ng'ombe _______ walifungwa kwa kamba.
3. Manesi wa hospitali _______ waliwatibu wagonjwa.
4. Meno _______ ni machafu.
5. Vitabu _______ vimewekwa kwenye maktaba.

**Hadithi ya mwalimu**

**Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.**

Familia ya Ntabo



55 Hakiuzwi

**Familia ya Ntabo (Sehemu ya Kwanza)**

Katika kijiji cha Amani, paliishi Bwana na Bi. Mwema na mjukuu wao Ntabo. Walipendana na kufaana kwa hali na mali. Waliitana rafiki. Waliamka pamoja, wakala pamoja, wakatembea pamoja na kucheka pamoja. Hata walilia pamoja.

Ntabo alisoma darasa la tatu katika shule ya msingi ya Amani. Alipokwenda shuleni, nyanya na babu walimsindikiza hadi kwenye lango la shule. Alipokuwa karibu kurudi nyumbani, walikuja na kumngojea langoni. Waliandamana naye tena hadi nyumbani. Walipoalikwa shuleni, walienda darasani kwa akina Ntabo na kuwasimulia hadithi tamutamu.

Siku moja, Bwana Mwema aliugua homa. Alipata joto jingi mwilini na kuumwa na kichwa. Makamasi yalimdondoka ndo! ndo! ndo! Bi. Mwema alimpeleka hospitalini akatibiwa. Akamwandalia vyakula alivyovipenda, akala. Ntabo naye alimkamulia maji ya limau, akachanganya na tangawizi iliyopondwapondwa, asali na maji moto. Akasema, "Babu, hii hapa dawa ya mafua. Ni tamu kama halua."

Bwana Mwema alipata nafuu kwa dawa na kwa pendo aliloonyeshwa na familia yake. Bwana Mwema alimnunulia mkewe zawadi ya saa iliyometameta kama nyota na kusema, "Rafiki, asante kwa yote uliyonifanyia. Twaa saa hii. Ivae. Popote uendapo, iwapo utanikosa iweke karibu na sikio lako. Ile tik! tak! yake itakukumbusha mdundo wa moyo wangu." Bwana Mwema alimwita Ntabo. Alisema, "Mjukuu wangu, subira huvuta heri. Tulia tuli, utapata mazuri." Akampa zawadi yake. Je, unafikiri alimpa nini?

## Msamiati

[Fungueni **ukurasa wa 55** wa vitabu vyenu. Tazama sehemu ya msamiati. Andika sentensi sahihi ukitumia maneno hayo.]

## Kusoma Maneno

**U:** Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.
Maneno: **kamba, kipya, vyakula, waliandamana, vyema, mpya, kiumbe, ndoto**

## Hadithi ya Mwalimu

**Kabla ya kusoma**

**T:** [Leo mtasikiliza kwa makini nikiwasomea hadithi kisha baadaye tuzungumzie hadithi hiyo tukiandika. Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi kisha tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma hadithi, kuna baadhi ya maneno mapya ambayo tutazungumzia kwanza. Neno la kwanza ni **waliandamana**. Neno hili humaanisha kutembea pamoja. *(Rudia hatua hii na maneno haya:* ***tangawizi iliyopondwapondwa, mdundo****.)*]

**Wakati wa kusoma**

**T:** [Sasa sikiliza kwa makini ninaposoma. Inua mkono wako wa kushoto utakaposikia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia ukisikia neno la pili. *(Soma hadithi kwa ufasaha.) Uliza wanafunzi ni kitu gani amabacho kinaweza kutokea)*]

**Baada ya kusoma**

**T:** [*Uliza maswali yafuatayo)*

1. Je, hadithi hii ilifanyika katika kijiji gani? (Amani)
2. Je, Ntabo alikuwa akisomea katika shule gani? (Amani)
3. Unafikiri ni kwa nini Bwana Mwema alimnunulia Mkewe Zawadi?

Hebu tuandike baadhi ya mambo tuliyoyasoma kwenye hadithi. *(Mwanafunzi aandike sentensi 1-2 kuhusu hadithi ya mwalimu)*]

## Sarufi: Vimilikishi

**T:** [Kimilikishi ni neno linaloonyesha kitu ni cha nani.]
**U:** Fungua kitabu chako **ukurasa wa 55**. Jaza mapengo kwa kutumia kimilikishi sahihi.]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Hadithi tuliyoisoma leo inatufunza nini?

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 56: Sokoni 2

Kipindi cha 56 na 57 **Sokoni 2**

**Matini**

**Soko la Luanda**



Kila kijiji kina soko ambalo watu huenda kuuza na kununua bidhaa. Vijiji vimetengewa siku mbalimbali za soko. Wafanyabiashara husafirisha bidhaa zao kutoka sehemu mbalimbali kupeleka sokoni. Siku ya Jumamosi imetengewa soko la Luanda. Soko hilo ni zuri na lina mpangilio mwema. Kuna majengo mazuri yaliyotengewa madalali. Madalali hung'ang'ana kupata nafasi sokoni. Ndani ya majengo hayo kuna vibanda vilivyojengewa madalali. Wafanyabiashara ambao hukosa nafasi hubakia kuwa wachuuzi kutembeza bidhaa zao.

Vibanda hutumiwa kuuzia mboga, matunda, nguo na hata nafaka. Asubuhi na mapema wauzaji na wanunuzi hufurika sokoni. Watu hupenda kununua nafaka kama vile dengu, maharagwe na mchele kwa bei nafuu. Wanunuzi wengine hununua bidhaa ili waziuze katika masoko mengine. Mnunuzi ana uhuru wa kutembea kila mahali sokoni ili achague bidhaa zinazompendeza.

Soko la Luanda lina vibanda vingi vya kuuzia nguo. Wafanyabiashara huuza nguo za kila aina. Wao hutumia mikokoteni kusafirisha bidhaa zao. Wanunuzi pia hutumia mbinu hiyohiyo kupeleka bidhaa zao nje ya soko. Serikali ya kaunti hufurahishwa na jinsi biashara inavyoendelezwa katika soko la Luanda. Baadaye wateja hurudi nyumbani wakiwa wamejaza bidhaa ndani ya vikapu vyao. Wachuuzi na madalali hupata faida kubwa. Biashara huwa na faida nyingi kwa mtu binafsi na kwa jamii nzima.



Kipindi cha 56 na 57 **Sokoni 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

hufurika madalali vibanda

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vimetengewa majengo hung'ang'ana dengu

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Soko lililotajwa katika hadithi ni gani?
2. Wafanyabiashara hutumia nini kusafirisha bidhaa zao?
3. Taja nafaka zilizotajwa katika hadithi.
4. Unafikiri ni kwa nini watu hufurika sokoni?

**Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'**

**Tumia vihusishi "ndani ya" au "nje ya" kujaza pengo.**

1. Amejaza bidhaa ___________ kikapu.
2. ___________ jengo hilo kuna kibanda cha dalali.
3. Mchuuzi hutembeza bidhaa zake ___________ soko.
4. Dalali yuko ___________ duka.



## Msamiati

Jadili picha.

1. Andika neno **hufurika** ubaoni.
2. Uliza maana.
3. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
4. Waulize wanafunzi wawaeleze wenzao maana.
5. Waagize wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno.

Rudia zoezi na maneno haya: **madalali, vibanda**

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya **ukurasa wa 57**.

## Kusoma Matini: Maelezo

**N:** [Leo tutasoma matini ya maelezo.]

**T/U:** Soma kichwa cha makala. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri.


**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

### Ramani Dhana

Chora ramani dhana



**T:** [Sasa tutajadili tuliyoyasoma kuhusu **Soko la Luanda.** Tutatumia ramani dhana. Je, ni nani anaweza kutueleza kuhusu **Soko la Luanda**?]

[Nitachora ramani dhana na kuandika ndani ya duara. *Andika 'Soka la Luanda' ndani ya duara.* Ni nani atakayeongezea jambo lingine kuhusu soko la Luanda? Waelekeze wanafunzi.]

Kwa kila wazo jipya unaliweka kwenye kisanduku kipya.

**U:** [Sasa ni wakati wa kuandika sentensi itakayotoa maelezo kuhusu soko la Luanda.]

### Maswali

*Wanafunzi wajibu maswali yafuatayo iwapo kuna muda.*

1. Soko lililotajwa katika hadithi ni gani? (Luanda)
2. Wafanyabiashara hutumia nini kusafirisha bidhaa zao? (Mkokoteni)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 56 na 57 **Sokoni 2**

**Matini**

**Soko la Luanda**



Kila kijiji kina soko ambalo watu huenda kuuza na kununua bidhaa. Vijiji vimetengewa siku mbalimbali za soko. Wafanyabiashara husafirisha bidhaa zao kutoka sehemu mbalimbali kupeleka sokoni. Siku ya Jumamosi imetengewa soko la Luanda. Soko hilo ni zuri na lina mpangilio mwema. Kuna majengo mazuri yaliyotengewa madalali. Madalali hung'ang'ana kupata nafasi sokoni. Ndani ya majengo hayo kuna vibanda vilivyojengewa madalali. Wafanyabiashara ambao hukosa nafasi hubakia kuwa wachuuzi kutembeza bidhaa zao.

Vibanda hutumiwa kuuzia mboga, matunda, nguo na hata nafaka. Asubuhi na mapema wauzaji na wanunuzi hufurika sokoni. Watu hupenda kununua nafaka kama vile dengu, maharagwe na mchele kwa bei nafuu. Wanunuzi wengine hununua bidhaa ili waziuze katika masoko mengine. Mnunuzi ana uhuru wa kutembea kila mahali sokoni ili achague bidhaa zinazompendeza.

Soko la Luanda lina vibanda vingi vya kuuzia nguo. Wafanyabiashara huuza nguo za kila aina. Wao hutumia mikokoteni kusafirisha bidhaa zao. Wanunuzi pia hutumia mbinu hiyohiyo kupeleka bidhaa zao nje ya soko. Serikali ya kaunti hufurahishwa na jinsi biashara inavyoendelezwa katika soko la Luanda. Baadaye wateja hurudi nyumbani wakiwa wamejaza bidhaa ndani ya vikapu vyao. Wachuuzi na madalali hupata faida kubwa. Biashara huwa na faida nyingi kwa mtu binafsi na kwa jamii nzima.

Mali ya Serikali ya Kenya

56

Kipindi cha 56 na 57 **Sokoni 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

hufurika madalali vibanda

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vimetengewa majengo hung'ang'ana dengu

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Soko lililotajwa katika hadithi ni gani?
2. Wafanyabiashara hutumia nini kusafirisha bidhaa zao?
3. Taja nafaka zilizotajwa katika hadithi.
4. Unafikiri ni kwa nini watu hufurika sokoni?

**Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'**

**Tumia vihusishi "ndani ya" au "nje ya" kujaza pengo.**

1. Amejaza bidhaa ___________ kikapu.
2. ___________ jengo hilo kuna kibanda cha dalali.
3. Mchuuzi hutembeza bidhaa zake ___________ soko.
4. Dalali yuko ___________ duka.

57

Hakiuzwi

3. Taja nafaka zilizotajwa katika hadithi. (Ndengu, maharagwe na mchele)
4. Ni kwa nini watu hufurika sokoni? (Kubali jibu sahihi.)

## Sarufi: Vihusishi: 'nje ya', 'ndani ya'

**N:** Mifano ya vihusishi ni: **nje ya, ndani ya** na kadhalika.

**T:** Wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye vihusishi kwenye hadithi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.

**U:** Wanafunzi watunge sentensi wakitumia vihusishi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Jaza pengo kwa kutumia 'ndani ya' au 'nje ya'**

1. Pesa ziko ____________ mfuko. (ndani ya)
2. Ulimi uko ____________ kinywa. (ndani ya)
3. Ng'ombe yuko ____________ nyumba. (nje ya)
4. Pua iko ____________ kinywa. (nje ya)

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 57: Sokoni 2

Kipindi cha 56 na 57 **Sokoni 2**

**Matini**

**Soko la Luanda**



Kila kijiji kina soko ambalo watu huenda kuuza na kununua bidhaa. Vijiji vimetengewa siku mbalimbali za soko. Wafanyabiashara husafirisha bidhaa zao kutoka sehemu mbalimbali kupeleka sokoni. Siku ya Jumamosi imetengewa soko la Luanda. Soko hilo ni zuri na lina mpangilio mwema. Kuna majengo mazuri yaliyotengewa madalali. Madalali hung'ang'ana kupata nafasi sokoni. Ndani ya majengo hayo kuna vibanda vilivyojengewa madalali. Wafanyabiashara ambao hukosa nafasi hubakia kuwa wachuuzi kutembeza bidhaa zao.

Vibanda hutumiwa kuuzia mboga, matunda, nguo na hata nafaka. Asubuhi na mapema wauzaji na wanunuzi hufurika sokoni. Watu hupenda kununua nafaka kama vile dengu, maharagwe na mchele kwa bei nafuu. Wanunuzi wengine hununua bidhaa ili waziuze katika masoko mengine. Mnunuzi ana uhuru wa kutembea kila mahali sokoni ili achague bidhaa zinazompendeza.

Soko la Luanda lina vibanda vingi vya kuuzia nguo. Wafanyabiashara huuza nguo za kila aina. Wao hutumia mikokoteni kusafirisha bidhaa zao. Wanunuzi pia hutumia mbinu hiyohiyo kupeleka bidhaa zao nje ya soko. Serikali ya kaunti hufurahishwa na jinsi biashara inavyoendelezwa katika soko la Luanda. Baadaye wateja hurudi nyumbani wakiwa wamejaza bidhaa ndani ya vikapu vyao. Wachuuzi na madalali hupata faida kubwa. Biashara huwa na faida nyingi kwa mtu binafsi na kwa jamii nzima.

Mali ya Serikali ya Kenya 56

Kipindi cha 56 na 57 **Sokoni 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

hufurika madalali vibanda

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vimetengewa majengo hung'ang'ana dengu

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Soko lililotajwa katika hadithi ni gani?
2. Wafanyabiashara hutumia nini kusafirisha bidhaa zao?
3. Taja nafaka zilizotajwa katika hadithi.
4. Unafikiri ni kwa nini watu hufurika sokoni?

**Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'**

**Tumia vihusishi "ndani ya" au "nje ya" kujaza pengo.**

1. Amejaza bidhaa __________ kikapu.
2. __________ jengo hilo kuna kibanda cha dalali.
3. Mchuuzi hutembeza bidhaa zake __________ soko.
4. Dalali yuko __________ duka.

57 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**T:** Andika maneno haya ubaoni: **vimetengewa, ngo'mbe, majengo, nguo, ng'ara**
Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya:
**N:** Maneno haya yana sauti ng na ng' Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **vimetengewa** *na* **ngo'mbe.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.)
**N/T/U: vimetengewa, ng'ombe.**
**U: nguo, ngára.**
**U:** Wanafunzi wanasoma maneno katika **ukurasa wa 57.**

## Kusoma Matini: Maelezo

**N:** [Nani anakumbuka nini tulijifunza wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **Soko la Luanda.**]
**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'

**T:** [Mifano ya vihusishi ni 'nje ya' na 'ndani ya'. Soma sentensi ya kwanza. Ni nani anajua jibu sahihi?
**U:** [Vizuri, hebu tujaribu sentensi kutoka **ukurasa wa 57** *(Rejelea sentensi zote).*]

**Majibu**

1. Amejaza bidhaa ndani ya kikapu.
2. Ndani ya jengo hilo kuna kibanda cha madalali.
3. Machuuzi hutembeza bidhaa zake nje ya soko.
4. Dalali yuko nje ya duka.

## Kuandika

**Maelezo - Nakala ya Kwanza**

**T:** [Leo tutaanza kuandika hadithi ya maelezo. Je, hadithi za maelezo ni nini? Vizuri, uandishi wa maelezo hueleza kuhusu mtu, shughuli ama jinsi jambo hufanywa kwa hatua. Tunapopanga uandishi wa maelezo tutafikiria kuhusu mambo manne. Hebu tujaribu kufanya sote:

1. Unatoa maelezo kuhusu nini?
2. Umbo lake ni lipi?
3. Hisia zako ni zipi?
4. Ina sauti ya aina gani?

*(Uliza kila swali huku ukitilia maanani michango ya wanafunzi. Andika majibu yao ubaoni na uyahifadhi kwa ajili ya wiki ifuatayo.)*]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Kamilisha sentensi zifuatazo ukitumia jibu sahihi kutoka kwenye mabano.**

1. Machungwa yako ________ kikapu. (**ndani ya,** juu ya)
2. Mchuuzi amesimama ________ kibanda. (chini ya, **kando ya**)
3. Mkokoteni uko __________ nyumba. (juu ya, **nje ya**)
4. Maria ameketi __________ duka. (chini ya, **ndani ya**)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 58: Sokoni 2

Kipindi cha 58 na 59 **Sokoni 2**

**Matini**

**Siku ya Soko**



Alhamisi ni siku ya soko katika kijiji cha Ng'uuni. Watu kutoka sehemu mbalimbali huja sokoni kufanya biashara. Wauzaji na wanunuzi hufanya shughuli mbalimbali. Kila mfanyabiashara hupatiwa risiti langoni baada ya kulipa ada ya soko. Wauzaji huhakikisha kuwa bidhaa zao zinawavutia wanunuzi. Watu wengine hutembea ndani ya soko kuangalia kinachotendeka.

Kuna wauzaji ambao huuza bidhaa kwa jumla na wengine kwa rejareja. Wauzaji wa mifugo kama vile kuku, ng'ombe,mbuzi na kondoo hufika sokoni asubuhi na mapema. Dalali hupiga kengele ili kuwavutia wateja. Wanunuzi wengi hukusanyika na kutaja bei wanazopenda kununulia wanyama hao. Mnunuzi anayetaja bei inayofaa huuziwa. Soko la wanyama hufanya vizuri sana.

Aina tofauti za matunda hupatikana sokoni. Wachuuzi huuza matunda kama vile nazi, machungwa, mapapai, tikitimaji na maembe. Mboga kama vile mchicha, sukumawiki, kabeji, kunde na mnavu hupatikana sokoni. Watu wengi hununua mboga za kienyeji. Vilevile, wao hununua nyama kwenye buchari. Katika buchari, nyama hupimwa kwa ratili.

Vibanda vya nguo nje ya soko vina wateja wengi pia. Akina mama huwapeleka watoto wao sokoni kuwanunulia nguo. Wakipata nguo zinazowafurahisha, wao hujipima ili kuhakikisha kwamba zinanawatoshea. Wauzaji wote hupata faida.

Mali ya Serikali ya Kenya



Kipindi cha 58 na 59 **Sokoni 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

dalali risiti ratili

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

ng'ombe kengele kuangalia Ng'uuni

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Siku ya soko ya Ng'uuni huwa ni siku gani?
2. Dalali hufanya kazi gani sokoni?
3. Eleza kazi ya ratili.
4. Taja aina za bidhaa zinazopatikana sokoni.

**Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'**

**Jaza pengo kwa kutumia "ndani ya" au "nje ya".**

1. Soko likifungwa wanunuzi hutoka __________ soko.
2. Bidhaa huletwa sokoni zikiwa __________ mkokoteni.
3. Wauzaji huweka pesa zao __________ mkoba.
4. Ng'ombe huuzwa __________ maduka.



Hakiuzwi

## Msamiati

Jadili picha.

1. Andika neno **dalali** ubaoni.
2. Uliza maana.
3. Tunga sentensi ukitumia neno kuonyesha maana.
4. Waulize wanafunzi waeleze wenzao maana.
5. Waulize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia neno.

Rudia zoezi na maneno haya: **risiti, ratili.**

**U:** [Sasa ni zamu yenu. Andika sentensi moja kwenye daftari lako ukitumia neno **dalali.**]

**U:** Wanafunzi wasome maneno mapya **ukurasa wa 59.**

## Kusoma Matini: Maelezo

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.


**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

### Ramani Dhana

Chora ramani dhana



**T:** [Tutajadili tuliyoyasoma kuhusu siku ya soko. Tutatumia ramani dhana. Ni nani anakumbuka kuhusu makala ya siku ya soko? Nitachora ramani dhana. *Andika 'Siku ya soko' ndani ya duara.* Ni nani anaweza kuongezea jambo lingine? (*Kwa kila wazo jipya, andika kwa kisanduku kipya. Waelekeze wanafunzi kuunda sentensi.*)]

**U:** Sasa ni wakati wa kuandika sentensi itakayotoa maelezo kuhusu siku ya soko.

### Maswali

*Wanafunzi wajibu maswali yafuatayo iwapo kuna muda.*

1. Siku ya soko ya Ng'uuni huwa ni siku gani? (Alhamisi)
2. Dalali hufanya kazi gani sokoni? (Hupiga kengele.)
3. Eleza kazi ya ratili. (Kupima bidhaa kama nyama,mchele)
4. Taja aina za bidhaa zinazopatikana sokoni. (Kubali jibu lolote sahihi.)

## Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'

**T:** [Mifano ya vihusishi ni 'nje ya' na 'ndani ya'. Fungua kitabu **ukurasa wa 59** sehemu ya sarufi. Ni neno gani sahihi tunaweza kutumia kujaza pengo kwenye sentensi? *(Waulize wanafunzi wajibu huku ukiwapa mwongozo.)*]

**U:** [Andika sentensi huku ukijaza mapengo kwa neno sahihi katika daftari lako hadi ukamilishe hadi zoezi katika **ukurasa wa 59.**]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Jadiliana na mlezi wako kuhusu soko lililoko mjini mwenu.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 59: Sokoni 2

Kipindi cha 58 na 59 **Sokoni 2**

**Matini**

### Siku ya Soko



Alhamisi ni siku ya soko katika kijiji cha Ng'uuni. Watu kutoka sehemu mbalimbali huja sokoni kufanya biashara. Wauzaji na wanunuzi hufanya shughuli mbalimbali. Kila mfanyabiashara hupatiwa risiti langoni baada ya kulipa ada ya soko. Wauzaji huhakikisha kuwa bidhaa zao zinawavutia wanunuzi. Watu wengine hutembea ndani ya soko kuangalia kinachotendeka.

Kuna wauzaji ambao huuza bidhaa kwa jumla na wengine kwa rejareja. Wauzaji wa mifugo kama vile kuku, ng'ombe,mbuzi na kondoo hufika sokoni asubuhi na mapema. Dalali hupiga kengele ili kuwavutia wateja. Wanunuzi wengi hukusanyika na kutaja bei wanazopenda kununulia wanyama hao. Mnunuzi anayetaja bei inayofaa huuziwa. Soko la wanyama hufanya vizuri sana.

Aina tofauti za matunda hupatikana sokoni. Wachuuzi huuza matunda kama vile nazi, machungwa, mapapai, tikitimaji na maembe. Mboga kama vile mchicha, sukumawiki, kabeji, kunde na mnavu hupatikana sokoni. Watu wengi hununua mboga za kienyeji. Vilevile, wao hununua nyama kwenye buchari. Katika buchari, nyama hupimwa kwa ratili.

Vibanda vya nguo nje ya soko vina wateja wengi pia. Akina mama huwapeleka watoto wao sokoni kuwanunulia nguo. Wakipata nguo zinazowafurahisha, wao hujipima ili kuhakikisha kwamba zinanawatoshea. Wauzaji wote hupata faida.

Mali ya Serikali ya Kenya 58

Kipindi cha 58 na 59 **Sokoni 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

dalali risiti ratili

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

ng'ombe kengele kuangalia Ng'uuni

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Siku ya soko ya Ng'uuni huwa ni siku gani?
2. Dalali hufanya kazi gani sokoni?
3. Eleza kazi ya ratili.
4. Taja aina za bidhaa zinazopatikana sokoni.

**Sarufi: Vihusishi 'ndani ya' na 'nje ya'**

**Jaza pengo kwa kutumia "ndani ya" au "nje ya".**

1. Soko likifungwa wanunuzi hutoka __________ soko.
2. Bidhaa huletwa sokoni zikiwa __________ mkokoteni.
3. Wauzaji huweka pesa zao __________ mkoba.
4. Ng'ombe huuzwa __________ maduka.

59 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**N:** Andika maneno haya ubaoni: **ng'ombe, kengele, kuangalia, Ng'uuni, ng'ambo, anguka.**

Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.

**N:** Maneno haya yana sauti **ng** na **ng'**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **ng'ombe** na **kengele.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: ng'ombe, kengele**

**U: ng'ambo, anguka**

**U:** Wanafunzi wanasoma maneno katika **ukurasa wa 59.**

## Kusoma Matini: Maelezo

**N:** [Nani anakumbuka tulichojifunza wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **Siku ya Soko.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

### Maelezo - Nakala ya Kwanza

**T:** [Leo ni zamu yako kupanga jinsi ya kuandika hadithi ya maelezo. Je, hadithi ya maelezo ni nini?]

**U:** [Kwenye vitabu vyenu mtayajibu maswali yafuatayo ili kupanga mtakavyoandika wiki ijayo:

1. Unatoa maelezo kuhusu nini?
2. Umbo lake ni lipi?
3. Hisia zako ni zipi?
4. Kina sauti ya aina gani?


*(Wasaidie wanafunzi kuyajibu maswali vitabuni mwao.)*]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika insha fupi kuhusu soko lililoko mjini mwenu.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 60: Sokoni 2



Kipindi cha 60 **Sokoni 2**

Tathmini ya msamiati

**Chagua maana sahihi ya maelezo uliyopewa katika sentensi.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ratili | buchari | faida | kunadi |

1. Mapato baada ya kuuza kitu na kuondoa gharama.
2. Mahali panapouzwa nyama.
3. Kifaa cha kupimia uzito.
4. Kutangaza bei kwa sauti kubwa.

Tathmini ya Sarufi

**Jaza pengo kwa kutumia kihusishi sahihi 'ndani ya' au 'nje ya'.**

1. Wanafunzi wanacheza _______________ uwanja.
2. Maji yamo _______________ pipa.
3. Wakati wa mapumziko wanafunzi walitoka _______________ darasa.
4. Zizi la ng'ombe hujengwa _______________ nyumba.

Mali ya Serikali ya Kenya 60

## Msamiati

[Fungueni wa **ukurasa wa 60** vitabu vyenu.
Tazama sehemu ya msamiati.
Kuna maelezo ya sentensi na maneno.
Ambatanisha neno na maana sahihi.]

**Majibu**

1. faida 2. buchari 3. ratili 4. nadi

## Kusoma Maneno

**U:** Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika katika madaftari yao.

**Maneno**: bidhaa, vibanda, mchuuzi, mkokoteni, faida, buchari, ratili, dalali, risiti

## Kuchambua Matini: Kusimulia Hadithi

**T:** [Leo tutarejelea hadithi tuliyoisoma na kuisimulia tena. Kwanza, hebu tujikumbushe tulichokisoma wiki hii. *(Waelekeze wanafunzi kukumbuka hadithi walizozisoma)*.]

**U:** [Msimulie mwenzako ulichojifunza kutokana na hadithi uliyoipenda. Jibu maswali haya matatu:

1. Hadithi inahusu nini hasa?
2. Ni nini kilichokufurahisha katika hadithi?
3. Je, unajua nini kingine kuhusu mada?]

## Sarufi: Vihusishi 'ndani ya'na 'njeya'

**U:** [Vihusishi ni maneno yanoyoonyesha uhusiano zaidi baina ya nomino na mazingira yake. Fungua wa **ukurasa wa 60** kitabu chako. Andika sentensi kitabuni mwako huku ukijaza mapengo kwa kutumia neno sahihi.]

**Majibu**

a. nje ya/ndani ya
b. ndani ya
c. nje ya
d. nje ya

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Tunga sentensi nne ukitumia maneno haya:**

1. ndani ya
2. nje ya
3. juu ya
4. chini ya

Tarehe: _______________ Muda: _______________ Idadi: _______________



Hakiuzwi

Kipindi cha 61 na 62 **Shambani 2**

Matini

**Kilimo cha Miti**

Kilimo cha miti kimepata umaarufu mwingi nchini. Miti hutumika kuhifadhi mazingira. Miti ni muhimu kwani inatupa mbao, kuni na kutengeneza vyombo mbalimbali. Je, utaanzisha vipi kilimo cha miti? Unachohitaji ni shamba la kupanda miti. Unaweza kununua au kukodisha shamba. Kwanza, fyeka shamba kwa kutumia kifyekeo. Kisha, tumia shoka kukata vipande vya miti mikubwa vilivyobaki shambani. Baadaye, lima na upande miche ya miti kwenye mistari. Miti inapoendelea kukua inafaa kunyunyiziwa maji isikauke. Baadaye, utaipalilia na kuitunza hadi itakapokua.



Kilimo cha miti ni rahisi kwa sababu hakihitaji plau kulima wala ghala la kuhifadhi mavuno mkulima anapovuna. Yeye huwauzia wateja miti kutoka shambani. Wateja hao hutumia miti hiyo kwa njia mbalimbali.

Zaidi ya hayo, unaweza kufuga nyuki katika shamba la miti. Nyuki huhitaji maji tu. Hawahitaji kutunzwa kama m fugo wengine. Ukifanya hivyo utaendelea kuvuna asali huku ukisubiri kupasua mbao katika shamba lao. Kilimo cha miti kina faida kubwa kwa maisha ya baadaye. Je,wewe unapenda kilimo gani?

61 Hakiluzwi

Kipindi cha 61 na 62 **Shambani 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

plau shoka kuvuna

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

unafyeka kwenye kwanza kifyekeo

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kwa nini kilimo cha miti kimepata umaarufu mwingi nchini?
2. Unafikiri mbao hutumiwa kufanya nini?
3. Taja vitu ambavyo hutahitaji unapofanya kilimo cha miti.
4. Taja aina nyingine ya mimea unayoijua.

Sarufi: Nafsi ya tatu, wakati ujao-Umoja na wingi

**Andika sentensi katika umoja au wingi kwa kutumia kiambishi '-ta'.**

| Umoja: -ta | Wingi: -ta |
|---|---|
| 1. ________________ | Vifyekeo vyao vitatumika shambani. |
| 2. Yeye atauza miti ikikua. | ________________ |
| 3. ________________ | Maghala yatajengwa na mafundi wao. |
| 4. Upanga wake utatumiwa kukata mti. | ________________ |

Mali ya Serikali ya Kenya 62

## Msamiati

Jadili picha. Funza maneno ya msamiati: **plau, shoka, kuvuna.**

Soma maneno mapya katika **ukurasa wa 62**

## Kusoma Matini: Maelezo


**N/T:** [Ninani anakumbuka nini tulifunza wakati uliopita? Tulifunza kuhusu kilimo cha miti.]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Ufahamu

**Ramani Dhana**

Chora ramani dhana



**N:** [Hebu tujadili tuliyoyasoma. Tulisoma kuhusu **Kilimo cha Miti.** Sasa tutatumia ramani dhana ili itusaidie kuelewa tuliyojifunza. Katikati tutaandika kilimo cha Miti. Je, ni nani anaweza kuniambia makala yalisema nini kuhusu kilimo cha miti? Nitachora mfano wa mkono hapa na kuandika ndani ya duara. Ni nani mwingine anaweza kuongeza jambo jingine kuhusu makala tuliyoyasoma? Jambo hilo linasikikaje? Linavutia vipi? *(Kwa kila wazo jipya unaliweka kwenye kisanduku kipya. Wanafunzi wakimaliza kutoa maelezo yao, waelekeze kuandika sentensi.)*

**U:** Sasa ni wakati wa kuandika sentensi ya kutoa maelezo kuhusu **Kilimo cha miti.**]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Kwa nini kilimo cha miti kimepata umaarufu nchini? (Kuhifadhi mazingira, kutoa mbao na kuni na kutengeneza vyombo.)
2. Unafikiri mbao hutumiwa kufanya nini? Kubali jibu sahihi.)
3. Taja vitu ambavyo utahitaji unapofanya kilimo cha miti. (shamba)
4. Taja aina nyingine ya mimea unayoijua. (Kubali jibu sahihi)

## Sarufi: Nafsi ya tatu

**N:** [Nasfi ni kiwakilishi cha mtu wa kwanza, wa pili au wa tatu, kwa mfano, mimi, wewe, yeye. *Soma sentensi kutoka kwenye matini.*]

**T:** Andika sentensi na wanafunzi.

**U:** Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Nakili maneno haya na umsomee mlezi wako**

1. ghala 2. kwekwe 3. fyeka 4. nyunyiza 5. ghamu

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

Kipindi cha 61 na 62 **Shambani 2**

Matini

**Kilimo cha Miti**

Kilimo cha miti kimepata umaarufu mwingi nchini. Miti hutumika kuhifadhi mazingira. Miti ni muhimu kwani inatupa mbao, kuni na kutengeneza vyombo mbalimbali. Je, utaanzisha vipi kilimo cha miti? Unachohitaji ni shamba la kupanda miti. Unaweza kununua au kukodisha shamba. Kwanza, fyeka shamba kwa kutumia kifyekeo. Kisha, tumia shoka kukata vipande vya miti mikubwa vilivyobaki shambani. Baadaye, lima na upande miche ya miti kwenye mistari. Miti inapoendelea kukua inafaa kunyunyiziwa maji isikauke. Baadaye, utaipalilia na kuitunza hadi itakapokua.



Kilimo cha miti ni rahisi kwa sababu hakihitaji plau kulima wala ghala la kuhifadhi mavuno mkulima anapovuna. Yeye huwauzia wateja miti kutoka shambani. Wateja hao hutumia miti hiyo kwa njia mbalimbali.

Zaidi ya hayo, unaweza kufuga nyuki katika shamba la miti. Nyuki huhitaji maji tu. Hawahitaji kutunzwa kama m fugo wengine. Ukifanya hivyo utaendelea kuvuna asali huku ukisubiri kupasua mbao katika shamba lao. Kilimo cha miti kina faida kubwa kwa maisha ya baadaye. Je,wewe unapenda kilimo gani?

61 Hakiuzwi

Kipindi cha 61 na 62 **Shambani 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

plau shoka kuvuna

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

unafyeka kwenye kwanza kifyekeo

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kwa nini kilimo cha miti kimepata umaarufu mwingi nchini?
2. Unafikiri mbao hutumiwa kufanya nini?
3. Taja vitu ambavyo hutahitaji unapofanya kilimo cha miti.
4. Taja aina nyingine ya mimea unayoijua.

Sarufi: Nafsi ya tatu, wakati ujao-Umoja na wingi

**Andika sentensi katika umoja au wingi kwa kutumia kiambishi '-ta'.**

| Umoja: -ta | Wingi: -ta |
|---|---|
| 1. ____________________ | Vifyekeo vyao vitatumika shambani. |
| 2. Yeye atauza miti ikikua. | ____________________ |
| 3. ____________________ | Maghala yatajengwa na mafundi wao. |
| 4. Upanga wake utatumiwa kukata mti. | ____________________ |

Mali ya Serikali ya Kenya 62

### Kusoma Maneno

**N:** Andika maneno haya ubaoni: **unafyeka, kwenye, fyeko, kwetu**

**T:** Funza sauti **fy** na **kw**

Wanafunzi wasome maneno **ukurasa wa 62.**

### Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

### Sarufi: Nafsi

**N:** [Nafsi ni kiwakilishi cha mtu wa kwanza, wa pili au wa tatu.]

**T/U:** [Tazama **ukurasa wa 64**. Tunga sentensi kwa kutumia nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu.]

### Kuandika

**Maelezo - Kuhakiki**

**T:** Nakili makala ya maelezo.

Andika sentensi ya kwanza.

Andika sentensi kutokana na maswali yaliyoulizwa wakati wa kupanga uandishi huu.

Andika sentensi ya mwisho ya kuhitimisha.

### Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika sentensi hizi katika wakati ujao**

1. Mwanafunzi anapewa zawadi. (Mwanafunzi **atapewa** zawadi.)
2. Mwalimu anasomesha vizuri. (Mwalimu **atasomesha** vizuri.)
3. Mtoto anapenda andazi. (Mtoto **atapenda** andazi.)
4. Mkulima anafyeka nyasi. (Mkulima **atafyeka** nyasi.)
5. Ali anaenda safari. (Ali **ataenda** safari.)

Tarehe: ____________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

Kipindi cha | 63 na 64 | **Shambani 2**

**Matini**

**Shamba la Bwana na Bi. Nakitare**



Bwana na Bi. Nakitare wanaishi katika kijiji cha Miambani. Shambani mwao kuna ng'ombe, ngamia, mbuzi na hata mbwa. Kila msimu kuna kazi mbalimbali shambani. Katika msimu huu wa kupanda, watatumia kifyekeo kukata magugu shambani. Iwapo kazi ni nyingi, watawaita walio na trekta kuwalimia kwa malipo.

Katika kipindi cha kupalilia, watafanya kazi shambani na watoto wao watatu: Ali, Mueni na Wafula. Hali ya hewa ikiwa nzuri wataweza kuvuna mazao mengi ya aina mbalimbali. Mazao haya yatauzwa kwa bei ghali. Yale yatakayobaki yatawekwa kwenye ghala.

Bi. Nakitare hutumia upanga kuwakatia mifugo wake majani mororo kutoka shambani. Vilevile, yeye hutumia panga pia kuwakatia ngamia wake matawi yenye majani matamu.

Msimu uliopita, Bwana na Bi. Nakitare walilitayarisha shamba lao. Bwana Nakitare akamwambia Bi. Nakitare, "Tukilima kwa bidii tutapata mavuno mengi." Walipanda mahindi shambani mwao. Waliweza kuvuna magunia mia moja ya mahindi na kuyaweka kwenye ghala. Siku moja, wanunuzi kutoka mjini walikuja na kuyanunua kwa bei ghali. Baadaye, Bwana Nakitare aliwalipia watoto wake nauli ya kwenda Mombasa kwani hawakuwa wamewahi kuutembelea mji huo. Msimu huu, Bwana Nakitare amewaahidi watoto wake kuwa atawapeleka nchi jirani iwapo watafanya bidii shambani na shuleni.

63 Hakiuzwi

Kipindi cha | 63 na 64 | **Shambani 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kifyekeo kupalilia tukilima

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

yatawekwa kwani kifyekeo chafya

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja wanyama walio shambani mwa Bwana na Bi. Nakitare.
2. Ni kipindi gani kilichotajwa katika hadithi?
3. Ni kifaa gani kilitumika kukata magugu shambani?
4. Upanga unaweza kutumika kufanya kazi gani nyingine?

**Sarufi: Nafsi ya tatu, wakati ujao-Umoja na wingi**

**Tunga sentensi sahihi ukitumia nafsi hizi.**

1. sisi
2. wao
3. yeye
4. nyinyi

**Kuandika**

**Andika insha kuhusu umuhimu wa wanyama wa shambani.**

Mali ya Serikali ya Kenya 64

## Msamiati

Jadili picha. Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati: **kifyekeo, kupalilia, tukilima**

Funza maneno ya msamiati.

Soma maneno mapya katika **ukurasa 64.**

## Kusoma Matini: Maelezo


**N/T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha.

Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

### Ramani Dhana

Chora ramani dhana.



[Tumemaliza kusoma makala yetu. Hebu sasa tujadili tuliyoyasoma. Tulisoma kuhusu **Shamba la Bwana na Bi. Nakitare.** Sasa tutatumia ramani dhana ili itusaidie kuelewa tuliyojifunza. Katikati tutaandika **Shamba la Bwana na Bi. Nakitare.** Je, ni nani anaweza kuniambia makala yalisema nini kuhusu shamba la bwana na bi nakitete? Nitachora mfano wa mkono hapa na kuandika ndani ya duara. Ni nani mwingine anaweza kuongeza jambo lingine kuhusu makala tuliyoyasoma?

Jambo hilo linasikikaje? Linavutia vipi? *(Kwa kila wazo jipya unaliweka kwa kisanduku kipya.*]

**T:** Wanafunzi wakimaliza kutoa maelezo yao, waelekeze kuandika sentensi.)

**U:** [Sasa ni wakati wa kuandika sentensi ya kutoa maelezo kuhusu Shamba la Bwana na Bi. Nakitare.]

**Maswali**]

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Taja wanyama walio shambani mwa Bwana na Bi. Nakitare.(ngo'mbe, ngamia, mbuzi, mbwa)
2. Ni kipindi gani kilichotajwa katika hadithi? (kupalilia)
3. Ni kifaa gani kilitumika kukata magugu shambani? (kifyekeo)
4. Upanga unaweza kutumika kufanya kazi gani nyingine? (kukata majani)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 63 na 64 **Shambani 2**

Matini

**Shamba la Bwana na Bi. Nakitare**



Bwana na Bi. Nakitare wanaishi katika kijiji cha Miambani. Shambani mwao kuna ng'ombe, ngamia, mbuzi na hata mbwa. Kila msimu kuna kazi mbalimbali shambani. Katika msimu huu wa kupanda, watatumia kifyekeo kukata magugu shambani. Iwapo kazi ni nyingi, watawaita walio na trekta kuwalimia kwa malipo.

Katika kipindi cha kupalilia, watafanya kazi shambani na watoto wao watatu: Ali, Mueni na Wafula. Hali ya hewa ikiwa nzuri wataweza kuvuna mazao mengi ya aina mbalimbali. Mazao haya yatauzwa kwa bei ghali. Yale yatakayobaki yatawekwa kwenye ghala.

Bi. Nakitare hutumia upanga kuwakatia mifugo wake majani mororo kutoka shambani. Vilevile, yeye hutumia panga pia kuwakatia ngamia wake matawi yenye majani matamu.

Msimu uliopita, Bwana na Bi. Nakitare walilitayarisha shamba lao. Bwana Nakitare akamwambia Bi. Nakitare, "Tukilima kwa bidii tutapata mavuno mengi." Walipanda mahindi shambani mwao. Waliweza kuvuna magunia mia moja ya mahindi na kuyaweka kwenye ghala. Siku moja, wanunuzi kutoka mjini walikuja na kuyanunua kwa bei ghali. Baadaye, Bwana Nakitare aliwalipia watoto wake nauli ya kwenda Mombasa kwani hawakuwa wamewahi kuutembelea mji huo. Msimu huu, Bwana Nakitare amewaahidi watoto wake kuwa atawapeleka nchi jirani iwapo watafanya bidii shambani na shuleni.

63

Hakiuzwi

Kipindi cha 63 na 64 **Shambani 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kifyekeo kupalilia tukilima

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

yatawekwa kwani kifyekeo chafya

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja wanyama walio shambani mwa Bwana na Bi. Nakitare.
2. Ni kipindi gani kilichotajwa katika hadithi?
3. Ni kifaa gani kilitumika kukata magugu shambani?
4. Upanga unaweza kutumika kufanya kazi gani nyingine?

Sarufi: Nafsi ya tatu, wakati ujao-Umoja na wingi

**Tunga sentensi sahihi ukitumia nafsi hizi.**

1. sisi
2. wao
3. yeye
4. nyinyi

Kuandika

**Andika insha kuhusu umuhimu wa wanyama wa shambani.**

Mali ya Serikali ya Kenya

64

## Sarufi: Nafsi

**T/U:** Nafsi ni kiwakilishi cha mtu wa kwanza, wa pili, au wa tatu. Soma sentensi.

**T:** Andika sentensi pamoja na wanafunzi.

**U:** Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika wingi wa nafsi hizi.**

1. mimi (sisi)
2. wewe (nyinyi)
3. yeye (wao)
4. yule (wale)

Andika insha kuhusu umuhimu wa wanyama shambani.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 64: Shambani 2

Kipindi cha 63 na 64 **Shambani 2**

Matini

**Shamba la Bwana na Bi. Nakitare**



Bwana na Bi. Nakitare wanaishi katika kijiji cha Miambani. Shambani mwao kuna ng'ombe, ngamia, mbuzi na hata mbwa. Kila msimu kuna kazi mbalimbali shambani. Katika msimu huu wa kupanda, watatumia kifyekeo kukata magugu shambani. Iwapo kazi ni nyingi, watawaita walio na trekta kuwalimia kwa malipo.

Katika kipindi cha kupalilia, watafanya kazi shambani na watoto wao watatu: Ali, Mueni na Wafula. Hali ya hewa ikiwa nzuri wataweza kuvuna mazao mengi ya aina mbalimbali. Mazao haya yatauzwa kwa bei ghali. Yale yatakayobaki yatawekwa kwenye ghala.

Bi. Nakitare hutumia upanga kuwakatia mifugo wake majani mororo kutoka shambani. Vilevile, yeye hutumia panga pia kuwakatia ngamia wake matawi yenye majani matamu.

Msimu uliopita, Bwana na Bi. Nakitare walilitayarisha shamba lao. Bwana Nakitare akamwambia Bi. Nakitare, "Tukilima kwa bidii tutapata mavuno mengi." Walipanda mahindi shambani mwao. Waliweza kuvuna magunia mia moja ya mahindi na kuyaweka kwenye ghala. Siku moja, wanunuzi kutoka mjini walikuja na kuyanunua kwa bei ghali. Baadaye, Bwana Nakitare aliwalipia watoto wake nauli ya kwenda Mombasa kwani hawakuwa wamewahi kuutembelea mji huo. Msimu huu, Bwana Nakitare amewaahidi watoto wake kuwa atawapeleka nchi jirani iwapo watafanya bidii shambani na shuleni.

63 Hakiuzwi

Kipindi cha 63 na 64 **Shambani 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kifyekeo kupalilia tukilima

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

yatawekwa kwani kifyekeo chafya

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja wanyama walio shambani mwa Bwana na Bi. Nakitare.
2. Ni kipindi gani kilichotajwa katika hadithi?
3. Ni kifaa gani kilitumika kukata magugu shambani?
4. Upanga unaweza kutumika kufanya kazi gani nyingine?

Sarufi: Nafsi ya tatu, wakati ujao-Umoja na wingi

**Tunga sentensi sahihi ukitumia nafsi hizi.**

1. sisi
2. wao
3. yeye
4. nyinyi

Kuandika

**Andika insha kuhusu umuhimu wa wanyama wa shambani.**

Mali ya Serikali ya Kenya 64

## Kusoma Maneno

N: Andika maneno haya ubaoni: **yatawekwa, fyata, kifyekeo, kwenda, kwake, chafya**

Funza sauti **fy, kw**

Soma maneno **ukurasa wa 64.**

## Kusoma Matini: Maelezo

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Maelezo - Kuhakiki**

**U:** Nakili makala ya maelezo.

Andika sentensi ya kwanza.

Andika sentensi kutokana na maswali yaliyoulizwa wakati wa kupanga uandishi huu.

Andika sentensi ya mwisho ya kuhitimisha.


## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Jaza nafasi kwa kutumia kiambishi cha wakati **na, me** au **ta**

1. Shamba li____fyekwa. (Shamba litafyekwa.)
2. Shamba li____fyekwa. (Shamba limefyekwa.)
3. Mashamba ya____fyekwa. (Mashamba yatafyekwa.)
4. Mashamba ya____fyekwa. (Mashamba yamefyekwa.)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 65: Shambani 2



Kipindi cha 65 **Shambani 2**

Tathmini ya msamiati

**Andika majina ya vifaa vifuatavyo.**

1. ____________
2. ____________
3. ____________
4. ____________

Tathmini ya sarufi

**Unda sentensi kwa kuambatanisha kiwakilishi cha wakati sahihi na maneno mengine.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Jana mama a_ | na | fyeka nyasi. |
| 2. Sasa Daudi a_ | ta | chinjwa. |
| 3. Kesho ng'ombe a_ | li | lima shamba. |

65 Hakiuzwi

## Tathmini ya Msamiati

**U:** [Andika majina ya vifaa vilivyochorwa katika **ukurasa wa 65**.]

## Kusoma Maneno


**N:** Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **yatawekwa, chafya, kifyekeo, kwenda, fyonza, fyeka, fyatuke, kupalilia, yatawekwa, plau**

## Kuchambua Matini

**Ramani Dhana**

Chora ramani dhana



**N/T/U:** [Leo tutatengeneza ramani dhana. Chagua makala yaliyokufurahisha kisha uchore ramani kuhusu lengo la makala hayo. Zungumzia mambo matatu muhimu. Andika sentensi kuhusu mada uliyochagua. Ramani dhana hufanana hivi: (*Onyesha wanafunzi mfano wa ramani dhana.*)]

## Tathmini ya Sarufi: Nafsi

**U:** [Fungueni **ukurasa wa 65** vitabu vyenu. Ambatanisha sentensi na kiwakilishi sahihi cha wakati.]

**Majibu**

1. Jana mama alilima shamba.
2. Sasa Daudi anafyeka nyasi.
3. Kesho ng'ombe atachinjwa.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora mchoro wa shambani ambao unaonyesha mimea na wanyama mbalimbali.

## Mapendekezo ya shughuli za huduma ya jamii zinazochangia ujifunzaji

Shiriki katika kulima ama kufyeka nyumbani.

## Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji

Shiriki katika vikundi vya ushirika shuleni vinavyohusu ukulima au shiriki kilimo shuleni.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 66 na 67 **Uzalendo 2**

Matini

**Mwananchi Mzalendo**



Mwananchi mzalendo ni mtu anayeipenda nchi yake. Mzalendo huwa tayari kuilinda na kuipigania nchi yake kwa kila hali. Mzalendo huwajibika na kuheshimu sheria na kat ba ya nchi yake. Mwananchi mzalendo ana jukumu la kufanya kazi kwa bidii kila siku ili kulijenga taifa lake. Kwa mfano, kuna wakati ambapo hatari ilitanda milimani na mabondeni. Wananchi walikuwa na uwoga wa vita na wa kuuawa na wazungu. Koitalel Arap Samoei aliliongoza jeshi lake kupigana na wakoloni. Wakoloni hawa walikuja kunyakua mashamba ya nchi yetu. Koitalel Arap Samoei na wenzake walikuwa wazalendo. Waliipenda nchi yao. Wakaamua kukabiliana na mkoloni kwa sababu ya kuitetea nchi yao.

Mzalendo pia ana jukumu la kulinda mali na siri za nchi yake. Kudumisha amani, upendo na umoja ni nguzo muhimu katika maisha ya mzalendo. Mzalendo anaiheshimu bendera ya taifa lake na kuimba wimbo wa taifa kwa heshima. Ni jukumu letu kama wazalendo kusaidia katika kutafuta suluhisho kwa matatizo yanayoikumba nchi yetu. Wakati wa majanga kama vile njaa, mafuriko na ukame tunapaswa kuwa katika mstari wa mbele kuwasaidia wengine. Tunafaa kuungana na raia wengine ili kuwasaidia waathiriwa. Kila mwaka tunafaa kushiriki sherehe za kitaifa kama siku ya Madaraka na Jamhuri ambapo tunashuhudia gwaride la jeshi linaloendeleza sherehe hizi. Mwananchi mzalendo huiwakilisha nchi yake katika michezo ya kitaifa na kimataifa.

Mali ya Serikali ya Kenya 66

Kipindi cha 66 na 67 **Uzalendo 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

mzalendo raia umoja gwaride

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

mwananchi mwaka kuimba yanayoikumba

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Mzalendo ni mtu gani?
2. Mzalendo huwajibika na kuiheshimu ________ na ________ ya nchi yake.
3. Ni kwa nini Koitalel Arap Samoei alipigana na wakoloni?
4. Taja mambo ambayo yatakufanya kuwa mzalendo halisi.

Sarufi: Vimilikishi –ake na –ao

**Tambua vimilikishi katika sentensi hizi.**

1. Mtoto wake anaitwa Amina.
2. Nyumba yao imejengwa vizuri.
3. Kiatu chake ni kizuri.
4. Nchi yao ina wanariadha wengi.

67 Hakizwi

## Msamiati

Jadili picha. Funza maneno ya msamiati: **mzalendo, raia, umoja, gwaride.** Soma maneno mapya katika **ukurasa wa 62.**

## Kusoma Matini: Maelezo

**T/U:** Soma kichwa cha makala. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## ? Ufahamu

### Maswali

1. Mzalendo ni mtu gani? (Mtu anayeipenda nchi yake.)
2. Mzalendo huwajibika na kuheshimu _____ na ___ ya nchi yake. (sheria na katiba.)
3. Kwa nini Koitatel Arap Samoei alipigana na wakolonihalisi? (Ili kuwazuia kunyakua mashamba yao.)
4. Taja mambo ambazo yatakufanya kuwa mzalendo?

(Kubali jibu lolote sahihi.)

## Sarufi: Vimilikishi -ake na -ao.

**N:** [Vimilikilishi ni maneno yanayotumika kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano yake, wake, wao, yao.]

**T:** Waulize wanafunzi wasome mifano ya sentensi zenye vimilikishi kutoka kwenye hadithi. Andika sentensi pamoja na wanafunzi.

**U:** Waelekeze wanafunzi watunge sentensi wakitumia vimilikishi vilivyo katika hadithi waliyosoma.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi nne ukitumia kimilikishi –ake pamoja na maneno haya.


(kikombe, meza, kuku, bendera)

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 66 na 67 **Uzalendo 2**

Matini

**Mwananchi Mzalendo**



Mwananchi mzalendo ni mtu anayeipenda nchi yake. Mzalendo huwa tayari kuilinda na kuipigania nchi yake kwa kila hali. Mzalendo huwajibika na kuheshimu sheria na katiba ya nchi yake. Mwananchi mzalendo ana jukumu la kufanya kazi kwa bidii kila siku ili kulijenga ta fa lake. Kwa mfano, kuna wakati ambapo hatari ilitanda milimani na mabondeni. Wananchi walikuwa na uwoga wa vita na wa kuuawa na wazungu. Koitalel Arap Samoei aliliongoza jeshi lake kupigana na wakoloni. Wakoloni hawa walikuja kunyakua mashamba ya nchi yetu. Koitalel Arap Samoei na wenzake walikuwa wazalendo. Waliipenda nchi yao. Wakaamua kukabiliana na mkoloni kwa sababu ya kuitetea nchi yao.

Mzalendo pia ana jukumu la kulinda mali na siri za nchi yake. Kudumisha amani, upendo na umoja ni nguzo muhimu katika maisha ya mzalendo. Mzalendo anaiheshimu bendera ya ta fa lake na kuimba wimbo wa taifa kwa heshima. Ni jukumu letu kama wazalendo kusaidia katika kutafuta suluhisho kwa matatizo yanayoikumba nchi yetu. Wakati wa majanga kama vile njaa, mafuriko na ukame tunapaswa kuwa katika mstari wa mbele kuwasaidia wengine. Tunafaa kuungana na raia wengine ili kuwasaidia waathiriwa. Kila mwaka tunafaa kushiriki sherehe za kitaifa kama s ku ya Madaraka na Jamhuri ambapo tunashuhudia gwaride la jeshi linaloendeleza sherehe hizi. Mwananchi mzalendo huiwakilisha nchi yake katika michezo ya kitaifa na kimataifa.

Mali ya Serikali ya Kenya 66

Kipindi cha 66 na 67 **Uzalendo 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

mzalendo raia umoja gwaride

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

mwananchi mwaka kuimba yanayoikumba

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Mzalendo ni mtu gani?
2. Mzalendo huwajibika na kuiheshimu _______ na _______ ya nchi yake.
3. Ni kwa nini Koitalel Arap Samoei alipigana na wakoloni?
4. Taja mambo ambayo yatakufanya kuwa mzalendo halisi.

Sarufi: Vimilikishi –ake na –ao

**Tambua vimilikishi katika sentensi hizi.**

1. Mtoto wake anaitwa Amina.
2. Nyumba yao imejengwa vizuri.
3. Kiatu chake ni kizuri.
4. Nchi yao ina wanariadha wengi.

67 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**N/T:** Andika maneno haya ubaoni:
**mwananchi, mwaka, mwamba, kizimba**
Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.
**N:** Maneno haya yana sauti **mw** na **mb**. Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **mwananchi** na **mwaka**. Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini ilikuonyesha sauti na silabi husika.
**N/T/U: mwananchi, mwaka**
**U: mwamba, kizimba**
**U:** Wanafunzi wasome maneno katika **ukurasa wa 67.**

## Kusoma Matini: Maelezo

**N/T:** [Nani anakumbuka tulijifunza nini wakati uliopita?Tulijifunza kuhusu **Mwananchi Mzalendo.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vimilikishi –ake na –ao.

**T/N:** [Vimilikishi ni maneno yanayoonyesha kitu ni cha nani kwa mfano, chao, zetu, vyetu. *Soma sentensi ya kwanza. Tambua kimilikishi katika sentensi hiyo.*]
**U:** Rudia kwa kurejelea sentensi zote.

**Majibu**
1. wake 2. yao 3. chake 4. yao

## Kuandika

### Maelezo - Kuhariri

**T:** [Leo tutaanza kuandika hadithi ya maelezo.
Je, hadithi za maelezo ni hadithi za aina gani? Vizuri, uandishi wa maelezo hueleza kuhusu mtu, shughuli ama jinsi jambo hufanywa kwa hatua. Tunapopanga uandishi wa maelezo tutafikiria kuhusu maswali haya manne. Hebu tujaribu kufanya sote:

1. Unatoa maelezo kuhusu nini?
2. Umbo lake ni vipi?
3. Hisia zako ni zipi?
4. Kina sauti ya aina gani?

*(Uliza kila swali huku ukitilia maanani michango ya wanafunzi. Andika majibu yao ubaoni na uyahifadhi kwa ajili ya wiki lifuatayo.)*]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Jaza mapengo kwa kutumia kimilikishi **–ake** au **–ao** kwa usahihi.

1. Alinipa kitabu _________. (chake, wake)
2. Kalamu _________ imepotea. (zake, yake)
3. Mikoba _________ ni mizuri. (yao, wake)
4. Tarakilishi _________ imeharibika. (chao, yao)

**Majibu**
1. chake 2. yake 3. yao 4. yao

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 68 na 69 **Uzalendo 2**

Matini

**Mwanariadha Shupavu**



Jepkemei ni mwanariadha shupavu kutoka katika kijiji cha Londiani. Yeye hufanya bidii katika kukuza kipaji chake cha kukimbia mbio za masafa marefu. Wanafunzi katika jamii yake na nchi nzima wanamwona kama kielelezo chema. Ijapokuwa ametoka katika familia maskini, hali hii haijaathiri vibaya hamu yake ya kutaka kufaulu. Jepkemei hurauka asubuhi na mapema kufanya mazoezi katika milima na mabonde ya kijiji chao. Vijana wa kijiji chake humpatia motisha kwa kumsindikiza wakati wa mazoezi yake. Wengine humsaidia kwa nguo na viatu ili atumie wakati wa mazoezi. Kunao wanaompa mawaidha ya lishe bora ili kuimarisha afya yake na kumpa ujuzi wa riadha. Wanakijiji wanatambua kuwa ushirikiano wao utaleta maendeleo makubwa katika eneo lao. Jepkemei akishinda katika mashindano ya kimataifa, sifa zitawaendea wanakijiji pia.

Jepkemei alishiriki mbio za nyika nchini Uingereza mwaka jana na kujishindia nishani ya dhahabu. Bendera ya Kenya ilipeperushwa uwanjani na wimbo wa taifa kuimbwa huko Uingereza. Ushindi huu ulipokelewa kwa shangwe katika taifa la Kenya. Wananchi walimkaribisha kwa nyimbo za kizalendo na kumsifu alipowasili nchini. Rais wa taifa la Kenya alimtuza kwa kuwa mwanariadha bora zaidi nchini. Jepkemei alitumia baadhi ya pesa alizotunukiwa kuisaidia familia yake. Kutokana na upendo mkubwa alio nao kwa wazazi wake, aliwajengea nyumba. Vilevile, alitumia pesa nyingine kujenga shule ya kisasa katika kijiji cha Londiani. Alianzisha vikundi vya kuwashauri vijana wakuze talanta zao ili kujiendeleza kimaisha. Yeye anapenda kuwahimiza vijana washirikiane kujenga taifa.

Mali ya Serikali ya Kenya 68

Kipindi cha 68 na 69 **Uzalendo 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

mwanariadha bendera upendo

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

wimbo kuimbwa mwanariadha wanatambua

Ufahamu

**Jibu maswali haya.**

1. Jepkemei anatoka katika kijiji kipi?
2. Jepkemei alishiriki katika mchezo upi?
3. Ni nani aliyemtuza Jepkemei?
4. Je, wewe hushiriki vipi katika kukuza uzalendo wako?

Sarufi: Kimilikishi -ake na -ao

**Andika wingi wa sentensi zifuatazo ukitumia kimilishi -ao.**

1. Jamii yake iliishi Londiani.
   ________________________________.
2. Talanta yake inamfanya ajiendeleze.
   ________________________________.
3. Ushindi wake ulimfurahisha mwalimu.
   ________________________________.
4. Kijana wa kijiji chake humpatia motisha.
   ________________________________.

69 Hakluzwi

## Msamiati

Jadili picha. Funza maneno ya msamiati: **Bendera, upendo, mwanariadha.** Soma maneno mapya katika **ukurasa wa 69.**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.

## Kusoma Matini: Maelezo

**T:** Soma kichwa cha hadithi pamoja na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri.

**T/U:** Soma hadithi.

**U:** Hakiki utabiri.

## Ufahamu

**Maswali**

1. Jepkemei anatoka katika kijiji kipi? (Kijiji cha Londiani.)
2. Jepkemei alishiriki katika mchezo upi? (Mbio za masafa marefu.)
3. Ni nani aliyemtuza Jepkemei? (Rais wa taifa la Kenya.)
4. Je, wewe hushiriki vipi katika kukuza uzalendo wako? (Kubali jibu lolote sahihi.)

## Sarufi: Vimilikishi –ake na –ao

**N/T:** [Fungua kitabu **ukurasa wa 69** sehemu ya sarufi. Ni neno gani sahihi tunaweza kutumia kujaza pengo kwenye sentensi? *(Waulize wanafunzi wajibu huku ukiwapa mwongozo).*]

**U:** [Andika wingi wa sentensi zifuatazo ukitumia kimilikishi -ao.]

**Majibu**

1. Jamii zao ziliishi Londiani.
2. Talanta zao zinawafanya wajiendeleze.
3. Ushindi wao uliwafurahisha walimu.
4. Vijana wa vijiji vyao huwapa motisha.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi nne ukitumia kimilikishi **–ake** na **– ao**

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 68 na 69 **Uzalendo 2**

Matini

**Mwanariadha Shupavu**



Jepkemei ni mwanariadha shupavu kutoka katika kijiji cha Londiani. Yeye hufanya bidii katika kukuza kipaji chake cha kukimbia mbio za masafa marefu. Wanafunzi katika jamii yake na nchi nzima wanamwona kama kielelezo chema. Ijapokuwa ametoka katika familia maskini, hali hii haijaathiri vibaya hamu yake ya kutaka kufaulu. Jepkemei hurauka asubuhi na mapema kufanya mazoezi katika milima na mabonde ya kijiji chao. Vijana wa kijiji chake humpatia motisha kwa kumsindikiza wakati wa mazoezi yake. Wengine humsaidia kwa nguo na viatu ili atumie wakati wa mazoezi. Kunao wanaompa mawaidha ya lishe bora ili kuimarisha afya yake na kumpa ujuzi wa riadha. Wanakijiji wanatambua kuwa ushirikiano wao utaleta maendeleo makubwa katika eneo lao. Jepkemei akishinda katika mashindano ya kimataifa, sifa zitawaendea wanakijiji pia.

Jepkemei alishiriki mbio za nyika nchini Uingereza mwaka jana na kujishindia nishani ya dhahabu. Bendera ya Kenya ilipeperushwa uwanjani na wimbo wa taifa kuimbwa huko Uingereza. Ushindi huu ulipokelewa kwa shangwe katika taifa la Kenya. Wananchi walimkaribisha kwa nyimbo za kizalendo na kumsifu alipowasili nchini. Rais wa taifa la Kenya alimtuza kwa kuwa mwanariadha bora zaidi nchini. Jepkemei alitumia baadhi ya pesa alizotunukiwa kuisaidia familia yake. Kutokana na upendo mkubwa alio nao kwa wazazi wake, aliwajengea nyumba. Vilevile, alitumia pesa nyingine kujenga shule ya kisasa katika kijiji cha Londiani. Alianzisha vikundi vya kuwashauri vijana wakuze talanta zao ili kujiendeleza kimaisha. Yeye anapenda kuwahimiza vijana washirikiane kujenga taifa.

Mali ya Serikali ya Kenya 68

Kipindi cha 68 na 69 **Uzalendo 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

mwanariadha bendera upendo

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

wimbo kuimbwa mwanariadha wanatambua

Ufahamu

**Jibu maswali haya.**

1. Jepkemei anatoka katika kijiji kipi?
2. Jepkemei alishiriki katika mchezo upi?
3. Ni nani aliyemtuza Jepkemei?
4. Je, wewe hushiriki vipi katika kukuza uzalendo wako?

Sarufi: Kimilikishi -ake na -ao

**Andika wingi wa sentensi zifuatazo ukitumia kimilishi -ao.**

1. Jamii yake iliishi Londiani.
   ________________________________.
2. Talanta yake inamfanya ajiendeleze.
   ________________________________.
3. Ushindi wake ulimfurahisha mwalimu.
   ________________________________.
4. Kijana wa kijiji chake humpatia motisha.
   ________________________________.

69 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

**N:** Andika maneno haya ubaoni:

**wimbo, mwanariadha, ubwabwa, mitambo.**

Waulize wanafunzi ni nini wanaweza kutambua kuhusu maneno haya.

**N:** Maneno haya yana sauti **mb** na **mw.** Eleza tofauti ya sauti ukitumia maneno: **wimbo** na **mwanariadha.** Yasome maneno huku ukipitisha kidole chini kuonyesha sauti na silabi husika.

**N/T/U: wimbo, mwanariadha**

**T/U: ubwabwa, mitambo.**

**U:** Wanafunzi wasome maneno kwenye **ukurasa wa 69.**

## Kusoma Matini: Maelezo

**N:** [Nani anakumbuka tulichojifunza wakati uliopita? Tulijifunza kuhusu **Mwanariadha Shupavu.**]

**U:** Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

### Maelezo - Kuhariri

**T:** [Leo ni zamu yako kuandika hadithi ya maelezo. Je, hadithi ya maelezo ni hadithi ya aina gani?]

**U:** [Jibu maswali huku ukiandika hadithi yako.

Unatoa maelezo kuhusu nini?

Umbo lake ni lipi?

Hisia zake ni zipi?

Ina sauti ya aina gani?


(*Wasaidie wanafunzi kuyajibu maswali vitabuni mwao.*)]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo:

1. Mwananchi
2. Bendera
3. Upendo
4. Raia

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Kipindi cha 70 **Uzalendo 2**

Tathmini ya Sarufi - Vimilikishi

**Tunga sentensi nne ukitumia maneno haya pamoja na kimilikishi -ake.**

1. chungwa
2. kabati
3. chombo
4. mtoto

Hadithi ya mwalimu

**Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.**

Familia ya Ntabo

Mali ya Serikali ya Kenya 70

**Familia ya Ntabo (Sehemu ya Pili)**

Siku moja, Bi. Mwema alienda shambani kuvuna mtama. Jioni, mumewe alimsaidia kubeba magunia kumi ya mtama. Walipofika nyumbani, Bi. Mwema aliandaa chakula cha jioni. Ntabo akaandaa meza, wakala. Baadaye, babu alimsimulia Ntabo hadithi. Akamalizia kwa kusema, "Ntabo, tulia maishani. Utapata mazuri."

Baada ya chakula cha jioni, Bi. Mwema alienda bafuni kuoga. Akataka kuivua saa yake. Ala! Saa haikuwepo. Bi. Mwema alirudi jikoni akaitafuta saa mekoni. Kisha akaenda sebuleni na **chumbani**. Akaitafuta mezani, kochini, kitandani na hata mvunguni. Haikuwepo. Alirudi sebuleni. Akasema, "Rafiki yangu, saa uliyoninunulia imepotea. Kesho nitarudi shambani. Huenda ilianguka huko."

Keshoye baada ya Ntabo kufikishwa shuleni, Bwana na Bi. Mwema walielekea shambani. Wakaitafuta saa mchana kutwa, wasiipate. Jioni walienda shuleni kumchukua Ntabo. Walipofika nyumbani nyanya alisema, "Ntabo, ingia ghalani unitafutie saa. Huenda ilianguka mle tulipoingiza mtama."Ntabo aliingia ghalani. Akapekuapekua magunia harakaharaka. Mara akatoka na kusema, "Nyanya, siioni." Nyanya alikosa furaha. Saa ilikuwa wapi?""Nitajuaje ni saa ngapi?"

Ntabo alienda sebuleni kufanya kazi zake. Akakumbuka nyanya alivyoipenda saa yake. Akakumbuka pia wasia wa babu."...Tulia tuli, utapata...." Ntabo alirudi ghalani harakaharaka. Muda mchache baadaye akaita, "Nyanya! Njoo unisaidie." Nyanya alifika haraka akidhani ameumia. Ntabo alisema,"Beba gunia hili." Nyanya alilibeba hadi nje. Walishirikiana kuumwaga mtama sakafuni. Nyanya akaiona saa yake. Nyanya aliuliza, "Ulijuaje saa iko kwenye gunia hili?" Ntabo alisema, "Niliingia ghalani nikatulia tuli. Nikasikia tik! tak! kwenye gunia hili." Nyanya alitabasamu na kumkumbatia Ntabo.

## Kusoma Maneno

**N:** Soma neno mara mbili polepole wanafunzi wakiliandika. Maneno: **wimbo, mwananchi, yanayoikumba, kuimbwa, mitambo, ubwabwa, mwanariadha, kizimba, wanatambua.**

## Hadithi ya Mwalimu

**Kabla ya kusoma**

**N:** [Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi kisha tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma, kuna maneno mapya ambayo tutayazungumzia. Kama vile **mvunguni**. Neno hili humaanisha kuwa chini ya kitu. *(Rudia hatua hii na maneno **mchana kutwa** , **ghalani** na **mekoni**).*]

**Wakati wa kusoma**

**N:** [Sikiliza na utambue maneno mapya. Inua mkono wako wa kushoto utakaposikia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia unaposikia neno la pili *(Soma hadithi kwa ufasaha. Uliza wanafunzi ni kitu gani ambacho kinaweza kutokea.)*]

**Baada ya kusoma**

**N/T:** Uliza maswali yafuatayo:
Je, hadithi hii ilifanyika wapi na wakati gani?
Wahusika ni akina nani?
*Waelekeze wanafunzi kusimulia hadithi tena.* Nini kilitendeka mwanzoni, katikati na mwishoni mwa hadithi?
Je, unakubaliana na ushauri wa babu kwa mjukuwe Ntabo?
Ikiwa hadithi hii ingeendelea, nini kingefanyika?

## Sarufi: Vimilikishi –ake na –ao.

**N:** [Vimilikishi ni maneno yanayoonyesha kitu ni cha nani]
**N/T/U:** [Fungua wa **ukurasa wa 70.** Andika sentensi ukitumia maneno uliyopewa pamoja na kimilishi -ake.]

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora uwanja wa shule yenu ikiwa ni siku ya michezo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 71: Miezi ya Mwaka 2

Kipindi cha 71 na 72 **Miezi ya Mwaka 2**

Matini

**Sikukuu Muhimu Nchini**



Sikukuu ni siku ambayo watu husherehekea au kuadhimisha tukio fulani muhimu. Nchi ya Kenya, imeweka sikukuu ambazo huadhimishwa katika miezi kadhaa ya mwaka.

Katika mwanzo wa mwaka, kuna sherehe za mwaka mpya ambazo hufanyika mnamo Januari mosi. Sherehe hizi huanzia usiku wa tarehe thelathini na moja Desemba. Wakenya wengi hujumuika pamoja kuukaribisha mwaka mpya.

Leba Dei ni siku ya wafanyakazi ambayo hufanyika tarehe mosi mwezi wa Mei. Sherehe ya Leba Dei ni ya kimataifa. Sherehe hizi huongozwa na wizara ya Leba pamoja na chama cha wafanyakazi nchini.

Tarehe mosi Juni ni sherehe ya Madaraka nchini. Wakenya huadhimisha siku ambayo nchi ya Kenya ilipata idhini ya kujitawala. Kuna sherehe ya Mashujaa ambayo huwa tarehe ishirini Oktoba. Siku hii huwatambua mashujaa waliopigania uhuru, wanariadha, wanasoka, wakulima bora na wengineo.

Mwezi wa Desemba huwa na sherehe mbili muhimu.Tarehe kumi na mbili wakenya huadhimisha siku ambayo nchi yao ilipata kuwa jamhuri. Sikukuu ya Krismasi husherehekewa tarehe ishirini na tano Desemba. Krismasi ni sikukuu ya Kikristo.

Vilevile, kuna sikukuu nyingine kama vile Diwali ambayo ni sikukuu ya Kihindi. Idi ul Fitr ni sikukuu ya Kiislamu inayosherehekewa baada ya mfungo wa Ramadhani. Ama kwa kweli, sherehe hizi huwa ni habari njema kwa wakenya wote.

71 Hakiuzwi

Kipindi cha 71 na 72 **Miezi ya Mwaka 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

huadhimishwa mosi Madaraka

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

wengineo nyingine huongozwa njema

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Siku ya wafanyakazi husherehekewa mwezi gani?
2. Sikukuu ya Mashujaa husherehekewa mwezi gani?
3. Ni mwezi gani ambao una sikukuu mbili nchini Kenya kama ilivyotajwa katika hadithi?
4. Je, wewe unaupenda mwezi gani?

Sarufi: Matumizi ya kikomo

**Akifisha sentensi hizi ifaavyo kwa kutumia alama ya kikomo.**

1. Alinipa kitabu chake
2. Ngamia anaishi jangwani
3. Mnunuzi alinunua njugu na ngano
4. Kunguru ni ndege mwoga

Mali ya Serikali ya Kenya 72

## Msamiati

**N/T:** Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **huadhimishwa, mosi, madaraka.** Soma maneno **ukurasa wa 72.**

## Kusoma Matini: Maelezo

**N/T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu:

### Kusimulia Hadithi

N: Chora umbo la nyumba.

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]

**N:** Simulia darasa lote hadithi.

**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Siku ya wafanyakazi husherehekewa mwezi gani? (Mei)
2. Sikukuu ya Mashujaa husherehekewa mwezi gani? (Oktoba)
3. Ni mwezi gani ambao una sikukuu mbili nchini Kenya kama ilivyotajwa katika hadithi? (Desemba)
4. Je, wewe unaupenda mwezi gani? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Matumizi ya Kikomo

**N/T/U:** Soma sentensi kutoka kwa matini zilizo na kikomo pamoja. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika miezi ya mwaka jinsi inavyofuatana ukianzia na mwezi wa kwanza hadi wa kumi na mbili.

**Majibu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Januari | April | Julai | Oktoba |
| Februari | Mei | Agosti | Novemba |
| Machi | Juni | Septemba | Desemba |

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 72: Miezi ya Mwaka 2

Kipindi cha 71 na 72 **Miezi ya Mwaka 2**

**Matini**

**Sikukuu Muhimu Nchini**



Sikukuu ni siku ambayo watu husherehekea au kuadhimisha tukio fulani muhimu. Nchi ya Kenya, imeweka sikukuu ambazo huadhimishwa katika miezi kadhaa ya mwaka.

Katika mwanzo wa mwaka, kuna sherehe za mwaka mpya ambazo hufanyika mnamo Januari mosi. Sherehe hizi huanzia usiku wa tarehe thelathini na moja Desemba. Wakenya wengi hujumuika pamoja kuukaribisha mwaka mpya.

Leba Dei ni siku ya wafanyakazi ambayo hufanyika tarehe mosi mwezi wa Mei. Sherehe ya Leba Dei ni ya kimataifa. Sherehe hizi huongozwa na wizara ya Leba pamoja na chama cha wafanyakazi nchini.

Tarehe mosi Juni ni sherehe ya Madaraka nchini. Wakenya huadhimisha siku ambayo nchi ya Kenya ilipata idhini ya kujitawala. Kuna sherehe ya Mashujaa ambayo huwa tarehe ishirini Oktoba. Siku hii huwatambua mashujaa waliopigania uhuru, wanariadha, wanasoka, wakulima bora na wengineo.

Mwezi wa Desemba huwa na sherehe mbili muhimu.Tarehe kumi na mbili wakenya huadhimisha siku ambayo nchi yao ilipata kuwa jamhuri. Sikukuu ya Krismasi husherehekewa tarehe ishirini na tano Desemba. Krismasi ni sikukuu ya Kikristo.

Vilevile, kuna sikukuu nyingine kama vile Diwali ambayo ni sikukuu ya Kihindi. Idi ul Fitr ni sikukuu ya Kiislamu inayosherehekewa baada ya mfungo wa Ramadhani. Ama kwa kweli, sherehe hizi huwa ni habari njema kwa wakenya wote.

71 Hakiuzwi

Kipindi cha 71 na 72 **Miezi ya Mwaka 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

huadhimishwa mosi Madaraka

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

wengineo nyingine huongozwa njema

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Siku ya wafanyakazi husherehekewa mwezi gani?
2. Sikukuu ya Mashujaa husherehekewa mwezi gani?
3. Ni mwezi gani ambao una sikukuu mbili nchini Kenya kama ilivyotajwa katika hadithi?
4. Je, wewe unaupenda mwezi gani?

**Sarufi: Matumizi ya kikomo**

**Akifisha sentensi hizi ifaavyo kwa kutumia alama ya kikomo.**

1. Alinipa kitabu chake
2. Ngamia anaishi jangwani
3. Mnunuzi alinunua njugu na ngano
4. Kunguru ni ndege mwoga

Mali ya Serikali ya Kenya 72

## Kusoma Maneno

**N/T:** Andika maneno haya ubaoni: **wengineo, nyingine, njugu, kunja**

Funza sauti **nj** na **ng**

Soma maneno **ukurasa wa 72.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Matumizi ya Kikomo (.)

**N/T/U:** Fungua **ukurasa wa 72.**

Akifisha sentensi hizi ifaavyo kwa kutumia alama ya kikomo.

**Majibu**

1. Alinipa kitabu chake.
2. Ngamia anaishi jangwani.
3. Mnunuzi alinunua njugu na ngano.
4. Kunguru ni ndege mwoga.

## Kuandika

### Maelezo - Kuchapisha

1. Mwanafunzi asome kisa kifupi kilichoandikwa na mwenzake.
2. Wakumbushe wanafunzi kuwa makini wanaposomewa makala.
3. Waulize wanafunzi wawili au watatu kuchangia walichofurahia kuhusu makala waliyosomeya.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Ambatanisha mwezi na tarakimu yake.

| Mwezi | Tarakimu |
|---|---|
| Januari | 6 |
| Februari | 12 |
| Juni | 5 |
| Desemba | 1 |
| Mei | 2 |

**Majibu**

| Mwezi | Tarakimu |
|---|---|
| Januari | 1 |
| Februari | 2 |
| Juni | 6 |
| Desemba | 12 |
| Mei | 5 |

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 73: Miezi ya Mwaka 2

Kipindi cha 73 na 74 **Miezi ya Mwaka 2**

Matini

**Biashara ya Bwana Ngao**




Ngao alikuwa mvuvi aliyeishi karibu na soko la Njozi Njema. Alifanya kazi yake ya uvuvi kwa bidii. Asubuhi na mapema aliamka na kwenda mtoni. Pale mtoni palikuwa na aina mbalimbali ya samaki kama vile ngege na mkunga. Ngao alivua samaki kila siku na mara nyingine alipenda kunadi samaki wake kwa kupaza sauti "Mia moja mia moja!" Wanakijiji walimpa jina la utani: 'Mia moja moja' Ngao, Mia moja moja, alizoea kuwaambia wateja wake, "Lazima uje na kikapu chako cha kubebea samaki kwani karatasi za plastiki haziruhusiwi kamwe."

Mnamo mwezi wa Aprili, msimu wa mvua ulianza. Maji yaliongezeka mtoni na samaki wakawa wengi sana. Siku moja Ngao alipotoka kuvua samaki alihisi kiu, akachota maji mtoni na kunywa. Punde, alisokotwa na tumbo hata hakuweza kusimama. Maji ya mto yalikuwa na uchafu. Uchafu huu ulitoka katika kiwanda kilichokuwa karibu. Kesho yake, samaki wengi walikufa na wakaanza kuelea majini. Wavuvi wengine walianza kuuza samaki waliokufa. Mpwa wake Ngao na watu wengine walimwombea apate nafuu haraka ili awauzie samaki wazuri. Baada ya wiki tatu, Ngao alirudi sokoni na mtungo wa samaki. Watu walifurahi kumwona. Kila mnunuzi aliweza kupata samaki kulingana na mapato yake na idadi aliyoitaka. Kuna wale walionunua kwa wingi na wengine mmoja mmoja. Ngao aliuza samaki kulingana na ukubwa wao. Aliwauza kwa shilingi themanini,tisini na tano,mia moja na hata zaidi.



Kipindi cha 73 na 74 **Miezi ya Mwaka 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

tarakimu themanini mia moja

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

ngao njozi ngege mkunga

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ngao alikuwa akifanya kazi gani?
2. Ngao alikuwa mgonjwa wakati gani?
3. Samaki wana manufaa gani kwa binadamu?
4. Ni aina ngapi za samaki zilizotajwa katika hadithi?

Sarufi: Matumizi ya kikomo (.)

**Akifisha sentensi hizi ifaavyo.**

1. Alinipa penseli yangu
2. Samaki anaishi majini
3. Wavuvi waliwauza samaki
4. Karatasi za plastiki haziruhusiwi
5. Msimu wa mvua ulianza mwezi Aprili



## Msamiati

**N:** Jadili picha. Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati: **tarakimu**
Funza maneno ya msamiati: **themanini, mia, moja**
Soma maneno **ukurasa wa 74**

## Kusoma Matini: Maelezo

Soma kichwa cha hadithi pamoja na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu:

### Kusimulia Hadithi

**N:** Chora umbo la nyumba.

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]
**N:** Simulia darasa lote hadithi.
**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

### Maswali

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Ngao alikuwa akifanya kazi gani? (Uvuvi)
2. Ngao alikuwa mgonjwa wakati gani? (Aprili)
3. Samaki wana manufaa gani kwa binadamu? (Afya)
4. Ni aina ngapi za samaki zilizotajwa katika hadithi? (Mbili)

## Sarufi: Matumizi ya kikomo

Waeleze wanafunzi sarufi.
Waelekeze wanafunzi kaukifisha sentensi ifaayo.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika tarakimu hizi kwa maneno**

1. 53 (Hamsini na tatu)
2. 85 (Themanini na tano)
3. 91 (Tisini na moja)
4. 100 (Mia moja)
5. 77 (Sabini na saba)

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 74: Miezi ya Mwaka 2

Kipindi cha | 73 na 74 | **Miezi ya Mwaka 2**

### Matini

**Biashara ya Bwana Ngao**




Ngao alikuwa mvuvi aliyeishi karibu na soko la Njozi Njema. Alifanya kazi yake ya uvuvi kwa bidii. Asubuhi na mapema aliamka na kwenda mtoni. Pale mtoni palikuwa na aina mbalimbali ya samaki kama vile ngege na mkunga. Ngao alivua samaki kila siku na mara nyingine alipenda kunadi samaki wake kwa kupaza sauti "Mia moja mia moja!" Wanakijiji walimpa jina la utani: 'Mia moja moja' Ngao, Mia moja moja, alizoea kuwaambia wateja wake, "Lazima uje na kikapu chako cha kubebea samaki kwani karatasi za plastiki haziruhusiwi kamwe."

Mnamo mwezi wa Aprili, msimu wa mvua ulianza. Maji yaliongezeka mtoni na samaki wakawa wengi sana. Siku moja Ngao alipotoka kuvua samaki alihisi kiu, akachota maji mtoni na kunywa. Punde, alisokotwa na tumbo hata hakuweza kusimama. Maji ya mto yalikuwa na uchafu. Uchafu huu ulitoka katika kiwanda kilichokuwa karibu. Kesho yake, samaki wengi walikufa na wakaanza kuelea majini. Wavuvi wengine walianza kuuza samaki waliokufa. Mpwa wake Ngao na watu wengine walimwombea apate nafuu haraka ili awauzie samaki wazuri. Baada ya wiki tatu, Ngao alirudi sokoni na mtungo wa samaki. Watu walifurahi kumwona. Kila mnunuzi aliweza kupata samaki kulingana na mapato yake na idadi aliyoitaka. Kuna wale walionunua kwa wingi na wengine mmoja mmoja. Ngao aliuza samaki kulingana na ukubwa wao. Aliwauza kwa shilingi themanini,tisini na tano,mia moja na hata zaidi.

73 Hakiuzwi

Kipindi cha | 73 na 74 | **Miezi ya Mwaka 2**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

tarakimu themanini mia moja

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

ngao njozi ngege mkunga

### Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ngao alikuwa akifanya kazi gani?
2. Ngao alikuwa mgonjwa wakati gani?
3. Samaki wana manufaa gani kwa binadamu?
4. Ni aina ngapi za samaki zilizotajwa katika hadithi?

### Sarufi: Matumizi ya kikomo (.)

**Akifisha sentensi hizi ifaavyo.**

1. Alinipa penseli yangu
2. Samaki anaishi majini
3. Wavuvi waliwauza samaki
4. Karatasi za plastiki haziruhusiwi
5. Msimu wa mvua ulianza mwezi Aprili

Mali ya Serikali ya Kenya 74

## Kusoma Maneno

N: Andika maneno ubaoni: **ngao, njozi , mpwa, njoo.**
Funza sauti **nj** na **ng.**
Soma maneno **ukurasa wa 74.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Maelezo - Kuchapisha**

1. Mwanafunzi asome kisa kifupi kilichoandikwa na mwenzake.
2. Wakumbushe wanafunzi kuwa makini wanaposomewa makala.
3. Waulize wanafunzi wawili au watatu kuchangia walichofurahia kuhusu makala waliyosomeya.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Tunga sentensi ukitumia tarakimu hizi.**

1. Mbuzi 53 (Mbuzi hamsini na watatu.)
2. Viti 85 (Viti themanini na vitano.)
3. Mikeka 91(Mikeka tisini na moja.)
4. Wanafunzi 100 (Wanafunzi mia moja.)

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 75: Miezi ya Mwaka 2

Kipindi cha 75 **Miezi ya Mwaka 2**

**Kuandika**

**Eleza sherehe zinazofanyika katika miezi hii: Januari, Mei, Juni na Desemba.**

**Tathmini ya Sarufi**

**Akifisha sentensi zifuatazo.**

1. mwalimu wetu anaitwa Cherono
2. mvuvi alienda kuvua saa ngapi
3. baba alizaliwa mwaka gani
4. karo ya shule ni kiasi gani

75 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili huku wanafunzi wakiandika.

**Maneno:**

1. Septemba
2. hamsini na nane
3. Februari
4. tisini na sita
5. Oktoba
6. Novemba
7. sabini na nane
8. sitini na sita
9. Machi
10. Aprili

## Kuchambua Matini: Mtiririko

**U:** [Leo ni zamu yenu. Tulisoma hadithi wiki hii. Tambua sikukuu **zilizoorodheshwa** kwenye hadithi. Orodhesha kwanza sikukuu zilizotajwa kwenye hadithi ya kwanza. Saidiana na mwenzako kuorodhesha sikukuu hizi.

**T:** *Waongoze wanafunzi na kuwakosoa ipasavyo.*]

## Sarufi

Andika sentensi kwa kutumia kikomo au kiulizi ipasavyo.

**Majibu**

1. Mwalimu wetu anaitwa Cherono.
2. Mvuvi alienda kuvua saa ngapi?
3. Baba alizaliwa mwaka gani?
4. Karo ya shule ni kiasi gani?

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika insha fupi kuhusu sikukuu uipendayo.

## Mapendekezo ya shughuli za huduma ya jamii zinazochangia ujifunzaji.

Tembelea majirani zako ambao ni wazee. Andika sentensi tatu kuwahusu.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 76: Kazi Mbalimbali 2

Kipindi cha 76 na 77 **Kazi Mbalimbali 2**

**Matini**

**Mkulima Hamisi Mchapakazi**



Bwana Hamisi anaishi katika kijiji cha Ngomeni. Yeye ni mkulima hodari. Kazi hii ya ukulima imemsaidia sana. Ameweza kununua gari jipya. Katika shamba lake amefuga ng'ombe wa maziwa na kuku wa mayai na wa nyama. Pia, amepanda mahindi, maharagwe na pojo.

Bwana Juma ni mfanyakazi pale shambani. Siku ya Bwana Juma huanza mapema alfajiri. Anapoamka, yeye huwaamsha wafanyakazi wake ili wasaidiane kuwakama ng'ombe. Mke wake huwaletea vifaa vyote vya kutumia kukama ng'ombe hao. Maziwa haya huuzwa sokoni na mchungaji mmoja. Baada ya maziwa kupelekwa sokoni, zizi huoshwa na ng'ombe kukatiwa majani ya kutosha. Kuku nao huwekewa vyakula vya aina ya nafaka. Ng'ombe na kuku pia hupewa maji ya kutosha. Wakati wa mchana mayai ya kuku hukusanywa na kupelekwa dukani kuuzwa.

Ifikapo saa nne, mifugo wote huwa wamepewa chakula na maji ya kutosha. Bwana Juma na wafanyakazi wake kisha huingia shambani kupalilia mimea. Wao hutumia vifaa vya kupalilia. Mimea ikikomaa na kukauka wao huivuna na kuiweka kwenye ghala ili kungojea mteja wa kuinunua. Baada ya mazao haya kuuzwa Bwana Hamisi hutumia pesa hizi kuwalipia watoto wake karo ya shule. Pia huzitumia kulipa mishahara ya wafanyakazi na katika matumizi ya nyumbani. Yeye pia huweka akiba ya pesa anazobakisha. Msimu uliopita aliwanunulia watoto wake viatu vipya. Bwana Hamisi huhakikisha kuwa amerekodi mapato yake na kuweka hesabu ya matumizi vizuri.

Mali ya Serikali ya Kenya

76

Kipindi cha 76 na 77 **Kazi Mbalimbali 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

mkulima ukulima mchungaji

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

jipya vipya vyote vyakula

**Ufahamu**

**Jibu maswali.**

1. Taja baadhi ya mifugo walio katika shamba la Bwana Hamisi.
2. Kuku wa Bwana Hamisi humpa nini?
3. Vyakula huwekwa wapi baada ya kuvunwa ili kusubiri mnunuzi?
4. Unafikiri Bwana Hamisi anapenda kazi ya ukulima? Kwa nini?

**Sarufi: Nyakati**

**Pigia mstari mahali kiambishi cha wakati kimetumiwa.**

1. Msimu uliopita aliwanunulia watoto wake viatu vipya.
2. Ukikosa kufanya kazi ya mwalimu utakuwa umemkosea.
3. Mutiso alipumzika baada ya mazoezi.
4. Mto mchafu utasafishwa.

77

Hakiuzwi

## Msamiati

**N:** Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **mkulima, ukulima, mchungaji.**

Soma maneno **ukurasa wa 77.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

**N:** Waeleze wanafunzi kuhusu hatua za matukio katika hadithi kama vile unavyojifunza kupika ugali.

**T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## ? Ufahamu

### Maswali

**Jibu maswali ya ufahamu**

1. Taja baadhi ya mifugo katika shamba la Bwana Hamisi? (Ng'ombe na kuku)
2. Kuku wa Bwana Hamisi humpa nini? (Mayai)
3. Baada ya kuvuna, vyakula huwekwa wapi ili kusubiri mnunuzi? (Kwenye ghala)
4. Unafikiri Bwana Hamisi anapenda kazi ya ukulima? Kwa nini? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

Ukanusho wa nyakati ni neno linalokana kutendeka kwa kitendo. Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika maneno haya kwa hati nadhifu.

1. Mwalimu Mkuu
2. mkulima
3. udaktari
4. uyaya

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 77: Kazi Mbalimbali 2

Kipindi cha 76 na 77 **Kazi Mbalimbali 2**

**Matini**

**Mkulima Hamisi Mchapakazi**



Bwana Hamisi anaishi katika kijiji cha Ngomeni. Yeye ni mkulima hodari. Kazi hii ya ukulima imemsaidia sana. Ameweza kununua gari jipya. Katika shamba lake amefuga ng'ombe wa maziwa na kuku wa mayai na wa nyama. Pia, amepanda mahindi, maharagwe na pojo.

Bwana Juma ni mfanyakazi pale shambani. Siku ya Bwana Juma huanza mapema alfajiri. Anapoamka, yeye huwaamsha wafanyakazi wake ili wasaidiane kuwakama ng'ombe. Mke wake huwaletea vifaa vyote vya kutumia kukama ng'ombe hao. Maziwa haya huuzwa sokoni na mchungaji mmoja. Baada ya maziwa kupelekwa sokoni, zizi huoshwa na ng'ombe kukatiwa majani ya kutosha. Kuku nao huwekewa vyakula vya aina ya nafaka. Ng'ombe na kuku pia hupewa maji ya kutosha. Wakati wa mchana mayai ya kuku hukusanywa na kupelekwa dukani kuuzwa.

Ifikapo saa nne, mifugo wote huwa wamepewa chakula na maji ya kutosha. Bwana Juma na wafanyakazi wake kisha huingia shambani kupalilia mimea. Wao hutumia vifaa vya kupalilia. Mimea ikikomaa na kukauka wao huivuna na kuiweka kwenye ghala ili kungojea mteja wa kuinunua. Baada ya mazao haya kuuzwa Bwana Hamisi hutumia pesa hizi kuwalipia watoto wake karo ya shule. Pia huzitumia kulipa mishahara ya wafanyakazi na katika matumizi ya nyumbani. Yeye pia huweka akiba ya pesa anazobakisha. Msimu uliopita aliwanunulia watoto wake viatu vipya. Bwana Hamisi huhakikisha kuwa amerekodi mapato yake na kuweka hesabu ya matumizi vizuri.

Mali ya Serikali ya Kenya

76

Kipindi cha 76 na 77 **Kazi Mbalimbali 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

mkulima ukulima mchungaji

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

jipya vipya vyote vyakula

**Ufahamu**

**Jibu maswali.**

1. Taja baadhi ya mifugo walio katika shamba la Bwana Hamisi.
2. Kuku wa Bwana Hamisi humpa nini?
3. Vyakula huwekwa wapi baada ya kuvunwa ili kusubiri mnunuzi?
4. Unafikiri Bwana Hamisi anapenda kazi ya ukulima? Kwa nini?

**Sarufi: Nyakati**

**Pigia mstari mahali kiambishi cha wakati kimetumiwa.**

1. Msimu uliopita aliwanunulia watoto wake viatu vipya.
2. Ukikosa kufanya kazi ya mwalimu utakuwa umemkosea.
3. Mutiso alipumzika baada ya mazoezi.
4. Mto mchafu utasafishwa.

77 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

N: Andika maneno haya ubaoni: **jipya, vipya, mapya, vyovyote.**

Funza sauti **vy** na **py.**

Soma maneno **ukurasa wa 77.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

N: [Ukanusho wa nyakati ni neno linalotokana na kutendeka kwa kitendo.]

T: [Fungua **ukurasa wa 77**. Pigia mstari mahali kiambishi cha wakati kimetumika.]

**Majibu**

1. Msimu uliopita aliwanunulia watoto wake viatu vipya.
2. Ukikosa kufanya kazi ya mwalimu utakuwa umemkosea.
3. Mutiso alipumzika baada ya mazoezi.
4. Mto mchafu unanuka.

## Kuandika

**Mtiririko - Kupanga**

T: [Chagua kitu au jambo lolote ambalo unafahamu vyema nmana ya kulifanya. Je, huanza vipi kufanya jambo hili? Hatua ipi hufuata? Hatua ya mwisho ni ipi?]

T: [Leo tutajifunza jinsi ya kuandika insha ya mtiririko. Ili kuandika chochote lazima tupange kwanza.]

### Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Kamilisha sentensi.**

1. Bawabu hufanya kazi ya __________. (ulinzi)
2. Nesi hufanya kazi ya __________. (uuguzi)
3. Mwalimu hufanya kazi ya __________. (ualimu)
4. Daktari hufanya kazi ya __________. (udaktari)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 78: Kazi Mbalimbali 2

Kipindi cha 78 na 79 **Kazi Mbalimbali 2**

**Matini**

**Shughuli za Siku ya Jumamosi**



Siku ya Jumamosi ni siku ya shughuli chungu nzima nyumbani. Sisi huwa hatuendi shuleni. Mama na baba yangu pia huwa hawaendi kazini. Sisi sote huamka asubuhi na mapema. Ninapoamka asubuhi, mimi huosha uso na kupiga mswaki. Baadaye, mimi huenda kuokota takataka uwanjani.

Yaya wetu Bi. Zaina, huanza siku kwa kuviosha vyombo kisha hutayarisha kiamshakinywa. Baadaye, yeye huhakikisha kuwa chakula cha mtoto kiko tayari. Zaina pia huandaa meza kwa kiamshakinywa. Huandaliwa vyakula vingi mezani. Wakati mwingine, Zaina hupiga deki vyumba vyote vya nyumba yetu. Mama kwa upande wake huamka na kutengeneza ratiba ya chakula. Yeye hupanga chakula cha kila siku. Kisha atafanya ratiba ya vitu vinavyohitaji kununuliwa.

Baba huamka na kuanza kupasua kuni za kutumia nyumbani. Yeye pia humsaidia mchungaji wa ng'ombe kukata majani shambani na kuwalisha ng'ombe. Daktari wa ng'ombe anapokuja, yeye humsaidia kumfunga ng'ombe ili atibiwe. Nakumbuka Jumamosi iliyopita daktari hakuja.

Baada ya shughuli hizi za asubuhi, sisi hujumuika mezani kunywa chai. Baadaye, mama na yaya huanza kufua nguo na kuzianika. Jioni mama huzianua nguo hizo. Mimi huchukua kibuyu kipya na kuchota maji kwa matumizi ya nyumbani huku baba akifyeka ua. Mchungaji huhakikisha kuwa mifugo wamenyunyiziwa dawa ya kuua kupe.

Chakula cha mchana hutayarishwa. Kabla ya kula, kila mtu huhakikisha kuwa amemaliza kazi yake. Ifikapo jioni sisi sote hujumuika sebuleni kutazama televisheni. Wakati wa kulala unapofika, kila mtu huenda chumbani mwake kuomba na kisha kulala.



Kipindi cha 78 na 79 **Kazi Mbalimbali 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

yaya hupiga deki daktari

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vyombo vyote vyumba kipya

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Mama hufanya nini anapoamka?
2. Yaya Zaina hufanya nini asubuhi?
3. Mimi hufanya nini ninapoamka?
4. Siku ya Jumamosi wewe hufanya kazi gani nyumbani?

**Sarufi: Ukanusho**

**Kanusha sentensi hizi kwa usahihi.**

1. Jioni mama atazianua nguo hizo.
2. Yohana alipata jeraha alipoanguka.
3. Unaitwa na Mwalimu Mkuu.
4. Andika vizuri.



## Msamiati

Jadili picha. Funza maneno ya msamiati: **yaya, daktari, hupiga deki.**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.

Soma maneno **ukurasa wa 79.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

**N/T:** Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## ? Ufahamu

**Maswali**

1. Mama hufanya nini anapoamka? (Hutengeneza ratiba ya chakula)
2. Yaya Zaina hufanya nini asubuhi? (Hupiga deki nyumba)
3. Mimi hufanya nini ninapoamka? (Kubali jibu lolote sahihi)
4. Siku ya Jumamosi wewe hufanya kazi gani nyumbani? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Ukanusho wa nyakati

Ukanusho wa nyakati ni neno linalotokana kutendeka kwa kitendo.

Kanusha sentensi hizi kwa **ukurasa wa 79** usahihi.

**Majibu**

1. Jioni mama hatazianua nguo hizo.
2. Yohana hakupata jeraha alipoanguka.
3. Huitwi na Mwalimu Mkuu.
4. Usiandike vizuri.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora picha ya mlezi wako kisha uipake rangi.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 79: Kazi Mbalimbali 2

Kipindi cha 78 na 79 **Kazi Mbalimbali 2**

Matini

**Shughuli za Siku ya Jumamosi**



Siku ya Jumamosi ni siku ya shughuli chungu nzima nyumbani. Sisi huwa hatuendi shuleni. Mama na baba yangu pia huwa hawaendi kazini. Sisi sote huamka asubuhi na mapema. Ninapoamka asubuhi, mimi huosha uso na kupiga mswaki. Baadaye, mimi huenda kuokota takataka uwanjani.

Yaya wetu Bi. Zaina, huanza siku kwa kuviosha vyombo kisha hutayarisha kiamshakinywa. Baadaye, yeye huhakikisha kuwa chakula cha mtoto kiko tayari. Zaina pia huandaa meza kwa kiamshakinywa. Huandaliwa vyakula vingi mezani. Wakati mwingine, Zaina hupiga deki vyumba vyote vya nyumba yetu. Mama kwa upande wake huamka na kutengeneza ratiba ya chakula. Yeye hupanga chakula cha kila siku. Kisha atafanya ratiba ya vitu vinavyohitaji kununuliwa.

Baba huamka na kuanza kupasua kuni za kutumia nyumbani. Yeye pia humsaidia mchungaji wa ng'ombe kukata majani shambani na kuwalisha ng'ombe. Daktari wa ng'ombe anapokuja, yeye humsaidia kumfunga ng'ombe ili atibiwe. Nakumbuka Jumamosi iliyopita daktari hakuja.

Baada ya shughuli hizi za asubuhi, sisi hujumuika mezani kunywa chai. Baadaye, mama na yaya huanza kufua nguo na kuzianika. Jioni mama huzianua nguo hizo. Mimi huchukua kibuyu kipya na kuchota maji kwa matumizi ya nyumbani huku baba akifyeka ua. Mchungaji huhakikisha kuwa mifugo wamenyunyiziwa dawa ya kuua kupe.

Chakula cha mchana hutayarishwa. Kabla ya kula, kila mtu huhakikisha kuwa amemaliza kazi yake. Ifikapo jioni sisi sote hujumuika sebuleni kutazama televisheni. Wakati wa kulala unapofika, kila mtu huenda chumbani mwake kuomba na kisha kulala.

Mali ya Serikali ya Kenya 78

Kipindi cha 78 na 79 **Kazi Mbalimbali 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

yaya hupiga deki daktari

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

vyombo vyote vyumba kipya

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Mama hufanya nini anapoamka?
2. Yaya Zaina hufanya nini asubuhi?
3. Mimi hufanya nini ninapoamka?
4. Siku ya Jumamosi wewe hufanya kazi gani nyumbani?

Sarufi: Ukanusho

**Kanusha sentensi hizi kwa usahihi.**

1. Jioni mama atazianua nguo hizo.
2. Yohana alipata jeraha alipoanguka.
3. Unaitwa na Mwalimu Mkuu.
4. Andika vizuri.

79 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **vyombo, vyote, vyenyewe, upya.**

Funza sauti **vy** na **py.**

Soma maneno **ukurasa wa 79.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Mtiririko - Kupanga**

**U:** Kupanga jinsi ya kuandika makala yanayofuata mtiririko maalum.

**U:** Chagua kitu au jambo lolote ambalo unafahamu vyema nmana ya kulifanya. Je, huanza vipi kufanya jambo hili? Hatua ipi hufuata? Hatua ya mwisho ni ipi?

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika wingi wa sentensi hizi.**

1. Nitafika shuleni mapema kesho.
2. Mwalimu anafundisha vizuri.
3. Mtoto alipewa uji na yaya.
4. Ng'ombe atakamuliwa jioni.

**Majibu**

1. Tutafika shuleni mapema kesho.
2. Walimu wanafundisha vizuri.
3. Watoto walipewa uji na yaya.
4. Ng'ombe watakamuliwa jioni.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 80: Kazi Mbalimbali 2

Kipindi cha 80 **Kazi Mbalimbali 2**

Tathmini ya msamiati

**Soma maneno haya:**

yaya mchungaji mkulima

Tathmini ya sarufi

**Kamilisha sentensi hizi kwa usahihi.**

1. ____________ hufanya kazi ya ukulima.
2. Daktari hutibu __________________.
3. ________________ hutusaidia kufanya kazi za nyumbani.
4. ________________ hulinda lango la shule.

Kazi ya ziada

**Eleza kazi ya watu hawa.**

1. Yaya
2. Mchungaji
3. Daktari

Mali ya Serikali ya Kenya 80

## Tathmini ya Msamiati

Fungueni **ukurasa wa 80** wa vitabu vyenu.

Tazama sehemu ya msamiati.

Soma maneno.

## Kusoma Maneno

Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **vyombo, vyote, vyumba, kipya, vyenyewe, upya, vyovyote, vyakula, mapya, jipya**

## Kuchambua Matini: Mtiririko

**U:** [Leo tutachambua matini tuliyosoma wiki hii. Kazi hii mtaifanya kwa vikundi vya wawili wawili. Mtafute mwenzako kisha mchague hadithi iliyowafurahisha wiki hii. Mtasoma hadithi kwa pamoja kisha mwandike hatua zifuatazo za mtiririko.

Hadithi ilizungumzia nini?

Ni nini kilifanyika kwanza?

Ni nini kilichofuata?

Ni nini kilichofanyika mwisho?]

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

Fungueni **ukurasa wa 80** wa vitabu vyenu. Tazama sehemu ya sarufi. Kamilisha sentensi kwa usahihi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Eleza kazi ya watu hawa:**

yaya, mchungaji, daktari

**Majibu**

1. Yaya - husaidia katika kazi za nyumbani
2. mchungaji - huchunga wanyama
3. daktari - hutibu wagonjwa

## Mapendekezo ya shughuli za huduma za jamii zinachangia ujifunzaji.

Chora picha ya vifaa vya ukulima kisha mjadiliane na yeyote mnayeishi naye kuhusu vifaa hivyo.

Tarehe: ________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 81 na 82 **Usalama 2 (Shuleni)**

**Matini**

**Usalama**



Usalama ni hali ya kutokuwa kwa hatari, vurugu au fujo katika mazingira. Usalama wa wanafunzi shuleni ni muhimu na unafaa kudumishwa.

Kuna njia mbalimbali ambazo usalama wa wanafunzi unaweza kuimarishwa pale shuleni. Kwanza, kila shule inafaa kuwa na ua unaoizunguka ili kuwazuia watu wabaya kuingia. Zaidi ya kuwa ua, kila shule inafaa kuwa na bawabu kwenye lango.

Wanafunzi wanapaswa kujitenga na kujiepusha na watu wasiowajua. Mbali na kutozungumza na watu wasiowajua, pia wasikubali kupewa vitu kama peremende, biskuti na vitu vinginevyo kutoka kwa watu hao. Mtu wasiyemjua akiwashawishi kutenda jambo baya ni vizuri kukataa katakata. Itakuwa bora zaidi kumjulisha mwalimu au mzazi kuhusu jambo hilo. Wanafunzi wakifanya hivyo, visa vya utekaji nyara wa wanafunzi vitapungua. Walimu wahakikishe kuwa wanafunzi wanapelekwa na kuchukuliwa shuleni na wazazi wao au walezi wao.

Walimu wawakumbushe wanafunzi umuhimu wa kutunza vifaa vyao shuleni ili kupunguza visa vya wizi miongoni mwao. Wanafunzi wanafaa kufunga milango na madirisha ya darasa kabla ya kwenda nyumbani.

Ni muhimu kwa wanafunzi kuvaa sare ya shule ili kutambulika. Ni muhimu pia waelezwe umuhimu wa usalama, hatari na jinsi ya kujikinga na hatari hizo. Ni muhimu kuripoti kwa walimu na wazazi visa ambavyo vinaweza kuhatarisha usalama wao.

81 Hakiuzwi

Kipindi cha 81 na 82 **Usalama 2 (Shuleni)**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

ua lango utekaji nyara

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

ambazo mbali kuzungumza miongoni

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Usalama ni hali ya kutokuwa na __________.
2. Ua wa shule husaidia vipi kuimarisha usalama wa wanafunzi shuleni?
3. Kila shule inafaa kuwa na _________ langoni.
4. Taja njia nyingine mbili ambazo zinaweza kuimarisha usalama wako shuleni.

**Sarufi: Kinyume cha vitenzi**

**Igiza kinyume cha vitenzi kisha uandike kwenye daftari lako.**

| Kitendo | Kinyume |
|---|---|
| anika | |
| tia | |
| jaza | |
| washa | |
| chota | |

Mali ya Serikali ya Kenya 82

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **ua, lango, utekaji nyara.**

Soma maneno **ukurasa 82.**


## Kusoma Matini: Maelezo

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Ramani Dhana**

Chora ramani dhana



[Sasa tutatumia ramani dhana ili kuelewa tuliyojifunza. Katikati tutaandika **Usalama.** Je, ni nani anaweza kuniambia makala yalisema nini kuhusu usalama? Nitachora mfano wa mkono hapa na kuandika ndani ya duara. Ni nani mwingine anaweza kuongezea jambo lingine kuhusu makala tuliyoyasoma?

Jambo hilo linasikikaje? Linavutia vipi? *(Kwa kila wazo jipya unaliweka kwa kisanduku kipya.*]

**U:** [*Wanafunzi wakimaliza kutoa maelezo yao, waelekeze kuandika sentensi.)* Sasa ni wakati wa kuandika sentensi ya kutoa maelezo kuhusu usalama.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Usalama ni hali ya kutokuwa na ________. (fujo, hatari au vurugu.)
2. Ua la shule husaidia vipi kuimarisha usalama wa wanafunzi shuleni? (huzuia watu wabaya kuingia shuleni.)
3. Kila shule inafaa kuwa na ________ langoni. (bawabu)
4. Taja njia nyingine mbili ambazo zinaweza kuimarisha usalama wako shuleni. (kubali jibu lolote sahihi.)

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Tunga sentensi ukitumia kinyume cha vitendo vifuatavyo.**

1. keti
2. nenda
3. amka

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

# Kipindi cha 82: Usalama 2 (Shuleni)

Kipindi cha | 81 na 82 | **Usalama 2 (Shuleni)**

### Matini

**Usalama**



Usalama ni hali ya kutokuwa kwa hatari, vurugu au fujo katika mazingira. Usalama wa wanafunzi shuleni ni muhimu na unafaa kudumishwa.

Kuna njia mbalimbali ambazo usalama wa wanafunzi unaweza kuimarishwa pale shuleni. Kwanza, kila shule inafaa kuwa na ua unaoizunguka ili kuzuia watu wabaya kuingia. Zaidi ya kuwa ua, kila shule inafaa kuwa na bawabu kwenye lango.

Wanafunzi wanapaswa kujitenga na kujiepusha na watu wasiowajua. Mbali na kutozungumza na watu wasiowajua, pia wasikubali kupewa vitu kama peremende, biskuti na vitu vinginevyo kutoka kwa watu hao. Mtu wasiyemjua akiwashawishi kutenda jambo baya ni vizuri kukataa katakata. Itakuwa bora zaidi kumjulisha mwalimu au mzazi kuhusu jambo hilo. Wanafunzi wakifanya hivyo, visa vya utekaji nyara wa wanafunzi vitapungua. Walimu wahakikishe kuwa wanafunzi wanapelekwa na kuchukuliwa shuleni na wazazi wao au walezi wao.

Walimu wawakumbushe wanafunzi umuhimu wa kutunza vifaa vyao shuleni ili kupunguza visa vya wizi miongoni mwao. Wanafunzi wanafaa kufunga milango na madirisha ya darasa kabla ya kwenda nyumbani.

Ni muhimu kwa wanafunzi kuvaa sare ya shule ili kutambulika. Ni muhimu pia waelezwe umuhimu wa usalama, hatari na jinsi ya kujikinga na hatari hizo. Ni muhimu kuripoti kwa walimu na wazazi visa ambavyo vinaweza kuhatarisha usalama wao.



Hakiuzwi

Kipindi cha | 81 na 82 | **Usalama 2 (Shuleni)**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

ua lango utekaji nyara

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

ambazo mbali kuzungumza miongoni

### Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Usalama ni hali ya kutokuwa na __________.
2. Ua wa shule husaidia vipi kuimarisha usalama wa wanafunzi shuleni?
3. Kila shule inafaa kuwa na _________ langoni.
4. Taja njia nyingine mbili ambazo zinaweza kuimarisha usalama wako shuleni.

### Sarufi: Kinyume cha vitenzi

**Igiza kinyume cha vitenzi kisha uandike kwenye daftari lako.**

| Kitendo | Kinyume |
|---|---|
| anika | |
| tia | |
| jaza | |
| washa | |
| chota | |

Mali ya Serikali ya Kenya



## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni:

**ambazo, mbali, mbwa, jenga**

Funza sauti **mb, ng**

Soma maneno **ukurasa wa 82.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

Fungua **ukurasa wa 82** wa vitabu vyenu. Igiza kinyume cha vitenzi.

**Majibu**

1. anua
2. toa
3. punguza
4. zima
5. Mwaga

## Kuandika

### Mtiririko - Nakala ya Kwanza

**T:** Kunakili jinsi ya kuandika makala yanayofuata mtiririko maalum.

- Andika sentensi ya utangulizi.
- Andika hatua za mtiririko ukitumia sentensi kamilifu.
- Andika sentensi ya kutamatisha.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika kinyume cha sentensi zifuatazo:**

1. Ali alifunga mlango jioni.
2. Wezi waliingia nyumbani.
3. Bawabu alifungua lango.
4. Mwanafunzi alipanga vitabu.

**Majibu**

1. Ali alifungua mlango asubuhi.
2. Wezi walitoka nyumbani.
3. Bawabu alifunga lango.
4. Mwanafunzi alipangua vitabu.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Mali ya Serikali ya Kenya

# Kipindi cha 83: Usalama 2 (Shuleni)



Kipindi cha 83 na 84 **Usalama 2 (Shuleni)**

Matini

**Usalama wa Wanafunzi**


Wanafunzi hutumia muda wao mwingi shuleni. Hivyo basi, ni muhimu wawe katika mazingira salama. Usalama ni muhimu kwa kusoma na kupata matokeo bora.

Kila mwanafunzi ana jukumu la kuhakikisha kwamba vifaa vyenye makali vimeondolewa kwenye mazingira ya shule. Vifaa hivi ni kama vile misumari na nyembe zenye kutu, miiba, mabati mabovu, chupa zilizovunjika na sindano. Mwanafunzi anapodungwa na vifaa vyenye kutu anaweza kuambukizwa ugonjwa wa pepopunda.

Ni muhimu kwa wanafunzi kujihadhari dhidi ya kugusa nyaya za stima zinazoning'inia. Kushika soketi za stima kwa mikono yenye maji huweza kusababisha vifo. Wanafunzi pia waepuke michezo ambayo huweza kusababisha ajali. Baadhi ya mifano ya michezo hii ni; kubembea ovyoovyo, kutegana na kuteguana, kukanyagana na kurushiana mawe na vijiti.

Vilevile, wanafunzi hawafai kutupa maganda ya matunda au kumwaga maji kwenye sakafu. Maji na maganda huifanya sakafu kuwa telezi na huweza kusababisha ajali. Wanafunzi wahakikishe kuwa wamepanga madawati,viti na meza vizuri darasani ili kujiepusha na ajali. Wakati wanafunzi wanataka kula chakula, ni vyema wanawe mikono yao. Kunawa mikono huondoa viini ambavyo husababisha maradhi.

83 Hakiuzwi



Kipindi cha 83 na 84 **Usalama 2 (Shuleni)**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kutu pepopunda maganda

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kuambukizwa kubembea wamepanga kumpongeza

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Usalama huwawezesha wanafunzi kufanya nini shuleni?
2. Taja vifaa vitatu vyenye makali vilivyotajwa kwenye hadithi.
3. Ugonjwa unaosababishwa na kukatwa na vitu vyenye kutu huitwa ____________.
4. Taja njia nyingine ambazo unaweza kujiepusha na ajali shuleni.

Sarufi: Kinyume cha vitenzi

**Andika kinyume cha vitenzi hivi.**

| | |
|---|---|
| 1. ______________ | kumwaga |
| 2. cheka | ______________ |
| 3. kutega | ______________ |
| 4. ______________ | panga |

Kuandika

**Andika kisa kifupi kuhusu usalama shuleni.**

Mali ya Serikali ya Kenya 84

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **kutu, pepopunda, maganda.**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati: **kutu,**

Soma maneno **ukurasa wa 84.**


## Kusoma Matini: Maelezo

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Ramani Dhana**

Chora ramani dhana



[Sasa tutatumia ramani dhana ili kuelewa tuliyojifunza. Katikati tutaandika **Usalama wa Wanafunzi.** Je, ni nani anaweza kuniambia makala yalisema nini kuhusu usalama wa wanafunzi? Nitachora mfano wa mkono hapa na kuandika ndani ya duara. Ni nani mwingine anaweza kuongezea jambo lingine kuhusu makala tuliyoyasoma?

Jambo hilo linasikikaje? Linavutia vipi? *(Kwa kila wazo jipya unaliweka kwa kisanduku kipya.*]

**U:** *Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi inayotoa maelezo kuhusu usalama.*

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Usalama huwawezesha wanafunzi kufanya nini shuleni? (kusoma na kupata matokeo bora)
2. Taja vifaa vitatu vyenye makali vilivyotajwa kwenye hadithi. (Misumari miiba, chupa zilizovunjika)
3. Ugonjwa unaosababishwa na kukatwa na vitu vyenye kutu huitwa (Pepopunda)
4. Taja njia nyingine ambazo unaweza kujiepusha na ajali shuleni. (kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Kinyume cha vitenzi

Andika kinyume cha vitenzi katika jedwali **ukurasa wa 84.**

**Majibu**

1. kuzoa 2. lia 3. kutegua 4. pangua

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Ambatanisha kitenzi na kinyume chake.

| Kitenzi | Kinyume |
|---|---|
| 1. andika | punguza |
| 2. tia | futa |
| 3. jaza | zima |
| 4. washa | toa |

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________




Hakiuzwi

Kipindi cha 83 na 84 **Usalama 2 (Shuleni)**

### Matini

**Usalama wa Wanafunzi**



Wanafunzi hutumia muda wao mwingi shuleni. Hivyo basi, ni muhimu wawe katika mazingira salama. Usalama ni muhimu kwa kusoma na kupata matokeo bora.

Kila mwanafunzi ana jukumu la kuhakikisha kwamba vifaa vyenye makali vimeondolewa kwenye mazingira ya shule. Vifaa hivi ni kama vile misumari na nyembe zenye kutu, miiba, mabati mabovu, chupa zilizovunjika na sindano. Mwanafunzi anapodungwa na vifaa vyenye kutu anaweza kuambukizwa ugonjwa wa pepopunda.

Ni muhimu kwa wanafunzi kujihadhari dhidi ya kugusa nyaya za stima zinazoning'inia. Kushika soketi za stima kwa mikono yenye maji huweza kusababisha vifo. Wanafunzi pia waepuke michezo ambayo huweza kusababisha ajali. Baadhi ya mifano ya michezo hii ni; kubembea ovyoovyo, kutegana na kuteguana, kukanyagana na kurushiana mawe na vijiti.

Vilevile, wanafunzi hawafai kutupa maganda ya matunda au kumwaga maji kwenye sakafu. Maji na maganda huifanya sakafu kuwa telezi na huweza kusababisha ajali. Wanafunzi wahakikishe kuwa wamepanga madawati,viti na meza vizuri darasani ili kujiepusha na ajali. Wakati wanafunzi wanataka kula chakula, ni vyema wanawe mikono yao. Kunawa mikono huondoa viini ambavyo husababisha maradhi.

83 Hak uzwi

Kipindi cha 83 na 84 **Usalama 2 (Shuleni)**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

kutu pepopunda maganda

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kuambukizwa kubembea wamepanga kumpongeza

### Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Usalama huwawezesha wanafunzi kufanya nini shuleni?
2. Taja vifaa vitatu vyenye makali vilivyotajwa kwenye hadithi.
3. Ugonjwa unaosababishwa na kukatwa na vitu vyenye kutu huitwa ____________.
4. Taja njia nyingine ambazo unaweza kujiepusha na ajali shuleni.

### Sarufi: Kinyume cha vitenzi

**Andika kinyume cha vitenzi hivi.**

| | |
|---|---|
| 1. ______________ | kumwaga |
| 2. cheka | ______________ |
| 3. kutega | ______________ |
| 4. ______________ | panga |

### Kuandika

**Andika kisa kifupi kuhusu usalama shuleni.**

Mali ya Serikali ya Kenya 84

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **kuambukizwa, kwamba, mazingira, wamepanga, nyembe, uangalifu.**

Funza sauti **mb** na **ng.**

Soma maneno **ukurasa wa 84.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Mtiririko - Nakala ya Kwanza**

**U:** Kunakili jinsi ya kuandika makala yanayofuata mtiririko maalum.

- Andika sentensi ya utangulizi.
- Andika hatua za mtiririko ukitumia sentensi kamilifu.
- Andika sentensi ya kutamatisha.

## Kazi ya Ziada

**Andika kisa kifupi kuhusu usalama.**

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 85: Usalama 2 (Shuleni)

Kipindi cha 85 **Usalama 2 (Shuleni)**

**Tathmini ya msamiati**

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda msamiati uliyosoma wiki hii kuhusu usalama.

| | | | |
|---|---|---|---|
| la | u | nda | sa |
| tu | ngo | ku | a |
| ga | ma | ki | ta |

**Tathmini ya sarufi**

Tunga sentensi nne sahihi ukitumia kinyume cha vitendo vifuatavyo: keti, enda, amka, washa

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.

Familia ya Ntabo



85

Hakiuzwi

**Familia ya Ntabo (Sehemu ya Tatu)**

Bi. Mwema alifurahi sana Ntabo alipoipata saa yake. Alienda sokoni na kurudi na kifuko kidogo. Alimwita Ntabo. Akasema, “Zawadi hii ni yako.” Ntabo alifungua kifuko. Akamwona kinyau, yani mtoto wa paka. Akasema, “Asante, nyanya. Nitamwita Zawadi.”

Kila siku. Ntabo alimpa Zawadi maziwa na kucheza naye. Zawadi alikua haraka kwa upendo alioupata kutoka kwa familia ya Ntabo. Naye akawafaa kwa kuwala panya pale nyumbani.

Jioni moja, Bi. Mwema aliandaa chakula jioni. Ntabo akamsaidia kuandaa meza, tayari kula. Walimpakulia Zawadi chakula. Ntabo akaita, “Zawadi! Zawadi! Zawadi!” Zawadi hakuja. Walikiacha chakula hicho chini ya meza na kuendelea kula. Baadaye, wakaenda kulala. Asubuhi ilipofika, chakula cha Zawadi kilikuwa palepale walipokiacha. Zawadi alikuwa wapi?

Mchana kutwa Ntabo hakutulia shuleni. Aliwaza na kuwazua juu ya paka wake Zawadi. Jioni hiyo Ntabo alijilazimisha kufanya kazi za shule. Akajilazimisha kula. Akajilazimisha kulala, lakini wapi? Alikumbuka alivyomsaidia nyanya kuipata saa. Alikumbuka wasia wa babu. Wazo likamjia. Ntabo akajilazimisha kutulia tuli. Akakaza sikio lake, ndi! Muda mchache baadaye alisikia sauti hafifu, “Miiiiau.” Ntabo aliruka na kuketi kitandani. Akatega tena sikio. Akasikia sauti hiyo hafifu, “Miiiiiau.” Akasikia na sauti zingine kama tatu hivi zikilia, “Miiii!. Miii!. Mii!.” Alitulia tuli hata akatambua zilikotokea sauti hizo. Alimwomba nyanya tochi. Akamulika mvunguni mwa kitanda chake. Je, unafikiri aliona nini?

## Msamiati

[Fungua wa **ukurasa wa 85** wa vitabu vyenu.
Tazama sehemu ya tathmini ya msamiati.
Kuna jedwali la silabi.
Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.]

**Majibu**

1. usalama 2. lango 3. maganda 4. kutu

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.
Maneno: **ambazo, kuzungumza, miongoni, kuambukizwa, kwamba, mazingira, kubembea, wamepanga, kumpongeza, pepopunda**

## Hadithi ya Mwalimu

**Kabla ya kusoma**

N: [Leo mtasikiliza kwa makini nikiwasomea hadithi kisha baadaye tuzungumzie hadithi hiyo tukiandika. Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi kisha tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma hadithi, kuna baadhi ya maneno mapya ambayo tutazungumzia kwanza. Neno la kwanza ni **kinyau**. Neno hili humaanisha mtoto wa paka *(Rudia hatua hii ukitumia maneno haya: **upendo, kuandaa meza**)*]

**Wakati wa kusoma**

N: [Sasa sikiliza kwa makini ninaposoma. Sikiliza na utambue maneno mapya. Inua mkono wako wa kushoto utakaposikia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia ukisikia neno la pili. *(Soma hadithi kwa ufasaha huku ukibadilisha sauti. Soma huku ukijieleza usoni. Sitisha unapofikia tukio la kufurahisha. Waulize wanafunzi ni kitu gani ambacho kinaweza kutokea.)*]

**Baada ya kusoma**

T: [Hebu tuandike baadhi ya mambo tuliyoyasoma kwenye hadithi.]

## Sarufi

Tunga sentensi nne sahihi ukitumia kinyume cha vitendo vifuatavyo: **keti, enda, amka, washa.**

## Kazi ya Ziada

**Tunga sentensi ukitumia kinyume cha vitendo hivi.**

1. funga 2. panga 3. rudi 4. lala 5. simama

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 86: Usafi wa Mazingira 2

Kipindi cha 86 na 87 **Usafi wa mazingira 2**

**Matini**

**Namna ya Kusafisha Mazingira**



Pahali popote tunapokaa au kuishi panafaa kuwa safi. Wanafunzi wanatakiwa kusoma katika mazingira safi ili kuzuia mkurupuko wa maradhi kama vile kipindupindu ambayo huenea kwa haraka.

Hatua ya kwanza inayofaa kuchukuliwa ni wanafunzi kuunda vikundi vyao vya usafi wa mazingira. Vikundi hivi vipewe majina kama vile, "chui" au "simba". Viwe vikundi vya kudumisha usafi shuleni. Linalofuata ni vikundi kugawiwa sehemu zao maalum, ili kuimarisha usafi. Sehemu hizo zinaweza kuwa katika uwanja wa shule wa michezo.

Kinachofuata, ni kufyeka nyasi kwa kutumia kifyekeo chenye makali. Ni vizuri kusubiri nyasi zilizofyekwa kukauka polepole. Nyasi hizi zilizokauka zikusanywa vyema kwa kutumia sepetu au vijiti virefu vilivyofungwa pamoja. Nyasi hizi zinaweza kusombwa na kutumbukizwa kwenye shimo. Shimo hilo likijaa kwa kuongezea matawi yaliyokauka, itakuwa mbolea ambayo inaweza kutumika shambani.

Ni muhimu kuyaweka mazingira yetu safi kwani mazingira safi huvutia na pia hutuepusha na magonjwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 86

Kipindi cha 86 na 87 **Usafi wa mazingira 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

mkurupuko kipindupindu sepetu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

uchafu tenga chuma itakuwa

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Pahali popote tunapoishi panafaa kuwa vipi?
2. Hatua ya kwanza ya kuhakikisha kuwa kuna mazingira safi ni kufanya nini?
3. Kwa nini ni muhimu kuyaweka mazingira yetu yakiwa safi?
4. Unafikiria ni kwa nini taka hufaa kutenganishwa baada ya kuokotwa?

**Sarufi: Vielezi**

**Kamilisha sentensi ukitumia "haraka" au "polepole".**

1. Konokono hutembea ____________.
2. Ukienda ____________ utafika upesi.
3. Ukiendelea kutembea ____________ nitakuacha nyuma.
4. Mvua inakaribia, fanya ____________ tumalizie kazi hii.

87 Hakizwi

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **mkurupuko, kipindupindu, sepetu.**

Soma maneno **ukurasa wa 87.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha

Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Mtiririko**

Jibu maswali haya kuhusu jinsi ya kusafisha mazingira ya shule.

Mwanzo → Katikati → Mwisho

1. Wanafunzi wanafaa kufanya nini mwanzo? (Kuunda kikundi cha usafi)
2. Wanafunzi wanafaa kufanya nini baadaye. (Kubali jibu lolote)
3. Wanafunzi wanafaa kufanya nini mwishowe? (Kubali jibu lolote sahihi)

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

## Sarufi: Vielezi

Vielezi ni maneno ambayo hutumika kuonyesha namna kitendo kilifanyika. Mifano ya maneno haya ni kasi, polepole, haraka, sana, vizuri, juu, chini, mapema, kivivu na mengineyo. Maneno haya huitwa vielezi. Soma sentensi kutoka kwa matini, andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada

Jaza mapengo ukitumia vielezi **haraka** na **polepole**

1. Mzee kobe hutembea __________ kwenda sokoni. (polepole)
2. Yaya huyu ni mvivu, husafisha nyumba __________. (polepole)
3. Polisi walikimbia _____ kumfuata mwizi ndipo. wakamkamata. (haraka)
4. Ukichelewa kuamka utaenda shuleni ________. (haraka)

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 86 na 87 **Usafi wa mazingira 2**

**Matini**

**Namna ya Kusafisha Mazingira**



Pahali popote tunapokaa au kuishi panafaa kuwa safi. Wanafunzi wanatakiwa kusoma katika mazingira safi ili kuzuia mkurupuko wa maradhi kama vile kipindupindu ambayo huenea kwa haraka.

Hatua ya kwanza inayofaa kuchukuliwa ni wanafunzi kuunda vikundi vyao vya usafi wa mazingira. Vikundi hivi vipewe majina kama vile, "chui" au "simba". Viwe vikundi vya kudumisha usafi shuleni. Linalofuata ni vikundi kugawiwa sehemu zao maalum, ili kuimarisha usafi. Sehemu hizo zinaweza kuwa katika uwanja wa shule wa michezo.

Kinachofuata, ni kufyeka nyasi kwa kutumia kifyekeo chenye makali. Ni vizuri kusubiri nyasi zilizofyekwa kukauka polepole. Nyasi hizi zilizokauka zikusanywa vyema kwa kutumia sepetu au vijiti virefu vilivyofungwa pamoja. Nyasi hizi zinaweza kusombwa na kutumbukizwa kwenye shimo. Shimo hilo likijaa kwa kuongezea matawi yaliyokauka, itakuwa mbolea ambayo inaweza kutumika shambani.

Ni muhimu kuyaweka mazingira yetu safi kwani mazingira safi huvutia na pia hutuepusha na magonjwa.

Mali ya Serikali ya Kenya

86

Kipindi cha 86 na 87 **Usafi wa mazingira 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

mkurupuko kipindupindu sepetu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

uchafu tenga chuma itakuwa

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Pahali popote tunapoishi panafaa kuwa vipi?
2. Hatua ya kwanza ya kuhakikisha kuwa kuna mazingira safi ni kufanya nini?
3. Kwa nini ni muhimu kuyaweka mazingira yetu yakiwa safi?
4. Unafikiria ni kwa nini taka hufaa kutenganishwa baada ya kuokotwa?

**Sarufi: Vielezi**

**Kamilisha sentensi ukitumia "haraka" au "polepole".**

1. Konokono hutembea ____________.
2. Ukienda ____________ utafika upesi.
3. Ukiendelea kutembea ____________ nitakuacha nyuma.
4. Mvua inakaribia, fanya ____________ tumalizie kazi hii.

87 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **chui, tui, chenga, tenga, chuma.**

Funza sauti **ch** na **t.**

Soma maneno kutoka **ukurasa wa 87.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vielezi

Kamilisha sentensi hizo ukitumia vielezi 'haraka' au 'polepole'. **Kwenye ukurasa wa 87.**

**Majibu**

1. polepole
2. haraka
3. polepole
4. haraka

## Kuandika

### Mtiririko - Kuhakiki

Hakiki makala ya maelezo.

**T:** Mwalimu na wanafunzi wahakiki nakala huku wakizingatia:

1. uakifisha
2. iwapo nakala inaeleweka
3. tahajia.

## Kazi ya Ziada

Andika sentensi nne ukitumia kielezi **haraka** au **polepole**

## Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji.

Mwalimu awaongoze wanafunzi kujiunga na vyama mbalimbali shuleni. Kwa vile: Chama Cha Mazingira.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 88 na 89 **Usafi wa mazingira 2**

**Matini**

**Mazingira Safi**





Watu wengi wana mawazo mbalimbali kuhusu mazingira safi. Watu hawa wanaweza kugawanywa katika makundi mawili. Kuna lile kundi lisilojali kuwa na mazingira safi. Kundi hili hudai kuwa mazingira safi huharibu uasili wa mahali polepole mpaka mahali hapo panabadilika. Wanaendelea kusema kuwa, tunapoyaweka mazingira safi, tunawakosea baadhi ya viumbe kama vile chatu kwa kuwanyima mahali pa kuishi. Wanatoa mfano wa panzi ambao hukosa mahali pa kuishi na kuzalia tunapofyeka nyasi. Wanyama na ndege wa porini kama vile tai hukosa makao tunapojaribu kuifanya misitu kuwa safi.

Kwa upande mwingine, kundi linalounga mkono kuwepo kwa mazingira safi lina sababu zake. Kwanza kabisa, kundi hili linanadai kuwa mazingira machafu ni chanzo cha maradhi. Hii ni kwa sababu, baadhi ya wadudu wanaobeba viini vinavyosababisha magonjwa fulani huishi mahali pachafu. Wanatoa mfano wa mbung'o anayesababisha ugonjwa wa malale. Vilevile, mazingira safi huvutia. Pia yanawatorosha wanyama hatari kama vile nyoka na panya. Vilevile, wadudu kama vile funza, viroboto na chawa hawawezi kumkaribia haraka binadamu anayeweka mazingira yake safi.

Ni vyema kuyatunza mazingira yetu ili yatufae na tuepukane na maradhi yanayotokana na uchafu.

Mali ya Serikali ya Kenya 88

Kipindi cha 88 na 89 **Usafi wa mazingira 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

ugonjwa wa malale | mbung'o | funza

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

chatu | machafu | chanzo | tai

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kuna makundi mangapi ya watu yaliyotajwa mwanzoni mwa hadithi?
2. Tunafaa kufanya nini ili kujiepusha na baadhi ya magonjwa?
3. Mbung'o husababisha ugonjwa gani?
4. Je, unapinga au unaunga mkono kuwepo kwa mazingira safi? Kwa nini?

**Sarufi: Vielezi-Matumizi ya "polepole" na "haraka"**

**Jaza mapengo kwa kutumia "haraka" au "polepole".**

1. Kinyonga hutembea ____________.
2. Tulitembea ____________ ili tusichelewe.
3. Hatukufika kwa wakati kwa sababu tulitembea ____________.
4. Nilitembea ____________ ili niwafikie.

89 Hakiluzwi

## Msamiati

Jadili picha.
Funza maneno ya msamiati: **ugonjwa wa malale, mbung'o, funza.**
Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.
Soma maneno kutoka **ukurasa wa 89.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha . Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

### Mtiririko

Jibu maswali haya kuhusu jinsi ya kusafisha mazingira ya shule.

Mwanzo
↓
Katikati
↓
Mwisho

1. Wanafunzi wanafaa kufanya nini mwanzo? (Kuunda kikundi cha usafi)
2. Wanafunzi wanafaa kufanya nini baadaye. (Kubali jibu lolote)
3. Wanafunzi wanafaa kufanya nini mwishowe? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Vielezi

Jaza mapengo kwa kutumia "haraka"au "polepole"

### Majibu

1. pole pole
2. haraka
3. polepole
4. haraka

## Kazi ya Ziada

Panga maneno haya ili kuunda sentensi sahihi.

1. Mtoto polepole hula.
2. Hazitang'ara nguo haraka ukiosha.
3. Kupanda baada ya ngazi alihema haraka.
4. Polepole mche hukua.

### Majibu


1. Mtoto hula polepole.
2. Ukiosha nguo haraka hazitang'ara.
3. Alihema baada ya kupanda ngazi haraka .
4. Mche unakua polepole.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

Kipindi cha 88 na 89 **Usafi wa mazingira 2**

**Matini**

**Mazingira Safi**



Watu wengi wana mawazo mbalimbali kuhusu mazingira safi. Watu hawa wanaweza kugawanywa katika makundi mawili. Kuna lile kundi lisilojali kuwa na mazingira safi. Kundi hili hudai kuwa mazingira safi huharibu uasili wa mahali polepole mpaka mahali hapo panabadilika. Wanaendelea kusema kuwa, tunapoyaweka mazingira safi, tunawakosea baadhi ya viumbe kama vile chatu kwa kuwanyima mahali pa kuishi. Wanatoa mfano wa panzi ambao hukosa mahali pa kuishi na kuzalia tunapofyeka nyasi. Wanyama na ndege wa porini kama vile tai hukosa makao tunapojaribu kuifanya misitu kuwa safi.

Kwa upande mwingine, kundi linalounga mkono kuwepo kwa mazingira safi lina sababu zake. Kwanza kabisa, kundi hili linanadai kuwa mazingira machafu ni chanzo cha maradhi. Hii ni kwa sababu, baadhi ya wadudu wanaobeba viini vinavyosababisha magonjwa fulani huishi mahali pachafu. Wanatoa mfano wa mbung'o anayesababisha ugonjwa wa malale. Vilevile, mazingira safi huvutia. Pia yanawatorosha wanyama hatari kama vile nyoka na panya. Vilevile, wadudu kama vile funza, viroboto na chawa hawawezi kumkaribia haraka binadamu anayeweka mazingira yake safi.

Ni vyema kuyatunza mazingira yetu ili yatufae na tuepukane na maradhi yanayotokana na uchafu.



Kipindi cha 88 na 89 **Usafi wa mazingira 2**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

ugonjwa wa malale mbung'o funza

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

chatu machafu chanzo tai

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kuna makundi mangapi ya watu yaliyotajwa mwanzoni mwa hadithi?
2. Tunafaa kufanya nini ili kujiepusha na baadhi ya magonjwa?
3. Mbung'o husababisha ugonjwa gani?
4. Je, unapinga au unaunga mkono kuwepo kwa mazingira safi? Kwa nini?

**Sarufi: Vielezi-Matumizi ya "polepole" na "haraka"**

**Jaza mapengo kwa kutumia "haraka" au "polepole".**

1. Kinyonga hutembea ______________.
2. Tulitembea ______________ ili tusichelewe.
3. Hatukufika kwa wakati kwa sababu tulitembea ____________.
4. Nilitembea ______________ ili niwafikie.



## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni: **chatu, tai, chafu, watu, tatu.**
Funza sauti **ch** na **t.**
Soma maneno **ukurasa wa 89.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Mtiririko - Kuhakiki**

Hakiki makala ya maelezo.


**U:** Wanafunzi wahakiki nakala huku wakizingatia:

1. uakifishaji
2. iwapo nakala inaeleweka,
3. tahajia.

## Kazi ya Ziada

Andika sentensi nne ukitumia **haraka** au **polepole**.
Msomee mlezi wako sentensi hizo.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Kipindi cha 90 Usafi wa mazingira 2

Tathmini ya msamiati

Chagua jibu linalofaa kulingana na maelezo.

| | | | |
|---|---|---|---|
| mbung'o | kipindupindu | kifyekeo | mkurupuko |

1. Aina ya ugonjwa.
2. Kutokea kwa maradhi katika jamii.
3. Kifaa cha kukatia nyasi.
4. Mdudu anayesababisha ugonjwa wa malale.

Tathmini ya sarufi

Tunga sentensi mbili ukitumia kielezi "polepole" na mbili ukitumia kielezi "haraka".

1. ______________________________
2. ______________________________
3. ______________________________
4. ______________________________

Chora vifaa vifuatavyo na uandike majina yake.

1. makasi
2. ufagio

Mali ya Serikali ya Kenya 90

## Msamiati

Fungueni **ukurasa wa 90** wa vitabu vyenu.
Chagua neno sahihi kutoka kwa jedwali kulingana na maelezo ya sentensi.

**Majibu**

1. kipindupindu
2. mkurupuko
3. kifyekeo
4. mbung'o

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiandika katika madaftari yao.

1. mkurupuko
2. tui
3. kifyekeo
4. sepetu
5. kina
6. ugonjwa wa malale
7. mbung'o
8. funza
9. chanzo
10. chenga

## Kuchambua Matini: Mtiririko

Kuchambua matini kwa kurejelea mbinu ya kufuata hatua maalum au mtiririko.

Hatua ya Kwanza
↓
Hatua Inayofuata
↓
Hatua ya Mwisho

**U:** Leo utashirikiana na mwenzako kuchambua matini ya mtiririko. Tambua matini ambayo ungependa kuchambua. Soma matini na mwenzako. Fuata hatua zifuatazo.

- Ni nini kilichofanyika mwanzo?
- Ni nini kilichofanyika katikati?
- Ni nini kilichofanyika mwisho?

## Sarufi

Tunga sentensi nne ukitumia vielezi **"haraka"** na **"polepole"**.

## Kazi ya Ziada

Chora kifyekeo na sepetu.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 91: Dukani 2

Kipindi cha 91 na 92 **Dukani 2**

Matini

**Mjarubi na Duka Lake**



Mjarubi ni muuzaji hodari wa bidhaa za dukani. Yeye ana duka lake sokoni. Asubuhi na mapema, Mjarubi hulifungua duka lake na kuanza kuwauzia wateja wake bidhaa kama vile maziwa, maandazi, sukari na majani chai. Unapoenda kununua bidhaa katika duka lake, yeye hukuuliza, "Unataka kununua nini?"

Ikifika saa tatu za asubuhi, Mjarubi hulifunga duka lake kwa muda kwenda kununua bidhaa zilizopungua. Yeye huenda kununua bidhaa hizo kwenye duka la jumla lililo mbali na soko.

Duka hili la jumla huuza vitu kwa bei ya chini ili naye muuzaji wa rejareja apate faida anapoviuza baadaye.

Saa kumi inapofika, Mjarubi huanza kupima sukari kwenye ratili. Yeye huzingatia uzito kamili bila kuwaibia wateja wake. Inapowadia saa kumi na mbili jioni, Mjarubi hujipatia kikombe cha chai. Chai hii humwezesha kufika saa tatu usiku anapolifunga duka lake.

Watu wanalipenda sana duka la Mjarubi. Kwa nini watu wanalipenda duka lake? Watu hulipenda duka lake kwa sababu wateja wake hupata kila wanachokitaka kutoka kwa duka lake. Kadhalika, Mjarubi ni karimu kwani wakati mteja amepungukiwa na senti, Mjarubi humkopesha.

91 Hakiuzwi

Kipindi cha 91 na 92 **Dukani 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

duka    duka la jumla    faida

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

bidhaa    mbili    mbali    bei

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni kwa nini Mjarubi ni muuzaji hodari?
2. Ni kwa sababu gani Mjarubi hulifunga duka lake saa tatu usiku?
3. Tunajifunza nini kutokana na muuzaji Mjarubi?
4. Taja uzuri wa muuzaji mwingine yeyote unayemjua.

Sarufi: Alama ya kiulizi (?)

**Tumia alama ya kiulizi (?) kuakifisha sentensi inavyofaa.**

1. Unataka kununua nini
2. Je, utakuja kwetu Jumapili
3. Shule zitafungwa lini
4. Tunaimba wimbo wa taifa siku gani

Mali ya Serikali ya Kenya    92

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **duka, duka la jumla, faida**

Soma maneno **ukurasa wa 92.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Maswali**

1. Kwa nini Mjarubi ni muuzaji hodari? (Kwa sababu yeye hulifungua duka lake asubuhi na mapema ili auze bidhaa.)
2. Ni kwa sababu gani Mjarubi hufunga duka lake saa tatu asubuhi? (Anafunga duka ili aende kwenye duka la jumla kununua bidhaa zilizopungua.)
3. Tunajifunza nini kutokana na muuzaji Mjarubi? (Kubali ibu lolote sahihi)
4. Taja uzuri wa muuzaji mwingine yeyote unayemjua. (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Alama ya Kiulizi

Waeleze wanafunzi kuhusu alama ya kuuliza.

Waeleze wanafunzi jinsi ya kutumia alama ya kiulizi kuakifisha sentensi. Elekeza wanafunzi kutambua sentensi zenye kiulizi kutoka kwenye matini.

Akifisha sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waakifishe sentensi peke yao.

## Kazi ya Ziada

Akifisha sentensi zifuatazo ukitumia alama ya kiulizi

1. Je, ulienda dukani
2. Muuzaji hufungua duka lake saa ngapi
3. Bidhaa zipi zinauzwa sokoni
4. Nani alifungua duka

**Majibu**

1. Je,ulienda dukani?
2. Muuzaji hufungua duka lake saa ngapi?
3. Bidhaa zipi zinauzwa sokoni?
4. Nani alifungua duka?

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 91 na 92 **Dukani 2**

Matini

**Mjarubi na Duka Lake**



Mjarubi ni muuzaji hodari wa bidhaa za dukani. Yeye ana duka lake sokoni. Asubuhi na mapema, Mjarubi hulifungua duka lake na kuanza kuwauzia wateja wake bidhaa kama vile maziwa, maandazi, sukari na majani chai. Unapoenda kununua bidhaa katika duka lake, yeye hukuuliza, "Unataka kununua nini?"

Ikifika saa tatu za asubuhi, Mjarubi hulifunga duka lake kwa muda kwenda kununua bidhaa zilizopungua. Yeye huenda kununua bidhaa hizo kwenye duka la jumla lililo mbali na soko.

Duka hili la jumla huuza vitu kwa bei ya chini ili naye muuzaji wa rejareja apate faida anapoviuza baadaye.

Saa kumi inapofika, Mjarubi huanza kupima sukari kwenye ratili. Yeye huzingatia uzito kamili bila kuwaibia wateja wake. Inapowadia saa kumi na mbili jioni, Mjarubi hujipatia kikombe cha chai. Chai hii humwezesha kufika saa tatu usiku anapolifunga duka lake.

Watu wanalipenda sana duka la Mjarubi. Kwa nini watu wanalipenda duka lake? Watu hulipenda duka lake kwa sababu wateja wake hupata kila wanachokitaka kutoka kwa duka lake. Kadhalika, Mjarubi ni karimu kwani wakati mteja amepungukiwa na senti, Mjarubi humkopesha.

91

Kipindi cha 91 na 92 **Dukani 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

duka | duka la jumla | faida

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

bidhaa | mbili | mbali | bei

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni kwa nini Mjarubi ni muuzaji hodari?
2. Ni kwa sababu gani Mjarubi hulifunga duka lake saa tatu usiku?
3. Tunajifunza nini kutokana na muuzaji Mjarubi?
4. Taja uzuri wa muuzaji mwingine yeyote unayemjua.

Sarufi: Alama ya kiulizi (?)

**Tumia alama ya kiulizi (?) kuakifisha sentensi inavyofaa.**

1. Unataka kununua nini
2. Je, utakuja kwetu Jumapili
3. Shule zitafungwa lini
4. Tunaimba wimbo wa taifa siku gani

Mali ya Serikali ya Kenya

92

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **bidhaa, mbili, boma, mbuzi**
Funza sauti: **b na mb**
Soma maneno **ukurasa wa 91.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Alama ya Kiulizi

Tumia alama ya kiulizi kwenye sentensi inavyofaa **Ukurasa wa 92.**

**Majibu**

1. Unataka kununua nini?
2. Je, utakuja kwetu Jumapili?
3. Shule zitafungwa lini?
4. Tunaimba wimbo wa taifa siku gani?

## Kuandika

**Mtiririko - Kuhariri**

T: Rekebisha makala yanayozingatia hatua maalum.

## Kazi ya Ziada

**Andika sentensi nne kisha ziakifishe ukitumia alama ya kiulizi.**

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 93: Dukani 2

**Kipindi cha** 93 na 94 — **Dukani 2**

### Matini

#### Duka la Juma



Juma alizaliwa katika familia maskini kijijini Mali. Baada ya kukamilisha masomo yake, alianza kufanya v barua vya hapa na pale akiwa kijana barobaro. Aliuza maji kutwa kucha huku akiwekeza hela kidogo kidogo. Baada ya muda, aliweza kujinunulia bidhaa kidogo na kuwa mchuuzi. Aliwauzia wakulima mbolea pia. Aliendelea kuwekeza katika shirika la wafanyabiashara wadogowadogo mbali na soko.

Baada ya muda, alitoa akiba yake na kufungua duka kwenye kibanda kilichokuwa na bidhaa nyingi. Kibanda cha Juma kilinawiri hadi akafungua duka kubwa kijijini Mali. Watu wengi wakaulizana, "Juma ametoa pesa wapi?"

Duka la Juma lilikuwa na bidhaa nyingi kuanzia sindano hadi spea za magari. Juma alikuja kuwa tajiri wa kutajika. Faida yake ikawa ni ya kujivunia. Pesa za sarafu zilibebwa kwa magunia na za noti kwenye bahasha ili kupelekwa benki.

Juma alikuwa mwema kwa watu wote, wakubwa kwa wadogo. Baada ya muda, Juma alibadil ka. Alipata kiburi na kuanza kuwadharau wateja wake.

Wateja walimtoroka na ndipo akaanza kupata hasara. Duka lake lilifilisika na bidhaa nyingi zikaanza kukosekana. Mwishowe, Juma alilifunga duka lake. Akakosa kulipa kodi na kutimuliwa kutoka dukani. Leseni ya kazi yake ikachukuliwa na baraza la mji. Baadaye, alirudia kufanya vibarua vidogovidogo. Watu wakashangaa na kuulizana, "Ni nini kilichofanyika?"



**Kipindi cha** 93 na 94 — **Dukani 2**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

hela benki hasara

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

mbio mbolea barobaro barua

### Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Familia ya Juma iliishi wapi?
2. Taja bidhaa mbili zilizopatikana katika duka la Juma.
3. Pesa za Juma ziliwekwa wapi?
4. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

### Sarufi: Alama ya kiulizi (?)

**Akifish asentensi zifuatazo kwa kutumia alama ifaayo.**

1. Jeni ametoa wapi pesa
2. Juma alikuwa anafanya kazi gani
3. Wanafunzi wamefunga shule
4. Pesa za Juma ziliwekezwa wapi

### Kuandika

**Tazama picha katika ukurasa wa 93. Andika sentensi tano kuhusu picha hiyo.**



## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **hela, hasara, benki.**

Soma maneno **ukurasa wa 94.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## ? Ufahamu

**Maswali**

1. Familia ya Juma iliishi wapi? (kijiji cha Mali.)
2. Taja bidhaa mbili zilizopatikana katika duka la Juma. (mafuta, mbegu na spea za magari.)
3. Pesa za Juma ziliekezwa wapi? (shirika la wafanyabiashara wadogowadogo.)
4. Umejifunza nini kutokana na hadithi ya Juma (Kubali jibu lolote kama; nimejifunza kuwa ni vibaya kuwa na kiburi na mengineyo.)

## Sarufi: Alama ya Kiulizi

Akifisha sentensi pamoja na wanafunzi. Wanafunzi waakifishe peke yao.

**Majibu**

1. Jeni ametoa wapi pesa?
2. Juma alikuwa anafanya kazi gani?
3. Wanafunzi wamefunga shule?
4. Pesa za Juma ziliwekwa wapi?

## Kazi ya Ziada

Msomee mlezi wako sentensi zifuatazo kwa ufasaha.

1. Mama alitumia senti kununua bidhaa.
2. Vitu vingi huuzwa katika duka gani?
3. Mimi sina hela.
4. Pesa ziliwekezwa wapi?

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 94: Dukani 2

Kipindi cha 93 na 94 **Dukani 2**

Matini

**Duka la Juma**



Juma alizaliwa katika familia maskini kijijini Mali. Baada ya kukamilisha masomo yake, alianza kufanya v barua vya hapa na pale akiwa kijana barobaro. Aliuza maji kutwa kucha huku akiwekeza hela kidogo kidogo. Baada ya muda, aliweza kujinunulia bidhaa kidogo na kuwa mchuuzi. Aliwauzia wakulima mbolea pia. Aliendelea kuwekeza katika shirika la wafanyabiashara wadogowadogo mbali na soko.

Baada ya muda, alitoa akiba yake na kufungua duka kwenye kibanda kilichokuwa na bidhaa nyingi. Kibanda cha Juma kilinawiri hadi akafungua duka kubwa kijijini Mali. Watu wengi wakaulizana, "Juma ametoa pesa wapi?"

Duka la Juma lilikuwa na bidhaa nyingi kuanzia sindano hadi spea za magari. Juma alikuja kuwa tajiri wa kutajika. Faida yake ikawa ni ya kujivunia. Pesa za sarafu zilibebwa kwa magunia na za noti kwenye bahasha ili kupelekwa benki.

Juma alikuwa mwema kwa watu wote, wakubwa kwa wadogo. Baada ya muda, Juma alibadil ka. Alipata kiburi na kuanza kuwadharau wateja wake.

Wateja walimtoroka na ndipo akaanza kupata hasara. Duka lake lilifilisika na bidhaa nyingi zikaanza kukosekana. Mwishowe, Juma alilifunga duka lake. Akakosa kulipa kodi na kutimuliwa kutoka dukani. Leseni ya kazi yake ikachukuliwa na baraza la mji. Baadaye, alirudia kufanya vibarua vidogovidogo. Watu wakashangaa na kuulizana, "Ni nini kilichofanyika?"

93 Hakluzwi

Kipindi cha 93 na 94 **Dukani 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

hela benki hasara

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

mbio mbolea barobaro barua

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Familia ya Juma iliishi wapi?
2. Taja bidhaa mbili zilizopatikana katika duka la Juma.
3. Pesa za Juma ziliwekwa wapi?
4. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

Sarufi: Alama ya kiulizi (?)

**Akifish asentensi zifuatazo kwa kutumia alama ifaayo.**

1. Jeni ametoa wapi pesa
2. Juma alikuwa anafanya kazi gani
3. Wanafunzi wamefunga shule
4. Pesa za Juma ziliwekezwa wapi

Kuandika

**Tazama picha katika ukurasa wa 93. Andika sentensi tano kuhusu picha hiyo.**

Mali ya Serikali ya Kenya 94

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **bidhaa, baada, ambacho, mbegu, mboga, bahasha.**

Funza sauti: **b** na **mb.**

Soma maneno **ukurasa wa 89.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Mtiririko - Kuhariri**

**U:** Katika makundi ya wanafunzi wawili andika insha kuhusu duka.

## Kazi ya Ziada

**Andika sentensi hizi kwa usahihi kisha ziakifishe.**

1. bidhaa senti nani ana za kununua
2. wapi pesa huwekwa
3. sukari je umenunua
4. dukani siku tutaenda gani

**Majibu**

1. Nani ana senti za kununua bidhaa?
2. Pesa huwekwa wapi?
3. Je, umenunua sukari?
4. Tutaenda dukani siku gani?

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 95: Dukani 2

Kipindi cha 95 **Dukani 2**

**Tathmini ya msamiati**

**Chagua jibu sahihi kulingana na maelezo.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| benki | duka | sarafu | hela |

1. Aina ya pesa zilizotengenezwa kwa chuma.
2. Mahali ambapo pesa huhifadhiwa.
3. Pahali ambapo bidhaa huuzwa.
4. Jina jingine la pesa.

**Tathmini ya sarufi**

**Akifisha sentensi zifuatazo kwa kutumia alama ya kiulizi.**

1. Je, ulienda dukani
2. Muuzaji hufungua duka lake saa ngapi
3. Ni bidhaa zipi zinauzwa sokoni
4. Nani alifungua duka

95 Hakiuzwi

## Tathmini ya Msamiati

Fungua **ukurasa wa 95** wa vitabu vyenu.
Chagua neno sahihi kutoka kwa jedwali kulingana na maelezo ya sentensi.

**Majibu**

1. sarafu 2. benki 3. duka 4. hela

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili huku wanafunzi wakiandika katika madaftari yao.

**bidhaa, dada, duka la jumla, senti, sarafu, hela, ambacho, benki, mbegu, bei**

## Kuchambua Matini: Mtiririko

Kuchambua matini kwa kurejelea mbinu ya kufuata hatua maalum au mtiririko.

Hatua ya Kwanza
↓
Hatua Inayofuata
↓
Hatua ya Mwisho

**U:** [Leo utashirikiana na mwenzako kuchambua matini ya mtiririko. Tambua matini ambayo ungependa kuchambua. Soma matini na mwenzako. Fuata hatua zifuatazo.
- Ni nini kilichofanyika mwanzo?
- Ni nini kilichofanyika katikati?
- Ni nini kilichofanyika mwisho?]

## Tathmini ya Sarufi

Akifisha sentensi ifaavyo.

**Majibu**

1. Je, ulienda dukani?
2. Muuzaji hufungua duka lake saa ngapi?
3. Ni bidhaa zipi zinauzwa sokoni?
4. Nani alifungua duka?

## Kazi ya Ziada

Andika insha fupi kuhusu pesa.

## Kazi ya Nyongeza

Waulize wanafunzi waigize muuzaji na mnunuzi katika duka lao la darasani.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

Kipindi cha 96 na 97 **Ndege Nimpendaye 2**

Matini

**Maisha ya Njiwa**



Njiwa hujenga viota juu ya miti, kama vile wafanyavyo ndege wengine. Wao huishi katika familia ya mama na baba. Hii ni tofauti na keremkeremu wanaojenga viota mitini na kuishi katika makundi.

Baada ya kujenga kiota, njiwa wa kike hutaga mayai mawili. Yeye huyaatamia usiku naye wa kiume huyaatamia wakati wa mchana. Wao hufanya hivi ili mayai yapate joto la kutosha yakiwa ndani ya kiota. Hii ni tofauti na tomboro ambaye mayai yake huatamiwa na tomboro wa kike pekee.

Makinda ni wana wa ndege wanaoanguliwa. Makinda wa njiwa huanguliwa kati ya siku kumi na nne na ishirini. Njiwa wote wawili, wa kike na wa kiume, huchangia katika malezi ya makinda. Wao hutafuta chakula na kuwalinda makinda wasiliwe na wanyama kama vile mbweha. Keremkeremu pia huwalisha na kuwatunza makinda wake vizuri kama njiwa. Baadaye, makinda hupata nguvu na uwezo wa kujitafutia chakula chao wenyewe.

Mayai na nyama ya ndege hawa huliwa na binadamu. Je, wajua kuwa njiwa, kama kasuku, akifunzwa polepole anaweza kutambua herufi zote za alfabeti? Sasa wajua.

Mali ya Serikali ya Kenya 96

Kipindi cha 96 na 97 **Ndege Nimpendaye 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

njiwa tomboro keremkeremu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

walioumbwa mbweha mbwembwe pambwa


Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ndege wengi hupenda kufanya nini?
2. Kwa nini ndege huatamia mayai yake?
3. Makinda wa njiwa huanguliwa baada ya muda gani?
4. Ndege wana umuhimu gani katika maisha ya mwanadamu?

Sarufi: Vihusishi

**Tunga sentensi kwa kuzingatia picha. Tumia vihusishi, "juu ya" na "chini ya".**




97 Hakiuzwi

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno yafuatayo ya msamiati: **njiwa**, **tomboro**, **keremkeremu.**

Soma maneno **ukurasa wa 97.**


## Kusoma Matini: Mtiririko

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabili. Soma hadithi.

## Ufahamu:

**Ramani Dhana**

Chora ramani dhana



**T:** [Sasa ni wakati wa kujadili tuliyoyasoma katika hadithi. Tulisoma kuhusu maisha ya njiwa. Tutatumia ramani dhana itakayotusaidia kuelewa hadithi hii vizuri. Katikati ya ramani hii, tutaandika neno **njiwa**. Je, ni nani anayeweza kutueleza kuhusu makala tuliyosoma kuhusu **maisha ya njiwa**?

Nitachora mfano wa mkono hapa na kuandika ndani ya duara. Ni nani mwingine anaweza kuongezea jambo lingine kuhusu makala tuliyoyasoma? Jambo hilo linasikikaje? Linakuvutia vipi? (*Kwa kila wazo jipya, andika kwa kisanduku kipya.) Waelekeze kuunda sentensi baada ya kutoa maelezo yao.)*]

**U:** [Sasa ni wakati wa kuandika sentensi itakayotoa maelezo kuhusu **maisha ya njiwa**. *(Waeleze kuunda sentensi baada ya kutoa maelezo yao.*]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Ndege wengi hupenda kufanya nini? (Kujenga viota juu ya miti.)
2. Kwa nini ndege huatamia mayai yake? (Ili mayai yake yapate joto la kutosha.)
3. Makinda wa njiwa huanguliwa baada ya muda gani? (siku kumi na nne.)
4. Ndege wana umuhimu gani katika maisha ya mwanadamu? (mayai yake na nyama huliwa na binadamu.)

## Sarufi: Vihusishi

Waeleze wanafunzi sarufi. Waeleze wanafunzi kusoma sentensi zenye sarufi kwenye matini. Akifisha sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waakifishe sentensi peke yao.

## Kazi ya Ziada

Wanafunzi wachore ndege wampendaye.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 97: Ndege Nimpendaye 2



**Matini**

**Maisha ya Njiwa**



Njiwa hujenga viota juu ya miti, kama vile wafanyavyo ndege wengine. Wao huishi katika familia ya mama na baba. Hii ni tofauti na keremkeremu wanaojenga viota mitini na kuishi katika makundi.

Baada ya kujenga kiota, njiwa wa kike hutaga mayai mawili. Yeye huyaatamia usiku naye wa kiume huyaatamia wakati wa mchana. Wao hufanya hivi ili mayai yapate joto la kutosha yakiwa ndani ya kiota. Hii ni tofauti na tomboro ambaye mayai yake huatamiwa na tomboro wa kike pekee.

Makinda ni wana wa ndege wanaoanguliwa. Makinda wa njiwa huanguliwa kati ya siku kumi na nne na ishirini. Njiwa wote wawili, wa kike na wa kiume, huchangia katika malezi ya makinda. Wao hutafuta chakula na kuwalinda makinda wasiliwe na wanyama kama vile mbweha. Keremkeremu pia huwalisha na kuwatunza makinda wake vizuri kama njiwa. Baadaye, makinda hupata nguvu na uwezo wa kujitafutia chakula chao wenyewe.

Mayai na nyama ya ndege hawa huliwa na binadamu. Je, wajua kuwa njiwa, kama kasuku, akifunzwa polepole anaweza kutambua herufi zote za alfabeti? Sasa wajua.





**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

njiwa tomboro keremkeremu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

walioumbwa mbweha mbwembwe pambwa


**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Ndege wengi hupenda kufanya nini?
2. Kwa nini ndege huatamia mayai yake?
3. Makinda wa njiwa huanguliwa baada ya muda gani?
4. Ndege wana umuhimu gani katika maisha ya mwanadamu?

**Sarufi: Vihusishi**

**Tunga sentensi kwa kuzingatia picha. Tumia vihusishi, "juu ya" na "chini ya".**






## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni: **mbwa, ameumbwa, walioumbwa, umbwa, mbwata.**
Funza sauti **mbw**
Soma maneno **ukurasa wa 97.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vihusishi

Waeleze wanafunzi sarufi. Tazama picha ya kwanza pamoja na wanafunzi. Sema, "Kikombe kiko juu ya meza!". Wanafunzi wasome sentensi ya pili. Wanafunzi waangalie picha ya 3 na ya 4 kisha watunge sentensi.

## Kuandika

**Mtiririko - Kuchapisha**

1. Mwanafunzi asomee mwenzake makala aliyoandika.
2. MKumbusha mwanafunzi awe makini anaposomewa makala.
3. Waulize wanafunzi 2-3 kuelezea juu ya makala waliyosomewa.

**Majibu**

1. Kikombe kiko juu ya meza.
2. Kikombe kiko chini ya meza.
3. Sahani iko juu ya meza.
4. Sahani iko chini ya meza.

## Kazi ya Ziada

Andika maneno manne yenye herufi –mbw uliyoyasoma leo.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 98 na 99 **Ndege Nimpendaye 2**

**Matini**

**Ziara ya Porini**

Wanafunzi wa darasa la tatu waliingojea siku ya Jumamosi kwa hamu na ghamu. Ilikuwa siku ya safari ya kuzuru msitu wa Mau. Siku hiyo ilipofika waliabiri basi upesiupesi na kuanza safari.

Mwalimu wao alikuwa amewafunza kuhusu ndege tofauti wa porini. Kila mmoja alitaka kuwa wa kwanza kuwatambua ndege hao. Wengine walibeba picha za ndege wakiwa juu ya mti ili waweze kuwatambua kwa urahisi.



Walipofika porini Mwaura alisema,"Yule pale chiriku," akiashiria kwa kidole."Si chiriku! Ni kasuku," akapinga Chebet.

"Shhh! Nyamazeni. Angalieni kwa makini kidona chake. Kimejikunja kumwezesha kula matunda na chipuka za mimea,"akasema mwalimu.

Mara ndege huyo akatoa mlio.Wakakumbuka jinsi mwalimu alivyokuwa ameigiza chiriku anavyolia. Ikadhibitisha kuwa ndege huyo alikuwa chiriku.

Walipofika mtoni, waliviona viota vingi vya mbayuwayu vilivyotengenezwa kwa udongo na nyasi chini ya daraja. Viota hivyo vilikuwa imara. Visingeweza kusombwa na maji.

Kando ya mto waliwaona minana, ndege wenye rangi ya manjano. Hao huishi kwenye miti mikubwa na kutafuta chakula kwenye makundi. Njiani walipokuwa wakirudi, walimwona mbweha na wanyama wengine wa porini. Walizungumza mengi kuhusu insha ambazo wangeandika kuhusu ndege wa porini.

Mali ya Serikali ya Kenya 98


Kipindi cha 98 na 99 **Ndege Nimpendaye 2**


**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

chiriku mbayuwayu minana

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

kusombwa mbweha bwawa lumbwi

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kwa nini wanafunzi wa darasa la tatu waliingojea siku ya Jumamosi kwa hamu?
2. Wanafunzi walipofika porini walimwona ndege yupi?
3. Nyumba ya ndege huitwaje?
4. Je, unafikiri wanafunzi walijifunza nini kuhusu ndege?

**Sarufi: Matumizi ya "chini ya" na "Juu ya"**

**Tunga sentensi nne ukitumia vihusishi "chini ya" na "juu ya".**

**Kwa mfano:** Kiatu kiko **chini ya** kabati.

99 Hakluzwi

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **chiriku, mbayuwayu, minana.**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.
Soma maneno **ukurasa wa 99.**


## Kusoma Matini: Mtiririko

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

### Ramani Dhana

Chora ramani dhana



**T:** [Sasa ni wakati wa kujadili tuliyoyasoma katika hadithi. Tulisoma kuhusu **ziara ya porini.** Tutatumia ramani dhana itakayotusaidia kuelewa hadithi hii vizuri. Katikati ya ramani hii, tutaandika neno porini. Je, ni nani anayeweza kutueleza kuhusu makala tuliyosoma kuhusu **ziara ya porini.** Nitachora mfano wa mkono hapa na kuandika ndani ya duara. Ni nani mwingine anaweza kuongezea jambo jingine kuhusu makala tuliyoyasoma? Jambo hilo linasikikaje? Linakuvutia vipi? (*Kwa kila wazo jipya, andika kwa kisanduku kipya.)*]

**U:** [Sasa ni wakati wa kuandika sentensi itakayotoa maelezo kuhusu **ziara ya porini**. *(Waeleze manafunzi kuunda sentensi baada ya kutoa maelezo yao.)*]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Kwa nini wanafunzi wa darasa la tatu waliingojea siku ya Jumamosi kwa hamu? (Ilikuwa ni siku ya safari kuzuru msitu wa Mau)
2. Wanafunzi walipofika porini walimwona ndege yupi? (Chiriku)
3. Nyumba ya ndege huitwaje? (Kiota)
4. Je, unafikiri wanafunzi walijifunza nini kuhusu ndege? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Vihusishi

Tunga sentensi ukitumia vihusishi '**juu ya**' na '**chini ya**'.
Andika sentensi.

## Kazi ya Ziada

**Jaza mapengo ukitumia "juu ya" au "chini ya"**

1. Kofia iko ____ kichwa. (juu ya)
2. Jiwe liko ____ mti. (chini ya)
3. Mto ulipita ____ ya daraja. (chini ya)
4. Panya alijificha ____ kitanda alipofukuzwa na paka. (chini ya)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 99: Ndege Nimpendaye 2

Kipindi cha 98 na 99 **Ndege Nimpendaye 2**

Matini

**Ziara ya Porini**

Wanafunzi wa darasa la tatu waliingojea siku ya Jumamosi kwa hamu na ghamu. Ilikuwa siku ya safari ya kuzuru msitu wa Mau. Siku hiyo ilipofika waliabiri basi upesiupesi na kuanza safari.

Mwalimu wao alikuwa amewafunza kuhusu ndege tofauti wa porini. Kila mmoja alitaka kuwa wa kwanza kuwatambua ndege hao. Wengine walibeba picha za ndege wakiwa juu ya mti ili waweze kuwatambua kwa urahisi.



Walipofika porini Mwaura alisema,"Yule pale chiriku," akiashiria kwa kidole."Si chiriku! Ni kasuku," akapinga Chebet.

"Shhh! Nyamazeni. Angalieni kwa makini kidona chake. Kimejikunja kumwezesha kula matunda na chipuka za mimea,"akasema mwalimu.

Mara ndege huyo akatoa mlio.Wakakumbuka jinsi mwalimu alivyokuwa ameigiza chiriku anavyolia. Ikadhibitisha kuwa ndege huyo alikuwa chiriku.

Walipofika mtoni, waliviona viota vingi vya mbayuwayu vilivyotengenezwa kwa udongo na nyasi chini ya daraja. Viota hivyo vilikuwa imara. Visingeweza kusombwa na maji.

Kando ya mto waliwaona minana, ndege wenye rangi ya manjano. Hao huishi kwenye miti mikubwa na kutafuta chakula kwenye makundi. Njiani walipokuwa wakirudi, walimwona mbweha na wanyama wengine wa porini. Walizungumza mengi kuhusu insha ambazo wangeandika kuhusu ndege wa porini.

Mali ya Serikali ya Kenya

98

Kipindi cha 98 na 99 **Ndege Nimpendaye 2**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

chiriku mbayuwayu minana

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kusombwa mbweha bwawa lumbwi

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kwa nini wanafunzi wa darasa la tatu waliingojea siku ya Jumamosi kwa hamu?
2. Wanafunzi walipofika porini walimwona ndege yupi?
3. Nyumba ya ndege huitwaje?
4. Je, unafikiri wanafunzi walijifunza nini kuhusu ndege?

Sarufi: Matumizi ya "chini ya" na "Juu ya"

**Tunga sentensi nne ukitumia vihusishi "chini ya" na "juu ya".**

**Kwa mfano:** Kiatu kiko **chini ya** kabati.

99

Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **kusoma, mbweha, mbwamwitu**

Funza sauti **mbw.**

Soma maneno **ukurasa wa 99.**

## Kusoma Matini: Mtiririko

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Mtiririko - Kuchapisha**

1. Mwanafunzi asomee mwenzake makala aliyoandika.
2. MKumbusha mwanafunzi awe makini anaposomewa makala.
3. Waulize wanafunzi 2-3 kuelezea juu ya makala waliyosomewa.

## Kazi ya Ziada

**Jaza mapengo kwa kutumia:**

chiriku, mbayuwayu, Tomboro, Keremkerem


1. ___________ wa kike huatamia mayai yake pekee.
2. ___________ hujenga viota mitini nakuishi kwa makundi.
3. Kidona cha ___________ kimejikunja.
4. Viota vya ___________ hutengenezwa kwa udongo na nyasi.

**Majibu**

1. Tomboro
2. Keremkeremu
3. chiriku
4. mbayuwayu

Tarehe: ___________________________ Muda: _______________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 100: Ndege Nimpendaye 2



Kipindi cha 100 Ndege Nimpendaye 2

Tathmini ya msamiati

Unda majina manne ya ndege kutokana na silabi ulizopewa kwenye jedwali hili.

| | | | |
|---|---|---|---|
| nji | ke | yu | va |
| chi | na | wa | re |
| m | mba | ku | ri |

Tathmini ya sarufi

Jaza mapengo kwa kutumia vihusishi "chini ya" na "juu ya".

1. Mnana amejenga kiota ____________ mti.
2. Machungwa yameanguka ____________ mti.
3. Mtoto amejificha ____________ kitanda.
4. Mwanafunzi anaandikia barua ______________ meza.

Mali ya Serikali ya Kenya 100

## Msamiati

[Fungua **ukurasa wa 100** wa vitabu vyenu. Tazama sehemu ya msamiati. Kuna jedwali la silabi.

Unda majina manne ya ndege kutokana na jedwali hilo.]

**Majibu**

1. njiwa
2. chiriku
3. mbayuwayu
4. kuku

## Kusoma Maneno

Soma neno mara mbili huku wanafunzi wakiliandika.


Maneno: **walioumbwa, mbwata, mbweha, sombwa, kusombwa, lumbwi, mbayuwayu, bwawa, mbwembwe, bweka**

## Kuchambua Matini

**Ramani Dhana**

Leo utachora ramani dhana peke yako.

**U:** [Chagua mojawapo ya hadithi mbili tulizosoma wiki hii. Soma hadithi hiyo na kisha uchore ramani dhana. Eleza mambo matatu muhimu ambayo hadithi hiyo imezungumzia. Andika sentensi moja kuhusu mada hiyo uliyoipenda. Kumbuka huu ndio mfano wa ramani dhana.]



## Sarufi: Vihusishi

Jaza mapengo kwa kutumia '**juu ya**' au '**chini ya**'.

**Majibu ya tathmini ya sarufi.**

1. juu ya
2. chini ya
3. chini ya
4. juu ya

## Kazi ya Ziada

**Tunga sentensi ukitumia vihusishi "juu ya" na "chini ya".**

Tunga sentensi mbili mbili ukitumia kila kihusishi.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 101: Marejeleo 3

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo**

**Matini**

### Arusi ya kufana



Kaloo alijitayarisha kwenda arusini. Alivalia nguo mpya nyekundu yenye madoadoa meupe ili aweze kujiunga na gwaride la arusi. Alikuwa anapendeza. "Uko wapi mwanangu? Harakisha, tusichelewe," Mama yake alimuuliza. "Mama, naja sasa hivi," alij bu Kaloo.

Kaloo na mamake walielekea kwenye kituo kidogo cha magari ya kwenda Rahani. "Mama! Mama! Muone mkulima yule anapalilia mahindi kwa kutumia trekta," alisema Kaloo. "Aah! Huyu ni mwananchi mzalendo na mwenye bidii. Atavuna mazao mengi yatakayowalisha wananchi wengi. Hebu nipe mkono wako nikushike ili tuvuke barabara," alisema mama Kaloo. Baada ya kuvuka barabara, Kaloo na mama yake waliabiri gari. Gari likang'oa nanga. Ndani ya gari, redio ya Mzalendo ilikuwa ikitangaza taarifa. Mtangazaji alisema kuwa katika taifa jirani kulikuwa na mkurupuko wa ugonjwa wa kipindupindu. Aliwatahadharisha watu dhidi ya kula vyakula ovyoovyo barabarani. Utingo akasema, "Senti! Leteni senti. Nauli ni shilingi hamsini." Mamake Kaloo alitoa pesa kwenye mkoba wake mpya polepole na kumpa utingo.

Walipofika Rahani walielekea kwenye bustani kulikoandaliwa arusi. Arusi ilifana sana. Bibi arusi alikuwa mrembo kama malaika. Bwana harusi naye alikuwa mtanashati mwenye umbo la kupendeza. Vyakula mbalimbali viliandaliwa kwenye mahema mapana katika bustani hiyo. Wanasarakasi waliwatumbuiza wageni.

Siku iliyofuata, Kaloo aliwasimulia marafiki zake kuhusu arusi hiyo. Marafiki zake walilia ngoa kwa kukosa kuhudhuria arusi.

101 Hakiuzwi

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

gwaride mkurupuko kipindupindu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

kwenye mpya nyekundu bwana

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kaloo na mama yake walienda arusini wapi?
2. Unafikiri ni kwa nini mama alimshika Kaloo mkono?
3. Kaloo aliona nini walipokuwa wakielea kwenye kituo cha magari?
4. Je, unafikiri ni vyakula gani viliandaliwa kwenye arusi?

**Sarufi: Vimilikishi**

**Jaza mapengo kwa kutumia vimilikishi sahihi.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Kituo chake kitafungwa. | Vituo _____ vitafungwa. |
| 2. Msichana _____ ataolewa Desemba. | Wasichana wao wataolewa Desemba. |
| 3. Rafiki yake alihudhuria arusi hiyo. | Marafiki _____ walihudhuria arusi hizo. |
| 4. Mtoto wake analia kwa uchungu. | Watoto _____ wanalia kwa uchungu. |

Mali ya Serikali ya Kenya 102

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **gwaride, mkurupuko, kipindupindu.**

Soma maneno **ukurasa wa 102.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

### Maswali

1. Kaloo na mamake walienda arusini wapi?(Rahani)
2. Unafikiri ni kwa nini mama alimshika Kaloo mkono? (ili amvukishe barabara)
3. Kaloo aliona nini walipokuwa wakielea kwenye kituo cha magari? (mkulima aliyepalilia mahindi kwa kutumia trekta)
4. Je, unafikiri ni vyakula gani vilivyoandaliwa kwenyearusi? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Vimilikishi

Vimilikishi ni maneno yanayoonyesha kitu ni cha nani.
Soma sentensi kutoka kwa matini.
Andika sentensi na wanafunzi.
Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi nne ukitumia maneno yafuatayo.

1. hudhuria
2. bustani
3. kipindupindu
4. ng'oa nanga

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 102: Marejeleo 3

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo**

Matini

**Arusi ya kufana**



Kaloo alijitayarisha kwenda arusini. Alivalia nguo mpya nyekundu yenye madoadoa meupe ili aweze kujiunga na gwaride la arusi. Alikuwa anapendeza. "Uko wapi mwanangu? Harakisha, tusichelewe," Mama yake alimuuliza. "Mama, naja sasa hivi," alijibu Kaloo.

Kaloo na mamake walielekea kwenye kituo kidogo cha magari ya kwenda Rahani. "Mama! Mama! Muone mkulima yule anapalilia mahindi kwa kutumia trekta," alisema Kaloo. "Aah! Huyu ni mwananchi mzalendo na mwenye bidii. Atavuna mazao mengi yatakayowalisha wananchi wengi. Hebu nipe mkono wako nikushike ili tuvuke barabara," alisema mama Kaloo. Baada ya kuvuka barabara, Kaloo na mama yake waliabiri gari. Gari likang'oa nanga. Ndani ya gari, redio ya Mzalendo ilikuwa ikitangaza taarifa. Mtangazaji alisema kuwa katika taifa jirani kulikuwa na mkurupuko wa ugonjwa wa kipindupindu. Aliwatahadharisha watu dhidi ya kula vyakula ovyoovyo barabarani. Utingo akasema, "Senti! Leteni senti. Nauli ni shilingi hamsini." Mamake Kaloo alitoa pesa kwenye mkoba wake mpya polepole na kumpa utingo.

Walipofika Rahani walielekea kwenye bustani kulikoandaliwa arusi. Arusi ilifana sana. Bibi arusi alikuwa mrembo kama malaika. Bwana harusi naye alikuwa mtanashati mwenye umbo la kupendeza. Vyakula mbalimbali viliandaliwa kwenye mahema mapana katika bustani hiyo. Wanasarakasi waliwatumbuiza wageni.

Siku iliyofuata, Kaloo aliwasimulia marafiki zake kuhusu arusi hiyo. Marafiki zake walilia ngoa kwa kukosa kuhudhuria arusi.

101 Hakiluzwi

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

gwaride mkurupuko kipindupindu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kwenye mpya nyekundu bwana

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kaloo na mama yake walienda arusini wapi?
2. Unafikiri ni kwa nini mama alimshika Kaloo mkono?
3. Kaloo aliona nini walipokuwa wakielea kwenye kituo cha magari?
4. Je, unafikiri ni vyakula gani viliandaliwa kwenye arusi?

Sarufi: Vimilikishi

**Jaza mapengo kwa kutumia vimilikishi sahihi.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Kituo chake kitafungwa. | Vituo _____ vitafungwa. |
| 2. Msichana _____ ataolewa Desemba. | Wasichana wao wataolewa Desemba. |
| 3. Rafiki yake alihudhuria arusi hiyo. | Marafiki _____ walihudhuria arusi hizo. |
| 4. Mtoto wake analia kwa uchungu. | Watoto _____ wanalia kwa uchungu. |

Mali ya Serikali ya Kenya 102

## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni: **kwenye, mpya, mbalimbali, mwenye, ndugu, bweha**

Funza sauti **kw py mw nd** na **bw.**

Soma maneno **ukurasa wa 102.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vimilikishi

Vimilikishi ni maneno yanayoonyesha kitu ni cha nani. Jaza mapengo kwa kutumia vimilikishi sahihi.

**Majibu**

1. vyao
2. wake
3. zao/wao
4. wao

## Kuandika

**Mjadala - Kupanga**

**T:** Panga - Kupanga jinsi ya kuandika insha fupi.

[Leo tutajifunza jinsi ya kupanga kuandika insha ya mjadala.]

- Chagua mada.
- Utangulizi
- Toa hoja kwa kila upande.
- Toa ushahidi kuhusu hoja zako.
- Tamatisha kwa kutoa uamuzi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Soma maneno haya kwa sauti.

1. ng'ara
2. ng'ambo
3. utingo
4. ng'ang'ana
5. nyang'anya
6. ngozi

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 103 na 104 **Marejeleo**

Matini

**Moseti na Ngiri**



Hapo zamani za kale, paliishi k jana aliyeitwa Moseti. Moseti alikuwa yatima. Moseti aliishi na nyanya yake aliyekuwa maskini hohehahe katika kijiji kizuri cha Wema. Wanakijiji walikuwa na moyo wa kuisaidia familia ya Moseti kwa kumpatia nyanya yake vibarua. Nyanya yake Moseti alikuwa akirauka kwenda kufanya vibarua vya kulima na kusafisha vibanda. Moseti alikuwa mwepesi wa kumsaidia nyanya yake kufanya kazi za nyumbani.

Kila alipokwenda mtoni kuchota maji, Moseti alikutana na wanyama mbalimbali. Akajifunza namna ya kuwasiliana na wanyama hao. Akawa rafiki wa ngiri mmoja mfupi mnene aliyekuwa na meno marefu. Kutokana na meno yake, Moseti alimwita ngiri huyo Meno.

Moseti aliishi na funza miguuni kutokana na mazingira machafu walimoishi. Miguu yake ilijaa vidonda vilivyomfanya asiweze kutembea vizuri. Meno alimhurumia. Akamuuliza, "Kwa nini huendi hospitali?" Moseti akamjibu, "Nyanya yangu hana pesa za kulipa hospitalini." Meno alisema, "Njoo nikupeleke mahali." Akamwongoza Moseti haraka hadi kwa ngiri mzee aliyekuwa daktari wa wanyama wa msituni. Moseti alipewa dawa ya majani yaliyosagwa akajipaka. Baada ya wiki moja, miguu yake ilikuwa iking'ara. Nyanya yake alifurahi. Akamuuliza, "Moseti, ulitoa wapi dawa ya kuwaangamiza funza?" Moseti alicheka na kumjibu, "Nilipewa dawa na ngiri mzee." Nyanya alishangazwa na tukio hilo. Siku iliyofuata, Moseti na nyanya yake walimtembelea yule ngiri mzee. Walimshukuru kwa kumtibu Moseti. Nyanya yake akaamua kuwa atakuwa akiweka makazi yao safi.



Hakiuzwi

Kipindi cha 103 na 104 **Marejeleo**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

vibanda funza daktari

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

akamwongoza nyumbani vidonda kwenda

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Moseti aliishi na nani?
2. Moseti alimsaidia nyanya yake kufanya kazi gani?
3. Ni kwa nini nyanya alishangaa baada ya Moseti kupona?
4. Je, wewe hufanya kazi gani kuwasaidia walezi wako?

Sarufi: Nafsi, wakati na vielezi

**Kamilisha sentensi kwa kuchagua jibu sahihi.**

1. Ukiwa na funza miguuni utatembea ____ (polepole, haraka).
2. Mtoto ____ shuleni kesho. (ataenda, alienda)
3. Tunda ____ limeiva vizuri. (wao, lao)
4. Watoto ____ wamepita mtihani. (yao, wao)

Kuandika

**Andika insha fupi kuhusu arusi uliyohudhuria.**

Mali ya Serikali ya Kenya



## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **vibanda, funza, daktari.**

Soma maneno **ukurasa wa 104.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Maswali**

1. Moseti aliishi na nani? (Nyanya yake)
2. Moseti alimsaidia nyanyake kufanya kazi gani? (kuchota maji.)
3. Kwa nini nyanya alishangaa baada ya Moseti kupona? (Nyanyake Moseti alishangaa kwa sababu Moseti alipewa dawa na ngiri.)
4. Je, wewe hufanya kazi gani kuwasaidia walezi wako? (Kubali jibu lolote k.m. kusaidia jikoni, kupika n.k.)

## Sarufi: Nafsi, Wakati na Vielezi

mapengo kwa kutumia vielezi sahihi

**Majibu**

1. polepole
2. haraka
3. haraka
4. polepole

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chagua kilekezi sahihi kujaza nafasi (mzuri, mnene, mazuri, kizuri).

1. Kikombe ____________ kimevunjika. (kizuri)
2. Mzazi ____________ amelipa karo. (mzuri)
3. Matunda ____________ yameiva. (mazuri)
4. Mtoto ____________ ana kalamu nzuri. (mnene)

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________



Hakiuzwi

Kipindi cha 103 na 104 **Marejeleo**

**Matini**

**Moseti na Ngiri**



Hapo zamani za kale, paliishi kijana aliyeitwa Moseti. Moseti alikuwa yatima. Moseti aliishi na nyanya yake aliyekuwa maskini hohehahe katika kijiji kizuri cha Wema. Wanakijiji walikuwa na moyo wa kuisaidia familia ya Moseti kwa kumpatia nyanya yake vibarua. Nyanya yake Moseti alikuwa akirauka kwenda kufanya vibarua vya kulima na kusafisha vibanda. Moseti alikuwa mwepesi wa kumsaidia nyanya yake kufanya kazi za nyumbani.

Kila alipokwenda mtoni kuchota maji, Moseti alikutana na wanyama mbalimbali. Akajifunza namna ya kuwasiliana na wanyama hao. Akawa rafiki wa ngiri mmoja mfupi mnene aliyekuwa na meno marefu. Kutokana na meno yake, Moseti alimwita ngiri huyo Meno.

Moseti aliishi na funza miguuni kutokana na mazingira machafu walimoishi. Miguu yake ilijaa vidonda vilivyomfanya asiweze kutembea vizuri. Meno alimhurumia. Akamuuliza, "Kwa nini huendi hospitali?" Moseti akamjibu, "Nyanya yangu hana pesa za kulipa hospitalini." Meno alisema, "Njoo nikupeleke mahali." Akamwongoza Moseti haraka hadi kwa ngiri mzee aliyekuwa daktari wa wanyama wa msituni. Moseti alipewa dawa ya majani yaliyosagwa akajipaka. Baada ya wiki moja, miguu yake ilikuwa iking'ara. Nyanya yake alifurahi. Akamuuliza, "Moseti, ulitoa wapi dawa ya kuwaangamiza funza?" Moseti alicheka na kumjibu, "Nilipewa dawa na ngiri mzee." Nyanya alishangazwa na tukio hilo. Siku iliyofuata, Moseti na nyanya yake walimtembelea yule ngiri mzee. Walimshukuru kwa kumtibu Moseti. Nyanya yake akaamua kuwa atakuwa akiweka makazi yao safi.

103 Hakiuzwi

Kipindi cha 103 na 104 **Marejeleo**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

vibanda funza daktari

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

akamwongoza nyumbani vidonda kwenda

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Moseti aliishi na nani?
2. Moseti alimsaidia nyanya yake kufanya kazi gani?
3. Ni kwa nini nyanya alishangaa baada ya Moseti kupona?
4. Je, wewe hufanya kazi gani kuwasaidia walezi wako?

**Sarufi: Nafsi, wakati na vielezi**

**Kamilisha sentensi kwa kuchagua jibu sahihi.**

1. Ukiwa na funza miguuni utatembea _____ (polepole, haraka).
2. Mtoto _____ shuleni kesho. (ataenda, alienda)
3. Tunda _____ limeiva vizuri. (wao, lao)
4. Watoto _____ wamepita mtihani. (yao, wao)

**Kuandika**

**Andika insha fupi kuhusu arusi uliyohudhuria.**

Mali ya Serikali ya Kenya 104

## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni: **bendera, kwanza mwingine, nyumbani, akamwongoza.**

Funza sauti - **mw, ny, nd** na **kw.**

Soma maneno **ukurasa wa 104.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Mjadala - Kupanga**

**U:** Panga - Kupanga jinsi ya kuandika insha fupi.

Leo tutajifunza jinsi ya kupanga kuandika insha ya mjadala.

- Chagua mada.
- Utangulizi
- Toa hoja kwa kila upande.
- Toa ushahidi kuhusu hoja zako.
- Tamatisha kwa kutoa uamuzi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. mbayuwayu
2. ilani
3. mtanashati
4. mba

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 105: Marejeleo 3

Kipindi cha 105 **Marejeleo**

**Tathmini ya msamiati**

**Andika sentensi nne ukitumia maneno haya.**

1. mkurupuko
2. kunadi
3. senti
4. keremkeremu

**Tathmini ya Sarufi**


**Tumia kivumishi sahihi kujaza mapengo.**

1. Mkoba wa mama Kaloo ulikuwa _______. (mzuri, nzuri)
2. Kaloo alimwona mbayuwayu _______. (mkubwa, kubwa)
3. Mbayuwayu _______ alipaa angani. (nono, mnono)
4. Mahema yalikuwa _______. (pana, mapana)

**Hadithi ya mwalimu**

**Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.**

Siku ya rangi



105

Hakiuzwi

**Siku ya Rangi**

Siku ya rangi ilikuwa muhimu sana kwa wanyama wote wa porini. Ni siku waliyoisherehekea kila mwisho wa mwaka. Siku hiyo, wanyama walijitokeza kwa wingi kwenye ukingo wa mto Rangirangile ili kuonyesha ujuzi wao wa rangi. Kila familia ya wanyama ilitakiwa kujipamba kwa rangi za aina yake. Familia tatu za wanyama zilichaguliwa kila mwaka kuingia katika shindano la rangi. Mfalme Simba na wasaidizi wake Tembo na Chui ndio waliokuwa wakaguzi na waamuzi wa shindano hili la rangi.

Wanyama walifungua sherehe kwa wimbo mtamu wa rangi za bendera yao. Kasuku ndiye aliyeongoza wimbo huo kwa sauti ya kuvutia. Sokwe naye aliipandisha bendera.

Bendera yetu wanyama yapendeza ×2

Inapepea rangi zaangaza ×2

Kwanza ni nyeupe,

Pili ni nyeusi,

Tatu ni nyekundu, mwisho ni kijani,

Mwisho ni kijani.

Nyeupe amani kwetu twatangaza,

Nyeusi ni ngozi tajiri angaza,

Nyekundu ni damu yetu yachiriza,

Kijani ni mali Afrika mejaza ×2

Mashindano yalipoanza Kipepeo na familia yake waliingia uwanjani kwa maringo. Wakapepeta mbawa zao za rangi aina aina. Vipepeo wengine walijichora maua ya kupendeza na wengine kujipaka rangi zote za upinde wa mvua. Baada ya maonyesho yao, wakaondoka uwanjani huku wanyama wakiwashangilia na kuwapigia makofi.

Tausi waliingia uwanjani kwa madaha punde tu Vipepeo walipotoka. Wakatanua mbawa zao walizozipamba kwa rangi. Wakaimba na kucheza kwa maringo:

Tausi unapendeza, tausi,

Hebu cheza kwa maringo tukuone ×2

Nyeusi cheza nyekundu cheza, kijani cheza nyeupe cheza ×2

Tembea kwa maringo tukuone ×2

Tausi aliwatumbuiza wanyama kwa urembo, densi na nyimbo zake. Ikawa shangwe na nderemo hapo ukingoni mwa mto Rangirangile.

## Kusoma Maneno

Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika: **akawaongoza,nyumbani,vidonda.**

## Hadithi ya Mwalimu

**Kabla ya Kusoma**

**T:** [Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi kisha tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma hadithi, kuna maneno mapya tutakayozungumzia. Neno la kwanza ni **kujipamba**. Neno hili humaanisha kujirembesha (*Rudia hatua hii na maneno:* ***wakaguzi*, *wakapepeta*, *wakatanua***.)]

**Wakati wa Kusoma**

**T:** [Inua mkono wako wa kushoto utakaposikia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia ukisikia neno la pili. (*Soma hadithi kwa ufasaha. Waulize wanafunzi ni kitu gani kitakachotokea*)]

**Baada ya Kusoma**

**Maswali**

1. Taja wahusika wa hadithi? (Mfalme Simba, Tembo, Chui.)
2. Je, ni kwa nini Simba alikuwa akiitwa mfalme? (Alikuwa akiwaongoza wanyama.)
3. Ungekuwa tausi ungejipamba vipi? (Kubali jibu lolote)

## Sarufi: Nafsi, Wakati na Vielezi

Tumia kivumishi sahihi kujaza mapengo katika **ukurasa wa 105** wa vitabu vyenu.

**Majibu**

1. mzuri 2. mkubwa 3. mnono 4. mapana

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora kifaa kimoja wanachotumia wafanyakazi hawa:


1. daktari 2. mkulima 3. bawabu

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha | 106 na 107 | **Shambani 3**

Matini

**Kilimo cha unyunyizaji maji**



Tulipofunga shule muhula uliopita, mimi na kaka yangu tulimtembelea baba mdogo. Baba mdogo ni mkulima hodari. Yeye hulima kwa kunyunyizia mimea maji. Maji haya hutoka kwenye bwawa kubwa. Maji yenyewe yameelekezwa shambani mwake kupitia mitaro aliyoichimba. Mitaro hii hufunguliwa asubuhi na jioni. Mimea hunyunyiziwa maji asubuhi na jioni kwani joto huwa chini nyakati hizi. Hili huliwezesha mimea kutumia maji. Tukiwa kwake alituelekeza na kutuonyesha jinsi ya kupanda na kukuza mboga na matunda. Kwanza tulilifyeka shamba lake kubwa kwa kutumia kifyekeo. Kufyeka huku huwa kazi ngumu iwapo shamba lina kwekwe nyingi. Hivyo basi, baba mdogo hukodisha trekta kutoka kwa majirani na kulilima shamba zima. Wao hulipisha ada kidogo.

Shamba likiwa tayari kwa upanzi, mashimo ya mbegu huchimbwa kwa jembe au kutumia plau. Mbolea ya mifugo huwekwa ndani ya mashimo. Miche hupandwa kisha hunyunyiziwa maji. Maji haya huifanya mimea isinyauke na iwe na afya. Baba mdogo alitueleza, "Ili kuwa na mavuno bora ni sharti uzingatie unyunyizaji wa maji, kutumia mbolea na kupiga dawa."

Mali ya Serikali ya Kenya

106

Kipindi cha | 106 na 107 | **Shambani 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

trekta jembe plau

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

Kwekwe afya bwawa kwenye

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Maji ya kunyunyizia mimea yalitoka wapi?
2. Maji yalielekezwa shambani kwa kutumia nini?
3. Kwekwe na nyasi shambani hukatwa kwa kutumia nini?
4. Unafikiri kilimo cha unyunyizaji maji kina umuhimu gani?

Sarufi: Nyakati

**Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.**

1. Mwanafunzi anapewa zawadi.
2. Mwalimu alisomesha vizuri.
3. Mtoto anapenda tunda.
4. Ali ameenda safari.

107

Hakluzwi

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno haya ya msamiati: **trekta, jembe, plau.**

Soma maneno **ukurasa wa 107.**


## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Matini ya aina hii huzingatia hoja za upande mmoja wa mjadala.

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Ramani Dhana**



Chora ramani dhana

**T:** [Sasa ni wakati wa kujadili tuliyoyasoma katika hadithi. Tulisoma kuhusu **kilimo cha unyunyizaji maji.** Tutatumia ramani dhana itakayotusadia kuelewa hadithi vizuri. Katikati ya ramani hii, tutaandika neno **kilimo.** Je, ni nani anayeweza kutueleza kuhusu makala tuliyosoma kuhusu **kilimo cha unyunyizaji maji.** Nitachora mfano wa mkono hapa na kuandika ndani ya duara. Ni nani mwingine anayeweza kuongezea jambo jingine kuhusu makala tuliyoyasoma? Jambo hilo lina sikikaje? Linakuvutia vipi *(Kwa kila wazo jipya andika kwa kisanduku kipya kupeana. Waelekeze kuunda sentensi baada ya maelezo.)*]

**T:** [Sasa ni wakati wa kutoa sentensi kuhusu kilimo cha unyunyizaji maji.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Maji ya kunyunyizia mimea yalitoka wapi? (kwenye bwawa)
2. Maji yalielekezwa shambani kwa kutumia nini?(mitaro)
3. Kwekwe na nyasi shambani hukatwa kwa kutumia nini? (kifyekeo)
4. Unafikiri kilimo cha unyunyizaji maji kina umuhimu gani?(Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Nyakati

Waeleze wanafunzi sarufi. Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Chora vifaa hivi**

1. jembe 2. kifyekeo 3. shoka


Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 107: Shambani 3

Kipindi cha 106 na 107 **Shambani 3**

Matini

**Kilimo cha unyunyizaji maji**



Tulipofunga shule muhula uliopita, mimi na kaka yangu tulimtembelea baba mdogo. Baba mdogo ni mkulima hodari. Yeye hulima kwa kunyunyizia mimea maji. Maji haya hutoka kwenye bwawa kubwa. Maji yenyewe yameelekezwa shambani mwake kupitia mitaro aliyoichimba. Mitaro hii hufunguliwa asubuhi na jioni. Mimea hunyunyiziwa maji asubuhi na jioni kwani joto huwa chini nyakati hizi. Hili huliwezesha mimea kutumia maji. Tukiwa kwake alituelekeza na kutuonyesha jinsi ya kupanda na kukuza mboga na matunda. Kwanza tulilifyeka shamba lake kubwa kwa kutumia kifyekeo. Kufyeka huku huwa kazi ngumu iwapo shamba lina kwekwe nyingi. Hivyo basi, baba mdogo hukodisha trekta kutoka kwa majirani na kulilima shamba zima. Wao hulipisha ada kidogo.

Shamba likiwa tayari kwa upanzi, mashimo ya mbegu huchimbwa kwa jembe au kutumia plau. Mbolea ya mifugo huwekwa ndani ya mashimo. Miche hupandwa kisha hunyunyiziwa maji. Maji haya huifanya mimea isinyauke na iwe na afya. Baba mdogo alitueleza, "Ili kuwa na mavuno bora ni sharti uzingatie unyunyizaji wa maji, kutumia mbolea na kupiga dawa."

Mali ya Serikali ya Kenya

106

Kipindi cha 106 na 107 **Shambani 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

trekta jembe plau

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

Kwekwe afya bwawa kwenye

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Maji ya kunyunyizia mimea yalitoka wapi?
2. Maji yalielekezwa shambani kwa kutumia nini?
3. Kwekwe na nyasi shambani hukatwa kwa kutumia nini?
4. Unafikiri kilimo cha unyunyizaji maji kina umuhimu gani?

Sarufi: Nyakati

**Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.**

1. Mwanafunzi anapewa zawadi.
2. Mwalimu alisomesha vizuri.
3. Mtoto anapenda tunda.
4. Ali ameenda safari.

107 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno yafuatayo ubaoni:
**kwekwe, afya, bwenyenye, fyata**
Funza sauti: **bw, fy** na **kw**
Soma maneno **ukurasa wa 107.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Nyakati

Andika sentensi zilizo katika **ukurasa wa 107** kwa wakati ujao.

**Majibu**

1. Mwanafunzi atapewa zawadi
2. Mwalimu atasomesha vizuri.
3. Mtoto atapenda tunda.
4. Ali ataenda safari.

## Kuandika

**Mjadala - Nakala ya Kwanza**

**T:** Mwelekeze mwanafunzi jinsi ya kuandika nakala ya kwanza.

- Andika makala kulingana na ilivyopangwa.
- Toa ushahidi.
- Tamatisha.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika maneno haya kwa wingi.**

1. kifyekeo
2. upanga
3. jembe
4. bwawa

**Majibu**

1. vifyekeo
2. panga
3. majembe
4. mabwawa

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 108 na 109 **Shambani 3**

Matini

**Ufugaji wa Kuku**



Bi. Pendo ni mshauri mkuu wa kilimo katika kijiji chetu cha Bwagamoyo. Ameifanya kazi hii ya ushauri kwa miaka mingi. Katika kazi yake, amezingatia sana kilimo cha ufugaji wa kuku. Alipowatembelea wakulima alianza kutoa ushauri wake kwa kusema, "Kuku atakupa mayai na nyama iwapo utamtunza vyema." Aliwahimiza wakulima kuzingatia usafi katika kizimba cha kuku. Wakulima walikumbushwa kuwa lishe bora kwa kuku huleta manufaa tele.

Zaidi ya usafi na lishe bora ni muhimu kuhakikisha kuwa kuku wanapata hewa safi. Nyumba yao iwe na mianya ya kuleta hewa safi. Mwangaza wa kutosha katika nyumba yao huhakikisha kuwa wanakiona chakula chao na kuweza kutembea ndani ya kizimba chao. Ni muhimu kuhakikisha kuwa nyumba yao ina maji safi. Wanapotaga mayai, ni vizuri kuyaondoa na kuyahifadhi kwani kuna kuku ambao huyadona na kuyaharibu mayai yao.

Kuku wa kienyeji huatamia mayai na kuangua vifaranga. Mayai pia huliwa ili kupata afya bora au kuuzwa sokoni kuinua hali ya maisha ya jamii. Ufugaji wa kuku una umuhimu mkubwa katika kuboresha maisha yetu.



Kipindi cha 108 na 109 **Shambani 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kizimba lishe bora huatamia

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

afya kuwekwa kwake bwagamoyo

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Bi. Pendo hufanya kazi gani?
2. Taja aina mbili za kuku wanaofugwa.
3. Nyumba ya kuku huitwaje?
4. Je, ufugaji wa kuku una umuhimu gani?

Sarufi: Viambishi vya wakati ujao

**Pigia mstari kiambishi cha wakati katika sentensi hizi.**

1. Nakitare atapenda kulima.
2. Wakulima wale watapanda kahawa.
3. Matunda haya yatapelekwa sokoni.
4. Mimi nitapanda miti nyumbani.



## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **kizimba, lishe bora, huatamia**

Soma maneno **ukurasa wa 109.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi


Matini ya aina hii huzingatia hoja za upande mmoja wa mjadala.

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Ramani Dhana**

Chora ramani dhana



**T:** [Sasa ni wakati wa kujadili tuliyoyasoma katika hadithi. Tulisoma kuhusu ufugaji wa kuku. Tutatumia ramani dhana itakayotusadia kuelewa hadithi vizuri. Katikati ya ramani hii, tutaandika maneno **ufugaji wa kuku.** Je, ni nani anayeweza kutueleza kuhusu makala tuliyosoma kuhusu **ufugaji wa kuku.**

Nitachora mfano wa mkono hapa na kuandika ndani ya duara. Ni nani mwingine anayeweza kuongeza jambo jingine kuhusu makala tuliyoyasoma? Jambo hilo lina sikikaje? Linakuvutia vipi *(Kwa kila wazo jipya andika kwa kisanduku kipya. Waelekeze wanafunzi kuunda sentensi.)*]

**U:** [Sasa ni wakati wa kutoa sentensi kuhusu ufugaji wa kuku.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

## Sarufi: Nyakati

Tambua mfano wa sentensi kutoka kwa hadithi. Pigia mstari kiambishi cha wakati katika sentensi hizi.

**Majibu**

1. Nakitare a<u>ta</u>penda kulima.
2. Wakulima wale wa<u>ta</u>panda kahawa.
3. Matunda haya ya<u>ta</u>pelekwa sokoni.
4. Mimi ni<u>ta</u>panda miti nyumbani.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi nne sahihi ukitumia **wakati ujao.**
**Mfano:** Mkulima atalima shamba lake.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 109: Shambani 3

Kipindi cha 108 na 109 **Shambani 3**

Matini

**Ufugaji wa Kuku**



Bi. Pendo ni mshauri mkuu wa kilimo katika kijiji chetu cha Bwagamoyo. Ameifanya kazi hii ya ushauri kwa miaka mingi. Katika kazi yake, amezingatia sana kilimo cha ufugaji wa kuku. Alipowatembelea wakulima alianza kutoa ushauri wake kwa kusema, "Kuku atakupa mayai na nyama iwapo utamtunza vyema." Aliwahimiza wakulima kuzingatia usafi katika kizimba cha kuku. Wakulima walikumbushwa kuwa lishe bora kwa kuku huleta manufaa tele.

Zaidi ya usafi na lishe bora ni muhimu kuhakikisha kuwa kuku wanapata hewa safi. Nyumba yao iwe na mianya ya kuleta hewa safi. Mwangaza wa kutosha katika nyumba yao huhakikisha kuwa wanakiona chakula chao na kuweza kutembea ndani ya kizimba chao. Ni muhimu kuhakikisha kuwa nyumba yao ina maji safi. Wanapotaga mayai, ni vizuri kuyaondoa na kuyahifadhi kwani kuna kuku ambao huyadona na kuyaharibu mayai yao.

Kuku wa kienyeji huatamia mayai na kuangua vifaranga. Mayai pia huliwa ili kupata afya bora au kuuzwa sokoni kuinua hali ya maisha ya jamii. Ufugaji wa kuku una umuhimu mkubwa katika kuboresha maisha yetu.

Mali ya Serikali ya Kenya 108

Kipindi cha 108 na 109 **Shambani 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kizimba lishe bora huatamia

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

afya kuwekwa kwake bwagamoyo

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Bi. Pendo hufanya kazi gani?
2. Taja aina mbili za kuku wanaofugwa.
3. Nyumba ya kuku huitwaje?
4. Je, ufugaji wa kuku una umuhimu gani?

Sarufi: Viambishi vya wakati ujao

**Pigia mstari kiambishi cha wakati katika sentensi hizi.**

1. Nakitare atapenda kulima.
2. Wakulima wale watapanda kahawa.
3. Matunda haya yatapelekwa sokoni.
4. Mimi nitapanda miti nyumbani.

109 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **afya, iwekwe, bweni, bwana, bofya, kwetu.**

Funza sauti: **kw, bw, fy.**

Soma maneno **ukurasa wa 109.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

### Mjadala - Nakala ya Kwanza

**T:** Mwelekeze mwanafunzi jinsi ya kuandika nakala ya kwanza.

- Andika nakala kulingana na ilivyopangwa.
- Toa ushahidi.
- Tamatisha.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika insha kuhusu **Shamba Letu.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Kipindi cha 110 Shambani 3

Tathmini ya msamiati

**Tafuta maneno tisa kutoka kwenye jedwali hili na uyaandike kwenye daftari lako.** Kwa mfano: mate

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| m | a | w | e | g | k | r | k | l | s | t |
| f | k | l | m | o | w | m | p | q | r | o |
| b | w | e | n | y | e | n | y | e | y | e |
| w | e | w | e | r | n | a | a | f | y | a |
| a | k | s | n | n | y | a | t | i | a | p |
| w | w | m | a | t | e | n | z | d | y | h |
| a | e | c | s | w | y | a | k | e | a | c |

Tathmini ya sarufi

**Piga mstari kiambishi cha wakati ujao katika sentensi zifuatazo.**

1. Mwanafunzi mwema atapewa zawadi.
2. Je, utaandika kwa hati nadhifu?
3. Swale atafua nguo zake kesho.
4. Wakulima watavuna mahindi wiki ijayo.

Mali ya Serikali ya Kenya 110

## Msamiati

Fungueni **ukurusa wa 110** wa vitabu vyenu. Tafuta maneno tisa kutoka kwenye jedwali na uyaandike kwenye daftari lako. Kwa mfano, mate.


## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiandika.

Maneno: **kwekwe, afya, bwawa, kwenye, fyata, bwenyenye, iwekwe, bweni, bofya, bwana**

## Kuchambua Matini: Mtiririko

**U:** Uchambuzi wa matini kwa kuzingatia wazo kuu kwenye hadithi.




- Chagua matini ambayo ungependa kuchambua.
- Soma matini na mwenzako.

Fuata hatua zifuatazo.

- Ni nini kilifanyika mwanzo?
- Ni nini kilifanyika katikati?
- Ni nini kilifanyika mwisho?

## Sarufi: Nyakati

Fungueni **ukurasa wa 110** wa vitabu vyenu. Pigia mstari kiambishi cha wakati ujao katika sentensi zifuatazo.

**Majibu**

1. Mwanafunzi mwema **ata**pewa zawadi.
2. Je, **uta**andika kwa hati nadhifu?
3. Swale **ata**fua nguo zake kesho.
4. Wakulima **wata**vuna mahindi wiki ijayo.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora vifaa hivi.

1. plau 2. reki 3. sepetu 4. upanga

## Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochanga ujifunzaji.

Mwanafunzi azuru shamba lolote lililo karibu na kwao na kunakili ya mimea ambayo imepandwa pale.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 111 na 112 **Sokoni**

**Matini**

**Uuzaji wa Samaki**

Bihija ni msichana wa miaka minane. Yeye ni msichana mwenye bidii na heshima. Mama yake huuza samaki katika soko la Kisiwani. Bihija anampenda mama yake. Siku za wikendi yeye hufurahia kumsaidia mama yake kuuza samaki ndani ya soko.



Bihija huenda na mama yake kando ya bahari kununua samaki kutoka kwa wavuvi. Baadaye, wao huwatoa utumbo na kuwaosha samaki. Kisha, huwapeleka sokoni, kuwapanga na kuwapiga bei samaki wale. Mama Bihija ana wateja wengi kwa sababu anajua kuwavutia wanunuzi. Samaki wakibakia, Bihija huwakaanga vizuri na kuwauza nje ya soko karibu na kituo cha magari. Ukimla samaki huyo, lo! utapata ni mtamu sana.

Biashara ya kuuza samaki huwa nzuri wakati wa kiangazi kunapokuwa na ukosefu wa mboga. Mama yake Bihija huwapa baadhi ya wateja wake mawaidha ya kumwandaa samaki kama kitoweo.

Biashara ikiwa nzuri, mama yake Bihija hupata faida kubwa. Mama humnunulia Bihija vitabu vya hadithi kumshukuru kwa bidii yake. Siku nyingine, biashara huwa mbaya na wao hupata hasara. Lakini mama yake Bihija hujaribu kulinda biashara ili wasipate hasara mara kwa mara.

111 Hakiuzwi

Kipindi cha 111 na 112 **Sokoni**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kuuza faida hasara

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

kula hasara rinda kulinda

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya.**

1. Mama yake Bihija huuza nini?
2. Bihija ana miaka mingapi?
3. Ni kwa nini watu hupenda kununua samaki kutoka kwa mama Bihija?
4. Je, unafikiri samaki ana faida gani kwa afya yetu?

**Sarufi: Vihusishi**

**Tumia "ndani ya" au "nje ya" kukamilisha sentensi.**

1. Wanafunzi huwa ___________ darasa wakati wa maakuli.
2. Samaki hutumbukizwa ___________ mafuta ili kukaangwa.
3. Meno ya Bihija yamo ___________ mdomo.
4. Mbu huwa ___________ chandarua usiku ninapolala.

Mali ya Serikali ya Kenya 112

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati yafuatayo: **kuuza, faida, hasara.**

Soma maneno **ukurasa wa 112.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Maswali**

1. Mama yake Bihija huuza nini? (Samaki)
2. Bihija ana miaka mingapi? (miaka minane )
3. Ni kwa nini watu hupenda kununua samaki wa mama Bihija? (Anajua kuwavutia wanunuzi.)
4. Je, unafikiri samaki ana faida gani kwa afya yetu? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Vihusishi

Vihusishi ni maneno yanayoonyesha uhusiano uliopo baina ya neno moja na jingine. Mara nyingi vihusishi huonyesha uhusiano kati ya majina na maneno mengine. Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Jibu swali lifuatalo kutokana na hadithi ya Uuzaji wa Samaki.**

Ni nini Bihija na mama yake hufanya mwisho wakati wanapouza samaki?

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 112: Sokoni 3

Kipindi cha 111 na 112 **Sokoni**

Matini

**Uuzaji wa Samaki**

Bihija ni msichana wa miaka minane. Yeye ni msichana mwenye bidii na heshima. Mama yake huuza samaki katika soko la Kisiwani. Bihija anampenda mama yake. Siku za wikendi yeye hufurahia kumsaidia mama yake kuuza samaki ndani ya soko.



Bihija huenda na mama yake kando ya bahari kununua samaki kutoka kwa wavuvi. Baadaye, wao huwatoa utumbo na kuwaosha samaki. Kisha, huwapeleka sokoni, kuwapanga na kuwapiga bei samaki wale. Mama Bihija ana wateja wengi kwa sababu anajua kuwavutia wanunuzi. Samaki wakibakia, Bihija huwakaanga vizuri na kuwauza nje ya soko karibu na kituo cha magari. Ukimla samaki huyo, lo! utapata ni mtamu sana.

Biashara ya kuuza samaki huwa nzuri wakati wa kiangazi kunapokuwa na ukosefu wa mboga. Mama yake Bihija huwapa baadhi ya wateja wake mawaidha ya kumwandaa samaki kama kitoweo.

Biashara ikiwa nzuri, mama yake Bihija hupata faida kubwa. Mama humnunulia Bihija vitabu vya hadithi kumshukuru kwa bidii yake. Siku nyingine, biashara huwa mbaya na wao hupata hasara. Lakini mama yake Bihija hujaribu kulinda biashara ili wasipate hasara mara kwa mara.

111 Hakiuzwi

Kipindi cha 111 na 112 **Sokoni**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kuuza faida hasara

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kula hasara rinda kulinda

Ufahamu

**Jibu maswali haya.**

1. Mama yake Bihija huuza nini?
2. Bihija ana miaka mingapi?
3. Ni kwa nini watu hupenda kununua samaki kutoka kwa mama Bihija?
4. Je, unafikiri samaki ana faida gani kwa afya yetu?

Sarufi: Vihusishi

**Tumia "ndani ya" au "nje ya" kukamilisha sentensi.**

1. Wanafunzi huwa ___________ darasa wakati wa maakuli.
2. Samaki hutumbukizwa ___________ mafuta ili kukaangwa.
3. Meno ya Bihija yamo ___________ mdomo.
4. Mbu huwa ___________ chandarua usiku ninapolala.

Mali ya Serikali ya Kenya 112

## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni: **rinda, linda, kula, kura.**
Funza sauti r na l.
Soma maneno **ukurasa wa 112.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vihusishi

Vihusishi ni maneno yanayoonyesha uhusiano uliopo baina ya neno moja na jingine. Mara nyingi vihusishi huonyesha uhusiano kati ya majina na maneno mengine. Mifano ya vihusishi ni: **nje ya, ndani ya** na kadhalika. Kwa mfano, Khamisi yuko **nje ya** nyumba. Wanafunzi watumie vihusishi kukamilisha sentenzi.

**Majibu**

1. nje ya
2. ndani ya
3. ndani ya
4. nje ya

## Kuandika

**Mjadala - Kuhakiki**

Hakiki makala ya mjadala.
**T:** Mwalimu na wanafunzi wahakiki nakala huku wakizingatia:

- Uakifishaji
- iwapo nakala inaeleweka
- Tahajia.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Tunga sentensi nne ukitumia vihusishi vifuatayo:**

1. ndani ya
2. nje ya

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

# Kipindi cha 113: Sokoni 3

Kipindi cha 113 na 114 **Sokoni**

Matini

**Shughuli Sokoni**



Soko la Mwembeni lililoko kwenye kaunti ya Kwale lina bidhaa nyingi. Kuna sehemu zilizotengwa kulingana na bidhaa zinazouzwa. Kuna vibanda vya kuuzia matunda, nyama, nguo na mboga.

Wafanyibiashara hupanga na kulinda bidhaa hizo kwa uangalifu mkubwa utafikiri ni kuku anayelinda kifaranga wake ndani ya kizimba. Wafanyibiashara hukata leseni na kupewa risiti. Bila leseni, huwezi kunadi au kuuza bidhaa zozote.

Watu wa kila rika huja sokoni kwa sababu mbalimbali. Wengine huja kuuza na kununua bidhaa. Wengine huja kutazama bei za bidhaa. Wengine huja kwa matembezi na kujistarehesha tu. Wengine huja kuona vyakula vipya.

Utawasikia wafanyibiashara nje ya soko wakiuza bidhaa zao na kuwabembeleza wapita njia kwa kusema, "Njoo hukuuu! Weee! Njoo! Bei rahisi! Nunua rinda! Hamsini yako, bahati yako!" Mwingine huitikia, "Hapa! Rahisi kama bure! Linda mali yako! Usidanganywe!" Wengine hupiga mbinja, wakichezacheza na kutumia vichekesho. Yeyote anayevutiwa husongea karibu na kununua bidhaa anazotaka. Wafanyibiashara hupata faida kubwa kwa kuuza bidhaa sokoni. Kama wewe ungeenda katika soko la Mwembeni ungenunua nini?


Hakiuzwi

Kipindi cha 113 na 114 **Sokoni**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kunadi wakiuza kununua

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

leso rangi lilia ruka

Ufahamu

**Jibu maswali haya.**

1. Soko la Mwembeni hupatikana katika kaunti gani?
2. Je, kwa nini ni muhimu kukata leseni kabla ya kuuza bidhaa sokoni?
3. Watu huenda sokoni kufanya nini?
4. Hadithi hii inatufundisha nini?

Sarufi: Vihusishi "Ndani ya" na "nje ya"

**Andika sentensi ulizopewa ukitumia kihusishi 'nje ya'.**

| "ndani ya" | "nje ya" |
|---|---|
| 1. Nyanya ziko ndani ya kibanda. | Nyanya ziko nje ya kibanda. |
| 2. Wafanyabiashara wamefungiwa ndani ya soko. | ____________________. |
| 3. Wanunuzi wanakula ndani ya mkahawa. | ____________________. |
| 4. Nyama ikibaki huwekwa ndani ya jokofu. | ____________________. |



## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati yafuatayo: **kunadi, wakiuza, kununua.** Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.

Soma maneno **ukurasa wa 114.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## ? Ufahamu

**Maswali**

1. Soko la Mwembeni hupatikana katika kaunti gani? (Nyeri)
2. Je, kuna umuhimu gani wa kukata leseni kabla ya kuuza bidhaa sokoni? (Ili waweze kunadi na kuuza bidhaa zozote)
3. Watu huenda sokoni kufanya nini? (Kuuza na kununua bidhaa.)
4. Hadithi hii inatufundisha nini? (Kubali jibu lolote sahihi.)

## Sarufi: Vihusishi

Wanafunzi waandike sentensi wakitumia "nje ya".

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi nne ukutumia vihusishi. **'ndani ya'** na **'nje ya'**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Hakiuzwi

# Kipindi cha 114: Sokoni 3

Kipindi cha 113 na 114 **Sokoni**

Matini

**Shughuli Sokoni**



Soko la Mwembeni lililoko kwenye kaunti ya Kwale lina bidhaa nyingi. Kuna sehemu zilizotengwa kulingana na bidhaa zinazouzwa. Kuna vibanda vya kuuzia matunda, nyama, nguo na mboga.

Wafanyibiashara hupanga na kulinda bidhaa hizo kwa uangalifu mkubwa utafikiri ni kuku anayelinda kifaranga wake ndani ya kizimba. Wafanyibiashara hukata leseni na kupewa risiti. Bila leseni, huwezi kunadi au kuuza bidhaa zozote.

Watu wa kila rika huja sokoni kwa sababu mbalimbali. Wengine huja kuuza na kununua bidhaa. Wengine huja kutazama bei za bidhaa. Wengine huja kwa matembezi na kujistarehesha tu. Wengine huja kuona vyakula vipya.

Utawasikia wafanyibiashara nje ya soko wakiuza bidhaa zao na kuwabembeleza wapita njia kwa kusema, "Njoo hukuuu! Weee! Njoo! Bei rahisi! Nunua rinda! Hamsini yako, bahati yako!" Mwingine huitikia, "Hapa! Rahisi kama bure! Linda mali yako! Usidanganywe!" Wengine hupiga mbinja, wakichezacheza na kutumia vichekesho. Yeyote anayevutiwa husongea karibu na kununua bidhaa anazotaka. Wafanyibiashara hupata faida kubwa kwa kuuza bidhaa sokoni. Kama wewe ungeenda katika soko la Mwembeni ungenunua nini?



Kipindi cha 113 na 114 **Sokoni**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kunadi wakiuza kununua

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

leso rangi lilia ruka

Ufahamu

**Jibu maswali haya.**

1. Soko la Mwembeni hupatikana katika kaunti gani?
2. Je, kwa nini ni muhimu kukata leseni kabla ya kuuza bidhaa sokoni?
3. Watu huenda sokoni kufanya nini?
4. Hadithi hii inatufundisha nini?

Sarufi: Vihusishi "Ndani ya" na "nje ya"

**Andika sentensi ulizopewa ukitumia kihusishi 'nje ya'.**

| "ndani ya" | "nje ya" |
|---|---|
| 1. Nyanya ziko ndani ya kibanda. | Nyanya ziko nje ya kibanda. |
| 2. Wafanyabiashara wamefungiwa ndani ya soko. | ____________________. |
| 3. Wanunuzi wanakula ndani ya mkahawa. | ____________________. |
| 4. Nyama ikibaki huwekwa ndani ya jokofu. | ____________________. |



## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **leseni, rika, leso, lilia, linda, bure.**

Funza sauti r na **l.**

Soma maneno **ukurasa wa 114.**

## Kusoma Matini: Maelezo

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

### Mjadala - Kuhakiki

Hakiki makala ya mjadala.

**T:** Mwalimu na wanafunzi wahakiki nakala huku wakizingatia:

- herufi kubwa,
- iwapo nakala inaeleweka,
- uakifishaji tahajia.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Jaza mapengo kwa jibu sahihi kutoka kwa mabano:**

1. Nilipata ______ baada ya kuuza samaki. (faida, nunua)
2. Nilipata ______ kubwa wakati samaki wangu waliibwa. (hasara, uza)
3. Niliwaona wachuuzi ______ samaki wengi. (faida, wakiuza)
4. Nilienda sokoni ______ samaki. (kununua, hasara)


**Majibu**

1. faida
2. hasara
3. wakiuza
4. kununua

**Wasomee walezi sentensi zifuatazo.**

1. Rono na Robi walikariri shairi mara kwa mara.
2. Leso la Lina na Lona ni laini.
3. Rinda la Linda na Lela lilinunuliwa Lamu.
4. Rika na Luka waliruka karibu na chadarua cha Rita.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Kipindi cha 115 **Sokoni**

Tathmini ya msamiati

**Tazama maneno yaliyomo kwenye gurudumu la maneno. Soma maneno hayo haraka iwezekanavyo huku mwenzako akihesabu kutoka moja hadi kumi.**

rinda
rangi
kulinda
hasara
lilia
kula

Tathmini ya Sarufi

***Jaza mapengo ukitumia "ndani ya" au "nje ya" kwa usahihi.***

1. Aliingia _____________ nyumba kulipoanza kunyesha.
2. Aliketi _____________ nyumba kuota jua.
3. Chura ameingia _____________ mkebe.
4. Mti ulioko _____________ nyumba una nyoka.

Kuandika

**Andika kisa kifupi kuhusu soko ulipendalo.**

115 Hakiuzwi

## Msamiati

[Tazama maneno yaliyomo kwenye gurudumu la maneno. Soma maneno hayo haraka iwezekanavyo huku mwenzako akihesabu kutoka moja hadi kumi.]

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.
Maneno: **chakula, chakura, rika, lika, leseni, leso, lilia, ruka, bure, sura.**

## Kuchambua Matini: Muhtasari

**T:** [Leo tutaandika muhtasari kwa kurejelea makala tuliyoyasoma wiki hii. Ni nani anaweza kutukumbusha makala tuliyoyasoma wiki hii? Chagua mojawapo ya makala haya na uandike muhtasari. Kumbuka muhtasari huzingatia mambo muhimu, haswa mawili au matatu. Huzingatia pia funzo au tamati ya makala.]
**U:** Tumia maswali yafuatayo kama mwongozo.

- Je makala yanahusu nani au nini?
- Mambo gani 2-3 uliyojifunza?
- Umejifunza nini kutoka kwa hadithi?

## Sarufi: Vihusishi

Fungueni **ukurasa wa 115** wa vitabu vyenu. Jaza mapengo ukitumia 'ndani ya' au 'nje ya' kwa usahihi.
Majibu

1. ndani ya
2. nje ya
3. ndani ya
4. nje ya

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Ukifika nyumbani, kumbuka kumuuliza mzazi namna ya kuwasaidia wasiojiweza katika karibu na mnakoishi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 116 na 117 **Uzalendo 3**

Matini

**Richard Leakey**



Richard Leakey alizaliwa mnamo mwaka wa 1944. Yeye ni mzalendo maarufu. Alitetea uhifadhi wa wanyama wa porini. Pia alikuwa mwanasiasa. Aliishi na wazazi wake jijini Nairobi. Alifunzwa umuhimu wa kutunza mazingira na wazazi wake Louis na Mary Leakey. Wakati wa likizo, walizuru mbuga za wanyama. Leakey aliwaona wanyama kama simba, fisi, chui, mbweha, ndovu, loma na nyani. Leakey aliwafurahia wanyama na kuwapiga picha.

Leakey aliteuliwa kuwa mwenyekiti wa kwanza wa Shirika la Huduma kwa Wanyamapori la Kenya (KWS) mnamo mwaka wa 1990. Alihakikisha kuwa wanyamapori wamelindwa. Kikosi chake cha walinzi wa wanyamapori kilikaa chonjo kukabiliana na raia waliokuwa wawindaji haramu. Wawindaji haramu walipungua kutokana na juhudi zake Leakey.

Wawindaji wengi walinusurika kifo katika mapambano na walinzi. Wengine wao walifungwa jela. Katika mwaka wa 1989, Leakey alimwalika Rais mstaafu Daniel Arap Moi katika sherehe za kuteketeza pembe za ndovu. Karibu tani kumi na mbili za pembe haramu ziliteketezwa moto. Leakey alitoka kwenye shirika hili mwaka wa 1994 na kuanza kujishughulisha na siasa na biashara.



Kipindi cha 116 na 117 **Uzalendo 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

mwanasiasa mzalendo raia

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

alipenda ziliambulia alimwalika mwenyekiti

Ufahamu

**Jibu maswali haya.**

1. Richard Leakey alizaliwa lini?
2. Taja wanyama ambao Leakey aliwaona mbugani.
3. Taja wanyama wengine wa porini ambao hawakutajwa katika hadithi.
4. Taja umuhimu wa wanyamapori.

Sarufi: Vimilikishi vya nafsi. Matumizi ya -ake na -ao

**Tumia -ake na -ao kukamilisha vifungu.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Kalamu ________. | Kalamu ________. |
| 2. Mtoto ________. | Watoto ________. |
| 3. Kiatu ________. | Viatu ________. |
| 4. Ndugu ________. | Ndugu ________. |



## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **mwanasiasa, mzalendo, raia.**

Soma maneno **ukurasa wa 116.**

## Kusoma Matini: Wasifu

[Makala haya huwa ya ukweli na hutoa wasifu juu ya mtu mashuhuri au mtu yeyote unayemjua.]

Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Maswali**

1. Richard Leakey alizaliwa lini? (mwaka wa 1944.)
2. Taja wanyama ambao Leakey aliwaona mbugani. (simba, fisi, chui, mbweha, ndovu, loma na nyani)
3. Taja wanyama wengine wa porini ambao hawakutajwa kwenye hadithi. (Kubali jibu lolote sahihi.)
4. Taja umuhimu wa wanyamapori. (Kubali jibu lolote sahihi.)

## Sarufi: Vimilikishi vya nafsi

Waeleze wanafunzi kutambua sarufi. Vimilikishi vya nafsi: Matumizi ya **-ake** na **-ao**. Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Wanafunzi wachague na kuchora picha za wanyama watatu kutoka kwa hadithi waliyoisoma.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 117: Uzalendo 3

Kipindi cha 116 na 117 **Uzalendo 3**

**Matini**

**Richard Leakey**



Richard Leakey alizaliwa mnamo mwaka wa 1944. Yeye ni mzalendo maarufu. Alitetea uhifadhi wa wanyama wa porini. Pia alikuwa mwanasiasa. Aliishi na wazazi wake jijini Nairobi. Alifunzwa umuhimu wa kutunza mazingira na wazazi wake Louis na Mary Leakey. Wakati wa likizo, walizuru mbuga za wanyama. Leakey aliwaona wanyama kama simba, fisi, chui, mbweha, ndovu, loma na nyani. Leakey aliwafurahia wanyama na kuwapiga picha.

Leakey aliteuliwa kuwa mwenyekiti wa kwanza wa Shirika la Huduma kwa Wanyamapori la Kenya (KWS) mnamo mwaka wa 1990. Alihakikisha kuwa wanyamapori wamelindwa. Kikosi chake cha walinzi wa wanyamapori kilikaa chonjo kukabiliana na raia waliokuwa wawindaji haramu. Wawindaji haramu walipungua kutokana na juhudi zake Leakey.

Wawindaji wengi walinusurika kifo katika mapambano na walinzi. Wengine wao walifungwa jela. Katika mwaka wa 1989, Leakey alimwalika Rais mstaafu Daniel Arap Moi katika sherehe za kuteketeza pembe za ndovu. Karibu tani kumi na mbili za pembe haramu ziliteketezwa moto. Leakey alitoka kwenye shirika hili mwaka wa 1994 na kuanza kujishughulisha na siasa na biashara.



Kipindi cha 116 na 117 **Uzalendo 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

mwanasiasa mzalendo raia

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

alipenda ziliambulia alimwalika mwenyekiti

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya.**

1. Richard Leakey alizaliwa lini?
2. Taja wanyama ambao Leakey aliwaona mbugani.
3. Taja wanyama wengine wa porini ambao hawakutajwa katika hadithi.
4. Taja umuhimu wa wanyamapori.

**Sarufi: Vimilikishi vya nafsi. Matumizi ya -ake na -ao**

**Tumia -ake na -ao kukamilisha vifungu.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Kalamu ________. | Kalamu ________. |
| 2. Mtoto ________. | Watoto ________. |
| 3. Kiatu ________. | Viatu ________. |
| 4. Ndugu ________. | Ndugu ________. |



## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni:

**simba, ziliambulia, alimwalika, pembe, mwelekeo**

Funza sauti: **mb nd mw.**

Soma maneno **ukurasa wa 116.**

## Kusoma Matini: Wasifu

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vimilikishi

Tumia –ake na –ao kukamilisha vifungu **ukurasa wa 117.**

**Majibu**

| | |
|---|---|
| 1. Kalamu yake | Kalamu zao |
| 2. Mtoto wake | Watoto wao |
| 3. Kiatu chake | Viatu vyao |
| 4. Ndugu yake | Ndugu zao |

## Kuandika

**Mjadala - Kuhariri**

**T:** Mwalimu na wanafunzi wahariri kifungu walichokiandika wiki iliyopita.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika sentensi zifuatazo kwa wingi.**

1. Kijana wake alifaulu mtihani. Vijana wao walifaulu mitihani)
2. Maziwa yake yalimwagika yote. (Maziwa yao yalimwagika yote)
3. Nyumba yake imepakwa rangi. (Nyumba zao zimepakwa rangi)
4. Kiti chake kimevunjika. (Viti vyao vimevunjika)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 118: Uzalendo 3

Kipindi cha 118 na 119 **Uzalendo 3**

Matini

**Michael Sampson Werikhe**




Michael Sampson Werikhe alizaliwa mwaka wa 1956 jijini Mombasa. Michael aliishi Nairobi wakati wa utoto wake. Alilelewa na mama wa kambo Bi. Sheila Margaret Werikhe. Akiwa na umri wa miaka 11, Michael alikuwa tayari anafuga wanyama kama vile nyoka, kobe na vinyonga nyumbani. Mama yake aliunga mkono juhudi zake. Michael alitia bidii na kukamilisha masomo ya shule ya msingi na ya upili katika shule ya St. George's Giriama.

Baadaye Michael alifanya kazi ya kuhifadhi orodha za wanyama waliokuwa wakiuawa na wawindaji haramu. Alihofia kuwa wanyama hawa wangeangamizwa kabisa. Michael aliamua kuwalinda simba, ndovu, kifaru na hata fisi. Aligundua pia wanyama wengine kama duma na chui walikuwa wanawindwa kwa kupigwa risasi na ngozi yao kuuzwa.

Michael alifanya matembezi ya kampeni ya kuhifadhi wanyama hawa wote. Alitembea kutoka Kampala hadi Dar es Salaam na kumalizia Mombasa. Alichangisha pesa za kusaidia katika uhifadhi wa wanyamapori. Popote alipoenda, alikaribishwa kwa tunu na tamasha na kutangazwa katika vyombo vya habari. Michael Werikhe pia alitembea katika nchi za ng'ambo kama Marekani, Italia, Uswizi na Ujerumani. Aliwahimiza watu kuwahifadhi wanyamapori wote. Werikhe aliamini kwamba wanyama wetu wakihifadhiwa, wawindaji haramu wataambulia patupu. Mnamo tarehe 9/8/1999 Michael aliaga dunia. Kifo chake kilileta huzuni hapa nchini na katika nchi zingine za ng'ambo. Tangu wakati huo, anafahamika Afrika Mashariki na ulimwenguni kote kwa jina la utani, "The Rhino Man", maana yake "Mwenye Kifaru".

Mali ya Serikali ya Kenya 118

Kipindi cha 118 na 119 **Uzalendo 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

mama wa kambo    wanyamapori    ambulia patupu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

aligundua    ulimwenguni    mwindaji    Mombasa

Ufahamu

**Jibu maswali haya.**

1. Michael Sampson Werikhe alizaliwa katika nchi gani?
2. Ni kwa nini Michael Werikhe aliwapenda wanyamapori?
3. Michael Werikhe aliamua kufanya nini alipogundua wanyamapori walikuwa hatarini?
4. Wanyama pori wana umuhimu gani?

Sarufi – Vimilikishi

**Tunga sentensi nne ukitumia:**

1. yetu
2. yao
3. vyako
4. chako

119 Hakiuzwi

## Msamiati

Jadili picha. Funza maneno ya msamiati: **mama wa kambo, wanyama pori, ambulia patupu.**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.

Soma maneno **ukurasa wa 119.**

## Kusoma Matini: Wasifu

Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## ? Ufahamu

**Maswali**

1. Michael Werikhe alizaliwa nchi gani? (Alizaliwa nchini Kenya, jijini Mombasa)
2. Kwa nini Michael Werikhe alipenda wanyamapori? (Alifuga wanyamapori akiwa na umri wa miaka 11)
3. Michael Warikhe aliamua kufanya nini alipogundua wanyamapori walikuwa hatarini? (Aliamua kuwalinda na kuwatunza)
4. Wanyamapori wana umuhimu gani? (Kubali jibu lolote sahihi. Kwa mfano hukuza uchumi wa nchi)

## Sarufi: Vimilikishi

Tunga sentensi ukitumia vimilikishi **yetu, yao, vyako, chako**

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia.

5. yetu
6. yao
7. vyako
8. chako

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 118 na 119 **Uzalendo 3**

Matini

### Michael Sampson Werikhe



Michael Sampson Werikhe alizaliwa mwaka wa 1956 jijini Mombasa. Michael aliishi Nairobi wakati wa utoto wake. Alilelewa na mama wa kambo Bi. Sheila Margaret Werikhe. Akiwa na umri wa miaka 11, Michael alikuwa tayari anafuga wanyama kama vile nyoka, kobe na vinyonga nyumbani. Mama yake aliunga mkono juhudi zake. Michael alitia bidii na kukamilisha masomo ya shule ya msingi na ya upili katika shule ya St. George's Giriama.

Baadaye Michael alifanya kazi ya kuhifadhi orodha za wanyama waliokuwa wakiuawa na wawindaji haramu. Alihofia kuwa wanyama hawa wangeangamizwa kabisa. Michael aliamua kuwalinda simba, ndovu, kifaru na hata fisi. Aligundua pia wanyama wengine kama duma na chui walikuwa wanawindwa kwa kupigwa risasi na ngozi yao kuuzwa.

Michael alifanya matembezi ya kampeni ya kuhifadhi wanyama hawa wote. Alitembea kutoka Kampala hadi Dar es Salaam na kumalizia Mombasa. Alichangisha pesa za kusaidia katika uhifadhi wa wanyamapori. Popote alipoenda, alikaribishwa kwa tunu na tamasha na kutangazwa katika vyombo vya habari. Michael Werikhe pia alitembea katika nchi za ng'ambo kama Marekani, Italia, Uswizi na Ujerumani. Aliwahimiza watu kuwahifadhi wanyamapori wote. Werikhe aliamini kwamba wanyama wetu wakihifadhiwa, wawindaji haramu wataambulia patupu. Mnamo tarehe 9/8/1999 Michael aliaga dunia. Kifo chake kilileta huzuni hapa nchini na katika nchi zingine za ng'ambo. Tangu wakati huo, anafahamika Afrika Mashariki na ulimwenguni kote kwa jina la utani, "The Rhino Man", maana yake "Mwenye Kifaru".

Mali ya Serikali ya Kenya 118

Kipindi cha 118 na 119 **Uzalendo 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

mama wa kambo    wanyamapori    ambulia patupu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

aligundua    ulimwenguni    mwindaji    Mombasa

Ufahamu

**Jibu maswali haya.**

1. Michael Sampson Werikhe alizaliwa katika nchi gani?
2. Ni kwa nini Michael Werikhe aliwapenda wanyamapori?
3. Michael Werikhe aliamua kufanya nini alipogundua wanyamapori walikuwa hatarini?
4. Wanyama pori wana umuhimu gani?

Sarufi - Vimilikishi

**Tunga sentensi nne ukitumia:**

1. yetu
2. yao
3. vyako
4. chako

119 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni: **aligundua, ulimwenguni, mwindaji, Mombasa.**

Funza sauti: **mb, mw, nd.**

Soma maneno **ukurasa wa 119.**

## Kusoma Matini: Wasifu

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Mjadala - Kuhariri**

**T:** Wanafunzi wahariri kifungu walichokiandika wiki iliyopita.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

1. Tumia maneno yafuatayo kutunga sentensi sahihi.
1. kuhifadhi
2. wanyamapori
3. mzalendo
4. raia

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 120 **Uzalendo 3**

Tathmini ya msamiati

**Soma maneno yafuatayo:**

1. angeingia
2. zambarau
3. manjano
4. kujiandaa

Tathmini ya sarufi

**Onyesha vitu vyako na vya wengine mkiwa katika makundi ya watu wawili mkitumia -ake na -ao.**

**Kwa mfano:** Hicho ni kitabu chake. Hivyo ni vitabu vyao.

Hadithi ya mwalimu

**Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.**

Siku ya rangi





Mali ya Serikali ya Kenya 120

**Siku ya Rangi (Sehemu ya pili)**

Mshindani wa tatu ambaye ni Kinyonga, sasa alingojewa kwa hamu kubwa. Wanyama walitarajia kuwa angeingia jukwaani mara tu Tausi walipotoka. Hawakujua kuwa Kinyonga na familia wake walikuwa na tatizo kubwa la rangi. Siku iliyotangulia hii ya mashindano, Kinyonga na familia yake walikuwa wameshindwa kuamua rangi ambazo wangejipaka.

Kwanza walijipaka nyekundu na samawati wakaona wamegeuka zambarau.

Halafu wakajipaka samawati na manjano wakageuka kijani.

Baadaye, walipoona rangi hizo hazifai, wakajipaka manjano na nyekundu wakawa rangi ya chungwa.

Rangi iliyokuwa mwilini mwao ilikuwa ni mchanaganyiko wa rangi. Haikuwapendeza. Kwa hivyo wakaamua kwenda mtoni kuoga. Kinyonga walitembea kwa mwendo wao wa kuhesabu hatua hadi mtoni. Walitumia muda mwingi njiani hadi rangi yote mwilini ikakauka. Walipoingia mtoni kuoga walishangaa sana. Wakioga nyekundu, waligeuka samawati. Wakioga samawati, waligeuka zambarau. Hali hii iliendelea hivyo hadi wakaamua kuenda zao nyumbani. Hawakujua la kufanya siku iliyofuata, ambayo ilikuwa ni siku ya mashindano.

Wanyama wengine hakuelewa yaliyojiri. Walibaki wameduwaa wakiulizana maswali kuhusu Kinyonga na familia yake. Wanyama hawa waliamua kungojea ili Kinyonga apewe muda wa kutosha kujiandaa kwa mashindano haya. Wanyama wengi walisikika wakisoma “Kinyonga na familia yake huwa na mwendo wa pole pole kwa hivyo hatuna budi ila kuwangojea tu.” Mfalme Simba naye akasema, “Hatutaki lawama kutoka kwa Kinyonga na familia yake.”

## Msamiati

Soma maneno kwenye **ukurasa wa 120.**

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **ziliambulia, alimwalika, mwenyekiti, pembe, mwelekeo, simba, aligundua, ulimwenguni, mwandani, pendeza.**

## Kusoma Matini: Hadithi ya Mwalimu

**Kabla ya kusoma**

**T:** [Leo mtasikiliza kwa makini nikiwasomea hadithi kisha baadaye tuzungumzie hadithi hiyo tukiandika. Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi kisha tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma hadithi, kuna baadhi ya maneno mapya ambayo tutayazungumzia kwanza. Neno la kwanza ni **kinyonga**. Neno hili humaanisha mnyama mdogo anayebadilisha rangi mara kwa mara kulingana na mazingira yake. (*Rudia hatua hii na maneno haya:* ***samawati, zambarau, mfalme***.)]

**Wakati wa kusoma**

**T:** [Sasa sikiliza kwa makini ninaposoma. Sikiliza na utambue maneno mapya. Inua mkono wako wa kushoto utakaposikilia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia ukisikia neno la pili. (*Soma hadithi kwa ufasaha huku ukibadilisha sauti kuashiria wahusika tofauti tofauti. Waulize wanafunzi ni kitu gani ambacho kinaweza kutokea.*)]

**Baada ya kusoma**

**T:** [Sasa tuzungumzie hadithi. *(Uliza maswali yafuatayo.)*

Kichwa cha hadithi ni ninin?

Je hadithi inazungumzia nini?

Ni akina nani wako kwenye hadithi?

Hebu tuandike baadhi ya mambo tuliyoyasoma kwenye hadithi.]

## Sarufi: Vimilikishi

Onyesha vitu vyako na vya wengine mkiwa katika vikundi vya wanafunzi wawili mkitumia **–ake** na **–ao.**

Waelekeze wanafunzi kuonyesha vitu mbalimbali.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika insha fupi kumhusu mzalendo unayemjua.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

# Kipindi cha 121: Kazi Mbalimbali 3

Kipindi cha 121 na 122 **Kazi mbalimbali 3**

**Matini**

**Mwalimu Ruth**

Ruth Ajando alizaliwa mwaka wa 1955 kijijini Oga, nchini Usafi. Watoto wengi siku hizo waliugua na hata kufa kutokana na magonjwa yaliyosababishwa na uchafu. Baba yake alimwambia awe akipiga mswaki vizuri kila baada ya kula. Kupiga mswaki husaidia kinywa kisinuke. Kinywa kikinuka, mtu hutorokwa na marafiki. Ni muhimu kununua mswaki mpya kila baada ya miezi mitatu. Mamake alimkumbusha kukata kucha ili kuzuia viini vinavyoleta magonjwa kama vile kipindupindu. Kutokana na ushauri huu, Ruth alitamani kufanya kazi ya ualimu ili awafunze watu kuhusu usafi.



Ruth alifanya vyema shuleni na baadaye akafuzu na kuwa mwalimu. Alifunza shule nyingi nchini Usafi. Alipokea zawadi maridhawa kutoka kwa wakuu wa elimu na Mwalimu Mkuu wa shule yake.

Mwalimu Ruth alisifika kwa kampeni zake dhidi ya uchafu. Aliwaelimisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa kusoma kwa bidii ili kupata kazi kama ya udaktari, ukulima na unesi. Pia aliwafundisha kuhusu usafi wa mwili. Aliwakumbusha kuwa kunawa mikono polepole na kwa sabuni huondoa viini vyote. Magonjwa yanayotokana na uchafu miongoni mwa watoto yalipungua kutokana na bidii yake.

Mnamo tarehe 12/12/1999, Mwalimu Ruth alipata Tuzo ya Heshima kutoka kwa Rais, ya kutambua mchango wake katika elimu. Pia alipata tuzo la Shirika la Afya Ulimwenguni kwa kuimarisha afya huko Oga. Mwalimu Ruth sasa amestaafu lakini anaendelea na kampeni zake za usafi. Yeye husema, "Usafi Kwanza."



Kipindi cha 121 na 122 **Kazi mbalimbali 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

Mwalimu Mkuu ukulima udaktari

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vyema vyote vinavyoleta mpya

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ruth alipokea nini kutoka kwa Mwalimu Mkuu na wakuu wa elimu?
2. Ruth alipata tuzo kutoka kwa Rais tarehe gani?
3. Wewe unatamani kufanya kazi gani utakapokamilisha masomo?
4. Taja kazi zingine ambazo hazijatajwa kwenye hadithi.

**Sarufi: Nyakati**

**Tumia 'li' au 'na' kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo.**

| Wakati uliopita | Wakati uliopo |
|---|---|
| **Mfano**: Mwalimu Ruth alipata tuzo. | Mwalimu Ruth anapata tuzo. |
| **1.** Daktari alienda mjini. | Daktari _____ enda mjini. |
| **2.** Mgojwa a ____ tibiwa hospitalini. | Mgojwa anatibiwa hospitalini. |
| **3.** Mwalimu alifundisha hesabu. | Mwalimu ______ fundisha hesabu. |
| **4.** Mkulima _____panda mbegu. | Mkulima anapanda mbegu. |



## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **mwalimu mkuu, ukuliwa, udaktari**

Soma maneno **ukurasa ya 122.**

## Kusoma Matini: Wasifu

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

### Hoja Kuu

| Nani au nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno kumi)* |
|---|---|---|
| | | |

**N:** [Ninataka tujadili hoja kuu kutokana na hadithi tuliyoisoma. Hoja kuu ni wazo au jambo muhimu linalojitokeza katika makala. Hebu tujibu maswali yatakayo tuongoza kutambua hoja kuu.

Je, ni nani au jambo lipi linalozungumziwa katika makala? Sasa tuandike sentensi kuhusu hoja kuu. *(Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi.)*]

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi**

1. Ni nani mhusika mkuu kwenye hadithi?
2. Ni jambo gani linalozungumziwa zaidi kwenye hadithi?
3. Tunajifunza nini kutokakwa hadithi hii?

**Maswali**

*Mwanafunzi ajibu maswali yafuatayo iwapo kuna muda wa kutosha.*

1. Ruth alipokea nini kutoka kwa Mwalimu Mkuu na wakuu wa elimu? (zawadi maridhawa kutoka kwa Mwalimu Mkuu na wakuu wa elimu.)
2. Ruth alipata tuzo kutoka kwa Rais tarehe gani? (tarehe 12/12/1999)
3. Wewe unatamani kufanya kazi gani unapo kamilisha masomo? (Kubali jibu lolote sahihi)
4. Taja kazi zingine ambazo hazijatajwa kwenye hadithi. (Uwakili, uhandisi na mengineo)

## Sarufi: Nyakati

Nyakati hurejesha wakati ambapo tukio fualni lilifanyika.

Waeleze wanafunzi sarufi. Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Tunga sentensi ukitumia maneno haya.**

1. daktari 2. nesi 3. mwalimu 4. bawabu

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 122: Kazi Mbalimbali 3

Kipindi cha 121 na 122 — Kazi mbalimbali 3

### Matini

**Mwalimu Ruth**

Ruth Ajando alizaliwa mwaka wa 1955 kijijini Oga, nchini Usafi. Watoto wengi siku hizo waliugua na hata kufa kutokana na magonjwa yaliyosababishwa na uchafu. Baba yake alimwambia awe akipiga mswaki vizuri kila baada ya kula. Kupiga mswaki husaidia kinywa kisinuke. Kinywa kikinuka, mtu hutorokwa na marafiki. Ni muhimu kununua mswaki mpya kila baada ya miezi mitatu. Mamake alimkumbusha kukata kucha ili kuzuia viini vinavyoleta magonjwa kama vile kipindupindu. Kutokana na ushauri huu, Ruth alitamani kufanya kazi ya ualimu ili awafunze watu kuhusu usafi.



Ruth alifanya vyema shuleni na baadaye akafuzu na kuwa mwalimu. Alifunza shule nyingi nchini Usafi. Alipokea zawadi maridhawa kutoka kwa wakuu wa elimu na Mwalimu Mkuu wa shule yake.

Mwalimu Ruth alisifika kwa kampeni zake dhidi ya uchafu. Aliwaelimisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa kusoma kwa bidii ili kupata kazi kama ya udaktari, ukulima na unesi. Pia aliwafundisha kuhusu usafi wa mwili. Aliwakumbusha kuwa kunawa mikono polepole na kwa sabuni huondoa viini vyote. Magonjwa yanayotokana na uchafu miongoni mwa watoto yalipungua kutokana na bidii yake.

Mnamo tarehe 12/12/1999, Mwalimu Ruth alipata Tuzo ya Heshima kutoka kwa Rais, ya kutambua mchango wake katika elimu. Pia alipata tuzo la Shirika la Afya Ulimwenguni kwa kuimarisha afya huko Oga. Mwalimu Ruth sasa amestaafu lakini anaendelea na kampeni zake za usafi. Yeye husema, "Usafi Kwanza."

121 Hakiuzwi

Kipindi cha 121 na 122 — Kazi mbalimbali 3

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

Mwalimu Mkuu ukulima udaktari

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

vyema vyote vinavyoleta mpya

### Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ruth alipokea nini kutoka kwa Mwalimu Mkuu na wakuu wa elimu?
2. Ruth alipata tuzo kutoka kwa Rais tarehe gani?
3. Wewe unatamani kufanya kazi gani utakapokamilisha masomo?
4. Taja kazi zingine ambazo hazijatajwa kwenye hadithi.

### Sarufi: Nyakati

**Tumia 'li' au 'na' kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo.**

| Wakati uliopita | Wakati uliopo |
|---|---|
| **Mfano**: Mwalimu Ruth alipata tuzo. | Mwalimu Ruth a**na**pata tuzo. |
| 1. Daktari alienda mjini. | Daktari _____ enda mjini. |
| 2. Mgojwa a ____ tibiwa hospitalini. | Mgojwa anatibiwa hospitalini. |
| 3. Mwalimu alifundisha hesabu. | Mwalimu ______ fundisha hesabu. |
| 4. Mkulima _____panda mbegu. | Mkulima anapanda mbegu. |

Mali ya Serikali ya Kenya 122

## Kusoma Maneno

Andika maneno ubaoni: **vyema, vyote, jipya, kipya**

Funza sauti: **vy** na **py.**

Soma maneno **ukurasa wa 122.**

## Kusoma Matini: Wasifu

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Nyakati

Nyakati hurejelea wakati ambapo tukio fulani lilifanyika.

Kwa mfano: wakati uliopo, wakati uliopita au wakati ujao.

Wakati mwingine nyakati hizi hukanushwa.

Tumia '**-li**' au '**-na**' kujaza mapengo katika **ukurasa wa 122.**

**Majibu**

1. na
2. li
3. na
4. li

## Kuandika

**Mjadala - Kuchapisha**

1. Mwanafunzi wasomeane makala aliyoandika.
2. Kumbusha mwanafunzi kuwa makini anaposomewa makala.
3. Waulize wanafunzi 2-3 kuelezea kuhusu makala waliyosomewa.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Kamilisha sentensi zifuatavyo ukitumia **-li, -ta** au **-na**.

1. Nyanya a _____ enda sokoni jana. (li)
2. Ni ___ soma hadithi kesho. (ta)
3. Mwalimu a _____ andika ubao sasa hivi. (na)
4. Jana ni _____ cheza mchezo wa mpira. (li)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 123: Kazi Mbalimbali 3

Kipindi cha | 123 na 124 | **Kazi mbalimbali 3**

Matini

**Kipawa chake Ali**




Ali Matonya alizaliwa tarehe mosi Januari mwaka wa elfu moja mia kenda tisini. Alitunzwa vyema na wazazi wake. Alikuwa mtoto mtiifu. Wazazi wake Bwana na Bi. Juma Hamisi walimpeleka katika shule ya Msingi ya Maji Mazuri. Ilikuwa shule ya umma kijijini Tongwe kaunti ya Bidii. Matonya alifanya vizuri darasani na hata michezoni, hasa katika mchezo wa kuigiza. Alifundishwa na walimu wake vyema ili kuhakikisha kuwa yeye na wanafunzi wote wanafua dafu.

Ali alikuwa na moyo wa kupenda kuwasaidia wenzake. Alijiunga na kikundi cha wanaskauti ili kupeana huduma ya kwanza kwa wenzake wakati wa michezo. Hili lilimfanya awe na ndoto ya kuwa daktari. Aliizidisha bidii yake darasani na kusoma bila kufa moyo. Alipomaliza masomo ya shule ya msingi, alijiunga na shule ya upili kuendelea na masomo yake.

Katika shule ya upili, alizidi kufuata ndoto yake huku akiwa na moyo wa ukarimu na kuwasaidia wenzake. Nesi wa shule yake alitambua kipawa chake. Alimhusisha sana katika kupeana huduma ya kwanza kwa wanafunzi waliopata majeraha shuleni. Ali alipendwa sana, hata mpishi na bawabu wa shule walitambua juhudi zake. Alifaulu katika mtihani wake wa shule ya upili na kujiunga na chuo kikuu nchini kusomea udaktari.

Baada ya masomo alifuzu na kuwa daktari. Aliajiriwa na serikali na kuenda kufanya kazi ya udaktari. Watu wakatoka mbali hata nje ya nchi kuja kutibiwa na Ali. Akapata tuzo tele kama daktari bora nchini.



Kipindi cha | 123 na 124 | **Kazi mbalimbali 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

bawabu nesi mpishi walimu

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

alihusishwa kuhakikisha akaizidisha alifundishwa

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ali alizaliwa mwaka gani?
2. Je, Ali alijiunga na kikundi gani shuleni?
3. Katika shule ya upili, ni nani alitambua kipawa chake?
4. Ungependa kufanya kazi gani ukiwa mkubwa? Kwa nini?

Sarufi

**Kamilisha vifungu vifuatavyo ukitumia viwakilishi -li, -ta au -na.**

1. A ____ kuwa mtoto mtiifu.
2. Ni ____ soma hadithi kesho.
3. Mwalimu a ____ andika ubaoni sasa hivi.
4. Jana ni ____ cheza mchezo wa mpira.

Kuandika

**Andika mambo unayoyakumbuka kuhusu Ali.**



## Msamiati

Jadili picha. Funza maneno ya msamiati: **bawabu, nesi, walimu, mpishi.** Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.

Soma maneno **ukurasa 124.**

## Kusoma Matini: Wasifu

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Hoja Kuu**

| Nani au nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno kumi)* |
|---|---|---|
| | | |

**N:** [Ninataka tujadili hoja kuu kutokana na hadithi tuliyoisoma. Hoja kuu ni wazo au jambo muhimu linalojitokeza katika makala. Hebu tujibu maswali yatakayo tuongoza kutambua hoja kuu.

Je, ni nani au jambo lipi linalozungumziwa katika makala? Sasa tuandike sentensi kuhusu hoja kuu. *(Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi.)*]

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi**

1. Ni nani mhusika mkuu kwenye hadithi?
2. Ni jambo gani linalozungumziwa zaidi kwenye hadithi?
3. Tunajifunza nini kutokana na hadithi hii?

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Ali alizaliwa mwaka gani?( (mwaka wa elfu mbili na nne)
2. Je, Ali alijiunga na kikundi gani shuleni? (kikundi cha kupeana huduma ya kwanza)
3. Katika shule ya upili nani alitambua kipawa chake? (Mpishi na bawabu)
4. Ungependa kufanya kazi gani? Kwa nini ukiwa mkubwa? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Nyakati.

Waeleze wanafunzi sarufi. Kamilisha vifungu ukitumia viwakilishi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi nne katika wakati uliopita kisha uzibadilishe katika wakati uliopo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 124: Kazi Mbalimbali 3

Kipindi cha 123 na 124 **Kazi mbalimbali 3**

**Matini**

**Kipawa chake Ali**




Ali Matonya alizaliwa tarehe mosi Januari mwaka wa elfu moja mia kenda tisini. Alitunzwa vyema na wazazi wake. Alikuwa mtoto mtiifu. Wazazi wake Bwana na Bi. Juma Hamisi walimpeleka katika shule ya Msingi ya Maji Mazuri. Ilikuwa shule ya umma kijijini Tongwe kaunti ya Bidii. Matonya alifanya vizuri darasani na hata michezoni, hasa katika mchezo wa kuigiza. Alifundishwa na walimu wake vyema ili kuhakikisha kuwa yeye na wanafunzi wote wanafua dafu.

Ali alikuwa na moyo wa kupenda kuwasaidia wenzake. Alijiunga na kikundi cha wanaskauti ili kupeana huduma ya kwanza kwa wenzake wakati wa michezo. Hili lilimfanya awe na ndoto ya kuwa daktari. Aliizidisha bidii yake darasani na kusoma bila kufa moyo. Alipomaliza masomo ya shule ya msingi, alijiunga na shule ya upili kuendelea na masomo yake.

Katika shule ya upili, alizidi kufuata ndoto yake huku akiwa na moyo wa ukarimu na kuwasaidia wenzake. Nesi wa shule yake alitambua kipawa chake. Alimhusisha sana katika kupeana huduma ya kwanza kwa wanafunzi waliopata majeraha shuleni. Ali alipendwa sana, hata mpishi na bawabu wa shule walitambua juhudi zake. Alifaulu katika mtihani wake wa shule ya upili na kujiunga na chuo kikuu nchini kusomea udaktari.

Baada ya masomo alifuzu na kuwa daktari. Aliajiriwa na serikali na kuenda kufanya kazi ya udaktari. Watu wakatoka mbali hata nje ya nchi kuja kutibiwa na Ali. Akapata tuzo tele kama daktari bora nchini.

123 Hakiuzwi

Kipindi cha 123 na 124 **Kazi mbalimbali 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

bawabu nesi mpishi walimu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

alihusishwa kuhakikisha akaizidisha alifundishwa

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ali alizaliwa mwaka gani?
2. Je, Ali alijiunga na kikundi gani shuleni?
3. Katika shule ya upili, ni nani alitambua kipawa chake?
4. Ungependa kufanya kazi gani ukiwa mkubwa? Kwa nini?

**Sarufi**

**Kamilisha vifungu vifuatavyo ukitumia viwakilishi -li, -ta au -na.**

1. A ____ kuwa mtoto mtiifu.
2. Ni ____ soma hadithi kesho.
3. Mwalimu a ____ andika ubaoni sasa hivi.
4. Jana ni ____ cheza mchezo wa mpira.

**Kuandika**

**Andika mambo unayoyakumbuka kuhusu Ali.**

Mali ya Serikali ya Kenya 124

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **alihusishwa, kuhakikisha, , kubishwa, alikalishwa**

Funza sauti: **sh, shw**

Soma maneno **ukurasa wa 124.**

## Kusoma Matini: Wasifu

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Mjadala - Kuchapisha**


1. Mwanafunzi wasomeane makala aliyoandika.
2. Kumbusha mwanafunzi kuwa makini anaposomewa makala.
3. Waulize wanafunzi 2-3 kuelezea kuhusu makala waliyosomewa.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Kanusha sentensi hizi.**

1. Ali alisoma kwa bidii. (Ali hakusoma kwa bidii.)
2. Mpishi atapika chakula. (Mpishi hatapika chakula.)
3. Daktari anamtibu mgonjwa. (Daktari hamtibu mgonjwa.)
4. Bawabu atamshika mwizi. (Bawabu hatamshika mwizi.)

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________



Kipindi cha 125 Kazi mbalimbali 3

Tathmini ya msamiati

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda misamiati uliyosoma wiki hii kuhusu kazi mbalimbali.

| | | | |
|---|---|---|---|
| mu | li | da | pi |
| ku | shi | ne | ba |
| ma | bu | ta | k |
| ri | si | m | wa |

Tathmini ya sarufi

Kanusha vitenzi vifuatavyo.

1. alikula ____________
2. alisoma ____________
3. hutibu ____________
4. alilala ____________

125 Hakiuzwi

## Msamiati

Fungueni **ukurasa wa 125.** Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda misamiati.

**Mfano**

1. nesi
2. mwalimu

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **vyema, vyote, vinavyoleta, mpya, alihusishwa, kuhakikisha, akaizidisha, alifundishwa, upya, kipya**

## Kuchambua Matini: Muhtasari

**U:** [Leo tutaandika muhtasari kwa kurejelea makala tuliyoyasoma wiki hii. Ni nani anaweza kutukumbusha makala tuliyoyasoma wiki hii? Chagua mojawapo ya makala haya na uandike muhtasari. Kumbuka muhtasari huzingatia mambo mawili matatu. Huzingatia pia funzo au tamati ya makala.]

## Sarufi

Fungueni **ukurasa wa 125** wa vitabu vyenu.
Kanusha vitenzi.

**Majibu**

1. hakula
2. hakusoma
3. hatibu
4. hakulala

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Kamilisha neno kwa kufuata mfano.**

**Mfano:** nesi–unesi.

1. daktari – (udaktari)
2. mwalimu –(ualimu)
3. bawabu – (ubawabu)
4. mpishi – (upishi)

## Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji.

Mwanafunzi azuru hospitali au zahanati iliyo karibu naye na kunakili kazi mbalimbali zinazofanywa pale.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 126 na 127 **Usalama 3**

**Matini**

**Inspekta Boru**



Boru alizaliwa katika Kijiji cha Madogo mwaka wa elfu moja mia kenda sitini na nne. Alisomea shule za msingi na upili huko Garissa, na kisha kujiunga na kikosi cha polisi, kitengo cha trafiki.

Mafunzo aliyopata akiwa shuleni yalikuwa na manufaa sana kwa wanakijiji na wananchi. Aliwapa mafunzo askari wenzake na kuwaelekeza vilivyo. Kila wakati alipokuwa akielekeza magari barabarani, madereva walitahadharishwa dhidi ya mwendo wa kasi. Kila mara alisisitiza umuhimu wa kuzingatia alama za barabarani. Aliwahimiza kuwa iwapo alama hizo za barabarani zitapuuzwa bila kuzingatiwa, basi huenda ajali zikatokea na kuleta hasara na majeruhi kwa watu.

Wakati wake wa mapumziko, Boru aliwatembelea wanafunzi na kuwaelimisha kuhusu usalama wa barabarani. Aliwakumbusha umuhimu wa kutazama kulia, kushoto na kulia tena, kabla ya kuvuka barabara bila kukimbia kwa haraka. Mambo mengine aliyowakumbusha wanafunzi ni kuwa ni hatari kucheza wanapoenda shuleni au nyumbani.

Siku ya Jumamosi na Jumapili aliwatembelea washirika wa makanisa na misikiti kuwahimiza umuhimu wa kufunga mishipi walipo safiri. Pia, aliwakumbusha hatari ya kuendesha magari kwa kasi.

Wakati wa kustaafu kwa Boru ulipofika, aliandaliwa sherehe kubwa na nchi yake na kutuzwa. Akatumia wakati wake wa kustaafu kuendeleza juhudi zake za kuwafundisha watu kuhusu usalama barabarani ili kuepuka majanga. Hivi sasa Inspekta Boru anaishi katika kijiji cha Iftin pamoja na familia yake.

Mali ya Serikali ya Kenya 126

Kipindi cha 126 na 127 **Usalama 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

mwendo wa kasi majanga majeruhi

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

kucheleweshwa kuangushwa
walitahadharishwa kuchekeshwa

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Inspekta Boru alisomea kazi gani?
2. Wakati wa mapumziko Inspekta Boru alifanya nini?
3. Jumamosi na Jumapili aliwatembelea akina nani?
4. Je, ni mambo gani ambayo unafaa kuyafanya ili kuwa salama barabarani?

**Sarufi**

**Andika kinyume cha maneno haya.**

1. Mwendo wa kasi __________
2. Funga mishipi __________
3. Zingatia __________
4. Kushoto __________

127 Hakiuzwi

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **mwendo wa kasi, majanga, majeruhi.**

Soma maneno **ukurasa 127.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Matini ya aina hii huzingatia hoja za upande mmoja wa mjadala.

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Kusimulia Hadithi**

**N:** Chora umbo la nyumba.

Kichwa
Wanaozungumziwa
Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?
Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?
Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata? Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]
**N:** Simulia darasa lote hadithi.
**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

Waeleze wanafunzi sarufi. Waelekeze kusoma sentensi kwenye hadithi zilizo na vinyume. Andika sentensi pamoja na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Tunga sentensi ukitumia maneno haya.**

1. mkanda
2. polepole
3. breki
4. majeruhi

Tarehe: ________ Muda: ________ Idadi: ________

# Kipindi cha 127: Usalama 3

Kipindi cha 126 na 127 **Usalama 3**

**Matini**

**Inspekta Boru**



Boru alizaliwa katika Kijiji cha Madogo mwaka wa elfu moja mia kenda sitini na nne. Alisomea shule za msingi na upili huko Garissa, na kisha kujiunga na kikosi cha polisi, kitengo cha trafiki.

Mafunzo aliyopata akiwa shuleni yalikuwa na manufaa sana kwa wanakijiji na wananchi. Aliwapa mafunzo askari wenzake na kuwaelekeza vilivyo. Kila wakati alipokuwa akielekeza magari barabarani, madereva walitahadharishwa dhidi ya mwendo wa kasi. Kila mara alisisitiza umuhimu wa kuzingatia alama za barabarani. Aliwahimiza kuwa iwapo alama hizo za barabarani zitapuuzwa bila kuzingatiwa, basi huenda ajali zikatokea na kuleta hasara na majeruhi kwa watu.

Wakati wake wa mapumziko, Boru aliwatembelea wanafunzi na kuwaelimisha kuhusu usalama wa barabarani. Aliwakumbusha umuhimu wa kutazama kulia, kushoto na kulia tena, kabla ya kuvuka barabara bila kukimbia kwa haraka. Mambo mengine aliyowakumbusha wanafunzi ni kuwa ni hatari kucheza wanapoenda shuleni au nyumbani.

Siku ya Jumamosi na Jumapili aliwatembelea washirika wa makanisa na misikiti kuwahimiza umuhimu wa kufunga mishipi waliposafiri. Pia, aliwakumbusha hatari ya kuendesha magari kwa kasi.

Wakati wa kustaafu kwa Boru ulipofika, aliandaliwa sherehe kubwa na nchi yake na kutuzwa. Akatumia wakati wake wa kustaafu kuendeleza juhudi zake za kuwafundisha watu kuhusu usalama barabarani ili kuepuka majanga. Hivi sasa Inspekta Boru anaishi katika kijiji cha Iftin pamoja na familia yake.

Mali ya Serikali ya Kenya

126

Kipindi cha 126 na 127 **Usalama 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

mwendo wa kasi    majanga    majeruhi

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

kucheleweshwa    kuangushwa
walitahadharishwa    kuchekeshwa

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Inspekta Boru alisomea kazi gani?
2. Wakati wa mapumziko Inspekta Boru alifanya nini?
3. Jumamosi na Jumapili aliwatembelea akina nani?
4. Je, ni mambo gani ambayo unafaa kuyafanya ili kuwa salama barabarani?

**Sarufi**

**Andika kinyume cha maneno haya.**

1. Mwendo wa kasi ____________
2. Funga mishipi ____________
3. Zingatia ____________
4. Kushoto ____________

127

Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **kucheleweshwa, kuangushwa, kurushwa, kuonyeshwa, shwari.**

Funza sauti: **shw**

Soma maneno **ukurasa wa 127.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

Fungueni **ukurasa wa 127** wa vitabu vyenu. Andika vinyume vya maneno hayo.

**Majibu**

1. Mwendo wa pole
2. Fungua mishipi
3. Puuza
4. Kulia

## Kuandika

**Wasifu - Kupanga**

**T:** Panga - Kupanga jinsi ya kuandika insha fupi.

Leo tutajifunza jinsi ya kupanga kuandika insha ya wasifu.

**T:** Chagua mtu yoyote katika familia yako na uandike wasifu wake.

U: Tumia kazi uliyopanga kuandika wasifu.

- Utangulizi.
- Mahali anapotoka mtu huyo.
- Mambo matatu muhimu.
- Umuhimu wake.
- Tamati.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika kinyume cha maneno haya.**

1. amka (lala)
2. jenga (bomoa)
3. osha (chafua)
4. lia (cheka)

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 128: Usalama 3

Kipindi cha 128 na 129 **Usalama 3**

### Matini

**Otari Hodari**



Otari ni mtu hodari anayetajika katika nchi ya Mitambo. Otari alizaliwa mwaka wa elfu moja mia tisa arobaini. Alisomea shule ya Miwani. Otari alikuwa mwepesi katika masomo. Alikuwa mwenye haraka ya kutatua matatizo yaliyowakumba wanafunzi wenzake. Wakati mwingi alifikiri kwa kina sana kabla ya kutenda jambo. Alijua ni vizuri kutahadhari kabla ya hatari.

Otari alitambulika wakati alipowaokoa wanafunzi wa shule ya Miwani waliokuwa wametekwa nyara na majambazi. Wanafunzi hao walikuwa wanatoka shuleni jioni moja. Gari lao lilipopunguza mwendo kuvuka matuta yaliyokuwa barabarani, majambazi walitokea na kulisimamisha. Walimpokonya dereva wa shule gari na kutoroka nalo kwa mwendo wa kasi. Watoto wakaanza kulia na kupiga kelele.

Wanakijiji wakampa Otari habari hii ya kusikitisha. Akatumia kipawa chake cha udadisi. Alibaini mahali watoto hao walikuwa wamefichwa. Aliwasiliana na watekaji nyara, waliodai dhamana ya shilingi milioni mbili. Otari alikubaliana nao na kukutana na watekaji nyara hao kwa ushirikiano na polisi. Walipokutana, aliwapa mkoba uliopangwa karatasi mfano wa pesa na wanafunzi wakakombolewa. Kwa ushirikiano na polisi wa kulinda usalama, majambazi hawa walishikwa na kufungwa jela. Otari alitumia uhodari wake kutegua mtego uliokuwa umetegwa na majambazi. Watoto hawa waliokolewa salama salmini. Usalama ukaimarishwa kote kijijini. Otari akawa ameingia katika vitabu vya kihistoria kwa kuwaokoa wanafunzi. Kwa sababu ya uhodari wake, wanakijiji wakaanza kumwita Otari hodari.

Mali ya Serikali ya Kenya 128

Kipindi cha 128 na 129 **Usalama 3**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

kutahadhari majambazi kulinda usalama

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

jambo mitambo kulinda kutenda

### Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Otari alisomea kat ka shule gani?
2. Wanafunzi walitekwa nyara na nani?
3. Otari alisaidiana na nani kuwaokoa watoto?
4. Ukitekwa nyara na jambazi utafanya nini?

### Sarufi: Kinyume cha vitenzi

**Ambatanisha kitenzi pamoja na kinyume chake.**

| Kitenzi | Kinyume |
|---|---|
| 1. lala | futa |
| 2. panda | lia |
| 3. andika | amka |
| 4. cheka | shuka |

129 Hakiuzwi

## Msamiati

Jadili picha. Funza maneno ya msamiati: **kutahadhari, majambazi, kulinda usalama.**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.

Soma maneno **ukurasa wa 129.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri wao. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Kusimulia Hadithi**

**Ni:** Chora umbo la nyumba.

Kichwa

Wanaozungumziwa

Mahali hadithi inafanyika

Nini kilifanyika mwanzoni mwa hadithi?

Nini kilichotendeka katikati mwa hadithi?

Nini kilifanyika mwishoni mwa hadithi?

**T/U:** [Kichwa cha hadithi ni nini? Hadithi hii inafanyika wapi? Hadithi hii inazungumzia nini sana? Nini kinafanyika mwanzoni mwa hadithi? Ni nini kinafuata?
Ni nini kinafanyika mwishoni mwa hadithi?]

**N:** Simulia darasa lote hadithi.

**U:** [Msimulie mwenzako hadithi.]

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

## Sarufi: Kinyume cha Vitenzi

Waelekeze wanafunzi sarufi. Ambatanisha kitenzi pamoja na kinyume.

**Majibu**

| Kitenzi | Kinyume |
|---|---|
| 1. lala | futa |
| 2. panda | lia |
| 3. andika | amka |
| 4. cheka | shuka |

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora picha inayoonyesha vitenzi hivi.

1. kulala 2. kucheka 3. kuandika 4. kupanda

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 129: Usalama 3

Kipindi cha 128 na 129 **Usalama 3**

## Matini

### Otari Hodari



Otari ni mtu hodari anayetajika katika nchi ya Mitambo. Otari alizaliwa mwaka wa elfu moja mia tisa arobaini. Alisomea shule ya Miwani. Otari alikuwa mwepesi katika masomo. Alikuwa mwenye haraka ya kutatua matatizo yaliyowakumba wanafunzi wenzake. Wakati mwingi alifikiri kwa kina sana kabla ya kutenda jambo. Alijua ni vizuri kutahadhari kabla ya hatari.

Otari alitambulika wakati alipowaokoa wanafunzi wa shule ya Miwani waliokuwa wametekwa nyara na majambazi. Wanafunzi hao walikuwa wanatoka shuleni jioni moja. Gari lao lilipopunguza mwendo kuvuka matuta yaliyokuwa barabarani, majambazi walitokea na kulisimamisha. Walimpokonya dereva wa shule gari na kutoroka nalo kwa mwendo wa kasi. Watoto wakaanza kulia na kupiga kelele.

Wanakijiji wakampa Otari habari hii ya kusikitisha. Akatumia kipawa chake cha udadisi. Alibaini mahali watoto hao walikuwa wamefichwa. Aliwasiliana na watekaji nyara, waliodai dhamana ya shilingi milioni mbili. Otari alikubaliana nao na kukutana na watekaji nyara hao kwa ushirikiano na polisi. Walipokutana, aliwapa mkoba uliopangwa karatasi mfano wa pesa na wanafunzi wakakombolewa. Kwa ushirikiano na polisi wa kulinda usalama, majambazi hawa walishikwa na kufungwa jela. Otari alitumia uhodari wake kutegua mtego uliokuwa umetegwa na majambazi. Watoto hawa waliokolewa salama salmini. Usalama ukaimarishwa kote kijijini. Otari akawa ameingia katika vitabu vya kihistoria kwa kuwaokoa wanafunzi. Kwa sababu ya uhodari wake, wanakijiji wakaanza kumwita Otari hodari.

Mali ya Serikali ya Kenya



Kipindi cha 128 na 129 **Usalama 3**

## Msamiati

**Soma maneno haya.**

kutahadhari majambazi kulinda usalama

## Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

jambo mitambo kulinda kutenda

## Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Otari alisomea kat ka shule gani?
2. Wanafunzi walitekwa nyara na nani?
3. Otari alisaidiana na nani kuwaokoa watoto?
4. Ukitekwa nyara na jambazi utafanya nini?

## Sarufi: Kinyume cha vitenzi

**Ambatanisha kitenzi pamoja na kinyume chake.**

| Kitenzi | Kinyume |
|---|---|
| 1. lala | futa |
| 2. panda | lia |
| 3. andika | amka |
| 4. cheka | shuka |



## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **jambo, mitambo, wimbo, ndimi.**

Funza sauti: **mb nd**

Soma maneno **ukurasa wa 129**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Wasifu - Kupanga**

**T:** Panga - Kupanga jinsi ya kuandika insha fupi.

Leo tutajifunza jinsi ya kupanga kuandika insha ya wasifu.

**U:** Tumia kazi uliyopanga kuandika wasifu.

- Utangulizi
- Mahali anapotoka mtu huyo.
- Mambo matatu muhimu.
- Umuhimu wake.
- Tamati.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa


**Andika vinyume vya vitenzi hivi.**

1. andika (futa)
2. lala (amka)
3. panda (shuka)
4. ongeza (punguza)

## Kazi ya Nyongeza

Andika sentensi nne kuhusu mtu yeyote maarufu huko kwenu.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________


Kipindi cha 130 **Usalama 3**

Tathmini ya msamiati

**Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia maneno haya: (breki, polisi, jeraha, mkanda)**

1. Wanaolinda usalama ni ____________.
2. Mtu akianguka hupata ____________.
3. Unapoingia garini ni sharti ujifunge ____________.
4. Dereva husimamisha gari kwa kutumia ____________.

Tathmini ya Sarufi

**Andika kinyume cha maneno haya.**

1. amka ________________
2. jenga ________________
3. osha ________________
4. lia ________________

Mali ya Serikali ya Kenya 130

## Msamiati

Fungua **ukurasa wa 130**. Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia maneno kwenye mabano.

**Majibu**

1. polisi
2. jeraha
3. mkanda
4. breki

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **machweo, mchwa, chwago, wanapofichwa, kichwa, kucheleweshwa, walitahadharishwa, kuchekeshwa, kuangushwa**

## Kuchambua Matini: Kusimulia Hadithi

Soma mojawapo ya matini tuliyosoma wiki hii na ujibu maswali yafuatayo.

1. Hadithi inazungumzia nini?
2. Ni jambo lipi lililokufurahisha?
3. Je, unaweza kusema nini kuhusu kichwa cha hadithi?

## Sarufi

Andika kinyume cha maneno kwenye **ukurasa wa 130**

**Majibu**

1. lala
2. bomoa
3. chafua
4. cheka

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora alama nne (4) za barabarani unazozijua.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 131: Usafi wa Mazingira 3

Kipindi cha 131 na 132 **Usafi wa Mazingira 3**

Matini

**Miti ni Uhai**

Umuhimu wa kuhifadhi mazingira umesisitizwa nchini na ulimwenguni. Nyumbani na shuleni tunahimizwa umuhimu wa kupanda na kulinda miti. Wanamazingira kama vile hayati Profesa Wangari Maathai, wametuzwa kwa juhudi zao za kuhifadhi mazingira.

Miti ina manufaa mengi katika maisha yetu. Miti huyafanya mazingira yetu kupendeza. Miti hutupa kivuli na husafisha hewa tunayotegemea. Vilevile, miti huzuia upepo mkali kuharibu paa za nyumba zetu. Ama kwa kweli, miti ni uhai.



Matunda matamu na yenye rangi za kuvutia hutoka kwenye miti. Matunda haya yanaboresha afya yetu. Miti huboresha uchumi wa nchi kwa kuleta pesa zinazotokana na mauzo yake. Mbao huuzwa na kuleta mapato. Mbao pia hutumika kutengeneza vyombo mbalimbali kama vile meza, madawati na stuli. Kilimo cha miti kimepata umaarufu mkubwa.

Ili kupata manufaa ya miti, ni muhimu kuiacha imee polepole hadi itakapokomaa. Tukiikata haraka kabla ya kukomaa faida itakuwa chini. Unafaa kufyeka nyasi zilizo kando ya miti na kutupa taka katika jaa. Ni muhimu kupanda miti miwili unapokata mti mmoja. Jambo hili litahakikisha kuwepo kwa miti kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

131 Hakiuzwi

Kipindi cha 131 na 132 **Usafi wa Mazingira 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

kuhifadhi mazingira    kufyeka nyasi    kuchoma taka

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kuhifadhi    fedha    thamani    usithubutu

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Wangari Maathai alituzwa kwa kufanya nini?
2. Ni kwa nini miti ni uhai?
3. Tunafaa kufanya nini tunapokata mti mmoja?
4. Eleza njia nyingine za kuhifadhi mazingira.

Sarufi: Matumizi ya vilezi polepole na haraka

**Tunga sentensi ukitumia vielezi 'polepole' na 'haraka'.**

**Mfano:** Mtoto akitumwa huenda dukani haraka.

1. polepole
2. haraka
3. polepole
4. haraka

Mali ya Serikali ya Kenya    132

## Msamiati

Jadili picha.

Funza ya msamiati ufuatao: **kuhifadhi mazingira, kufyeka nyasi, kutupa taka.**

Soma maneno **ukurasa wa 132.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala na Ushawishi

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha ua uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Hoja Kuu**

| Nani au nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno kumi)* |
|---|---|---|
| | | |

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi**

1. Ni nani mhusika mkuu kwenye hadithi hii?
2. Ni jambo lipi linalozungumziwa zaidi kwenye hadithi?
3. Hadithi hii inatufundisha nini?

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

Jibu maswali yafuatayo kulingana na hadithi.

1. Wangari Maathai alituzwa kwa kufanya nini? (juhudi zake za kuhifadhi mazingira)
2. Kwa nini miti ni uhai? (hutupatia matunda, hewa safi ya kupumua)
3. Tunafaa kufanya nini tunapokata mti mmoja? (kupanda miti miwili.)
4. Eleza njia zingine za kuhifadhi mazingira. (Kubali jibu lolote sahihi.

## Sarufi: Vielezi

Waeleze wanafunzi sarufi. Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Andika sentensi zifuatazo kisha umsomee mlezi wako.**

1. Usafi wa mazingira ni muhimu kwa afya yetu.
2. Kukata nyasi hupunguza wadudu kama mbu.
3. Tuimarishe usafi nyumbani ili kuepuka kipindupindu.
4. Ni muhimu kuosha mikono unapotoka chooni.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 132: Usafi wa Mazingira 3

Kipindi cha | 131 na 132 | **Usafi wa Mazingira 3**

**Matini**

**Miti ni Uhai**

Umuhimu wa kuhifadhi mazingira umesisitizwa nchini na ulimwenguni. Nyumbani na shuleni tunahimizwa umuhimu wa kupanda na kulinda miti. Wanamazingira kama vile hayati Profesa Wangari Maathai, wametuzwa kwa juhudi zao za kuhifadhi mazingira.

Miti ina manufaa mengi katika maisha yetu. Miti huyafanya mazingira yetu kupendeza. Miti hutupa kivuli na husafisha hewa tunayotegemea. Vilevile, miti huzuia upepo mkali kuharibu paa za nyumba zetu. Ama kwa kweli, miti ni uhai.



Matunda matamu na yenye rangi za kuvutia hutoka kwenye miti. Matunda haya yanaboresha afya yetu. Miti huboresha uchumi wa nchi kwa kuleta pesa zinazotokana na mauzo yake. Mbao huuzwa na kuleta mapato. Mbao pia hutumika kutengeneza vyombo mbalimbali kama vile meza, madawati na stuli. Kilimo cha miti kimepata umaarufu mkubwa.

Ili kupata manufaa ya miti, ni muhimu kuiacha imee polepole hadi itakapokomaa. Tukiikata haraka kabla ya kukomaa faida itakuwa chini. Unafaa kufyeka nyasi zilizo kando ya miti na kutupa taka katika jaa. Ni muhimu kupanda miti miwili unapokata mti mmoja. Jambo hili litahakikisha kuwepo kwa miti kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

131 Hakiuzwi

Kipindi cha | 131 na 132 | **Usafi wa Mazingira 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

kuhifadhi mazingira    kufyeka nyasi    kuchoma taka

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

kuhifadhi    fedha    thamani    usithubutu

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Wangari Maathai alituzwa kwa kufanya nini?
2. Ni kwa nini miti ni uhai?
3. Tunafaa kufanya nini tunapokata mti mmoja?
4. Eleza njia nyingine za kuhifadhi mazingira.

**Sarufi: Matumizi ya vilezi polepole na haraka**

**Tunga sentensi ukitumia vielezi 'polepole' na 'haraka'.**

**Mfano:** Mtoto akitumwa huenda dukani haraka.

1. polepole
2. haraka
3. polepole
4. haraka

Mali ya Serikali ya Kenya 132

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **kuhifadhi, kadhalika, thamani, dhambi, theluji.**

Funza sauti: **dh, th**

Soma maneno **ukurasa wa 132.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Ufahamu

### Hoja kuu

| Nani au nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno kumi)* |
|---|---|---|
| | | |

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi**

1. Mhusika mkuu kwenye hadithi hii ni nani?
2. Ni jambo lipi linalozungumziwa zaidi kwenye hadithi?
3. Hadithi hii inatufundisha nini?

## Sarufi: Vielezi

Fungueni **ukurasa wa 132** wa vitabu vyenu.

Tunga sentensi ukitumia vielezi "**polepole**" na "**haraka**".

## Kuandika

### Wasifu - Nakala ya Kwanza

**T:** Nakili insha ya mjadala.

- Mwelekeze mwanafunzi jinsi ya kuandika nakala ya kwanza.
- Andika makala kulingana na ilivyopangwa.
- Toa ushahidi.
- Tamatisha.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Muelezee mlezi wako umuhimu wa usafi wa mazingira.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 133 na 134 **Usafi wa Mazingira 3**

Matini

**Athari za Mazingira Machafu**

Watu wanapaswa kupumua hewa safi kila mara. Miti husaidia kusafisha hewa. Takataka kama plastiki zikichomwa hutoa moshi wenye gesi ya sumu inayochafua hewa. Hewa hiyo chafu huleta madhara kama vile shida ya kupumua, kuumwa na kifua na saratani au kansa ya ngozi. Takataka za plastiki hazipaswi kuchomwa. Wafanyabiashara sokoni hupenda kutupa takataka ovyoovyo. Tabia hii husababisha madhara mengi. Takataka zinapooza hutoa harufu mbaya inayochafua mazingira. Tena, wanyama kama panya na wadudu wadogo wanaoleta maradhi mbalimbali hujificha humo ndani. Ni muhimu kudumisha usafi kwa kutupa takataka kwenye pipa au jaa haraka iwezekanavyo.



Ni vyema kuishi katika mazingira safi ili kuepuka maradhi. Nyasi ndefu uwanjani zinafaa zikatwe. Wadudu wanaoleta magonjwa mbalimbali huishi pia ndani ya maji chafu. Ni muhimu maji yaliyotuama yanyunyiziwe dawa ili kuuwa wadudu hawa.

Wizara ya afya huwahimiza watu wote kutilia maanani usafi wa mazingira. Kulinda mazingira ni wajibu wa kila mmoja wetu. Tukiwa shuleni na hata nyumbani tuhakikishe kwamba mazingira yetu ni safi. Tunapocheza kule uwanjani tuokote takataka zilizotapakaa na kuzitupa katika pipa la taka. Vilevile, tuwahimize marafiki zetu kulinda mazingira.

133 Hakiuzwi

Kipindi cha 133 na 134 **Usafi wa Mazingira 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

madhara kudumisha usafi maradhi

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

athari madhara thieta maradhi

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kuchoma takataka za plastiki kuna madhara gani?
2. Kutupa takataka ovyoovyo kunasababisha nini?
3. Taja njia za kudumisha mazingira safi?
4. Taja magonjwa mengine yanayoletwa na mazingira machafu?

Sarufi: Vielezi

**Andika sentensi nne ukitumia vielezi “polepole” na “haraka”.**

1. ______________________.
2. ______________________.
3. ______________________.
4. ______________________.

Kuandika

**Andika kisa kifupi kuhusu madhara ya uchafuzi wa mazingira.**

Mali ya Serikali ya Kenya 134

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno yafuatayo ya msamiati: **madhara, kudumisha usafi, maradhi.**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Hoja Kuu**

| Nani au nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno kumi)* |
|---|---|---|
| | | |

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi**

1. Mhusika mkuu kwenye hadithi hii ni nani?
2. Ni jambo lipi linalozungumziwa zaidi kwenye hadithi?
3. Hadithi hii inatufundisha nini?

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Kuchoma takataka za plastiki kuna madhara gani? (Hewa inayotokana na kuchomwa kwa takataka za plastiki huleta shida ya kupumua, na kuumwa na kifua.)
2. Kutupa taka ovyoovyo kunasababisha nini?
   (Harufu mbaya zinapooza, kuchafua mazingira, kuleta wanyama kama panya na vidudu vidogo vinavyoleta maradhi. )
3. Taja njia za kudumisha mazingira safi? (Kunyunyiza dawa katika maji yaliyotulia, kukata nyasi ndefu, Kuokota takataka, kutupa taka katika pipa.)
4. Taja magonjwa yanayoletwa na mazingira machafu? (Kubali jibu lolote sahihi kwa mfano malaria, kipindupindu na kadhalika.)

## Sarufi: Vielezi

Waelekeze wanafunzi kuandika sentensi wakitumia ''pole pole' na 'haraka'.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Panga maneno haya ili kuunda sentensi sahihi.**

1. darasani mzuri ulileta mchoro.
2. sana yanavutia maua.
3. haya yanapendeza mazingira sana.
4. shuleni mzuri alitutembelea mwalimu.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 133 na 134 **Usafi wa Mazingira 3**

Matini

**Athari za Mazingira Machafu**

Watu wanapaswa kupumua hewa safi kila mara. Miti husaidia kusafisha hewa. Takataka kama plastiki zikichomwa hutoa moshi wenye gesi ya sumu inayochafua hewa. Hewa hiyo chafu huleta madhara kama vile shida ya kupumua, kuumwa na kifua na saratani au kansa ya ngozi. Takataka za plastiki hazipaswi kuchomwa. Wafanyabiashara sokoni hupenda kutupa takataka ovyoovyo. Tabia hii husababisha madhara mengi. Takataka zinapooza hutoa harufu mbaya inayochafua mazingira. Tena, wanyama kama panya na wadudu wadogo wanaoleta maradhi mbalimbali hujificha humo ndani. Ni muhimu kudumisha usafi kwa kutupa takataka kwenye pipa au jaa haraka iwezekanavyo.

Ni vyema kuishi katika mazingira safi ili kuepuka maradhi. Nyasi ndefu uwanjani zinafaa zikatwe. Wadudu wanaoleta magonjwa mbalimbali huishi pia ndani ya maji chafu. Ni muhimu maji yaliyotuama yanyunyiziwe dawa ili kuuwa wadudu hawa.



Wizara ya afya huwahimiza watu wote kutilia maanani usafi wa mazingira. Kulinda mazingira ni wajibu wa kila mmoja wetu. Tukiwa shuleni na hata nyumbani tuhakikishe kwamba mazingira yetu ni safi. Tunapocheza kule uwanjani tuokote takataka zilizotapakaa na kuzitupa katika pipa la taka. Vilevile, tuwahimize marafiki zetu kulinda mazingira.

133 Hakiuzwi

Kipindi cha 133 na 134 **Usafi wa Mazingira 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

madhara kudumisha usafi maradhi

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

athari madhara thieta maradhi

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kuchoma takataka za plastiki kuna madhara gani?
2. Kutupa takataka ovyoovyo kunasababisha nini?
3. Taja njia za kudumisha mazingira safi?
4. Taja magonjwa mengine yanayoletwa na mazingira machafu?

Sarufi: Vielezi

**Andika sentensi nne ukitumia vielezi "polepole" na "haraka".**

1. ______________________.
2. ______________________.
3. ______________________.
4. ______________________.

Kuandika

**Andika kisa kifupi kuhusu madhara ya uchafuzi wa mazingira.**

Mali ya Serikali ya Kenya 134

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **kadhalika, thamani, usithubutu, dhahabu, nadharia.**

Funza sauti: **dh** na **th**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Wasifu - Nakala ya Kwanza**

**U:** Nakili insha ya mjadala.

- Mwelekeze mwanafunzi jinsi ya kuandika nakala ya kwanza.
- Andika makala kulingana na ilivyopangwa.
- Toa ushahidi.
- Tamatisha.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Tumia kielelezi kutoka kwenye mabano kujaza mapengo.**

1. Msichana _____alifyeka nyasi. (nzuri, mzuri)
2. Mtoto mdogo_____ alienda shuleni.(sana, vizuri)
3. Alitembea kwa ____ili afike shuleni mapema. (haraka, polepole)
4. Wanafunzi walikata nyasi _____wakachelewa kwenda darasani. (haraka, polepole)

**Majibu**

1. mzuri
2. sana
3. haraka
4. polepole

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Kipindi cha 135 Usafi wa Mazingira 3

Tathmini ya msamiati

**Jaza mapengo kwa kutumia neno sahihi kutoka kwenye mabano.**

1. Mwalimu alitufunza jinsi ya ________ mazingira. (kuhifadhi, kudhuru)
2. Mazingira safi huzuia _______ kwa magonjwa. (maradhi, kusambaa)
3. __________ ni jina lingine la ugonjwa. (Maradhi, Mazingira)
4. Kutupa taka ovyo husababisha ________ mengi kwa mazingira. (kuhifadhi, madhara)

Tathmini ya sarufi

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia vielezi 'polepole' au 'haraka'.**

1. Msichana mvivu alifyeka nyasi ___________.
2. Ukikata mti unafaa upande miti mingine ___________.
3. Alitembea kwa _________ ili afike shuleni mapema.
4. Wanafunzi waliokota takataka __________ hadi wakachelewa kufika darasani.

Hadithi ya mwalimu

**Tazama picha. Msikilize mwalimu anaposoma hadithi.**

Siku ya rangi

135 Hakiuzwi

**Siku ya Rangi (Sehemu ya tatu)**

Kinyonga na familia yake walifika jukwaani wakiwa wamechelewa. Wanyama walikuwa wamechoka kuwangojea. Kinyonga walitaka kuomba msamaha kwa ajili ya kuchelewa lakini hawakupata nafasi. Walitaka pia kuelezea tatizo lao la rangi, ili wasiingie kwenye shindano la rangi lakini hawakusikilizwa. Kinyonga alijaribu kusema kwa kusitasita.

"Tafa...dha...li nao...mba"

Wanyama walishangilia na kupiga makofi.

"Ingieni uwanjani Kinyonga" alitangaza Tembo, huku Chui naye pia akiwahimiza.

"Fanyeni hima" alinguruma Simba.

Kinyonga waliingia jukwaani wakiwa wameinamisha vichwa kwa woga. Uwoga huu uliwafanya watembee kwa mwendo wa polepole. Wanyama wengine walifurahia mwendo huu wakidhani ni wa madaha na mbwembwe. Wapokanyaga majani ya miti waligeuka rangi ya kijani. Wapotembea juu ya maua mekundu waligeuka wekundu. Hali hii ya kujigeuza rangi iliendelea hadi mwisho wa mashindano.

Wanyama walistaajabishwa sana na uvumbuzi huu wa Kinyonga. Waliwashangilia zaidi na kuwaimbia shairi la sifa:

Kinyonga rangi wajulia,
Za majani na za maua,
Kipepeo hajafikia,
Na Tausi wa kutanua.

Kinyonga hakuamini aliyoyaona na kuyasikia. Aliposikia vigelegele vya kumshangilia vimezidi, alianza kujiamini zaidi. Kinyonga alianza kukodolea wanyama wengine macho yake ya gololi. Hii ilifanya wanyama wengi kutoamini waliyokuwa wakiyaona. Siku hiyo kinyonga akatangazwa mshindi na kuvishwa taji la mjuzi wa rangi.

## Msamiati

[Fungueni **ukurasa wa 135**. Jaza mapengo kwa kutumia neno sahihi kutoka kwenye mabano.]

**Majibu**

1. kuhifadhi 2. kusambaa 3. maradhi 4. madhara

## Kusoma Maneno

Soma kila neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiandika.

Maneno: **athari, madhara, maradhi, dhambi, theluji, kadhalika, thamani, usithubutu, kuhifadhi.**

## Kusoma Matini: Hadithi ya Mwalimu

**Kabla ya kusoma**

**T:** [Tutaanza kwa kusoma kichwa cha hadithi kisha tujadili picha. Je, mnaona nini kwenye picha? Mnafikiria hadithi hii inahusu nini? Mwambie mwenzako kitakachotokea kwenye hadithi. Kabla ya kusoma hadithi, kuna baadhi ya maneno mapya ambayo tutazungumzia kwanza. Neno la kwanza ni **kusitasita**. Neno hili humaanisha kufanya jambo kwa wasiwasi. (*Rudia hatua hii na maneno haya:* ***fanyeni hima, madaha, uvumbuzi***.)]

**Wakati wa kusoma**

**T:** [Sikiliza na utambue maneno mapya. Inua mkono wako wa kushoto utakaposikia neno la kwanza. Inua mkono wako wa kulia ukisikia neno la pili. (*Soma hadithi kwa ufasaha*)]

**Baada ya kusoma**

**T:** [Sasa tuizungumzie hadithi. *(Uliza maswali yafuatayo.)*

1. Taja wahusika katika hadithi hii. (Kinyonga Simba, Tembe na chui)
2. Kwa nini kinyonga walitaka kuomba msamaha. (Kwa sababu walikuwa wamechelewa.)
3. Je hadithi hii inatufundisha nini? (Kubali jibu lolote)]

## Sarufi: Vielezi

Fungua **ukurasa wa 135**. Tumia kielezi sahihi kukamilisha sentensi hizo.

**Majibu**

1. polepole 2. haraka 3. haraka 4. polepole

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Eleza mlezi ulichojifunza kutokana na hadithi ya mwalimu.

## Kazi ya Nyongeza

Wanafunzi waigize matukio katika hadithi ya mwalimu.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 136: Kazi Mbalimbali 4

Kipindi cha 136 na 137 **Kazi mbalimbali 4**

**Matini**

**Bawabu na Yaya**

Kazi ni shughuli zozote ambazo mtu hufanya ili kujipatia riziki yake. Kuna kazi mbalimbali kama vile ubawabu na uyaya.

Kazi kuu ya bawabu ni kulinda lango au jengo fulani. Baadhi ya majengo ambayo bawabu hulinda ni ya kibiashara au makazi ya watu. Wakati mwingine, bawabu hulinda sehemu fulani ya shamba, mali au vyombo vilivyotengwa mahali. Kazi ya ubawabu hufanywa usiku na mchana. Bawabu hulinda mali isiibwe au isiharibiwe. Vilevile, yeye hufungua lango na kuwaelekeza wageni wanaotembelea wakazi. Iwapo kuna uvamizi, itambidi apige firimbi au kuripoti uvamizi huo kwa polisi mara moja. Bawabu hafai kuwaruhusu wageni waingie katika jengo bila kuwakagua.



Kazi ya yaya nayo ni kulea watoto, kuhakikisha kuwa wamekula kuoga. Asipowaogesha wataugua. Vilevile, yaya huosha nyumba. Yeye hufua nguo, huzipiga pasi na kuzikunja.

Watu wengi hupendelea kazi ya ubawabu kwa sababu husaidia katika kudumisha usalama. Wanaopendelea kazi ya uyaya husema kuwa kazi hii ina jukumu la kuwalinda na kuwatunza watoto. Hata hivyo, kazi hizi zote ni muhimu kwani zote huchangia katika kupata riziki na ujenzi wa taifa. Je, wewe ungependa kufanya kazi gani? Kwa nini?



Kipindi cha 136 na 137 **Kazi mbalimbali 4**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

ubawabu yaya bawabu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

mpya vyombo vilivyotengwa hivyo

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Taja kichwa cha hadithi hii.
2. Ni kazi gani zinazozungumziwa katika hadithi?
3. Bawabu hufanya kazi gani?
4. Je, ungependa kufanya kazi gani? Kwa nini?

**Sarufi: Ukanusho wa Nyakati**

**Kanusha sentensi hizi.**

1. Jeni anafanya kazi ya uyaya.
2. Bawabu atawaelekeza wageni.
3. Mwanafunzi alimpongeza bawabu wao.
4. Yaya atampa mtoto chakula.



## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno yafuatayo ya msamiati: **ubawabu, yaya, bawabu.**

Soma maneno **ukurasa wa 137.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Hoja Kuu**

| Nani au nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno kumi)* |
|---|---|---|
| | | |

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi**

1. Mhusika mkuu kwenye hadithi hii ni nani?
2. Ni jambo lipi linalozungumziwa zaidi kwenye hadithi?
3. Hadithi hii inatufundisha nini?

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Taja kichwa cha hadithi hii. (Bawabu na Yaya)
2. Ni kazi gani zinazozungumziwa katika hadithi? (Ubawabu na uyaya)
3. Bawabu hufanya kazi gani? (Kulinda lango)
4. Je, ungependa kufanya kazi gani? Kwa nini? (Kubali jibu lolote)

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

Waeleze wanafunzi sarufi. Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Unda maneno ya kazi mbalimbali kutoka kwa jedwali **ukurasa wa 140.**

**Majibu**

1. daktari
2. yaya
3. mwalimu
4. bawabu

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 137: Kazi Mbalimbali 4

Kipindi cha 136 na 137 **Kazi mbalimbali 4**

**Matini**

**Bawabu na Yaya**

Kazi ni shughuli zozote ambazo mtu hufanya ili kujipatia riziki yake. Kuna kazi mbalimbali kama vile ubawabu na uyaya.

Kazi kuu ya bawabu ni kulinda lango au jengo fulani. Baadhi ya majengo ambayo bawabu hulinda ni ya kibiashara au makazi ya watu. Wakati mwingine, bawabu hulinda sehemu fulani ya shamba, mali au vyombo vilivyotengwa mahali. Kazi ya ubawabu hufanywa usiku na mchana. Bawabu hulinda mali isiibwe au isiharibiwe. Vilevile, yeye hufungua lango na kuwaelekeza wageni wanaotembelea wakazi. Iwapo kuna uvamizi, itambidi apige firimbi au kuripoti uvamizi huo kwa polisi mara moja. Bawabu hafai kuwaruhusu wageni waingie katika jengo bila kuwakagua.



Kazi ya yaya nayo ni kulea watoto, kuhakikisha kuwa wamekula kuoga. Asipowaogesha watauguа. Vilevile, yaya huosha nyumba. Yeye hufua nguo, huzipiga pasi na kuzikunja.

Watu wengi hupendelea kazi ya ubawabu kwa sababu husaidia katika kudumisha usalama. Wanaopendelea kazi ya uyaya husema kuwa kazi hii ina jukumu la kuwalinda na kuwatunza watoto. Hata hivyo, kazi hizi zote ni muhimu kwani zote huchangia katika kupata riziki na ujenzi wa taifa. Je, wewe ungependa kufanya kazi gani? Kwa nini?

Mali ya Serikali ya Kenya



Kipindi cha 136 na 137 **Kazi mbalimbali 4**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

ubawabu yaya bawabu

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

mpya vyombo vilivyotengwa hivyo

**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Taja kichwa cha hadithi hii.
2. Ni kazi gani zinazozungumziwa katika hadithi?
3. Bawabu hufanya kazi gani?
4. Je, ungependa kufanya kazi gani? Kwa nini?

**Sarufi: Ukanusho wa Nyakati**

**Kanusha sentensi hizi.**

1. Jeni anafanya kazi ya uyaya.
2. Bawabu atawaelekeza wageni.
3. Mwanafunzi alimpongeza bawabu wao.
4. Yaya atampa mtoto chakula.



Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **mpya, afanyavyo, vyombo, vilivyotengwa, wapya, vyote**

Funza sauti: **vy, py**

Soma maneno **ukurasa wa 137**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi

Wanafunzi wakanushe sentensi katika **ukurasa wa 137**.

**Majibu**

1. Jane hafanyi kazi ya uyaya.
2. Bawabu hatawaelekeza wageni.
3. Mwanafunzi hakumpongeza bawabu wao.
4. Yaya hatampa mtoto chakula.

## Kuandika

**Wasifu - Kuhakiki**

Hakiki makala ya mjadala.

**T:** Mwalimu na wanafunzi wahakiki nakala huku wakizingatia:

- Uakifishaji
- iwapo nakala inaeleweka
- Tahajia.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi tano kuhusu kazi ya mkulima.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 138: Kazi Mbalimbali 4

Kipindi cha 138 na 139 **Kazi mbalimbali 4**

Matini

**Daktari au Mkulima**





Maisha ya binadamu hutegemea afya bora. Afya bora hutokana na vyakula tunavyokula hasa lishe bora. Usipokula lishe bora afya hudhoofika. Afya ikidhoofika, ni muhimu kumuona daktari. Je, kati ya daktari na mkulima ni nani bora?

Mkulima ndiye huendesha nchi kwani ukiwa na njaa huwezi kufanya kazi vizuri. Vyakula vyote tunavyokula ili tupate nguvu na afya bora hutokana na kazi ya ukulima. Wasomi husema ukila tufaha moja kila siku basi hutamwona daktari kwa urahisi. Ukila lishe bora utakuwa na afya njema. Kilimo humletea mkulima pesa za kukidhi mahitaji yake baada ya kuuza mazao yake.

Kazi ya daktari nayo ni muhimu pia. Maradhi yanapotukumba ni sharti tumwone daktari ili tupate matibabu. Usipotibiwa huenda ukafa. Kazi hii ya udaktari inalipwa mshahara mzuri. Baadhi ya madaktari hutumia kompyuta katika kazi zao. Wao hujivunia kazi zao.

Kati ya kazi hizi mbili yaani, ukulima na udaktari ni gani bora? mimi nafikiri kazi zote ni bora. Ukipata matibabu bila lishe bora, hutapona haraka. Mkulima asipokuwa duniani watu hawatapata lishe bora na hawatakuwa na afya. Tukimkosa daktari basi hatutapata matibabu. Tukimkosa mkulima basi hatutapata chakula. Mambo haya si mapya kwetu kwani huzungumziwa na kujadiliwa kila wakati katika vyombo vya mawasiliano.

Mali ya Serikali ya Kenya 138

Kipindi cha 138 na 139 **Kazi mbalimbali 4**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

udaktari mkulima daktari ukulima

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

tunavyokula vyakula mapya kompyuta

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kazi ambazo mwandishi amezungumzia?
2. Daktari hufanya kazi gani?
3. Kazi ya mkulima huwa ni gani?
4. Ungekuwa mkulima au daktari ungewasaidia watu vipi?

Sarufi: Ukanusho wa nyakati

**Kanusha neno lilopigiwa mstari.**

1. Wewe utakuwa na afya njema.
2. Mwalimu alisahihisha vitabu jana.
3. Daktari anamtibu mgonjwa.
4. Mkulima atalima vizuri sana.

139 Hakiuzwi

## Msamiati

Jadili picha. Funza maneno yafuatayo ya msamiati:

**mkulima, udaktari, ukulima.**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.
Soma maneno **ukurasa wa 139.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushairi

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri wao.

## Ufahamu

**Hoja Kuu**

| Nani au nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno kumi)* |
|---|---|---|
| | | |

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi**

1. Mhusika mkuu kwenye hadithi hii ni nani?
2. Ni jambo lipi linalozungumziwa zaidi kwenye hadithi?
3. Hadithi hii inatufundisha nini?

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Taja kazi ambazo mwandishi amezungumzia? (Udaktari na ukulima)
2. Daktari hufanya kazi gani? (Daktari hutibu watu.)
3. Kazi ya mkulima huwa ni gani? (Kazi ya mkulima ni ukulima)
4. Ungekuwa mkulima au daktari ungewasaidia watu vipi? (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Ukanusho wa Nyakati

Wanafunzi wakanushe neno lililopiwa mstari katika **ukurasa wa 139.**

**Majibu**

1. Wewe na afya njema.
2. Mwalimu hakusahihisha vitabu jana.
3. Daktari hakumtibu mgonjwa.
4. Mkulima hatalima vizuri sana.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi tano kuhusu kazi ya daktari.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 138 na 139 **Kazi mbalimbali 4**

### Matini

**Daktari au Mkulima**





Maisha ya binadamu hutegemea afya bora. Afya bora hutokana na vyakula tunavyokula hasa lishe bora. Usipokula lishe bora afya hudhoofika. Afya ikidhoofika, ni muhimu kumuona daktari. Je, kati ya daktari na mkulima ni nani bora?

Mkulima ndiye huendesha nchi kwani ukiwa na njaa huwezi kufanya kazi vizuri. Vyakula vyote tunavyokula ili tupate nguvu na afya bora hutokana na kazi ya ukulima. Wasomi husema ukila tufaha moja kila siku basi hutamwona daktari kwa urahisi. Ukila lishe bora utakuwa na afya njema. Kilimo humletea mkulima pesa za kukidhi mahitaji yake baada ya kuuza mazao yake.

Kazi ya daktari nayo ni muhimu pia. Maradhi yanapotukumba ni sharti tumwone daktari ili tupate matibabu. Usipotibiwa huenda ukafa. Kazi hii ya udaktari inalipwa mshahara mzuri. Baadhi ya madaktari hutumia kompyuta katika kazi zao. Wao hujivunia kazi zao.

Kati ya kazi hizi mbili yaani, ukulima na udaktari ni gani bora? mimi nafikiri kazi zote ni bora. Ukipata matibabu bila lishe bora, hutapona haraka. Mkulima asipokuwa duniani watu hawatapata lishe bora na hawatakuwa na afya. Tukimkosa daktari basi hatutapata matibabu. Tukimkosa mkulima basi hatutapata chakula. Mambo haya si mapya kwetu kwani huzungumziwa na kujadiliwa kila wakati katika vyombo vya mawasiliano.

Mali ya Serikali ya Kenya 138

Kipindi cha 138 na 139 **Kazi mbalimbali 4**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

udaktari mkulima daktari ukulima

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

tunavyokula vyakula mapya kompyuta

### Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Taja kazi ambazo mwandishi amezungumzia?
2. Daktari hufanya kazi gani?
3. Kazi ya mkulima huwa ni gani?
4. Ungekuwa mkulima au daktari ungewasaidia watu vipi?

### Sarufi: Ukanusho wa nyakati

**Kanusha neno lilopigiwa mstari.**

1. Wewe utakuwa na afya njema.
2. Mwalimu alisahihisha vitabu jana.
3. Daktari anamtibu mgonjwa.
4. Mkulima atalima vizuri sana.

139 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **tunavyokula, vyakula, jipya, vyenye.**

Funza sauti: **vy py**

Soma maneno **ukurasa wa 139.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao

## Kuandika

**Wasifu - Kuhakiki**

Hakiki makala ya mjadala.

**U:** Wanafunzi wahakiki nakala huku wakizingatia:

- Uakifishaji
- iwapo nakala inaeleweka
- Tahajia.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi mbili katika wakati ujao na mbili katika wakati uliopita.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 140 **Kazi mbalimbali 4**

Tathmini ya msamiati

**Tunga sentensi ukitumia maneno haya.**

1. udaktari
2. daktari
3. ukulima
4. mkulima

Tathmini ya sarufi

**Kanusha sentensi hizi.**

1. Mwandawiro atafanya kazi ya uyaya.
2. Mwalimu aliwapongeza wanafunzi kwa kupita mtihani.
3. Bawabu amefungua lango la shule.
4. Mama alipika chakula kitamu.
5. Mimi ninaandika vizuri.

Kazi ya Ziada

**Tumia silabi kuunda majina ya wafanyakazi mbalimbali. Kwa mfano: bawabu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| da | wa | ya | mwa |
| li | k | ta | ta |
| bu | ba | ri | mu |

1. ______________________.
2. ______________________.
3. ______________________.
4. ______________________.

Mali ya Serikali ya Kenya 140

### Msamiati
Tunga sentensi ukitumia maneno haya: **udaktari, mkulima, daktari, ukulima.**

### Kusoma maneno
Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika.

Maneno: **onjwa, kunjwa, punjwa, magonjwa, chanjwa tunavyokula, vyakula, mapya, kompyuta, jipya, vyenye, mpya, afanyavyo, vyombo, vilivyotengwa, wapya, vyote**

### Kuchambua Matini: Muhtasari
**U:** [Leo tutaandika muhtasari kwa kurejelea makala tuliyoyasoma wiki hii. Ni nani anaweza kutukumbusha makala tuliyoyasoma wiki hii? Chagua mojawapo ya makala haya na uandike muhtasari. Kumbuka muhtasari huzingatia mambo mawili au matatu. Huzingatia pia funzo au tamati ya makala.]

Tumia maswali yafuatayo kama mwongozo.

- Je makala yanahusu nani au nini?
- Mambo gani 2-3 uliyojifunza?
- Umejifunza nini kutoka kwa hadithi?

### Tathmini ya Sarufi
Kanusha sentensi zilizo katika kitabu **ukurasa wa 140.**

**Majibu**

1. Mwandawiro hatafanya kazi ya uyaya.
2. Mwalimu hakuwapongeza wanafunzi kwa kupita mtihani.
3. Bawabu hakufungua lango la shule.
4. Mama hakupika chakula kitamu.
5. Mimi siandiki vizuri.

### Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa
Andika kuhusu kazi ambayo ungependa kufanya.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha | 141 na 142 | **Dukani 3**

**Matini**

**Noti au Sarafu**

Pesa ni pesa, iwe ya sarafu au noti. Hata hivyo, watu wengi hupendelea noti. Noti ya shilingi elfu moja ni rahisi kubeba kuliko sarafu za shilingi elfu moja. Noti hiyo pia inaweza kukunjwa na kubebwa mkononi. Aliye na sarafu je? Itambidi kutafuta begi.




Noti pia ni rahisi kuhesabu. Ukiwa na noti ya shilingi mia moja, noti ya shilingi hamsini na sarafu ya shilingi arobaini, ni rahisi kujumlisha haraka. Huwezi kupunjwa hata ukifanyiwa hesabu hiyo.

Wanaoweka hela kwenye simu au kadi huwa salama zaidi kuliko wanaobeba pesa taslimu. Unapobeba bunda la noti au sarafu wezi watajua kuwa una pesa. Wezi hao wanaweza kukunyang'anya pesa hizo na hata kukuumiza iwapo utakataa kuwapa hela.

Kuna watu wanaopendelea hela zenyewe na wale wanaopendelea kuweka pesa kwenye simu. Baadhi yao husema wanapenda kubeba hela zenyewe, ni rahisi kufanya biashara ukiwa na pesa mkononi. Wale wanaotumia kadi au simu kununua bidhaa huona ni afueni kwani hawana wasiwasi wa hela hizo kuibwa na wezi. Unaponunua kitu dukani, huna haja ya kungoja muuzaji atafute baki.

Ni vizuri tuende na wakati na kuwa digitali. Ukiweka pesa kwenye simu au kadi, utajipunguzia wasiwasi wa kuporwa. Je, unapenda kununua bidhaa? Wewe hubeba pesa zako aje?

141 Hakiuzwi

Kipindi cha | 141 na 142 | **Dukani 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

Pesa taslimu | sarafu | bunda la noti

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

kupunjwa | ugonjwa | onjwa | kunjwa

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Watu wengi hupendelea pesa gani?
2. Ni njia gani salama ya kubeba pesa?
3. Je, wewe unapenda pesa za aina gani?
3. Taja vitu ambavyo unaweza kununua dukani ukiwa na pesa.

**Sarufi: Matumizi ya alama ya kuuliza (?)**

**Akifisha sentesi zifuatazo kwa kutumia alama ya kuuliza (?).**

1. Je, unapenda pesa za sarafu au za noti
2. Ni nani aliyepoteza noti ya shilingi mia moja
3. Kwa nini ulimpatia mwenye duka pesa
4. Kati ya sarafu na noti ni pesa gani nzito

Mali ya Serikali ya Kenya 142

## Msamiati

Jadili picha pamoja na wanafunzi.

Funza maneno ya msamiati: **pesa taslimu, sarafu, bunda la noti.**

Soma maneno **ukurasa wa 142**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au ushawishi

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Hoja Kuu**

| Nani au Nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno 10 )* |
|---|---|---|
| | | |

**Jibu maswali**

1. Ni jambo gani linalozungumziwa zaidi kwenye kifungu?
2. Mwandishi anatoa sababu gani kwa msimamo wake?
3. Je, wewe unapenda pesa za aina gani?

Mwalimu awahimize wanafunzi umuhimu wa pesa katika ununuzi. Pia asisitize ni vyema kutumia pesa kwa uadilifu.

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Watu wengi hupendelea pesa gani? (Noti)
2. Ni njia gani salama ya kubeba pesa? (Kuweka kwenye simu)
3. Je, wewe unapenda pesa za aina gani? (Kubali jibu lolote sahihi)
3. Taja vitu ambavyo unaweza kununua dukani ukiwa na pesa. (Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Alama ya Kiulizi

Waeleze wanafunzi sarufi. Soma sentensi zenye alama ya kuulizi katika matini. Wanafunzi waandike sentensi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Pesa hutumika kufanya nini?

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 141 na 142 **Dukani 3**

Matini

**Noti au Sarafu**




Pesa ni pesa, iwe ya sarafu au noti. Hata hivyo, watu wengi hupendelea noti. Noti ya shilingi elfu moja ni rahisi kubeba kuliko sarafu za shilingi elfu moja. Noti hiyo pia inaweza kukunjwa na kubebwa mkononi. Aliye na sarafu je? Itambidi kutafuta begi.

Noti pia ni rahisi kuhesabu. Ukiwa na noti ya shilingi mia moja, noti ya shilingi hamsini na sarafu ya shilingi arobaini, ni rahisi kujumlisha haraka. Huwezi kupunjwa hata ukifanyiwa hesabu hiyo.

Wanaoweka hela kwenye simu au kadi huwa salama zaidi kuliko wanaobeba pesa taslimu. Unapobeba bunda la noti au sarafu wezi watajua kuwa una pesa. Wezi hao wanaweza kukunyang'anya pesa hizo na hata kukuumiza iwapo utakataa kuwapa hela.

Kuna watu wanaopendelea hela zenyewe na wale wanaopendelea kuweka pesa kwenye simu. Baadhi yao husema wanapenda kubeba hela zenyewe, ni rahisi kufanya biashara ukiwa na pesa mkononi. Wale wanaotumia kadi au simu kununua bidhaa huona ni afueni kwani hawana wasiwasi wa hela hizo kuibwa na wezi. Unaponunua kitu dukani, huna haja ya kungoja muuzaji atafute baki.

Ni vizuri tuende na wakati na kuwa digitali. Ukiweka pesa kwenye simu au kadi, utajipunguzia wasiwasi wa kuporwa. Je, unapenda kununua bidhaa? Wewe hubeba pesa zako aje?

141 Hakiluzwi

Kipindi cha 141 na 142 **Dukani 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

Pesa taslimu sarafu bunda la noti

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

kupunjwa ugonjwa onjwa kunjwa

Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Watu wengi hupendelea pesa gani?
2. Ni njia gani salama ya kubeba pesa?
3. Je, wewe unapenda pesa za aina gani?
3. Taja vitu ambavyo unaweza kununua dukani ukiwa na pesa.

Sarufi: Matumizi ya alama ya kuuliza (?)

**Akifisha sentensi zifuatazo kwa kutumia alama ya kuuliza (?).**

1. Je, unapenda pesa za sarafu au za noti
2. Ni nani aliyepoteza noti ya shilingi mia moja
3. Kwa nini ulimpatia mwenye duka pesa
4. Kati ya sarafu na noti ni pesa gani nzito

Mali ya Serikali ya Kenya 142

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **magonjwa**, **chinjwa**, **onjwa**, **kunjwa**, **punjwa.**

Funza sauti, **njw**

Soma maneno **ukurasa wa 142.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Alama ya Kuilizi

Fungueni **ukurasa wa 142** wa vitabu vyenu.

Akifisha sentensi kwa kutumia alama ya kuuliza.

**Majibu**

1. Je, unapenda pesa za sarufi au za noti?
2. Ni nani aliyepoteza noti ya mia moja?
3. Kwa nini ulimpatia mwenye duka pesa?
4. Kati ya sarafu na noti ni pesa gani nzito?

## Kuandika

**Wasifu - Kuhariri**

**T:** Hariri insha ya mjadala na wanafunzi.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tamka maneno haya huku ukiyaandika.

1. punjwa
2. ugonjwa
3. onjwa
4. kunjwa
5. vunjwa

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 143: Dukani 3

Kipindi cha 143 na 144 **Dukani 3**

**Matini**

**Malipo kwa njia ya simu**

Teknolojia ya kisasa imetuwezesha kuweka pesa kwenye simu. Huna haja ya kubeba pesa mfukoni unapoenda dukani. Unaweza kulipia bidhaa dukani kwa njia ya simu. Unaweza kufanya hivyo wakati wowote na mahali popote.



Wanaotumia teknolojia hii hufanya mambo mengi zaidi kuliko walio na pesa taslimu. Kuna baadhi ya huduma zinazoweza kununuliwa kwa kutumia pesa kwenye simu.

Kukitokea dharura kama vile mgonjwa anayehitaji kupelekwa hospitalini, aliye na pesa kwenye simu atazituma mara moja. Je, aliye na zake mfukoni atafanya nini? Atachukua muda mrefu kuzituma kwa kupitia njia nyingine. Hivyo basi, noti ya shilingi mia moja au noti ya shilingi hamsini iliyo mfukoni haitamsaidia mgonjwa huyo haraka. Wanaobeba pesa kwenye simu pia husema wanafanya hivyo ili kulinda usalama wao na wa pesa zao. Je, unakubaliana nao?

Tusiwasahau watu ambao bado wanabeba noti za shilingi mia moja mfukoni. Wao hushikilia kuwa wakati mwingine mitandao ya simu hufeli. Kweli, mitandao hufeli. Lakini hutengenezwa mara moja ikaanza kufanya kazi tena. Jamani, tumieni teknolojia ya kisasa. Itawarahisishia shughuli za kila siku. Ukitaka kuhakikisha, uliza wanaoitumia teknolojia hiyo.

143 Hakiuzwi

Kipindi cha 143 na 144 **Dukani 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

noti ya shilingi mia teknolojia noti ya shilingi hamsini

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vunjwa magonjwa chanjwa ilikunjwa

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kichwa cha hadithi ni kipi?
2. Taja njia rahisi ya kumtumia mtu pesa akiwa mbali.
3. Teknolojia mpya ina upungufu gani?
4. Je, wewe ungependa kulipia bidhaa zako kwa njia ipi? Kwa nini?

**Sarufi: Alama ya kuuliza**

**Tunga sentensi nne huku ukiziakifisha kwa alama ya kuuliza.**

1. ____________________
2. ____________________
3. ____________________
4. ____________________

**Kuandika**

**Andika kisa kifupi ukiwa na mwenzako, kuhusu shughuli za dukani.**

Mali ya Serikali ya Kenya 144

## Msamiati

Jadili picha pamoja na wanafunzi.

Funza maneno ya msamiati: **noti ya shilingi mia moja, teknolojia, noti ya shilingi hamsini**

Andika sentensi moja ukitumia neno la msamiati.

Soma maneno **ukurasa wa 144.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi

Soma kichwa cha hadithi Jadili picha. Uliza wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Hoja Kuu**

| Nani au Nini *(mtu au jambo kuu)* | Jambo maalum *(kuhusu nani au nini)* | Dhana kuu *(chini ya maneno 10 )* |
|---|---|---|
| | | |

**Jibu maswali**

1. Ni jambo gani linalozungumziwa zaidi kwenye kifungu?
2. Mwandishi anatoa sababu gani kwa msimamo wake?
3. Je, wewe ungependa kuweka pesa wapi?

Mwalimu awaeleze wanafunzi umuhimu wa kuhifadhi pesa mahali salama kama vile kwenye simu au benki. Mwanafunzi ajibu maswali yafuatayo iwapo kuna muda wa kutosha.

**Maswali**

*Muda ukiruhusu baada ya kufunza ufahamu, wanafunzi wajibu maswali yaliyoko kwenye vitabu vyao.*

1. Kichwa cha hadithi ni kipi? (Malipo kwa njia ya simu)
2. Taja njia rahisi ya kumtumia mtu pesa akiwa mbali. (Kupitia kwa njia ya simu)
3. Teknolojia mpya ina upungufu gani? ( Kufeli kwa mitambo ya simu)
4. Je, wewe ungependa kulipia bidhaa zako kwa njia ipi? Kwa nini? ( Kubali jibu lolote sahihi)

## Sarufi: Alama ya Kuilizi

Tunga sentensi na uziakifishe kwa alama ya kuuliza.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika sentensi nne huku ukiziakifisha kwa alama ya kiulizi.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 144: Dukani 3

Kipindi cha 143 na 144 **Dukani 3**

**Matini**

### Malipo kwa njia ya simu

Teknolojia ya kisasa imetuwezesha kuweka pesa kwenye simu. Huna haja ya kubeba pesa mfukoni unapoenda dukani. Unaweza kulipia bidhaa dukani kwa njia ya simu. Unaweza kufanya hivyo wakati wowote na mahali popote.



Wanaotumia teknolojia hii hufanya mambo mengi zaidi kuliko walio na pesa taslimu. Kuna baadhi ya huduma zinazoweza kununuliwa kwa kutumia pesa kwenye simu.

Kukitokea dharura kama vile mgonjwa anayehitaji kupelekwa hospitalini, aliye na pesa kwenye simu atazituma mara moja. Je, aliye na zake mfukoni atafanya nini? Atachukua muda mrefu kuzituma kwa kupitia njia nyingine. Hivyo basi, noti ya shilingi mia moja au noti ya shilingi hamsini iliyo mfukoni haitamsaidia mgonjwa huyo haraka. Wanaobeba pesa kwenye simu pia husema wanafanya hivyo ili kulinda usalama wao na wa pesa zao. Je, unakubaliana nao?

Tusiwasahau watu ambao bado wanabeba noti za shilingi mia moja mfukoni. Wao hushikilia kuwa wakati mwingine mitandao ya simu hufeli. Kweli, mitandao hufeli. Lakini hutengenezwa mara moja ikaanza kufanya kazi tena. Jamani, tumieni teknolojia ya kisasa. Itawarahisishia shughuli za kila siku. Ukitaka kuhakikisha, uliza wanaoitumia teknolojia hiyo.

143 Hakiuzwi

Kipindi cha 143 na 144 **Dukani 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

noti ya shilingi mia    teknolojia    noti ya shilingi hamsini

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

vunjwa    magonjwa    chanjwa    ilikunjwa

**Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kichwa cha hadithi ni kipi?
2. Taja njia rahisi ya kumtumia mtu pesa akiwa mbali.
3. Teknolojia mpya ina upungufu gani?
4. Je, wewe ungependa kulipia bidhaa zako kwa njia ipi? Kwa nini?

**Sarufi: Alama ya kuuliza**

**Tunga sentensi nne huku ukiziakifisha kwa alama ya kuuliza.**

1. ____________________
2. ____________________
3. ____________________
4. ____________________

**Kuandika**

**Andika kisa kifupi ukiwa na mwenzako, kuhusu shughuli za dukani.**

Mali ya Serikali ya Kenya 144

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **chinjwa**, **ugonjwa**, **vunjwa**, **magonjwa.**

Funza sauti, **njw**

Soma maneno **ukurasa 144.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi.

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Wasifu - Kuhariri**

**U:** Hariri insha ya mjadala.

Wanafunzi wahariri kifungu walichokiandika wiki iliyo pita

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa


Taja aina za noti nne zinazotumika nchini Kenya.

**Majibu**

1. Noti ya shilingi hamsini.
2. Noti ya shilingi mia moja.
3. Noti ya shilingi mia mbili.
4. Noti ya shilingi mia tano, elfu moja n.k.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 145: Dukani 3


Kipindi cha 145 **Dukani 3**

Tathmini ya msamiati

**Jumlisha. Andika majibu yako kwa maneno.**

1. Noti ya shilingi hamsini + Sarafu ya shillingi ishirini = ______
2. Sarafu ya shilingi arobaini + Sarafu ya shilingi kumi = ______
3. Nikiwa na shilingi mia moja kwenye simu, nitoe shilingi hamsini nitabaki na ngapi?
4. Je, unafikiria kifutio huuzwa shilingi ngapi?

Tathmini ya Sarufi

**Tumia maneno yafuatavyo kuunda sentensi.**

1. langu
2. wako
3. lake
4. wangu

145

Hakiuzwi

## Msamiati

Kamilisha zoezi la msamiati **ukurasa wa 45.**

**Majibu**

1. Shilingi sabini.
2. Shilingi hamsini.
3. Shilingi hamsini.
4. Kubali jibu lolote sahihi.

## Kuchambua Matini: Muhtasari

**U:** [Leo tutaandika muhtasari kwa kurejelea makala tuliyoyasoma wiki hii. Ni nani anaweza kutukumbusha makala tuliyoyasoma wiki hii? Chagua mojawapo ya makala haya na uandike muhtasari. Kumbuka muhtasari huzingatia mambo mawili au matatu muhimu. Huzingatia pia funzo na tamati ya makala.]

Tumia maswali yafuatayo kama mwongozo.

- Je makala yanahusu nani au nini?
- Mambo gani 2-3 uliyojifunza?
- Umejifunza nini kutoka kwa hadithi?

## Sarufi: Vimilikishi

Tumia vimilikishi vifuatavyo kuunda sentensi.

**langu, wako, lake, wangu**

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Chora noti ya shilingi mia moja au hamsini.

## Kazi ya Nyongeza

Ukiwa na marafiki yako, jadili umuhimu wa pesa.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Hakiuzwi

Kipindi cha 146 na 147 **Ndege Nimpendaye 3**

Matini

### Ndege



Ndege ni viumbe wenye umuhimu mwingi. Kuna aina mbili za ndege. Kuna ndege wa nyumbani na ndege wa porini. Mimi ninaonelea kuwa ndege wa nyumbani ni bora kuliko wale wa porini.

Ndege wa nyumbani kama bata na kuku, hufugwa kwa sababu ya nyama yao tamu. Baada ya kuuzwa mkulima hujipatia pesa. Vilevile, mayai yao yana virutubisho kama protini na vitamini ambazo ni muhimu kwa afya yetu.

Ndege wa nyumbani, hasa kuku hujengewa kizimba. Kinyesi cha ndege wa nyumbani hutumika kama rutuba shambani.

Zaidi ya nyama, kuku, hutupa manyoya ambayo huweza kutumika kutengeneza foronya au mto.

Ndege wa porini nao ni muhimu pia. Hapa nchini, ndege wa porini ni kivutio cha watalii ambao huleta pesa za kigeni nchini. Ndege wa porini pia wanasaidia kuwala baadhi ya wadudu wanaoishi chini ya mchanga na huharibu mimea.

Kuna baadhi ya watu ambao hukata misitu. Kitendo hiki huvuruga viota vya ndege wa mwituni vilivyo juu ya miti. Watu wengine huwawinda ndege ili kupata nyama. Ni muhimu sote kuyatunza mazingira ya ndege. Kwa kufanya hivyo, tutatosheleza mahitaji yetu ya nyama na mayai. Pia tutaimarisha uchumi wetu.

Ingawa ndege wote ni muhimu kwetu, ninaolelea kuwa ndege wa nyumbani ni bora kuliko wale wa porini. Je, unakubaliana nami?

Mali ya Serikali ya Kenya 146

Kipindi cha 146 na 147 **Ndege Nimpendaye 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

hufugwa virutubisho viota

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

ndege wanapochinjwa nyumbani manyoya

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**


1. Ndege wa nyumbani wana umuhimu gani?
2. Ndege wa porini wana umuhimu gani?
3. Pesa zinazotokana na utalii hutumiwa vipi hapa nchini?
4. Taja ndege wa nyumbani na wa mwituni unaowajua.

Sarufi: Vihusishi

**Tunga sentensi ukitumia "juu ya" au "chini ya" kwa kuzingatia picha ulizopewa.**

1. 

2. 

3. 

4. 

147 Hakiluzwi

## Msamiati

Jadili picha.

Funza maneno ya msamiati: **hufugwa, virutubisho, viota.**

Soma maneno **ukurasa wa 147.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mijadala au Ushawishi.

Soma kichwa cha hadithi na wanafunzi. Jadili picha. waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Maswali**

1. Ndege wa nyumbani wana umuhimu gani? (mayai na nyama. Kinyesi chao hutumika kama mbolea. Pia manyoya yao yanatumiwa kutengeneza foronya.)
2. Pesa zinazotokana na utalii hutumiwa vipi hapa nchini? (Kuimarisha uchumi nchini.)
3. Ndege wa porini wana umuhimu gani? (huwavutia watalii.)
4. Taja baadhi ya ndege wa nyumbani unaowajua. (njiwa, bata bukini na wengineo.)

## Sarufi: Matumizi ya Vihusishi

Waeleze wanafunzi sarufi. Soma sentensi kutoka kwa matini. Andika sentensi na wanafunzi. Wanafunzi waandike peke yao.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

**Chora picha zinazoonyesha:**

1. Kikombe kikiwa juu ya meza.
2. Mpira ukiwa chini ya kitanda.
3. Paka akiwa juu ya kiti.
4. Kitabu kikiwa juu ya meza.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 147: Ndege Nimpendaye 3

Kipindi cha 146 na 147 **Ndege Nimpendaye 3**

**Matini**

**Ndege**



Ndege ni viumbe wenye umuhimu mwingi. Kuna aina mbili za ndege. Kuna ndege wa nyumbani na ndege wa porini. Mimi ninaonelea kuwa ndege wa nyumbani ni bora kuliko wale wa porini.

Ndege wa nyumbani kama bata na kuku, hufugwa kwa sababu ya nyama yao tamu. Baada ya kuuzwa mkulima hujipatia pesa. Vilevile, mayai yao yana virutubisho kama protini na vitamini ambazo ni muhimu kwa afya yetu.

Ndege wa nyumbani, hasa kuku hujengewa kizimba. Kinyesi cha ndege wa nyumbani hutumika kama rutuba shambani.

Zaidi ya nyama, kuku, hutupa manyoya ambayo huweza kutumika kutengeneza foronya au mto.

Ndege wa porini nao ni muhimu pia. Hapa nchini, ndege wa porini ni kivutio cha watalii ambao huleta pesa za kigeni nchini. Ndege wa porini pia wanasaidia kuwala baadhi ya wadudu wanaoishi chini ya mchanga na huharibu mimea.

Kuna baadhi ya watu ambao hukata misitu. Kitendo hiki huvuruga viota vya ndege wa mwituni vilivyo juu ya miti. Watu wengine huwawinda ndege ili kupata nyama. Ni muhimu sote kuyatunza mazingira ya ndege. Kwa kufanya hivyo, tutatosheleza mahitaji yetu ya nyama na mayai. Pia tutaimarisha uchumi wetu.

Ingawa ndege wote ni muhimu kwetu, ninaolelea kuwa ndege wa nyumbani ni bora kuliko wale wa porini. Je, unakubaliana nami?

Mali ya Serikali ya Kenya

146

Kipindi cha 146 na 147 **Ndege Nimpendaye 3**

**Msamiati**

**Soma maneno haya.**

hufugwa virutubisho viota

**Kusoma maneno**

**Soma maneno haya.**

ndege wanapochinjwa nyumbani manyoya


**Ufahamu**

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ndege wa nyumbani wana umuhimu gani?
2. Ndege wa porini wana umuhimu gani?
3. Pesa zinazotokana na utalii hutumiwa vipi hapa nchini?
4. Taja ndege wa nyumbani na wa mwituni unaowajua.

**Sarufi: Vihusishi**

**Tunga sentensi ukitumia "juu ya" au "chini ya" kwa kuzingatia picha ulizopewa.**




147 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

*Andika maneno ubaoni*: **hujengewa, mazingira, huwawinda, ndege, kibanda, mchanga**

Funza sauti: **ng, nd**

Soma maneno **ukurasa wa 146**

## Kusoma Matini: Makala ya Mijadala au Ushawishi.

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Sarufi: Vihusishi: Kutunga

Waelekeze wanafunzi kutunga sentensi zinazorejelea vihusishi **"juu ya"** na **"chini ya"** kwa kuzingatia picha zilizo kwenye **ukurasa wa 147**.

**Majibu**

1. Ndege yuko juu ya mti/tawi.
2. Kitabu kiko juu ya kiti.
3. Kalamu iko juu ya meza.
4. Jiwe liko chini ya meza.

## Kuandika

**Wasifu - Kuchapisha**

Kuchapisha nakala. Mwanafunzi amsomee mwenzake insha ya mjadala aliyoandika.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Tunga sentensi ukitumia maneno haya: **viota, ndege, njiwa, kulinda**

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 148: Ndege Nimpendaye 3

Kipindi cha 148 na 149 **Ndege Nimpendaye 3**

Matini

**Ndege Nimpendaye**



Siku moja niliyatembelea makao ya wanyama. Nilimwona njiwa mmoja aliyekuwa amevunjika ubawa. Wafanyakazi pale walimtengenezea kiota kizuri na kumpa maji na chakula. Waliweka ua wa waya ili kuzuia wanyama wengine kuja kumdhuru yule njiwa. Nilifurahi sana kuona kuwa tunaweza kuonyesha ukarimu kwa viumbe wengine.

Niliporudi nyumbani, nilimwona ndege aina ya mnana aliyekuwa ameanguka chini ya mti wa maembe. Kidona chake kilikuwa kimeumia na alikuwa na maumivu. Nilimchukua nikamweka ndani ya sanduku lenye tundu. Nikaliweka lile sanduku kando ya jiko letu. Baadaye, nilimpa maji na unga wa mahindi.

Ikawa kazi yangu ni kumlea yule mnana huku akiendelea kupata nafuu. Alipoanza kuimba na kuonekana mchangamfu, nilifurahi. Baada ya wiki kadhaa, alionekana kuwa mpweke. Nilijua alihitaji kwenda kuishi na wenzake. Nilimruhusu mnana kwenda zake, japo kwa huzuni kwani nilikuwa nimemzoea kama rafiki.

Asubuhi na mapema siku iliyofuata, niliamshwa na kelele za ndege waliokuwa kwenye mti nje ya nyumba yetu. Nilipotoka nje niliona kikundi kikubwa cha ndege. Walikuwa wanajenga viota juu ya miti. Nilipotazama kwa makini nilimwona yule mnana niliyemtunza akiwa miongoni mwao. Ndege nimpendaye alikuwa amerejea nyumbani na wenzake. Nikaelewa zaidi umuhimu wa kuwatunza ndege.



Kipindi cha 148 na 149 **Ndege Nimpendaye 3**

Msamiati

**Soma maneno haya.**

ubawa mnana kidona

Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

mchangamfu lenye tundu mahindi

Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ndege aliyeonekana katika makao ya wanyama alikuwa ndege yupi?
2. Nyumba ya ndege huitwaje?
3. Taja ndege wawili wa porini unaowajua.
4. Je, unawapenda ndege? Taja ndege umpendaye.

Sarufi: Vihusishi

**Tumia "chini ya" au "juu ya" kujaza mapengo.**

1. Ndege ametua _______ mti.
2. Mgeni amelala ______ kitanda.
3. Meli imeelea _______ maji.
4. Maji yaliteremka _______ mlima.



## Msamiati

Jadili picha.

Funza msamiati ufuatao: **bawa, mnana, kidona**

Andika sentensi moja ukitumia msamiati.

Soma maneno **ukurasa wa 149.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi.

Soma kichwa cha hadithi Jadili picha. Waulize wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi.

## Ufahamu

**Maswali**

1. Ndege aliyeonekana katika makao ya wanyama alikuwa ndege yupi? (Njiwa)
2. Nyumba ya ndege huitwaje? (Nyumba ya ndege huitwa kiota.)
3. Taja ndege wawili wa porini unaowajua. (Watoto wataje ndege kama mbuni, mbayuwayu na kadhalika.)
4. Je, unawapenda ndege? Taja ndege umpendaye. (Wanafunzi wataje ndege wawapendao.)

## Sarufi: Vihusishi

Jaza mapengo kwa kutumia vihusishi "**juu ya**" na "**chini ya**"

**Majibu**

1. juu ya
2. juu ya
3. juu ya
4. chini ya

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Jaza mapengo ukitumia maneno haya: **mnana, kuku, mbuni, tausi**

1. _______________ ana shingo ndefu.
2. _______________ ni ndege wa nyumbani.
3. _______________ ana rangi nzuri.
4. _______________ ni ndege mdogo.

**Majibu**

1. Mbuni
2. Kuku
3. Tausi
4. Mnana

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

# Kipindi cha 149: Ndege Nimpendaye 3

Kipindi cha 148 na 149 **Ndege Nimpendaye 3**

### Matini

**Ndege Nimpendaye**



Siku moja niliyatembelea makao ya wanyama. Nilimwona njiwa mmoja aliyekuwa amevunjika ubawa. Wafanyakazi pale walimtengenezea kiota kizuri na kumpa maji na chakula. Waliweka ua wa waya ili kuzuia wanyama wengine kuja kumdhuru yule njiwa. Nilifurahi sana kuona kuwa tunaweza kuonyesha ukarimu kwa viumbe wengine.

Niliporudi nyumbani, nilimwona ndege aina ya mnana aliyekuwa ameanguka chini ya mti wa maembe. Kidona chake kilikuwa kimeumia na alikuwa na maumivu. Nilimchukua nikamweka ndani ya sanduku lenye tundu. Nikaliweka lile sanduku kando ya jiko letu. Baadaye, nilimpa maji na unga wa mahindi.

Ikawa kazi yangu ni kumlea yule mnana huku akiendelea kupata nafuu. Alipoanza kuimba na kuonekana mchangamfu, nilifurahi. Baada ya wiki kadhaa, alionekana kuwa mpweke. Nilijua alihitaji kwenda kuishi na wenzake. Nilimruhusu mnana kwenda zake, japo kwa huzuni kwani nilikuwa nimemzoea kama rafiki.

Asubuhi na mapema siku iliyofuata, niliamshwa na kelele za ndege waliokuwa kwenye mti nje ya nyumba yetu. Nilipotoka nje niliona kikundi kikubwa cha ndege. Walikuwa wanajenga viota juu ya miti. Nilipotazama kwa makini nilimwona yule mnana niliyemtunza akiwa miongoni mwao. Ndege nimpendaye alikuwa amerejea nyumbani na wenzake. Nikaelewa zaidi umuhimu wa kuwatunza ndege.

Mali ya Serikali ya Kenya 148

Kipindi cha 148 na 149 **Ndege Nimpendaye 3**

### Msamiati

**Soma maneno haya.**

ubawa mnana kidona

### Kusoma maneno

**Soma maneno haya.**

mchangamfu lenye tundu mahindi

### Ufahamu

**Jibu maswali haya kulingana na hadithi.**

1. Ndege aliyeonekana katika makao ya wanyama alikuwa ndege yupi?
2. Nyumba ya ndege huitwaje?
3. Taja ndege wawili wa porini unaowajua.
4. Je, unawapenda ndege? Taja ndege umpendaye.

### Sarufi: Vihusishi

**Tumia "chini ya" au "juu ya" kujaza mapengo.**

1. Ndege ametua _______ mti.
2. Mgeni amelala ______ kitanda.
3. Meli imeelea _______ maji.
4. Maji yaliteremka _______ mlima.

149 Hakiuzwi

## Kusoma Maneno

Andika maneno haya ubaoni: **kuwalinda, akaendelea, iliyotengewa, wamtengenezee, maandalizi, angamiza**

Funza sauti: **ng, nd.**

Soma maneno **ukurasa wa 149.**

## Kusoma Matini: Makala ya Mjadala au Ushawishi.

Wanafunzi wawasomee wenzao.

## Kuandika

**Wasifu - Kuchapisha**

1. Mwanafunzi asomee mwenzake makala aliyoandika.
2. Kumbusha mwanafunzi kuwa makini anaposomewa makala.
3. Waulize wanafunzi 2-3 kuelezea kuhusu makala.

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Andika kisa kifupi kuhusu ndege umpendaye.

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 150: Ndege Nimpendaye 3

Kipindi cha 150 **Ndege Nimpendaye 3**

Tathmini ya msamiati

**Tazama picha**

Andika sentensi nne kuhusu picha hii.



Tathmini ya Sarufi: Vihusishi

1. Tunga sentensi mbili ukitumia kihusishi "chini ya".
2. Tunga sentensi mbili ukitumia kihusishi "juu ya".

Mali ya Serikali ya Kenya 150

## Tathmini ya msamiati

Fungueni **ukurasa wa 150** wa vitabu vyenu. Andika sentensi nne kuhusu picha hii.

Hakikisha kuwa umetumia vihusishi hivi. "**Juu ya**," "**ndani ya**," "**nje ya**," "**kando ya**".

## Kusoma Maneno

Soma neno mara mbili polepole huku wanafunzi wakiliandika: **kuwalinda, akaendelea, iliyotengewa, wamtengenezee, maandalizi, angamiza, mchangamfu, tundu, wanapochanjwa, manyoya**

## Kuchambua Matini

**Muhtasari**

N: Leo tutaandika muhtasari kwa kurejelea makala tuliyoyasoma wiki hii. Ni nani anaweza kutukumbusha makala tuliyoyasoma wiki hii? Chagua mojawapo ya makala haya na uandike muhtasari. Kumbuka muhtasari huzingatia mambo mawili au matatu muhimu. Huzingatia pia funzo au tamati ya makala.

## Sarufi: Tathmini ya Sarufi

1. Tunga sentensi mbili  ukitumia kihusishi "chini ya"
2. Tunga sentensi mbili ukutumia kihusishi "juu ya"

## Kazi ya Ziada Iliyopendekezwa

Msomee mlezi wako sentensi zifuatazo. Sahihisha sentensi sahihi.

1. Tunda liko juu ya meza.
2. Mtoto ameketi juu ya kitanda.
3. Pakiti iko chini ya kabati.
4. Rununu iko chini ya kiti.

## Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji.

Mwanafunzi atambue vitu mbalimbali na kusema ikiwa viko '**chini ya**' au '**juu ya**' pale vilipo.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

JAMHURI YA KENYA
Mali ya
Serikali ya Kenya
HAKIUZWI

# Kiswahili 3

## Mazoezi ya Lugha

### Mwongozo wa Mwalimu

Mwongozo huu wa mwalimu wa gredi ya 3 umetayarishwa kwa kurejelea pakubwa mbinu za utafiti ili kumsaidia mwalimu anapofundisha kuwasaidia wanafunzi kukuza ujuzi wao katika lugha ya Kiswahili. **Mwongozo huu umeshughulikia uhusiano na maadili, uhusiano na masuala mutambuko, sehemu nne za ujifunzaji lugha – kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika, vilevile mada zote na maadili yaliyojadiliwa katika mtaala.** Mwongozo huu unamwezesha mwalimu kuwapa wanafunzi wa gredi ya 3 mbinu tofauti za kusoma, kujifundisha na kujitathmini na hivyo basi kuakifia malengo lengwa kwa kurejelea sehemu husika za kipindi/somo.

Mwongozo huu unarejelea yaliyojiri wakati wa muda wa majaribio ya Tusome. Tusome imedhaminiwa na USAID na kutekelezwa na Wizara ya Elimu. Malengo ya kitabu hiki ni kuwa wanafunzi watakaokamilisha vipindi na masomo kwenye vitabu vya wanafunzi watakuwa wamejikimu na ujuzi wa kuweza kusoma katika gredi ya 3. Pia, wanafunzi wataweza kusoma kwa ufasaha na kuelewa wanachokisoma na kuandika. Hivyo, wanafunzi wakimaliza masomo ya gredi ya 3 watakuwa na uwezo wa kusoma na kujifunza kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya ujifunzaji katika gredi za juu.

Vipengele muhimu vilivyopewa kipao mbele kwenye mwongozo huu wa gredi ya 3 ni:

- Shughuli za ufundishaji ambazo ni za kufurahisha wakati wa kufundisha mada zilizomo kwenye mtaala KICD.
- Mpangilio maalum wa shughuli za ufundishaji zilizopangwa kwa mtiririko na msambao ufaao kwa kurejelea utafiti uliofanywa katika kufunza na kujifunza Kiswahili.
- Nakala za kitabu cha mwanafunzi kenye mwongozo huu ili kumwenzesha mwalimu kufanya marejeleo ya moja kwa moja na kwa urahisi anapofundisha.
- Hadithi tamu zinazolandana na tamaduni na umri wa mwanafunzi zitakazo msaaidia pakubwa katika kukuza ujuzi wake wa kusoma.
- Maelekezo yaliyopangwa vizuri kumwongoza mwalimu katika kuutumia mwongozo kwa urahisi.
- Hadithi zilizoandikwa za kiwango cha mwanafunzi na rahisi kusoma ambazo zitamwenzesha mwanafunzi kusoma na kuelewa hadithi husika.
- Hadithi za mwalimu ambazo zinalenga kukuza msamiati na ujuzi wa kusikiliza wa mwanafunzi.

Mwongozo huu umetayarishwa na wataalamu wenye tajriba kubwa kutoka Wizara ya Elimu, Tume ya Huduma ya Walimu, Taasisi ya Masomo Maalumu ya Kenya, na Taasisi ya usimamizi wa Elimu nchini Kenya.

USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa U.S. Agency for International Development (USAID) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

ISBN 978-9966-110-03-9

© 2018